# MPANGO WA KIMUNGU WA ZAMA

# MASOMO

**KATIKA**

# MAANDIKO

**“Njia ya wenye haki ni kama nuru ya kwanza yamapambazuko, ambayo hung’aa zaidi na zaidi hadi mchana mkamilifu”**

**JUZUU YA I**

# Mpango wa Kimungu wa zama

**Utetezi juu ya Tabia na utawala wa Mungu:**

Kuonyesha, kwa Kutambua na Kuunganisha Maandiko Yote, Kwamba Kuruhusiwa kwa Uovu, Zamani na Sasa, ni kwa Madhumuni ya Kufundisha na Kuandaa Wanadamu kwa Ajili ya Kuingia Katika **ENZI YA DHAHABU YA UNABII** Ambayo Familia Zote za Duniani Zitabarikiwa kwa Ujuzi mkamilifu wa Mungu na Fursa Kamili ya Kufikia Uzima wa Milele Kupitia Mkombozi, Ambaye Wakati Huo Atakuwa Mrejeshaji Mkuu na Mtoaji wa Uzima. **Matendo 3:19-21**

**--------------**

**KAZI HII IMETOLEWA:**

**Kwa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana**

KWA MASLAHI YA

WATAKATIFU WAKE WALIOJITOA,

WANAOSUBIRI KUKUBALIWA KAMA WATOTO,

--NA YA--

"WOTE WANAOMWITA BWANA KILA MAHALI,"

"JUMUIYA YA WAAMINI,"

--NA YA--

UUMBAJI UNAOGUA, UNAOUMIA NA KUSUBIRI

KUFUNULIWA KWA WANA WA MUNGU.

"Ili wote waone ushirika wa fumbo lililofichwa katika Mungu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." "Ambalo ndani yake ametujaza tele kwa hekima na busara zote, akitujulisha fumbo la mapenzi yake, kwa kadiri ya kusudi lake jema aliloliweka mwenyewe; kwamba katika utawala wa utimilifu wa nyakati aweze kukusanya vitu vyote pamoja, katika Kristo." **Waefeso 3:4,5,9; 1:8-10**

**Kimeandikwa Mwaka 1886 Na Mch.Charles Taze Russell.**

## UTANGULIZI

MWANDISHI na wachapishaji wanapenda kutoa shukrani zao za wazi kwa fadhila za Mungu ambazo zimewaruhusu kuhusika na usambazaji wa Kitabu hiki, na matokeo yake—nuru, furaha, amani, ushirika na Mungu, kwa nafsi nyingi zenye njaa, zenye kiu, na zilizofadhaika. Toleo la kwanza katika muundo wake wa sasa lilitolewa mwaka 1886. Tangu wakati huo, toleo moja limefuata lingine kwa kasi kubwa na katika lugha ishirini tofauti, hadi sasa kuna nakala karibu milioni tano za kitabu hiki mikononi mwa watu duniani kote.

Hatuwezi kutarajia kuwa vitabu hivi vyote vimesomwa; lakini barua zinazoendelea kutufikia zinatuhakikishia kwamba vinafanya kazi kwa nguvu katika mioyo na akili za watu kila mahali. Maelfu wanatuandikia kwamba wameshawishika—baadhi yao ambao hapo awali hawakuamini kabisa Biblia kama Ufunuo wa Kimungu kwa wanadamu. Wengine wanaandika kwamba walikuwa hawamwamini Mungu (atheists) au karibu hivyo, kwa sababu hawakuwa wamejua hapo awali Mungu wa kweli na Mpango wake wa Kweli wa Zama Zote, na hawakuweza kukubali, kuthamini au kumwabudu Mungu anayewasilishwa kwao katika Imani za Kimadhehebu (creeds).

Kwa zaidi ya miaka mitano kabla ya kuchapishwa kwa mara ya kwanza kwa Kitabu hiki, tulikuwa na maudhui yale yale yaliyochapishwa chini ya jina lingine na kuwasilishwa tofauti. Kitabu hicho kiliitwa "*Chakula kwa ajili ya Wakristo Wenye Fikra.*" Mtindo wake ulikuwa tofauti kwa kuwa kwanza kilishambulia makosa—yakiyabomoa; na kisha, badala yake, kikawa kinajenga muundo wa Kweli. Hatimaye tulijifunza kuwa hii haikuwa njia bora zaidi—kwamba wengine waliogopa walipoona makosa yao yakianguka, na walishindwa kusoma zaidi vya kutosha ili

kupata mtazamo wa muundo mzuri wa Kweli badala ya makosa yaliyobomolewa.

Kitabu hiki cha sasa kiliandikwa kutoka kwenye mtazamo tofauti. Kinawasilisha Kweli, kinaonyesha nguvu na uzuri wake, na kisha kinapendekeza kuondolewa kwa makosa, si tu kama yasiyo ya lazima, bali kama yasiyo na maana kabisa na yenye madhara makubwa. Hivyo, msomaji wa MPANGO WA MUNGU WA NYAKATI ZOTE kila hatua anapata uimarishwaji wa imani na ukaribu mkubwa zaidi na Bwana, na kwa hiyo anapata uhakika kwamba yuko katika njia sahihi. Baada ya kuona Kweli, makosa yanaonekana zaidi na zaidi kuwa ya kipumbavu, yasiyo na thamani, yenye madhara, na yanaachwa kwa furaha.

Adui mkuu, bila shaka, hana upendo kwa chochote kinachofungua macho ya watu wa Mungu, kuongeza heshima yao kwa Kitabu cha Mungu, na kuvunja utegemezi wao kwa Imani za Kibinadamu (creeds). Kwa hiyo, Adui mkuu, kama ambavyo tungeweza kutarajia, anakipinga sana kitabu hiki. Wachache wanatambua nguvu na ujanja wa Shetani; wachache wanatambua maana ya maneno ya Mtume kuhusu Mkuu huyu wa Giza anayejigeuza kuwa malaika wa nuru, ili kupigana na Kweli na kuharibu ushawishi wake. Wachache wanatambua kwamba Adui wetu mjanja anatafuta kuwatumia watu bora zaidi, wenye nguvu zaidi, na wenye ushawishi mkubwa zaidi wa Mungu kuzuia nuru ising'ae na kuweka Mpango wa Kimungu wa Zama Zote mbali na watu.

Wachache wanatambua kwamba tangu kutungwa kwa imani za kimadhehebu kuanza, mwaka 325 B.K., hakukuwa na uchunguzi wa Biblia kwa miaka 1260. Wachache wanatambua kwamba katika kipindi hicho, imani za kimadhehebu zilifungwa imara katika akili za mamilioni ya watu, zikiwafunga katika makosa mabaya, na kuwapofusha wasione tabia ya Kimungu ya Hekima, Haki, Upendo, na Nguvu. Wachache wanatambua kwamba tangu Matengenezo ya Kiprotestanti — tangu Biblia ilipoanza kurudi mikononi mwa watu — marekebisho yenye nia njema lakini

yaliyopotoshwa yamepofushwa na kulemazwa na makosa ya zamani, na, kwa upande wao, yametumika kuwaweka watu gizani.

Wachache wanatambua kwamba uchunguzi halisi wa Biblia, kama ule uliofanywa katika Kanisa la kwanza katika siku za Mitume, sasa umerejea tu kwa wanafunzi wa Biblia.

Katika matoleo ya kwanza ya Kitabu hiki, kilichoitwa "Millennial Dawn" (Mwanzo wa Milenia) kilitumika; lakini tuligundua kwamba baadhi walidanganywa na kufikiria kuwa ni riwaya. Ili asiwepo yeyote atakayedanganyika, na kwamba asiwepo yeyote atakayenunua kwa udanganyifu kama huo, baadaye tulipitisha jina la mfululizo la sasa, **'Masomo katika Maandiko,'** ambalo hakuna anayeweza kulielewa vibaya.

Maswali mengi yametufikia kuhusu kwa nini vitabu hivi haviwezi kupatikana katika maduka ya vitabu. Jibu letu ni kwamba ingawa wachapishaji wa vitabu wangefurahi kuwa na vitabu hivi, kuna baadhi ya washupavu wa kidini ambao hawaruhusu kuuzwa kwake—wakitishia kususia. Mwanzoni hili lilionekana kama janga kubwa—kana kwamba nguvu za Adui zingeruhusiwa kuzuia kusambazwa kwa Kweli. Lakini Mungu kwa neema yake alibadilisha hali, hivi kwamba leo labda hakuna kitabu kingine chenye usambazaji mkubwa na endelevu kama Kitabu hiki. Wale ambao, kwa chuki, walikataa kusoma kitabu na kukipiga vita, walifanya hivyo kwa sababu waliamini uongo na upotoshaji.

Vitabu vingi vimechomwa na watu ambao hawakuwahi kuvisoma, lakini walioathiriwa na upotoshaji. Ndivyo ilivyokuwa wakati wa Zama za Giza kuhusiana na wafuasi wa Yesu, walioshambuliwa. Ndio, Yesu Mwenyewe aliteseka mikononi mwa wale ambao hawakumuelewa Yeye au mafundisho Yake, kama vile Mtakatifu Petro anavyotamka waziwazi: "*Na sasa, ndugu zangu, najua ya kuwa mlifanya kitendo hicho kwa kutokujua, kama walivyofanya watawala wenu*" *(Matendo 3:17); "kwani kama wangalijua, wasingalimsulubisha Bwana wa Utukufu." 1 Wakorintho 2:8.*

Lakini ikiwa maadui wa kitabu hiki wamekuwa wakali, wasio wa haki, na wasio wa kweli, marafiki zake wamekuwa na upendo na bidii kwa kiwango sawa. Mamilioni ya nakala mikononi mwa watu zimetolewa karibu zote kupitia marafiki wa kitabu, ambao, kwa upendo wa Kweli, wametoa muda na nguvu zao kwa ajili ya usambazaji wake mpana. Tunapoandika mistari hii, tunajua ukweli kwamba takriban Wakristo mia sita kutoka nyanja mbalimbali za maisha wame "acha yote"—biashara za kidunia, wito, na matamanio—ili wamtukuze Bwana na kuwabariki watakatifu Wake wenye njaa kwa kuwawekea Kitabu hiki kidogo mikononi mwao. Hawa ni pamoja na madaktari, walimu wa shule, wauguzi, wachungaji, vinyozi, mafundi—watu kutoka kila nyanja ya maisha ambao, wakiwa wameguswa mioyoni mwao na upendo wa Mungu, wana hamu ya kueneza baraka kwa mioyo na akili zingine.

Vitabu hivi vinauzwa kwa bei ndogo, na hawa wauza vitabu wanaovisambaza kwa umma wanaweza tu kujikimu gharama zao. Hata hivyo, wanashangilia zaidi ikiwa wakati mwingine wanapata matatizo na kuhesabiwa kuwa wanastahili kuteseka usumbufu na mahitaji kwa ajili ya Bwana, Kweli, na Ndugu. Kazi njema inaendelea, Ujumbe wa Uzima katika Kristo unapita kutoka mkono mmoja hadi mwingine. Uzalishaji wa sasa wa Kitabu hiki ni mkubwa sana. Na baraka zake katika siku zijazo ziwe kubwa sawia na zile za zamani. Mwandishi na wachapishaji hawawezi kuomba zaidi.

Nikiwatakia kila la kheri wasomaji wote,

Mtumishi wenu katika Bwana,

**Charles T. Russell**

Brooklyn, N.Y., Oktoba 1, 1916

# YALIYOMO


## SOMO LA I

## USIKU WA DHAMBI WA DUNIA KUKOMA KATIKA ASUBUHI YA FURAHA

SIKU WA VILIO NA ASUBUHI YA FURAHA — NJIA MBILI ZA KUTAFUTA KWELI — NJIA ILIYOFUATWA HAPA — UPEO WA KAZI HII — TOFAUTI KATI YA UCHUNGUZI WA MAKINI WA MAANDIKO NA TABIA YA HATARI YA KUKISIA— LENGO LA UNABII — HALI YA KIDINI YA SASA YA ULIMWENGU IKITAZAMWA KUTOKA MITAZAMO MIWILI — GIZA LA MISRI — UPINDE WA AHADI — NJIA YA WENYE HAKI INASONGA MBELE — CHANZO CHA UKENGEUFU MKUU — MATENGENEZO — SABABU ILE ILE TENA INAZUIA MAENDELEO YA KWELI — UKAMILIFU WA MAARIFA SI JAMBO LA WAKATI ULIOPITA, BALI LA WAKATI UJAO. ..............................1

## SOMO LA 2

## UWEPO WA MUUMBA MWENYE AKILI WATHIBITISHWA

USHAHIDI NJE YA BIBLIA, UKICHUNGUZWA KWA NURU YA AKILI— NADHARIA ISIYOWEZA KUTETEWA—NADHARIA YENYE MASHIKO—TABIA YA MUNGU YADHIHIRISHWA—HITIMISHO ZA KIMANTIKI ...........21

## SOMO LA III

## BIBLIA KAMA UFUNUO WA KIMUNGU IKITAZAMWA KATIKA NURU YA MANTIKI

MADAI YA BIBLIA NA USHAHIDI WAKE WA AWALI WA KUAMINIKA — UKALE WAKE NA KUHIFADHIWA KWAKE — USHAWISHI WAKE WA KIADILI — MALENGO YA WAANDISHI — SIFA ZA JUMLA ZA MAANDIKO HAYO — VITABU VYA MUSA — SHERIA YA MUSA — UPEKEE WA SERIKALI ILIYOSIMIKWA NA MUSA — HAIKUWA MFUMO WA UTAWALA WA MAKUHANI — MAAGIZO KWA WATAWALA WA KIRAIA — TAJIRI NA MASKINI KATIKA DARAJA MOJA MBELE YA SHERIA — KINGA DHIDI YA KUINGILIA HAKI ZA WATU — UKUHANI SIO TABAKA LINALOPENDELEWA, JINSI WALIVYOTUNZWA, NK. — UONEVU DHIDI YA WAGENI, WAJANE, YATIMA NA WATUMISHI ULIZUIWA — MANABII WA BIBLIA — JE, KUNA KIUNGO CHA PAMOJA CHA UMOJA KATI YA SHERIA, MANABII NA WAANDISHI WA AGANO JIPYA? — MIUJIZA SI JAMBO LISILO NA MANTIKI — HITIMISHO LA KIMANTIKI. ......................................................31

## SOMO LA IV

## ENZI NA VIPINDI VILIVYOAINISHWA KATIKA MAENDELEO YA MPANGO WA MUNGU

MPANGO WA MUNGU NI DHAHIRI NA WENYE UTARATIBU — ENZI KUU TATU ZA HISTORIA YA ULIMWENGU — SIFA ZAKE MAHUSUSI — "DUNIA HUDUMU MILELE" — ULIMWENGU UJAO, MBINGU MPYA NA DUNIA MPYA — MIGAWANYO YA ENZI HIZI KUU — VIPENGELE MUHIMU VYA MPANGO WA MUNGU VINAVYOONEKANA HIVYO — UTARATIBU ULIOBAINIKA UNAFUNUA UWIANO — KULIGAWANYA SAWA NENO LA KWELI........ 59

## SOMO LA V

## SIRI ILIYOFICHWA KWA ZAMA NA VIZAZI, LAKINI SASA IMEDHIHIRISHWA KWA WATAKATIFU WAKE"—Kol. 1:26

NURU HAFIFU YA AHADI YA KWANZA — AHADI KWA IBRAHIMU — KUCHELEWESHWA KWA TUMAINI — SIRI INAANZA KUFUMBULIWA WAKATI WA PENTEKOSTE — SIRI HIYO NI NINI — KWA NINI IMEWEKWA KUWA SIRI KWA MUDA MREFU HIVYO — BADO NI SIRI KWA ULIMWENGU — KUDHIHIRISHWA KWA WOTE KWA WAKATI WAKE — WAKATI SIRI ITAKAPOKAMILIKA........ 71

## SOMO LA VI

## KURUDI KWA BWANA WETU—KUSUDI LAKE, KUFANYWA UPYA KWA VITU VYOTE

KURUDI KWA BWANA WETU MARA YA PILI: NI YEYE MWENYEWE NA NI KABLA YA MILENIA — UHUSIANO WAKE NA KUJA KWAKE MARA YA KWANZA — UCHAGUZI WA KANISA NA KUONGOLEWA KWA ULIMWENGU — UCHAGUZI NA NEEMA — WAFUNGWA WA TUMAINI — USHUHUDA WA KIUNABII KUHUSIANA NA KUFANYWA UPYA — KURUDI KWA BWANA WETU: TUMAINI DHAHIRI LA KANISA NA ULIMWENGU. . 83

## SOMO LA VII

## KURUHUSIWA KWA UOVU NA UHUSIANO WAKE NA MPANGO WA MUNGU

KWA NINI UOVU ULIRUHUSIWA — HAKI NA UOVU KAMA KANUNI — HISIA YA MAADILI — MUNGU ALIRUHUSU UOVU, NA ATAUGEUZA ULETE WEMA — MUNGU SIYE MWANZILISHI WA DHAMBI — KUJARIBIWA KWA ADAMU HAKUKUWA MZAHA — KISHAWISHI CHAKE KILIKUWA KIKALI — ALITENDA DHAMBI KWA KUSUDI — ADHABU YA DHAMBI SIYO DHALIMU, WALA SI KALI MNO — HEKIMA, UPENDO NA HAKI

ZIKIDHIHIRISHWA KATIKA KUWAHUKUMU WOTE NDANI YA ADAMU — SHERIA YA MUNGU IMEENEA POTE.......113

## SOMO LA VIII

## SIKU YA HUKUMU

MTAZAMO WA JUMLA JUU YA SIKU YA HUKUMU — JE, NI WA KIMAANDIKO? — KUFAFANULIWA KWA MANENO: HUKUMU NA SIKU — SIKU KADHAA ZA HUKUMU ZILIZOTAJWA KATIKA MAANDIKO — SIKU YA KWANZA YA HUKUMU NA MATOKEO YAKE — SIKU NYINGINE IMEWEKWA — HAKIMU — TABIA YA HUKUMU IJAYO — KUFANANA NA KUTOFANANA KWA SIKU YA KWANZA NA YA PILI YA HUKUMU — KUWAJIBIKA KWA SASA KWA ULIMWENGU — HUKUMU MBILI ZA KATIKATI NA KUSUDI LAKE — MITAZAMO TOFAUTI SANA JUU YA HUKUMU IJAYO — JINSI MANABII NA MITUME WALIVYOITAZAMA......135

## SOMO LA IX

## FIDIA NA UREJESHO

UREJESHO ULIOHAKIKISHWA KWA FIDIA — SI UZIMA WA MILELE, BALI KUJARIBIWA KWA AJILI YAKE, KULIKOPATIKANA KWA FIDIA — MASHARTI NA MANUFAA YA KUJARIBIWA HUKO — DHABIHU YA KRISTO ILIKUWA YA LAZIMA — JINSI JAMII ILIVYOWEZA NA ILIVYOKOMBOLEWA KWA KIFO CHA MMOJA — IMANI NA MATENDO BADO NI VYA LAZIMA — MSHAHARA WA DHAMBI YA MAKUSUDI NI HAKIKA — JE, KUTAKUWA NA NAFASI DUNIANI KWA AJILI YA MAMILIONI WATAKAOFUFULIWA? — UREJESHO DHIDI YA MAGEUZI.......147

## SOMO LA X

## ASILI ZA KIROHO NA ZA KIBINADAMU ZIMETENGANISHWA NA NI TOFAUTI

DHANA POTOFU ZA KAWAIDA—ASILI ZA KIDUNIA AU KIBINADAMU NA ZA MBINGUNI AU KIROHO—UTUKUFU WA KIDUNIA NA UTUKUFU WA MBINGUNI—USHUHUDA WA BIBLIA KUHUSU VIUMBE WA ROHO—HALI YA KUFA NA HALI YA KUTOKUFA—JE, VIUMBE WENYE HALI YA KUFA WANAWEZA KUWA NA UZIMA WA MILELE?—HAKI KATIKA UTOAJI WA HISANI—KANUNI INAYODHANIWA YACHUNGUZWA—AINA MBALIMBALI KATIKA UKAMILIFU—HAKI ZA ENZI KUU YA MUNGU—MAANDALIZI YA MUNGU KWA MWANADAMU NI FUNGU LA KURIDHISHA—UCHAGUZI WA MWILI WA KRISTO—JINSI MABADILIKO YA ASILI YAO YANAVYOFANYIKA.......173

## SOMO LA XI

## NJIA TATU—NJIA PANA, NJIA NYEMBAMBA, NJIA KUU

NJIA PANA IENDAYO UPOTEVUNI—NJIA NYEMBAMBA IENDAYO UZIMANI—UZIMA NI NINI?—ASILI YA UUNGU—UHUSIANO WA ASILI YA UUNGU NA YA KIBINADAMU—THAWABU MWISHONI MWA NJIA NYEMBAMBA—WITO MKUU UMEWEKEWA MPAKA KATIKA ZAMA YA INJILI—MAGUMU NA HATARI ZA NJIA NYEMBAMBA—NJIA KUU YA UTAKATIFU ........ 207

## SOMO LA XII

## UFAFANUZI WA CHATI INAYOWAKILISHA MPANGO WA ZAMA

ZAMA—MAVUNO—NGAZI ZA NAFASI HALISI NA YA KUHESABIWA—SAFARI YA BWANA WETU YESU—SAFARI YA WAFUASI WAKE—MAKUNDI MATATU KATIKA KANISA LA JINA—UTENGANISHO KATIKA MAVUNO—KUNDI LA WATIWA-MAFUTA LIKIWA LIMETUKUZWA—KUNDI LA DHIKI KUU—MAGUGU YANACHOMWA—ULIMWENGU UNABARIKIWA—MATOKEO MATUKUFU........ 223

## SOMO LA XIII

## FALME ZA ULIMWENGU HUU

MAMLAKA YA KWANZA—KUPOTEZWA KWAKE—KUKOMBOLEWA NA KUREJESHWA KWAKE—UFALME WA MUNGU ULIO MFANO—MNYANG'ANYI—SURA MBILI ZA MAMLAKA YA SASA—MAMLAKA ZILIZOPO, ZIMEAMRIWA NA MUNGU—MTAZAMO WA NEBUKADNEZA KUZIHUSU—MTAZAMO WA DANIELI NA TAFSIRI YAKE—FALME ZA ULIMWENGU HUU ZIKITAZAMWA KUTOKA MTAZAMO MWINGINE—UHUSIANO SAHIHI WA KANISA NA SERIKALI ZA SASA—HAKI YA KIMUNGU YA WAFALME IKICHUNGUZWA KWA UFUPI—MADAI YA UKRISTO WA JINA NI YA UONGO—TUMAINI BORA KATIKA UFALME WA TANO WA ULIMWENGU........ 251

## SOMO LA XIV

## UFALME WA MUNGU

UMUHIMU WA SOMO HILI—TABIA YA UFALME—UFALME WAKATI WA ZAMA YA INJILI—MITAZAMO YA UONGO IKISAHIHISHWA NA PAULO—MATOKEO YA MAWAZO YA UONGO JUU YA UFALME—SURA MBILI ZA UFALME WA MUNGU—SURA YA KIROHO NA KAZI YAKE—SURA YA KIDUNIA NA KAZI YAKE—UTENDAJI WAO WA PAMOJA KWA UWIANO—UTUKUFU WA SURA YA KIDUNIA—UTUKUFU WA SURA YA MBINGUNI—MZIZI WA AGANO AMBAKO MATAWI HAYA HUOTEA—SURA YA KIDUNIA YA UFALME, YA KIISRAELI—MAKABILA YALIYOPOTEA—YERUSALEMU WA MBINGUNI—ISRAELI WATU WA MFANO—KUPOTEZWA NA KUREJESHWA KWA ISRAELI—MADARAJA YA WATEULE—WARITHI WA UFALME—UTAWALA WA CHUMA—KIELELEZO CHA LENGO LA UTAWALA WA MIAKA ELFU—UFALME UKIKABIDHIWA KWA BABA—KUSUDI LA ASILI LA MUNGU LIKIKAMILISHWA KIKAMILIFU. ........ 281

## SOMO LA XV

## SIKU YA YEHOVA

"SIKU YA YEHOVA," "SIKU YA KISASI," "SIKU YA GHADHABU"—WAKATI WA TAABU KUU—CHANZO CHAKE—USHUHUDA WA BIBLIA KUIHUSU—MOTO NA DHORUBA YAKE, KUTETEMESHWA NA KUYEYUSHWA KWAKE, VINAONYESHWA KUWA NI VYA MFANO—USHUHUDA WA DAUDI—USHUHUDA WA MWANDISHI WA UFUNUO—HALI YA SASA NA MTAZAMO WA BAADAYE KAMA UNAVYOTAZAMWA NA PANDE ZINAZOPINGANA, WENYE MITAJI NA WAFANYAKAZI WA UJIRA—SULUHISHO AMBALO HALITAFANIKIWA—PAZIA LIMEINULIWA NA NURU KUINGIZWA SAWASAWA NA WAKATI ULIOWEKWA—UTHIBITISHO WA HILI—HALI YA WATAKATIFU WAKATI WA TAABU, NA MTAZAMO WAO SAHIHI KUELEKEA HIYO. ....... 317

## SOMO LA XVI

## MAWAZO YA HITIMISHO

WAJIBU WETU KWA ILE KWELI—GHARAMA YAKE, THAMANI YAKE, NA FAIDA YAKE ....... 353

## SOMO LA I

# USIKU WA DHAMBI WA DUNIA KUKOMA KATIKA ASUBUHI YA FURAHA

SIKU WA VILIO NA ASUBUHI YA FURAHA — NJIA MBILI ZA KUTAFUTA KWELI — NJIA ILIYOFUATWA HAPA — UPEO WA KAZI HII — TOFAUTI KATI YA UCHUNGUZI WA MAKINI WA MAANDIKO NA TABIA YA HATARI YA KUKISIA — LENGO LA UNABII — HALI YA KIDINI YA SASA YA ULIMWENGU IKITAZAMWA KUTOKA MITAZAMO MIWILI — GIZA LA MISRI — UPINDE WA AHADI — NJIA YA WENYE HAKI INASONGA MBELE — CHANZO CHA UKENGEUFU MKUU — MATENGENEZO — SABABU ILE ILE TENA INAZUIA MAENDELEO YA KWELI — UKAMILIFU WA MAARIFA SI JAMBO LA WAKATI ULIOPITA, BALI LA WAKATI UJAO.

JINA la mfululizo huu wa Mafunzo—**"MPANGO WA KIMUNGU WA ZAMA,"**—linadokeza kuwepo kwa mwendelezo wenye utaratibu katika mpango mtakatifu, ambao Mungu wetu aliujua tangu awali. Tunaamini kwamba mafundisho ya ufunuo wa Mungu yanaweza kuonekana kuwa maridadi na yenye uwiano kamili kwa kutumia mtazamo huu, na si kwa mtazamo mwingine wowote. Kipindi ambacho dhambi imeruhusiwa kimekuwa kama usiku wa giza kwa wanadamu, usiku ambao hautasahaulika kamwe; lakini ile siku tukufu ya haki na upendeleo wa Mungu, itakayoletwa na Masihi, itakuwa fidia iliyo bora zaidi. Yeye, akiwa Jua la Haki, atachomoza na kuangaza kikamilifu juu ya wote, akileta uponyaji na baraka, na kuzidi urefu wa usiku wa kutisha wa kilio, kuugua, maumivu, magonjwa na Mauti, ambamo viumbe vyote vimekaa vikiteseka kwa muda mrefu. *"…….Huenda kilio huja kukaa usiku, Lakini asubuhi huwa furaha." Zab. 30:5*

Kama kwa silika, viumbe vyote, huku vikiugua na kuwa katika uchungu, vinaingojea, vinaitamani, na vinaitumainia SIKU ile, vikiita **Zama za Dhahabu;** lakini wanadamu wanapapasa gizani, kwa sababu hawayatambui makusudi makuu ya neema ya Yehova. Hata hivyo, mawazo yao makuu zaidi kuhusu zama hizo hayafikii hata kidogo jinsi hali halisi itakavyokuwa. Muumba mkuu anaandaa **"karamu ya vitu vinono**,"

itakayowashangaza viumbe vyake, na itakuwa zaidi ya yote wangeweza kuomba au kutarajia. Na kwa viumbe vyake vina-vyostaajabu, wanapotazama upana na urefu, kimo na kina cha upendo wa Mungu unaopita matarajio yote, yeye anaeleza: *"Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA; kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu." Isa. 55:8,9*

Ingawa katika kazi hii tutajitahidi, na tunaamini tutafanikiwa, kuweka wazi mbele ya msomaji mwenye nia na asiye na upen-deleo mpango wa Mungu unaohusu na unaoeleza matendo yake ya zamani, ya sasa, na ya wakati ujao, kwa njia yenye uwiano, uzuri na mantiki zaidi ya jinsi inavyoeleweka na wengi, lakini, tunakanusha katakata kwamba mafanikio haya ni matokeo ya hekima au uwezo wa kipekee wa mwandishi. Ni nuru kutoka kwa Jua la Haki katika mapambazuko haya ya Siku ya Milenia ndiyo inayofunua mambo haya kama **"kweli ya wakati huu,"** ambayo sasa imewadia kueleweka na kuthaminiwa na wale wanyofu—walio wasafi wa moyo.

Kwa kuwa hali ya mashaka imeenea sana, msingi wenyewe wa dini ya kweli, na msingi wa ukweli, unahojiwa mara nyingi, hata na watu wanyofu. Tumejitahidi kufunua sehemu ya kutosha ya ule msingi ambao juu yake imani yote inapaswa kujengwa—yaani, Neno la Mungu—ili kutoa uhakika na usalama katika ushuhuda wake, hata kwa mtu asiyeamini. Na tumejitahidi kufanya hivi kwa namna itakayovutia na kukubalika na akili kama msingi.

Kisha, tumejitahidi kujenga juu ya msingi huo mafundisho ya Maandiko, kwa namna ambayo, kwa kadiri iwezekanavyo, hukumu ya kibinadamu pekee iweze kupima mantiki na usahihi wake kwa kutumia kanuni kali zaidi za haki inazoweza kutumia.

Tukiwa tunaamini kwamba Maandiko yanafunua mpango wenye mantiki na uwiano, ambao, unapoeleweka, ni lazima

ukubalike kwa kila dhamiri iliyotakaswa, kazi hii inachapishwa kwa matumaini ya kuwasaidia wanafunzi wa Neno la Mungu, kwa kupendekeza njia za fikra zinazopatana zenyewe kwa zenyewe na pia na Neno lililoongozwa na Mungu. Wale wanaotambua Biblia **kuwa ni ufunuo wa mpango wa Mungu**—na ndio tunaowalenga hasa—bila shaka watakubali kwamba, ikiwa imeongozwa na Mungu, mafundisho yake, yatakapochukuliwa kwa ujumla wake, ni lazima yafunue mpango unaopatana na wenye mantiki ndani yake, na unaopatana pia na tabia ya Mwandishi wake yaani Mungu. Lengo letu kama watafuta-kweli linapaswa kuwa ni kuupata mpango kamili wa Mungu uliofunuliwa, ukiwa umekamilika na wenye uwiano; na hili, tukiwa watoto wa Mungu, tuna sababu ya kulitarajia, kwa kuwa imeahidiwa kwamba roho wa kweli atatuongoza kwenye kweli yote. *Yohana 16:13*

Kama watafutaji , tuna njia mbili zilizo wazi mbele yetu. Njia ya kwanza ni kutafuta miongoni mwa maoni yote yanayotolewa na madhehebu mbalimbali ya kanisa, na kuchukua kutoka kila moja kile kipengele tunachoweza kufikiri ni kweli hii itakuwa kazi isiyo na mwisho. Ugumu ambao tungekutana nao kwa njia hii ni kwamba, ikiwa hukumu yetu imepinda na kupotoka, au mapendeleo yetu yameegemea upande wowote—na ni nani asiye na hali hiyo?—ugumu huu ungetuzuia kufanya uchaguzi sahihi, na tungeweza kuchagua uongo na kuikataa Kweli. Tena, kama tungechagua hii kuwa njia yetu, tungepoteza mengi, kwa sababu kweli inaendelea kung'aa, ikizidi kuongezeka mpaka mchana mkamilifu, kwa wale wanaoifuata na kutembea katika nuru yake; wakati ambapo kanuni za imani za madhehebu mbalimbali zimesimama na hazibadiliki, na ziliwekwa hivyo karne nyingi zilizopita. Na ni lazima kila moja iwe na sehemu kubwa ya makosa, kwa kuwa kila moja inapingana na nyingine katika mambo muhimu. Njia hii ingeongoza katika mkanganyiko wa mashaka na kutokueleweka.

Njia ya pili ni kuondoa kabisa hisia zote za upendeleo akilini mwetu, na kukumbuka kwamba hakuna anayeweza kujua zaidi kuhusu mipango ya Mungu kuliko vile alivyofunua katika Neno lake, na kwamba Neno hilo lilitolewa kwa ajili ya watu wanyenyekevu na wapole wa moyo; na, tukiwa hivyo, tukitafuta kwa bidii na uaminifu mwongozo na mafundisho yake pekee, tutaongozwa na Mwandishi wake mkuu kulielewa, kadiri inavyopasa lieleweke, kwa kutumia misaada mbalimbali iliyoandaliwa na Mungu. *Tazama Waefeso 4:11-16.*

Kazi hii imeandaliwa mahususi kama msaada kwa kundi hili la wanafunzi. Ijulikane kwamba rejea zake zote ni za Maandiko pekee, isipokuwa pale ambapo historia ya kidunia inaweza kutumika kuthibitisha utimilifu wa kauli za Maandiko. Ushuhuda wa wanatheolojia wa kisasa haujapewa uzito wowote, na ule wa wale waitwao Mababa wa Kanisa wa Kwanza haujazingatiwa. Wengi wao wameshuhudia kwa kupatana na fikra zilizoelezwa humu, lakini tunaamini kwamba ni udhaifu wa kawaida wa sasa na wa nyakati zote kwa watu kuamini mafundisho fulani kwa sababu wengine waliyaamini, watu ambao waliwaamini. Ni wazi kwamba hiki ni chanzo kikuu cha makosa, kwa kuwa watu wengi wema wameamini na kufundisha makosa wakiwa na dhamiri safi kabisa. (*Matendo 26:9*) Watafuta-kweli wanapaswa kumwaga kutoka kwenye vyombo vyao maji machafu ya mapokeo na kuvijaza kwenye chemchemi ya kweli—Neno la Mungu. Na hakuna fundisho lolote la kidini linalopaswa kuwa na uzito isipokuwa kama linamwongoza mtafuta-kweli kwenye chemchemi hiyo.

Hata kwa ajili ya uchunguzi wa jumla na wa harakaharaka wa Biblia nzima na mafundisho yake, kitabu hiki ni kidogo sana; lakini, kwa kutambua haraka ya siku zetu, tumejitahidi kufupisha maelezo kwa kadiri umuhimu wa masomo haya ulivyoruhusu.

Kwa mwanafunzi mwenye nia, tungependa kumweleza kwamba haitamfaa kitu kupitia kitabu hiki juu juu tu na

kutegemea kupata nguvu na uwiano wa mpango unaopendekezwa, pamoja na uthibitisho wa Kimaandiko uliowasilishwa humu. Tumejitahidi kote kuwasilisha chembechembe mbalimbali za kweli, si tu kwa lugha inayofaa, bali pia kwa mpangilio ambao utawawezesha wasomaji wa aina zote kuielewa mada na mpango mkuu kwa uwazi. Ingawa funzo la kina na lenye utaratibu ni la lazima ili kuthamini sayansi yoyote, ni muhimu hasa katika sayansi ya ufunuo wa Mungu. Na katika kazi hii jambo hilo ni la lazima mara mbili, kutokana na ukweli kwamba mbali na kuwa ni andiko la Kweli zilizofunuliwa na Mungu, pia ni uchunguzi wa somo hili kutoka katika mtazamo tofauti kabis, kwa kadiri tunavyojua, na ule wa kazi nyingine yoyote. Hatuna haja ya kuomba msamaha kwa kujadili mada nyingi ambazo kwa kawaida hupuuzwa na Wakristo—miongoni mwa hizo, ni kuja kwa Bwana wetu, na unabii na ishara za Agano la Kale na Jipya.

Hakuna mfumo wowote wa theolojia unaopaswa kuwasilishwa, au kukubaliwa, unaopuuza au kuacha sehemu muhimu zaidi za mafundisho ya Maandiko. Hata hivyo, tunaamini kwamba utofauti mkubwa utatambuliwa kati ya funzo la dhati, la makini na la heshima la unabii na maandiko mengine, katika nuru ya matukio ya kihistoria yaliyotimia, ili kupata hitimisho ambalo akili ya kawaida iliyotakaswa inaweza kulikubali, na ile tabia ya kawaida ya kufanya dhana za jumla, ambazo, zinapotumiwa kwenye unabii wa Mungu, huelekea kutoa nafasi kwa nadharia zisizo na msingi na mawazo yasiyoeleweka. **Wale wanaoangukia katika tabia hii hatari mara nyingi hugeuka kuwa manabii (?) badala ya kuwa wanafunzi wa unabii.**

Hakuna kazi iliyo adhimu na yenye heshima kuliko kusoma kwa uchaji makusudi ya Mungu yaliyofunuliwa—*"…Mambo hayo malaika wanatamani kuyachungulia."* (*1 Petro 1:12*) Ukweli kwamba hekima ya Mungu ilitoa unabii wa mambo ya wakati ujao, pamoja na maelezo kuhusu wakati wa sasa na uliopita, peke yake ni karipio la Yehova dhidi ya upumbavu wa baadhi ya watoto wake, ambao wametoa udhuru wa ujinga wao na kule kupuuza

kujifunza Neno lake kwa kusema: "*Kuna mambo ya kutosha katika sura ya tano ya Mathayo kumwokoa mtu yeyote*." Wala hatupaswi kudhani kwamba unabii ulitolewa ili tu kutosheleza udadisi kuhusu wakati ujao. Ni wazi kwamba lengo lake ni kumfanya mtoto wa Mungu aliyejiweka wakfu ajue mipango ya Baba yake, na hivyo kuamsha shauku na huruma yake katika mipango hiyo hiyo, na kumwezesha kuutazama wakati wa sasa na ujao kwa mtazamo wa Mungu. Anapokuwa na shauku hivyo katika kazi ya Bwana, anaweza kutumika kwa roho na kwa akili pia; si kama mtumishi tu, bali kama mtoto na mrithi. Kuwaonyesha watu kama hawa mambo yajayo, kunapinga nguvu ya mambo ya sasa. Matokeo ya kujifunza kwa umakini hayawezi kuwa tofauti isipokuwa kuimarisha imani na kuchochea utakatifu.

Kwa kutojua mpango wa Mungu wa kuukomboa ulimwengu **kutoka katika dhambi** na matokeo yake, na chini ya wazo potofu kwamba kanisa la jina tu, katika hali yake ya sasa, ndilo chombo pekee cha kutimiza hilo, hali ya ulimwengu leo, baada ya Injili kuhubiriwa kwa karibu karne kumi na tisa, ni ya namna ya kuamsha mashaka mazito katika kila akili inayotafakari ambayo imepotoshwa kiasi hicho. Na mashaka kama hayo hayawezi kuondolewa kwa urahisi na kitu kingine chochote isipokuwa **kweli**. Kwa hakika, kwa kila mwangalizi mwenye kufikiri, moja kati ya mambo mawili ni lazima liwe wazi: ama kanisa limefanya kosa kubwa kwa kudhani kwamba katika zama hizi, na katika hali yake ya sasa, jukumu lake limekuwa ni kuugeuza ulimwengu, au mpango wa Mungu umeshindwa vibaya sana. Je, tukubali upande upi wa mkanganyiko huu? Wengi wamekubali, na bila shaka wengi zaidi watakubali, upande wa pili, na kuongeza idadi ya wasioamini, iwe kwa siri au kwa wazi. Kuwasaidia wale wanaoanguka hivyo kwa unyoofu, ni moja ya malengo ya kitabu hiki.

Kwenye ukurasa wa kumi na sita tunawasilisha mchoro, uliochapishwa na "Shirika la Kimisionari la London," na baadaye nchini Marekani na "Bodi ya Misheni ya Wanawake

Wapresbiteri." Unaitwa "Ombi la Kimya kwa Niaba ya Misheni za Kigeni." Unaeleza hadithi ya kuhuzunisha ya giza na ujinga kuhusu jina pekee lililotolewa chini ya mbingu, au kati ya wanadamu, ambalo kwa hilo twapasa kuokolewa.

Jarida la The Watchman—jarida la "Y.M.C.A." la Chicago—lilichapisha mchoro huu huu, na likitoa maoni juu yake likisema:

> *"Mawazo ya watu wengine hayako wazi na hayaeleweki vizuri kuhusu hali ya kiroho ya ulimwengu. Tunasikia kuhusu kazi tukufu za uamsho nyumbani na nchi za nje, kuhusu juhudi mpya za kimisionari katika pande mbalimbali, kuhusu nchi moja baada ya nyingine ikifunguliwa kwa ajili ya injili, na kuhusu kiasi kikubwa cha fedha kinachotolewa kwa ajili ya kuieneza: na tunapata wazo kwamba juhudi za kutosha zinafanywa kwa ajili ya uinjilishaji wa mataifa ya dunia. Inakadiriwa leo kwamba idadi ya watu duniani ni 1,424,000,000, na kwa kuuchunguza mchoro tutaona kwamba zaidi ya nusu – karibu theluthi mbili – bado ni wapagani kabisa, na waliosalia wengi wao ni ama wafuasi wa Muhammad au washiriki wa yale makanisa makuu yaliyoasi ambayo dini yao kivitendo ni ibada ya sanamu iliyovikwa Ukristo, na ambao ni vigumu kusema kwamba wanashika au kufundisha injili ya Kristo.*
>
> *Hata kuhusu Waprotestanti wa jina tu milioni 116, ni lazima tukumbuke jinsi sehemu kubwa nchini Ujerumani, Uingereza na nchi hii wameangukia katika ukafiri – giza zito zaidi, kama inawezekana, hata kuliko lile la upagani – na jinsi wengi wamepofushwa na ushirikina, au wamezama katika ujinga uliokithiri; kiasi kwamba wakati ambapo Wayahudi milioni nane bado wanamkataa Yesu wa Nazareti, na wakati ambapo zaidi ya milioni 300 wanaolitumia jina lake wameiasi imani yake, wengine milioni 170 wanamwinamia Muhammad, na idadi kubwa iliyobaki ya wanadamu hadi leo ni waabudu wa magogo na mawe, wa mababu zao, wa mashujaa waliokufa au wa Ibilisi mwenyewe; wote, kwa namna moja au nyingine, wakimwabudu na kumtumikia kiumbe badala ya Muumba, aliye Mungu juu ya yote, ahimidiwe milele. Je, hakuna mambo ya kutosha hapa ya kuuhuzunisha moyo wa Mkristo mwenye kufikiri?"*

Kweli hii ni picha ya kuhuzunisha. Na ingawa mchoro unaonyesha viwango vya tofauti kati ya Wapagani, Waislamu na Wayahudi, wote wako sawa katika hali ya kutomjua Kristo kabisa.

Huenda wengine mwanzoni wakadhani kwamba maoni haya kuhusu idadi ya Wakristo ni ya giza sana na yametiwa chumvi, lakini sisi tunafikiri kinyume chake. Inauonyesha Ukristo wa jina tu katika rangi angavu zaidi iwezekanavyo.

Kwa mfano, idadi ya milioni 116,000,000 iliyoandikwa kama Waprotestanti inazidi sana idadi ya kweli. Tunaamini, milioni



kumi na sita ingeikaribia zaidi idadi halisi ya washiriki wa kanisa wanaokiri imani wenye umri wa utu uzima, na tuna hofu, milioni moja yangekuwa ni makadirio yaliyozidishwa sana kwa ajili ya “kundi dogo,” wale “waliotakaswa katika Kristo Yesu,” ambao “hawaendi kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho.” Ikumbukwe kwamba sehemu kubwa ya washiriki wa kanisa, ambao daima huhesabiwa katika takwimu, ni watoto wadogo na wachanga. Hali hii ni ya kawaida hasa katika nchi za Ulaya. Katika nchi nyingi kati ya hizi, watoto huhesabiwa kuwa washiriki wa kanisa tangu utotoni mwao.

Lakini ingawa picha hii inaonekana kuwa ya giza, si picha ya giza zaidi ambayo wanadamu walioanguka wanaiwakilisha. Mchoro uliotajwa hapo juu unawakilisha tu vizazi vya sasa vilivyo hai. Tunapofikiria ukweli kwamba karne baada ya karne kwa miaka elfu sita iliyopita zimepoteza umati mwingine mkubwa wa watu, ambao karibu wote walikuwa wamegubikwa na ujinga na dhambi ileile, mandhari hii ni ya giza mno! Ikitazamwa kwa mtazamo unaokubalika na wengi, kwa kweli ni picha ya kutisha.

Imani mbalimbali za leo zinafundisha kwamba mabilioni haya yote ya wanadamu, wakiwa hawalijui lile Jina pekee chini ya mbingu litupasalo kuokolewa kwalo, wapo katika njia ya moja kwa moja ielekeayo kwenye mateso ya milele; na si hivyo tu, bali hata wale Waprotestanti milioni 116,000,000, isipokuwa watakatifu wachache sana, nao wana hakika ya kupata hatima hiyohiyo. Basi, haishangazi kwamba wale wanaoamini mambo ya kutisha kama hayo kuhusu mipango na makusudi ya Yehova wanakuwa na bidii katika kuendeleza shughuli za kimisionari—la kushangaza ni kwamba hawachanganyikiwi kabisa na jambo

hilo. Hakika kuamini hivu, na kutambua uzito wa hitimisho kama hilo, kungeondolea maisha kila furaha, na kugubika kwa giza kila mandhari nzuri ya uumbaji.

Ili kuonyesha kwamba hatujapotosha maoni ya "Imani Rasmi ya Wengi (orthodoxy)" juu ya somo la hatima ya wapagani, tunanukuu kutoka kwenye kijitabu—"**Ombi la Kimya kwa Niaba ya Misheni za Kigeni**"—ambamo mchoro huo ulichapishwa. Sentensi yake ya kumalizia inasema:

> *"Wainjilisheni vizazi vyenye nguvu vya nchi za nje—nafsi bilioni moja wanaokufa katika hali ya kukata tamaa bila Kristo kwa kiwango cha watu 100,000 kwa siku."*

Lakini ingawa huu ni mtazamo wa kuhuzunisha kutoka kwa maoni ya mafundisho ya wanadamu, Maandiko yanawasilisha mtazamo angavu zaidi, ambao ndio lengo la kurasa hizi kuuonyesha. Tukiongozwa na Neno, hatuwezi kuamini kwamba mpango mkuu wa Mungu wa wokovu uliwahi kukusudiwa kuwa, au utawahi kuwa, wenye kushindwa vibaya kiasi hicho. Itakuwa ni faraja kwa mtoto wa Mungu aliyetatanishwa kutambua kwamba Nabii Isaya alitabiri hali hii hii ya mambo, na tiba yake, akisema:

> *"Maana, tazama, giza litaifunika dunia, Na giza kuu litazifunika kabila za watu; Bali Bwana atakuzukia wewe, Na utukufu wake utaonekana juu yako. Na mataifa [Wapagani] wataijilia nuru yako, Na wafalme kuujia mwanga wa kuzuka kwako.." (Isa. 60:2,3)*

Katika unabii huu, lile giza nene linaangaziwa na upinde wa ahadi: "Mataifa [mataifa ya dunia kwa ujumla] wataijilia nuru yako."

Si tu kwamba mateso na giza vinavyoendelea ulimwenguni, na maendeleo ya polepole ya kweli, vimekuwa fumbo kwa Kanisa, bali ulimwengu wenyewe umejua na kuihisi hali yake. Kama lile lililoizingira Misri, limekuwa ni giza ambalo unaweza kulihisi. Kama uthibitisho wa hili, zingatia roho ya mistari ifuatayo, iliyochukuliwa kutoka kwenye jarida la Philadelphia. Mashaka na

giza, vilivyozidishwa na mafundisho yanayopingana ya madhehebu mbalimbali, vilikuwa bado havijaondolewa akilini mwa mwandishi kwa ile miale ya kweli ya Mungu itokayo moja kwa moja katika Neno la Mungu.

"*Uhai! fumbo kuu! Nani awezaye kusema Mungu ana haja gani na udongo huu duni? Uliofinyangwa na mkono wake kwa ustadi mkuu – Akili, mwili, nafsi na utashi mgumu; Kuzaliwa ili kufa tu: hatima ya hakika – mauti. Kisha wapi, oo! wapi pumzi hii ipitayo? Hata mmoja katika ule umati usiohesabika,*

*Walioishi na kufa na kuteseka kwa muda mrefu, Hajarejea kueleza ule mchoro mkuu – Hiyo hatima, ambayo ni yako na yangu. Tunasihi, Ee Mungu! tupate mwanzi mpya Wa nuru ya kutuongoza njiani mwetu; Isiyo na msingi wa imani tu, bali kuona dhahiri, Ikifukuza haya mawingu meusi ya usiku; Mashaka haya, hofu hii, woga huu wa kutetemeka; Wazo hili linaloharibu baraka zetu hapa. Akili hii isiyotulia, kwa msukumo wa ujasiri, Yakataa itikadi za siku za leo Zifundishwazo na madhehebu na shule zinazopingana, Ili kufunga akili kwa sheria zao. Twatafuta kukujua Wewe kama ulivyo – Nafasi yetu na Wewe – na kisha ile sehemu Tunayotenda katika huu mpango wa ajabu, Muumba Asiye na Mwisho, na mwanadamu. Inua pazia hili linalozіba kuona; Amuru tena: 'Na iwe nuru!' Funua siri hii ya kiti chako cha enzi; Twatafuta gizani kisichojulikana.*"

*Kwa hili tunajibu: Fumbo la uhai lililofunguliwa hivi karibuni litasema Ni furaha gani Mungu aliyonayo katika udongo huu duni, Uliofinyangwa na mkono wake kwa ustadi mkuu, Uliopigwa chapa ya mfano wake – akili na utashi; Kuzaliwa si ili kufa – la, uzawa wa pili Hufuata baada ya hukumu ile – "udongo kwa udongo." Maana Mmoja kati ya jeshi lile kuu, Aliyeishi na kufa na kuteseka kuliko wote, Alifufuka, na kuthibitisha mchoro mkuu wa Mungu – Hiyo hatima, basi, ni yako na yangu. Neno Lake linafunua mwanzi huu mpya Wa nuru, kwa mwongozo njiani mwetu; Uliojengwa sasa juu ya imani, lakini hakika kama kuona, Ikifukuza haya mawingu meusi ya usiku: Yale mashaka, ile hofu, ule woga wa kutetemeka, Mawazo yale yaliyoharibu baraka zetu hapa.*

*Sasa, Bwana, akili hizi, ambazo kwa msukumo wa ujasiri Zakataa itikadi za siku za leo, Zifundishwazo na madhehebu na shule zinazopingana, Zikifunga akili kwa sheria zao, Zinaweza kutafuta, na kukujua Wewe kama ulivyo, Nafasi yetu na Wewe, na kisha ile sehemu Tunayotenda katika huu mpango wa ajabu, Muumba Asiye na Mwisho, na mwanadamu. Huinua pazia, na kufunua kabisa Kwa wale wanaotembea katika nuru ya mbingu Lile fumbo tukufu la kiti chake cha enzi Lililofichwa tangu zama, sasa limejulikana*.

Baraka kama hiyo sasa inakuja ulimwenguni kupitia kufunuliwa kwa kusudi la Mungu na kufunguliwa kwa Neno la Mungu, ambapo tunaamini kitabu hiki ni sehemu ya baraka na ufunuo huo.

Wale watakaoacha dhana tupu za wanadamu, na kutumia muda kulichunguza Neno la Mungu, bila kuiondoa akili, ambayo Mungu anatualika tuitumie (*Isa. 1:18*), watagundua kwamba upinde wenye baraka wa ahadi umezingira mbingu. Ni kosa kudhani kwamba wale wasio na imani, na hivyo hawajahesabiwa haki, wanaweza kuielewa kweli kwa uwazi: haikuwa kwa ajili ya watu kama hao. Mtunga-zaburi anasema, *"Nuru[kweli] imemzukia mwenye haki..."* (*Zab. 97:11*) Kwa ajili ya mtoto wa Mungu, taa imeandaliwa ambayo mwanga wake huondoa giza jingi kutoka kwenye njia yake. *"Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu."* (*Zab. 119:105*) Lakini ni 'njia ya mwenye haki' tu ambayo *"ni kama nuru ing'aayo, Ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu."* (*Mit. 4:18*) Kwa hakika, hakuna mwenye haki, *"Hakuna mwenye haki hata mmoja"* (*Rum. 3:10*); kundi linalorejelewa ni lile la 'waliohesabiwa haki kwa imani.'

Ni fursa ya kundi hili pekee kutembea katika njia inayoendelea kung'aa zaidi na zaidi—kuona si tu ufunuo wa sasa wa mpango wa Mungu, bali pia mambo yajayo. Ingawa ni kweli kwamba njia ya kila muumini mmoja mmoja ni yenye kung'aa, matumizi maalumu ya kauli hii ni kwa wenye haki (waliohesabiwa haki)

kama kundi. Mababu, manabii, mitume na watakatifu wa zamani na wa sasa wametembea katika nuru yake inayoongezeka; na nuru itaendelea kuongezeka zaidi ya sasa—"**hata mchana mkamilifu**." Ni njia moja inayoendelea, na nuru moja inayoendelea na kuongezeka ni Andiko la Mungu, likiangaza kadiri wakati unavyowadia.

Kwa hiyo, "*Furahini katika BWANA, enyi wenye haki*," mkitarajia utimilifu wa ahadi hii. Wengi wana imani haba kiasi kwamba hawatafuti nuru zaidi, na, kwa sababu ya ukosefu wao wa uaminifu na kutojali, wanaruhusiwa kukaa gizani, wakati ambapo wangeweza kuwa wanatembea katika nuru inayoongezeka.

Roho wa Mungu, aliyetolewa kuliongoza Kanisa kwenye kweli, atachukua katika yale yaliyoandikwa na kutuonyesha sisi; lakini zaidi ya yale yaliyoandikwa hatuhitaji kitu, kwa maana Maandiko Matakatifu yanaweza kukuhekimisha hata upate wokovu, kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. *2 Tim. 3:15*

Ingawa bado ni kweli kwamba "giza linaifunika dunia, na giza nene huwafunika watu," dunia haitabaki katika hali hii milele. Tumehakikishiwa kwamba "*asubuhi inakuja*." (*Isaya 21:12*) Kama vile ambavyo sasa Mungu analifanya jua la kawaida liwaangazie wenye haki na wasio haki, vivyo hivyo Jua la Haki, katika siku ya Milenia, litaangaza kwa manufaa ya ulimwengu wote, na "*ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza*." (*1 Wakorintho 4:5*) Itaondoa mivuke yenye sumu ya uovu, na kuleta uzima, afya, amani na furaha.

Tukitazama wakati uliopita, tunaona kwamba nuru ilimulika kwa udhaifu. Ahadi za zama zilizopita zilikuwa hafifu na zisizoeleweka wazi. Ahadi alizopewa Abrahamu na wengine, ambazo ziliwakilishwa kwa namna ya mfano katika sheria na sherehe za Israeli ya kimwili, zilikuwa vivuli tu na zilitoa wazo lisilo dhahiri kuhusu makusudi ya Mungu ya ajabu na yaliyojaa neema. Tunapofikia siku za Yesu, nuru inaongezeka. Hadi wakati huo, matarajio makuu ya watu yalikuwa kwamba Mungu

angeleta mkombozi ili kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa maadui wao na kuwainua kama taifa kubwa duniani, ambapo katika nafasi hiyo ya nguvu na ushawishi, Mungu angewatumia kama chombo chake cha kubariki familia zote za dunia.

Lakini, ofa waliyopewa ya kuwa warithi katika Ufalme wa Mungu ilikuwa tofauti sana, kutokana na masharti yaliyohitajika, tofauti na walivyotarajia. Kwa mtazamo wa kibinadamu, uwezekano wa kundi lililokuwa linachaguliwa kufikia ukuu ulioahidiwa ulionekana kuwa mdogo sana, kiasi kwamba wote isipokuwa wachache walipofushwa wasiuone ujumbe huo. Na upofu na uadui wao dhidi yake uliongezeka kiasili pale ambapo, katika utaratibu wa mpango wa Mungu, wakati uliowekwa ulipowadia wa kueneza ujumbe huo, na kuufanya mwaliko wa kushiriki katika Ufalme wa ahadi umhusu kila kiumbe chini ya mbingu ambaye, kwa kudhihirisha imani, angehesabiwa kuwa mtoto wa Ibrahimu mwaminifu na mrithi wa ahadi aliyopewa yeye.

Lakini injili aliyoifundisha Yesu ilipoeleweka baada ya Pentekoste, Kanisa liliona kwamba baraka kwa ajili ya ulimwengu zingekuwa za asili ya kudumu, na kwamba ili kutimiza kusudi hili, Ufalme ungekuwa wa kiroho, ukiundwa na Waisraeli wa kweli, yaani, "kundi dogo" lililochaguliwa kutoka miongoni mwa Wayahudi na Wamataifa, ili liinuliwe kwenye asili na nguvu za kiroho. Hivyo, tunasoma kwamba Yesu ali *funua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili;*. (*2 Timotheo 1:10*) Na tangu siku za Yesu nuru zaidi inaangaza, kama alivyotabiri aliposema, "*Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*" (*Yohana 16:12,13*)

Hata hivyo, ulifika wakati, baada ya mitume kulala (kufariki), ambapo wengi katika Kanisa walianza kuipuuza taa (Neno la Mungu), na badala yake wakawatafuta walimu wa kibinadamu

ili wawaongoze. Walimu hao, wakijivuna kwa kiburi, walijitwalia vyeo na madaraka, na wakaanza kuwatawala watu wa Mungu. Kisha, hatua kwa hatua, likatokea kundi maalum lililoitwa "makasisi" (the clergy), ambao walijiona wenyewe, na walionwa na wengine, kama viongozi sahihi wa imani na matendo, bila hata kulijali Neno la Mungu. Hivyo, baada ya muda, mfumo mkuu wa Upapa uliibuka kutokana na heshima isiyo ya kawaida kwa mafundisho ya wanadamu wenye mapungufu, na kupuuza Neno la Mungu lisilo na kosa.

Kwa kweli, matokeo maovu yaliyoletwa na upuuzaji huu wa kweli yamekuwa makubwa. Kama wote wanavyojua, kanisa na ulimwengu uliostaarabika vilikuwa karibu kutumikishwa kabisa na mfumo huo, na kuongozwa kuabudu mapokeo na mafundisho ya madhehebu. Kutoka katika utumwa huu, pigo la ujasiri na lenye baraka kwa ajili ya uhuru na Biblia lilifanywa, katika kile kinachojulikana kama **Matengenezo ya Kidini**. Mungu aliwainua watetezi hodari wa Neno lake, miongoni mwao wakiwa Luther, Zwingli, Melanchthon, Wycliffe, Knox na wengineo. Hawa walielekeza umakini kwenye ukweli kwamba Upapa ulikuwa umeweka Biblia kando na badala yake kuweka maagizo na mafundisho ya kanisa, na walionyesha baadhi ya mafundisho na mazoea yake yaliyopotoka, wakionyesha kwamba yalijengwa juu ya mapokeo, kinyume na kweli, na yalipingana na Neno la Mungu. Wanamatengenezo hawa na wafuasi wao waliitwa Waprotestanti, kwa sababu walipinga Upapa, na kulidai Neno la Mungu kuwa ndiyo kanuni pekee sahihi ya imani na matendo.

Nafsi nyingi za waaminifu katika siku za Matengenezo ya Kidini zilienenda katika nuru, kwa kadiri ilivyokuwa ikiangaza wakati huo. Lakini tangu siku zao, Waprotestanti wamepata maendeleo kidogo, kwa sababu, badala ya kutembea katika nuru, wamesimama wakiwazunguka viongozi wao wapendwa, wakiwa tayari kuona kile tu walichokiona wao na si zaidi. Waliweka mipaka kwenye maendeleo yao katika njia ya kweli, wakizungushia ukuta, pamoja na kweli kidogo waliyokuwa nayo,

makosa mengi waliyoyabeba kutoka kanisa "**mama**." Kwa ajili ya mafundisho ya kimadhehebu yaliyootungwa hivyo miaka mingi iliyopita, Wakristo walio wengi wana uchaji wa imani potofu, wakidhani kwamba haiwezekani kujua zaidi kuhusu mipango ya Mungu sasa kuliko ilivyojulikana na Wanamatengenezo.

Kosa hili limekuwa na gharama kubwa; kwa kuwa, mbali na ukweli kwamba ni kanuni chache tu kuu za kweli zilizookolewa wakati huo kutoka kwenye takataka ya makosa, kuna vipengele maalum vya kweli vinavyoendelea kuwadia, ambavyo Wakristo wamenyimwa kwa sababu ya vizuizi vya mafundisho ya kimadhehebu(Creeds). Kwa mfano: Ilikuwa ni kweli katika siku za Nuhu, na kweli iliyohitaji imani ya wote waliotaka kutembea katika nuru wakati huo, kwamba gharika ilikuwa inakuja, wakati ambapo Adamu na wengine hawakujua lolote kuihusu. Haitakuwa ni kuhubiri kweli sasa kuhubiri kuhusu gharika inayokuja, lakini kuna kweli nyingine za vipindi maalum zinazoendelea kuwadia, ambazo, kama tunatembea katika nuru ya taa, tutazijua; hivyo, kama tuna nuru yote iliyowadia mamia kadhaa ya miaka iliyopita, na hiyo pekee, basi kwa kiasi fulani tuko gizani.

Neno la Mungu ni ghala kubwa la chakula kwa ajili ya wasafiri wenye njaa katika njia ing'aayo. Kuna maziwa kwa ajili ya watoto wachanga, na chakula kigumu kwa wale waliokomaa zaidi (*1 Pet. 2:2; Ebr. 5:14*); na si hivyo tu, bali lina chakula kinachofaa kwa nyakati na hali tofauti; na Yesu alisema mtumishi mwaminifu anapaswa kutoa chakula kwa wakati wake kwa ajili ya nyumba ya imani—"vitu vipya na vya kale," kutoka ghalani. (*Luka 12:42; Mt. 13:52*) Haiwezekani kutoa vitu kama hivyo kutoka kwenye kanuni ya imani ya kimadhehebu au ghala lolote la kimadhehebu. Tunaweza kutoa mambo fulani ya kale na mazuri kutoka kwa kila mojawapo, lakini hakuna jipya lolote. Kweli iliyomo ndani ya kanuni za imani za madhehebu mbalimbali imefunikwa na kuchanganywa na makosa kiasi kwamba uzuri

wake wa asili na thamani yake halisi havionekani. Mafundisho mbalimbali ya kimadhehebu hupingana na kukinzana na kila wakati; na kwa kuwa kila moja inadai msingi wa Kibiblia, fujo ya mawazo, na upingamizi ulio wazi, husingiziwa Neno la Mungu. Hili limezua msemo wa kawaida: ***"Biblia ni kama fidla ya zamani, ambayo kila mtu anaweza kupiga wimbo anaotaka."***

Jinsi gani hili linaeleza wazi ukafiri wa nyakati zetu, unaosababishwa na upotoshaji wa Neno la Mungu na tabia yake kupitia mapokeo ya wanadamu, pamoja na ukuaji wa akili ambao hautainama tena kwa heshima ya upofu na ya upotoshaji, bali inadai sababu ya tumaini lililo ndani yetu. Mwanafunzi mwaminifu wa Neno anapaswa kuwa tayari siku zote kutoa sababu ya tumaini lake. Neno la Mungu pekee ndilo linaweza kumfanya mtu awe na hekima, na lafaa kwa mafundisho, maonyo, n.k., "*ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema*." (*1 Pet. 3:15; 2 Tim. 3:15-17*) Ghala hili moja tu ndilo lina hazina isiyoisha ya vitu vipya na vya kale—chakula kwa wakati wake kwa ajili ya nyumba ya imani. Hakika hakuna anayeiamini kauli ya Maandiko kwamba *"njia ya mwenye haki hung'aa zaidi na zaidi hata mchana mkamilifu"* atakayedai kwamba mchana mkamilifu ulifika wakati wa Luther; na kama haikuwa hivyo, tunafanya vyema tukiangalia taa yetu kama *"taa ing'aayo* ***mahali penye giza*** *HATA KUTAKAPOPAMBAZUKA." 2 Pet. 1:19*

Wala haitoshi kwamba sasa tunajikuta tuko katika njia ya nuru; ni lazima "**tutembee katika nuru,"** tuendelee kupiga hatua, la sivyo nuru, ambayo haisimami, itaendelea mbele na kutuacha gizani. Tatizo la wengi ni kwamba wao hukaa chini, na hawaendelei mbele katika njia ya nuru. Chukua konkodansi na uchunguze maandiko yaliyo chini ya maneno ***kaa*** na ***simama,*** kisha yalinganishe na yale yaliyo chini ya maneno ***tembea*** na ***kimbia***, na utapata tofauti kubwa: Wanadamu "***hukaa*** gizani," pamoja na "wenye dharau," na ***husimama*** miongoni mwa wasiomcha Mungu, lakini "***hutembea*** katika nuru," na "***hukimbia*** ili kupata tuzo." *Isa. 42:7; Zab. 1:1; Ebr. 12:1*

Ukamilifu wa maarifa si jambo la wakati uliopita, bali la wakati ujao—wakati ujao ulio karibu sana, tunatumaini; na hadi tutambue ukweli huu, hatuko tayari kuthamini na kutarajia mafunuo mapya ya mpango wa Baba yetu. Ni kweli, bado tunarudi kwenye maneno ya manabii na mitume kwa ajili ya maarifa yote ya sasa na yajayo; hata hivyo, si kwa sababu wao daima walielewa mipango na makusudi ya Mungu vizuri kuliko sisi, bali kwa sababu Mungu aliwatumia kama vinywa vyake ili **kuwasiliana nasi**, na Kanisa lote katika Kipindi chote cha Kikristo, kweli inayohusu mipango yake, punde tu inapowadia. Ukweli huu unathibitishwa kwa wingi na mitume. Paulo anatuambia kwamba Mungu amelifunulia Kanisa la Kikristo siri ya mapenzi yake ambayo alikuwa amekusudia ndani yake, na ambayo hakuwahi kuifunua hapo awali, ingawa alikuwa ameiandika katika maneno ya mafumbo ambayo hayangeweza kueleweka hadi wakati ufaao, ili macho ya ufahamu wetu yafunguliwe ili tuuthamini "**mwito mkuu**" uliokusudiwa kwa ajili ya waumini wa Kipindi cha Kikristo pekee. (*Efe. 1:9,10,17,18; 3:4-6*)

Hili linatuonyesha wazi kwamba manabii wala malaika hawakuelewa maana ya unabii uliotolewa. Petro anasema kwamba walipouliza kwa shauku kujua maana yake, Mungu aliwaambia kwamba kweli zilizofichwa katika unabii wao hazikuwa kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yetu sisi wa Kipindi cha Kikristo. Na analihimiza Kanisa kutumaini neema (upendeleo, baraka) zaidi katika upande huu—yaani maarifa zaidi ya mipango ya Mungu. *1 Pet. 1:10-13*

Ni dhahiri kwamba ingawa Yesu aliahidi kuwa Kanisa lingeongozwa kwenye kweli yote, ulikuwa ni ufunuo wa hatua kwa hatua. Wakati Kanisa, katika siku za mitume, lilikuwa huru kutokana na makosa mengi yaliyoibuka chini ya Upapa na ndani yake, bado hatuwezi kudhani kwamba kanisa la awali liliona kwa undani au kwa uwazi mpango wa Mungu kama inavyowezekana leo. Ni dhahiri, pia, kwamba mitume mbalimbali walikuwa na viwango tofauti vya ufahamu wa mpango wa

Mungu, ingawa *maandishi yao yote* yaliongozwa na kutiwa uvuvio na Mungu, kama vile yalivyokuwa maneno ya manabii. Ili kuonyesha tofauti za maarifa, tunapaswa tu kukumbuka mwendo wa kusuasua, kwa muda, wa Petro na mitume wengine, isipokuwa Paulo, wakati injili ilipoanza kwenda kwa Wamataifa. (*Mdo. 10:28; 11:1-3; Gal. 2:11-14*) Kusuasua kwa Petro kulikuwa tofauti kabisa na uhakika wa Paulo, uliochochewa na maneno ya manabii, matendo ya Mungu ya zamani, na mafunuo ya moja kwa moja aliyopewa.

Ni wazi kwamba Paulo alikuwa na mafunuo mengi zaidi kuliko mtume mwingine yeyote. Mafunuo haya hakuruhusiwa kuyafanya yajulikane kwa Kanisa, wala kuyaeleza kikamilifu na kwa uwazi hata kwa mitume wengine (*2 Kor. 12:4; Gal. 2:2*), lakini bado tunaweza kuona thamani kwa kanisa zima katika njozi na mafunuo hayo aliyopewa Paulo; kwa kuwa ingawa hakuruhusiwa kueleza alichokiona, wala kueleza kwa undani yote aliyoyajua kuhusu siri za Mungu zinazohusu "zama zijazo," lakini kile alichokiona kiliyapa maneno yake nguvu, kivuli na kina cha maana ambacho, katika nuru ya matukio yaliyofuata, utimilifu wa unabii na uongozi wa Roho, tunaweza kukithamini kikamilifu zaidi kuliko kanisa la awali lilivyoweza.

Ili kuthibitisha kauli iliyotangulia, tunakumbuka kitabu cha mwisho cha Biblia—Ufunuo, kilichoandikwa yapata mwaka 96 B.K. Maneno yake ya utangulizi yanakitangaza kuwa ni ufunuo maalum wa mambo ambayo hayakueleweka hapo awali. Hii inathibitisha pasipo shaka kwamba angalau hadi wakati huo, mpango wa Mungu haukuwa umefunuliwa kikamilifu. Wala kitabu hicho hakijawahi kuwa, hadi sasa, kile ambacho jina lake linamaanisha—ufunuo. Kwa upande wa kanisa la awali, yawezekana hakuna aliyeelewa sehemu yoyote ya kitabu hicho. Hata Yohana, aliyeziona njozi hizo, yawezekana hakujua umuhimu wa kile alichokiona. Alikuwa nabii na mtume; na wakati akiwa mtume alielewa na kufundisha kile kilichokuwa "chakula kwa wakati wake," akiwa nabii alitamka mambo ambayo

yangekuwa "chakula" katika nyakati zijazo kwa ajili ya nyumba ya imani.

Katika zama za Kikristo, baadhi ya watakatifu walijaribu kuelewa wakati ujao wa Kanisa kwa kukichunguza kitabu hiki cha ishara, na bila shaka wote waliosoma na kuelewa hata sehemu ya mafundisho yake walibarikiwa kama ilivyoahidiwa. (*Ufu. 1:3*) Kitabu kiliendelea kufunguka kwa watu kama hao, na katika siku za Matengenezo ya Kidini kilikuwa msaada muhimu kwa Luther kuamua kwamba Upapa, ambapo alikuwa mhudumu wake mwenye dhamiri safi, kwa kweli ulikuwa ndiye "Mpinga-Kristo" aliyetajwa na Mtume, ambaye historia yake sasa tunaona inajaza sehemu kubwa sana ya unabii huo.

Hivyo, Mungu huifunua kweli yake hatua kwa hatua na kuudhihirisha utajiri upitao kiasi wa neema yake; na kwa hiyo nuru nyingi zaidi inawadia sasa kuliko wakati mwingine wowote uliopita katika historia ya Kanisa.

"*Na bado uzuri mpya tutaushuhudia,*

*Na nuru izidiyo daima kuangazia.*

## SOMO LA 2

# UWEPO WA MUUMBA MWENYE AKILI WATHIBITISHWA

USHAHIDI NJE YA BIBLIA, UKICHUNGUZWA KWA NURU YA AKILI—NADHARIA ISIYOWEZA KUTETEWA—NADHARIA YENYE MASHIKO—TABIA YA MUNGU YADHIHIRISHWA—HITIMISHO ZA KIMANTIKI

HATA kwa mtazamo wa mtu mwenye mashaka, utafiti wa kimantiki na wa wazi kuhusu mambo yasiyojulikana, kwa kutumia nuru ya yale yanayojulikana, utamwongoza mtu mwenye akili asiye na upendeleo kuelekea kwenye ukweli. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba bila ufunuo wa moja kwa moja wa mipango na makusudi ya Mungu, wanadamu wangeweza tu kuikaribia kweli na kufikia hitimisho lisilo dhahiri. Lakini kwa sasa, tuiweke kando Biblia, na tuyatazame mambo kwa mtazamo wa akili pekee.

Mtu anayeweza kutazama angani kwa darubini, au hata kwa macho yake ya kawaida, na kuona huko ukuu wa uumbaji, mpangilio wake, uzuri, mpangilio, uwiano na utofauti wake, na bado akatilia shaka kwamba Muumba wa vitu hivi ni mkuu zaidi yake kwa hekima na nguvu, au anayeweza kufikiria kwa muda kwamba mpangilio kama huo ulitokea kwa bahati nasibu, bila Muumba, mtu huyo amepoteza au amepuuza uwezo wa kufikiri kiasi cha kustahili kuitwa kile ambacho Biblia inamwita, mpumbavu (mtu anayepuuza au asiye na akili): *"Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu."* Vyovyote ilivyotokea, angalau sehemu hiyo ya Biblia ni ya kweli, kama ambavyo kila akili timamu haina budi kuhitimisha; kwa maana ni kweli isiyohitaji uthibitisho kwamba matokeo ni lazima yasababishwe na vyanzo vyenye uwezo.

Kila mmea na kila ua, hata lenyewe, linatoa ushuhuda mwingi kuhusu somo hili. Yakiwa na muundo tata, na umbo na nakshi za kupendeza mno, kila kimoja kinazungumzia hekima na ustadi ulio juu ya ule wa mwanadamu. Ni upuuzi ulioje unaojivuna

kwa ustadi na akili ya mwanadamu, na kusingizia bahati nasibu tu kwa ajili ya mpangilio, usawa na uwiano wa maumbile; unaokubali kuwepo kwa sheria za asili, huku ukikana kwamba asili ina Mtoa-sheria mwenye akili.

Baadhi ya watu wanaokanusha kuwepo kwa Muumba mwenye akili hudai kwamba asili ndiyo Mungu pekee. Wao husema kwamba viumbe vyote, yaani wanyama na mimea, vilitokana na asili bila kuwepo kwa mpangilio wowote wenye akili. Badala yake, wanadai viumbe hivyo viliongozwa na ile wanayoiita **"sheria ya walio hodari ndio wanaosalia"** kupitia mchakato wa mageuzi.

Nadharia hii haina uthibitisho, kwa maana pande zote zinazotuzunguka tunaona kwamba viumbe mbalimbali vina asili isiyobadilika ambayo haibadiliki kuwa asili ya juu zaidi; na ingawa wale wanaoshikilia nadharia hii wamefanya jitihada za mara kwa mara, hawajawahi kufanikiwa ama kuchanganya spishi tofauti au kuzalisha aina mpya isiyobadilika. Hakuna kisa kinachojulikana ambapo aina moja imegeuka kuwa aina nyingine*. Ingawa kuna samaki wanaoweza kutumia mapezi yao kwa muda kama mabawa na kuruka nje ya maji, na vyura wanaoweza kuimba, hawajawahi kujulikana wakigeuka kuwa ndege; na ingawa kuna wanyama wengine wanaofanana kidogo na wanadamu, ushahidi haupo kabisa kwamba mwanadamu alitokana na viumbe kama hivyo. Kinyume chake, uchunguzi unathibitisha kwamba ingawa aina tofauti za spishi moja zinaweza kuzalishwa, haiwezekani kuzichanganya spishi mbalimbali, au kwa moja kuibuka kutoka kwa nyingine. Kwa sababu hiyohiyo, punda na farasi, ingawa wanafanana, hawawezi kudaiwa kuwa wanahusiana, kwa maana inajulikana sana

---

* *Kwa faida ya baadhi ya wasomaji, tunaeleza kwamba mabadiliko kama vile ya viwavi kuwa vipepeo si mabadiliko ya asili; kiwavi si kitu kingine bali ni funza anayeanguliwa kutoka kwenye yai la kipepeo*

kwamba watoto wao si wakamilifu na hawawezi kuendeleza spishi yoyote kati ya hizo.

Hakika kama asili isiyo na akili ndiyo ingekuwa Muumba au mleta mageuzi, ingeendeleza mchakato huo, na kusingekuwa na kitu kama spishi thabiti, maana bila akili hakuna ambacho kingefikia hali thabiti. Mageuzi yangekuwa ni uhalisia leo, na tungeona karibu yetu samaki wakibadilika kuwa ndege, na nyani kuwa wanadamu. Tunahitimisha kwamba nadharia hii inapingana na akili ya mwanadamu na pia na Biblia, inapodai kwamba viumbe vyenye akili viliumbwa na nguvu isiyo na akili.

Kuna nadharia moja kuhusu uumbaji (isipokuwa mwanadamu) kupitia mchakato wa mageuzi, ambayo hatuoni kuwa ina pingamizi kubwa, na tunaieleza kwa ufupi kama ifuatavyo:

Nadharia hii inadhania kwamba spishi mbalimbali za sasa ni thabiti na haziwezi kubadilika, kwa kadiri ya asili au aina zao. Ingawa asili za sasa zinaweza kuendelezwa hadi kufikia kiwango cha juu zaidi, hata ukamilifu, spishi hizi au asili zitabaki zilezile milele. Nadharia hii pia inadhania kwamba hakuna hata moja ya spishi hizi thabiti iliyoumbwa hivyo tangu mwanzo. Bali kwamba katika nyakati za kale sana ziliibuka kutoka katika ardhi, na kupitia michakato ya taratibu ya mageuzi kutoka umbo moja kwenda jingine..

Mageuzi haya, chini ya sheria zilizowekwa na Mungu, ambapo mabadiliko ya chakula na hali ya hewa yalikuwa na jukumu muhimu, yanaweza kuwa yaliendelea hadi spishi thabiti, kama zinavyoonekana sasa, zilipowekwa. Baada ya hapo, mabadiliko zaidi hayawezekani, kwani inaonekana kuwa kusudi la mwisho la Muumba katika suala hili lilikuwa limefikiwa. Ingawa kila moja ya familia mbalimbali za mimea na wanyama ina uwezo wa kuboreshwa au kudorora, hakuna hata moja kati yao inayoweza kubadilika na kuwa, wala haziwezi kutolewa kutoka, familia au aina nyingine. Ingawa kila moja kati ya hizi inaweza kufikia ukamilifu wa asili yake thabiti, kusudi la Muumba kuhusu asili

likiwa limefikiwa, mabadiliko zaidi katika suala hili hayawezekani.

Inadaiwa kwamba mimea na wanyama wa asili, ambao ndio chimbuko la aina thabiti za sasa, walitoweka kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu. Mifupa na **mabaki ya kale** ya wanyama na mimea ambavyo havipo sasa, vilivyopatikana ndani kabisa ya uso wa dunia, vinaunga mkono nadharia hii. Mtazamo huu haupingi wala kukataa mafundisho ya Biblia kwamba mwanadamu aliumbwa moja kwa moja na mkamilifu, akifanywa kwa mfano wa kiakili na kimaadili wa Muumba wake, na si maendeleo kupitia mchakato wa mageuzi, labda uliokuwa wa kawaida kwa viumbe vingine vyote. Mtazamo huu haungebatilisha kwa njia yoyote, bali ungeunga mkono, dai la Biblia kwamba asili kama ilivyo leo inafundisha kuwa Kiumbe Mwenye Akili Aliupangilia, na ndiye alikuwa chanzo chake cha kwanza.

Acha akili ya mwanadamu ifanye bidii yake kufuata ukweli unaojulikana hadi sababu zinazofaa na zenye uwezo, ikitoa sifa stahiki kwa sheria za asili katika kila hali. Hata hivyo, licha ya utata wote wa asili, nguvu ya Muumba wake mkuu ndiyo inayoongoza kila kitu, Mungu mwenye hekima na uweza wote.

Basi, tunadai kwamba kuwepo kwa Muumba Mwenye Akili ni kweli iliyothibitishwa wazi, ambayo uthibitisho wake uko pande zote zinazotuzunguka: naam, na ndani yetu pia; kwa maana sisi ni kazi ya mikono yake, ambaye kila uwezo wetu wa akili na mwili unatangaza ustadi wa ajabu upitao ufahamu wetu. Na yeye pia ndiye Mbunifu na Muumba wa kile tunachokiita maumbile/asili. Tunadai kwamba yeye ndiye aliyeratibu na kuziweka sheria za asili, ambazo tunauona na kuustaajabia uzuri na uwiano wa utendaji wake. Huyu ambaye hekima yake iliubuni ulimwengu, na ambaye uweza wake unautegemeza na kuuongoza Yeye ambaye hekima na uweza wake vinapita wetu kwa kiasi kisichopimika,tunamwabudu na kumwadhimisha kwa silika.

Kutambua uwepo wa Mungu mwenye nguvu ni sawa na kuogopa nguvu zake zisizo na kikomo, isipokuwa tuweze kuona pia kuwa ana wema na ukarimu unaolingana na uweza wake. Ushahidi uleule unaothibitisha uwepo, nguvu, na hekima yake, ndio unaotuhakikishia kikamilifu ukweli huu pia. Siyo tu kwamba tunalazimika kufikia hitimisho kuwa Mungu yupo, na kwamba nguvu na hekima yake ni kubwa zaidi isivyopimika kuliko yetu, Lakini, akili inatulazimisha kuhitimisha kwamba kiumbe kilicho bora zaidi hakiwezi kuwa bora kuliko Muumba wake; Hivyo, ni lazima tuhitimishe kwamba hata udhihirisho mkuu zaidi wa wema na haki miongoni mwa wanadamu bado ni duni kwa kiwango ukilinganishwa na ule wa Muumba, kama vile hekima na nguvu za mwanadamu zilivyo duni mbele zake. Kwa njia hii, tunapata picha akilini mwetu ya tabia na sifa za Muumba mkuu. Yeye ni mwenye hekima, haki, upendo, na nguvu; na kwa lazima, upana wa sifa zake ni mkuu zaidi isivyopimika kuliko ule wa kiumbe wake mkuu zaidi.

Lakini zaidi ya hayo: baada ya kufikia hitimisho hili la kimantiki kuhusu kuwepo na tabia ya Muumba wetu, hebu tujiulize, Tunapaswa kutarajia nini kutoka kwa kiumbe kama huyo? Jibu linakuja, kwamba kuwa na sifa kama hizo kunatoa hoja ya kimantiki kwamba ni lazima zitumike. Nguvu ya Mungu ni lazima itumike, na itumike kwa kupatana na asili yake mwenyewe—yaani, kwa hekima, haki na wema. Vyovyote vile vitakavyokuwa vyombo vya kufikia lengo hilo, vyovyote vile vitakavyokuwa vitendo vya nguvu ya Mungu, matokeo ya mwisho ni lazima yapatane na asili na tabia yake, na kila hatua ni lazima idhibitishwe na hekima yake isiyo na kikomo.

Ni nini kinachoweza kuwa cha kimantiki zaidi kuliko utumiaji wa nguvu kama tunavyouona ukidhihirishwa katika uumbaji wa ulimwengu usiohesabika unaotuzunguka, na katika utofauti wa ajabu wa dunia? Ni nini kinachoweza kuwa cha kimantiki zaidi kuliko kuumbwa kwa mwanadamu, aliyejaliwa akili na hukumu, mwenye uwezo wa kuthamini kazi za Muumba wake,

na kuhukumu ustadi wake—hekima yake, haki yake, nguvu zake na upendo wake? Yote haya ni ya kimantiki, na yote yanapatana kikamilifu na ukweli tunaoujua.

Na sasa inakuja hoja yetu ya mwisho. Je, si jambo la kimantiki kudhani kwamba kiumbe mwenye hekima na wema usio na kikomo, baada ya kumuumba kiumbe mwenye uwezo wa kumthamini yeye mwenyewe na mpango wake, angesukumwa na upendo na haki yake kukidhi mahitaji ya asili ya kiumbe huyo, kwa kumpa UFUNUO fulani? Je, haingekuwa ni dhana ya kimantiki, kwamba Mungu angempa mwanadamu taarifa kuhusu lengo la kuwepo kwake, na mipango yake kwa ajili ya wakati wake ujao? Kinyume chake, tunauliza, je, haingekuwa jambo lisilo la kimantiki kudhani kwamba Muumba kama huyo angemuumba kiumbe kama mwanadamu, akampa nguvu za akili zinazotazama wakati ujao, na bado asitoe ufunuo wowote wa mipango yake ili kukidhi matamanio hayo? Mwenendo kama huo haungekuwa wa kimantiki, kwa sababu unapingana na tabia ambayo kwa kimantiki tunamhusisha nayo Mungu; unapingana na mwenendo unaofaa wa kiumbe anayeongozwa na haki na upendo.

Tunaweza kutoa hoja kwamba katika kumuumba mwanadamu, kama Hekima ya Mungu ingeamua kuwa haifai kumpa maarifa ya hatima yake ya baadaye, na sehemu yake katika mipango ya Muumba wake, basi hakika Haki ya Mungu, pamoja na Upendo wa Mungu, vingesisitiza kwamba kiumbe huyo awekewe mipaka katika uwezo wake ili asiwe anateseka na kuchanganyikiwa daima na mashaka, na hofu, na ujinga; na matokeo yake Nguvu ya Mungu ingetumika chini ya mipaka hiyo. Ukweli, basi, kwamba mwanadamu ana uwezo wa kuthamini ufunuo wa mpango wa Mungu, ukichukuliwa pamoja na tabia inayokubalika ya Muumba wake, ni sababu tosha ya kutarajia kwamba Mungu angetoa ufunuo kama huo, kwa wakati na namna ambayo hekima yake ingeona inafaa. Hivyo basi, kwa kuzingatia mambo haya, hata kama tungekuwa hatuijui Biblia, akili

ingetuelekeza kutarajia na kuwa macho kwa ajili ya ufunuo fulani kama ule ambao Biblia inadai kuwa nao. Na zaidi ya hayo, tukizingatia mpangilio na uwiano wa uumbaji kwa ujumla, jinsi ambavyo sayari na mifumo inavyofuata wakati na mahali pake katika mwandamano mkuu, hatuna budi kuhitimisha kwamba kasoro ndogo ndogo, kama vile matetemeko ya ardhi, vimbunga, n.k., ni ishara tu kwamba utendaji kazi wa pamoja wa elementi mbalimbali katika ulimwengu huu kwa sasa si mkamilifu. Uhakikisho kwamba kila kitu hatimaye kitakuwa kikamilifu na chenye uwiano duniani kama ilivyo mbinguni, pamoja na maelezo fulani kwa nini sivyo ilivyo kwa sasa, ni maombi ambayo si yasiyo ya kimantiki kwa wanadamu wenye kufikiri kuuliza, wala kwa Muumba, ambaye hekima, nguvu na wema wake vimethibitishwa, kujibu. Hivyo tunapaswa kutarajia ufunuo tunaoutafuta ujumuishe uhakikisho na maelezo kama hayo.

Baada ya kuthibitisha mantiki ya kutarajia ufunuo wa mapenzi na mpango wa Mungu kuhusu jamii yetu, katika sura inayofuata tutachunguza tabia ya jumla ya Biblia ambayo inadai kuwa ndiyo ufunuo huo hasa. Na kama itawasilisha tabia ya Mungu kwa uwiano kamili na kile ambacho akili, kama ilivyojadiliwa hapo juu, inasema, tunapaswa kuhitimisha kwamba hivyo inajithibitisha yenyewe kuwa ndio ufunuo unaohitajika na unaotarajiwa kimantiki kutoka kwa Mungu, na kisha tunapaswa kuukubali ushuhuda wake kama huo. Kama ni ya Mungu, mafundisho yake, yatakapothaminiwa kikamilifu, yatapatana na tabia yake, ambayo akili inatuhakikishia kuwa ni kamilifu katika hekima, haki, upendo na nguvu.

Enyi akili zenye shauku, mnaozurura mbali,
Mkifuatilia maajabu ya uumbaji kila upande,
Kubali nyayo za Mungu wenu,
Msujudieni mbele zake, na mumwabudu.

Mbingu zatangaza utukufu wako, Ee Bwana;
Katika kila nyota hekima yako hung'aa;

Lakini macho yetu yanapolitazama Neno lako,
Hapo ndipo jina lako lasomeka kwa mistari iliyo bora zaidi.

Mwanga wa Jua Juu ya Wote

"Ni upumbavu gani basi," asema mkosoaji asiye na imani,
Kwa mdomo wa dhihaka na macho yanayodai kujua dunia yote,
Wakati ngome kwa ngome, kituo kwa kituo,
Midundo isiyokoma ya ngoma ya vita yarudia changamoto,
Na kuzunguka dunia iliyo kijani, kwa sauti ya kengele za kanisa,
Midundo ya asubuhi ya kambi za askari hupiga kwa wakati mmoja,
Kuota ndoto za amani katikati ya dunia iliyojaa silaha;
Kuona panga zikibadilishwa kuwa majembe kwa hirizi za Maandiko;
Kuona mataifa, yamelewa kwa divai ya damu,
Yakitetereka kuchukua kiapo cha undugu,
Kama walevi wakijibu wito wa Baba Mathew.

"Zuieni Bau au Kaizari kwa kizuizi
Cha 'majani ya mizeituni' na maazimio yaliyotungwa;
Chomeni mizinga kwa maandiko makali ya Maandiko, na mtarajie
Kuzamisha majeshi ya majini kwa maneno ya upepo mtupu;
Hata hivyo, utukufu na fahari ya vita
Bado itavuta mamilioni yanayopiga kelele;
Bado kazi yenye giza itamsalimu shujaa aondokaye
Kwa kuvua kofia, na uzuri utapeperusha kitambaa;
Bado mshairi ataimba nyimbo za ushujaa;
Bado ibada ya mashujaa itapiga magoti mbele ya wenye nguvu;
Akiwa mnene na mchangamfu, mhubiri aliyevaa joho jeusi,

Juu ya chupa yake ya tatu ya divai ya kushawishi,
Atathibitisha kwa wasikilizaji wenye manyoya na mapanga
Kwamba kazi yao yalingana na sheria ya upendo;
Na Kanisa kwa ajili ya Serikali, na Serikali kwa ajili ya **Kanisa** vitapigana,
Na zote zitakubaliana kwamba nguvu peke yake ndiyo haki."

Licha ya dhihaka kama hizi, enyi wachache waaminifu,
Mnaothubutu kulishika Neno la Mungu na kulishuhudia kweli,
Ambalo imani yenu yenye macho safi yavuka nyakati zetu mbaya,
Na juu ya jangwa la sasa la uhalifu
Huona wakati ujao ulio tulivu, wenye mavazi ya kijani,
Milima iliyochanganyika na manyoya ya kondoo, na mito laini katikati,
Endeleeni kushika njia ile ile ambayo wajibu wenu wawataka,
Hata hekima ya dunia itingishe vichwa vya tahadhari.
Hakuna kweli itokayo mbinguni ishukayo duniani
Bila kupokelewa kwanza na dhihaka ya mwenye mashaka;
Hukataliwa, hudhihakiwa, hata baraka zake zishuke
Na kuwa za kawaida kama umande na mwanga wa jua juu ya wote.

— *Whittier*

## SOMO LA III

# BIBLIA KAMA UFUNUO WA KIMUNGU IKITAZAMWA KATIKA NURU YA MANTIKI

MADAI YA BIBLIA NA USHAHIDI WAKE WA AWALI WA KUAMINIKA — UKALE WAKE NA KUHIFADHIWA KWAKE — USHAWISHI WAKE WA KIADILI — MALENGO YA WAANDISHI — SIFA ZA JUMLA ZA MAANDIKO HAYO — VITABU VYA MUSA — SHERIA YA MUSA — UPEKEE WA SERIKALI ILIYOSIMIKWA NA MUSA — HAIKUWA MFUMO WA UTAWALA WA MAKUHANI — MAAGIZO KWA WATAWALA WA KIRAIA — TAJIRI NA MASKINI KATIKA DARAJA MOJA MBELE YA SHERIA — KINGA DHIDI YA KUINGILIA HAKI ZA WATU — UKUHANI SIO TABAKA LINALOPENDELEWA, JINSI WALIVYOTUNZWA, NK. — UONEVU DHIDI YA WAGENI, WAJANE, YATIMA NA WATUMISHI ULIZUIWA — MANABII WA BIBLIA — JE, KUNA KIUNGO CHA PAMOJA CHA UMOJA KATI YA SHERIA, MANABII NA WAANDISHI WA AGANO JIPYA? — MIUJIZA SI JAMBO LISILO NA MANTIKI — HITIMISHO LA KIMANTIKI.

BIBLIA ni **mwangaza** wa ustaarabu na uhuru. Ushawishi wake kwa ajili ya mema katika jamii umetambuliwa na wanasiasa wakuu, hata ingawa wengi wao wameitazama kupitia miwani mbalimbali ya mafundisho ya kimadhehebu yanayokinzana, ambayo, huku yakiitetea Biblia, yanapotosha sana mafundisho yake. Kitabu hicho kikuu cha kale kinawakilishwa vibaya bila kukusudia lakini kwa kuhuzunisha na marafiki zake, ambao wengi wao wangeutoa uhai wao kwa ajili yake; na bado wanakidhuru zaidi kuliko maadui zake, kwa kudai kwamba kinaunga mkono maoni yao potofu waliyoyarithi kwa muda mrefu kuhusu kweli yake, waliyoyapokea kupitia mapokeo ya baba zao. Laiti watu kama hao wangeamka, wakichunguze upya kitabu chao kitakatifu, na kuwaaibisha maadui zake kwa kuwapokonya silaha zao!

Kwa kuwa nuru ya asili inatuongoza kutarajia ufunuo kamili zaidi wa Mungu kuliko ule unaotolewa na asili yenyewe, basi akili timamu yenye kutafakari itakuwa tayari kuchunguza madai ya kitu chochote kinachojinasibu kuwa ni ufunuo wa Kimungu, mradi tu kioneshe ushahidi wa awali wenye mashiko wa ukweli wa madai hayo. Biblia inadai kuwa ni ufunuo kama huo kutoka kwa Mungu, na inakuja kwetu ikiwa na ushahidi wa kutosha wa

awali kuhusu uwezekano wa usahihi wa madai yake, na inatupa tumaini la kimantiki kwamba uchunguzi wa kina zaidi utafunua ushahidi kamili zaidi na thabiti kwamba kwa kweli ni Neno la Mungu.

Biblia ndicho kitabu cha zamani zaidi kilichopo; kimehimili dhoruba za karne thelathini. Wanadamu wamejaribu kwa kila njia iwezekanavyo kukifuta kutoka uso wa dunia: wamekificha, wamekiteketeza, wamefanya kuwa kosa la jinai linaloadhibiwa kwa kifo kuwa nacho, na mateso makali na yasiyo na huruma yameendeshwa dhidi ya wale waliokuwa na imani nacho; lakini bado kitabu hicho kipo. Leo, wakati maadui zake wengi wamelala usingizi wa mauti, na mamia ya vitabu vilivyoandikwa ili kukidhalilisha na kupindua ushawishi wake vimesahaulika zamani, Biblia imepata njia ya kuingia katika kila taifa na lugha duniani, kukiwa na zaidi ya tafsiri mia mbili tofauti zake zilizofanywa. Ukweli kwamba kitabu hiki kimestahimili karne nyingi hivyo, licha ya jitihada zisizo na kifani za kukifuta na kukiangamiza, angalau ni ushahidi thabiti wa kimazingira kwamba Kiumbe mkuu ambaye kinadai kuwa ndiye Mwandishi wake, pia amekuwa Mlinzi wake.

Pia ni kweli kwamba ushawishi wa kimaadili wa Biblia daima ni mzuri. Wale wanaokuwa wanafunzi makini wa kurasa zake daima huinuliwa kwenye maisha safi zaidi. Maandiko mengine juu ya dini na sayansi mbalimbali yamefanya mema na yameboresha na kubariki wanadamu, kwa kiasi fulani; lakini vitabu vingine vyote kwa pamoja vimeshindwa kuleta furaha, amani na baraka kwa viumbe vinavyougua kama ambavyo Biblia imeleta kwa matajiri na maskini, kwa wasomi na wasio wasomi. Biblia si kitabu cha kusomwa tu: ni kitabu cha kujifunza kwa uangalifu na tafakari; kwa maana mawazo ya Mungu yako juu kuliko mawazo yetu, na njia zake kuliko njia zetu. Na kama tunataka kuuelewa mpango na mawazo ya Mungu asiye na kikomo, ni lazima tuelekeze nguvu zetu zote kwenye kazi hiyo

muhimu. **Hazina tajiri zaidi za kweli hazipatikani juu juu kila wakati.**

Kitabu hiki, mwanzo hadi mwisho, kinamlenga na kumtaja daima mhusika mmoja mashuhuri, Yesu wa Nazareti, ambaye, kinadai, alikuwa Mwana wa Mungu. Kuanzia mwanzo hadi mwisho, jina lake, cheo chake, na kazi yake, vimepewa umuhimu. Kwamba mtu aliyeitwa Yesu wa Nazareti aliishi, na alikuwa anajulikana kwa kiasi fulani, yapata wakati ulioonyeshwa na waandishi wa Biblia, ni ukweli wa historia hata nje ya Biblia, na umethibitishwa kwa njia mbalimbali na kikamilifu. Kwamba Yesu huyu alisulubishwa kwa sababu alikuwa amewaudhi Wayahudi na makuhani wao ni ukweli mwingine uliothibitishwa na historia, mbali na ushahidi uliotolewa na waandishi wa Agano Jipya. Waandishi wa Agano Jipya (isipokuwa Paulo na Luka) walikuwa ni watu waliomfahamu binafsi na wanafunzi wa Yesu wa Nazareti, ambao maandishi yao yanaeleza mafundisho yake.

Kuwepo kwa kitabu chochote kunamaanisha kuwepo kwa lengo kwa upande wa mwandishi. Kwa hiyo tunahoji: Je, ni malengo gani yaliyoweza kuwachochea watu hawa kuunga mkono na kutetea kusudi la mtu huyu? Alihukumiwa kifo na kusulubishwa kama mhalifu na Wayahudi, huku watu wa dini zaidi miongoni mwao wakikubaliana na kudai kifo chake, kama mtu asiyefaa kuishi. Na katika kuitetea kesi yake, na kueneza mafundisho yake, watu hawa walikabili dharau, kunyimwa, na mateso makali, wakaihatarisha mioyo yao, na katika visa vingine hata wakafa kama mashujaa wa Imani. Tukikubali kwamba alipokuwa hai Yesu alikuwa mtu wa ajabu, katika maisha yake na mafundisho yake, ni lengo gani lingeweza kuwepo kwa yeyote kutetea kusudi lake baada ya kufa kwake?—hasa wakati kifo chake kilikuwa cha aibu sana? Na kama tutadhani kwamba waandishi hawa walibuni hadithi zao, na kwamba Yesu alikuwa shujaa wao wa kuwaziwa au wa mfano, ingekuwa ni upuuzi kiasi gani kudhani kwamba watu wenye akili timamu, baada ya

kudai kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, kwamba alikuwa amezaliwa kwa njia isiyo ya kawaida, alikuwa na nguvu zisizo za kawaida ambazo kwazo alikuwa amewaponya wakoma, kuwarudishia kuona waliozaliwa vipofu, kuwafanya viziwi wasikie, na hata kuwafufua wafu—ni upuuzi mkubwa kiasi gani kudhani kwamba wangehitimisha hadithi ya mhusika kama huyo kwa kueleza kwamba kikundi kidogo cha maadui zake kilimnyonga kama mhalifu, huku marafiki zake wote na wanafunzi, na miongoni mwao waandishi wenyewe, wakimwacha na kukimbia katika wakati huo wa majaribu?

Ukweli kwamba historia ya kawaida haikubaliani katika baadhi ya mambo na waandishi hawa haupaswi kutufanya tuone maandishi yao kuwa si ya kweli. Wale wanaofikia hitimisho hilo wanapaswa kutoa na kuthibitisha lengo fulani kwa upande wa waandishi hawa kwa kutoa taarifa za uongo. Ni malengo gani yaliyoweza kuwasukuma? Je, wangeweza kutarajia kimantiki kupata utajiri, au umaarufu, au mamlaka, au faida yoyote ya kidunia? Umaskini wa marafiki wa Yesu, na kutopendwa kwa shujaa wao mwenyewe na viongozi wakuu wa dini wa Yudea, kunapinga wazo kama hilo; wakati ambapo ukweli kwamba alikufa kama mhalifu, mvunjifu wa amani, na kwamba hakufanywa kuwa na sifa yoyote, haukutoa tumaini la umaarufu wa kutamanika au faida ya kidunia kwa wale ambao wangejaribu kuanzisha tena mafundisho yake. Kinyume chake, kama hilo lingekuwa ndilo lengo la wale waliohubiri juu ya Yesu, je, wasingeacha haraka walipogundua kwamba lilileta aibu, mateso, kifungo, mapigo na hata mauti? Mantiki ya wazi inafundisha kwamba watu waliojitolea nyumba, sifa, heshima na maisha; ambao hawakuishi kwa ajili ya anasa za sasa; bali ambao lengo lao kuu lilikuwa ni kuwainua wanadamu wenzao, na ambao walisisitiza maadili ya hali ya juu kabisa, si tu kwamba walikuwa na lengo, bali zaidi kwamba lengo lao ni lazima lilikuwa safi na kusudi lao kuu lilikuwa tukufu mno. Mantiki inaendelea kutangaza kwamba ushuhuda wa watu kama hao, uliochochewa tu na malengo safi na mema, una thamani mara

kumi zaidi na unastahili kuzingatiwa zaidi kuliko ule wa waandishi wa kawaida. Wala watu hawa hawakuwa na ushupavu wa kidini usio na akili: walikuwa watu wenye akili timamu na ya kimantiki, na walitoa katika kila jambo sababu ya imani na tumaini lao; na walikuwa waaminifu kwa uvumilivu kwa misimamo hiyo ya kimantiki.

Na kile tumeona hapa kinatumika vivyo hivyo kwa waandishi mbalimbali wa Agano la Kale. Wao walikuwa, kwa ujumla, watu waliojulikana kwa uaminifu wao kwa Bwana; na historia hii inaandika na kukemea udhaifu na mapungufu yao bila upendeleo kama inavyosifu fadhila na uaminifu wao. Hili ni lazima liwashangaze wale wanaodhani Biblia ni historia iliyotungwa, iliyokusudiwa kuwatisha watu ili waheshimu mfumo wa kidini. Kuna unyoofu katika Biblia unaoithibitisha kuwa ni kweli. Watu waongo, wanaotamani kumwakilisha mtu kama mkuu, na hasa kama wanatamani kuwasilisha baadhi ya maandishi yake kama yaliyoongozwa na Mungu, bila shaka wangechora tabia ya mtu kama huyo kuwa isiyo na lawama na adhimu kwa kiwango cha juu kabisa. Ukweli ni kwamba mwenendo kama huo haujafuatwa katika Biblia ni ushahidi wa **kimantiki** kwamba haikutungwa kwa udanganyifu ili kudanganya.

Basi, kwa kuwa tuna sababu ya **kutarajia** ufunuo wa mapenzi na mpango wa Mungu, na kwa kuwa tumegundua kwamba Biblia, inayodai kuwa ndiyo ufunuo huo, iliandikwa na watu ambao hatuoni sababu ya kutilia shaka malengo yao, bali, kinyume chake, tunaona sababu ya kuyakubali, hebu tuchunguze tabia ya maandishi yanayodaiwa kuwa yamevuviwa, ili kuona kama mafundisho yake yanalingana na tabia ambayo **kimantiki** tumemhusisha nayo Mungu, na kama yana ushahidi wa ndani wa ukweli wake.

Vitabu vitano vya kwanza vya Agano Jipya na kadhaa vya Agano la Kale ni masimulizi au historia za matukio yaliyojulikana kwa waandishi na kuthibitishwa na tabia zao. Ni dhahiri kwa wote kwamba haikuhitaji ufunuo maalum ili tu kusema

ukweli kuhusu mambo ambayo walikuwa wanayafahamu kwa undani na kikamilifu. Hata hivyo, kwa kuwa Mungu alitamani kutoa ufunuo kwa wanadamu, ukweli kwamba historia hizi za matukio ya wakati huo zina uhusiano na ufunuo huo ungekuwa msingi tosha wa kufanya dhana iwe ya kimantiki, kwamba Mungu angesimamia, na kupanga, ili mwandishi mnyoofu aliyemchagua kwa kazi hiyo aweze kukutana na ukweli unaohitajika. Kuaminika kwa sehemu hizi za kihistoria za Biblia kunategemea karibu kabisa tabia na malengo ya waandishi wake. Watu wema hawatazungumza uongo. Chemchemi safi haitatoa maji machungu. Na ushuhuda wa pamoja wa maandishi haya unanyamazisha shaka yoyote kwamba waandishi wake wangesema au kufanya uovu, ili mema yafatie.

Haikubatilisha kwa vyovyote vile ukweli wa vitabu fulani vya Biblia, kama vile Wafalme, Mambo ya Nyakati, Waamuzi, n.k., tunaposema kwamba ni historia za kweli na zilizotunzwa kwa uangalifu za matukio na watu mashuhuri wa nyakati zao. Inapokumbukwa kwamba Maandiko ya Kiebrania yana historia, pamoja na sheria na unabii, na kwamba historia zao, nasaba, n.k., zilikuwa wazi zaidi katika kuelezea mazingira kwa sababu ya matarajio kwamba Masihi aliyeahidiwa angekuja katika ukoo maalum kutoka kwa Abrahamu, tunaona sababu ya kuandikwa kwa baadhi ya matukio ya historia yanayoonekana kuwa ya aibu kwa mtazamo wa karne hii ya ishirini. Kwa mfano, kumbukumbu wazi ya asili ya mataifa ya Wamoabi na Waamoni, na uhusiano wao na Abrahamu na Waisraeli, yawezekana ndiyo ilikuwa hitaji katika akili ya mwanahistoria kwa ajili ya historia kamili ya kuzaliwa kwao. (*Mwa. 19:36-38*) Vivyo hivyo, maelezo ya kina sana ya watoto wa Yuda yametolewa, ambaye kutoka kwake alitoka Daudi, Mfalme, ambaye kupitia yeye nasaba ya Mariamu, mama yake Yesu, pamoja na ile ya Yusufu, mumewe (*Luka 3:23,31,33,34; Mathayo. 1:2-16*), inarudi nyuma hadi kwa Abrahamu. Bila shaka umuhimu wa kuthibitisha ukoo kikamilifu ulikuwa muhimu zaidi, kwa kuwa kutoka katika kabila hili (*Mwa. 49:10*) ndipo angetoka Mfalme mtawala wa Israeli,

pamoja na Masihi aliyeahidiwa, na hivyo maelezo ya kina ambayo hayakutolewa katika visa vingine. *Mwa. 38*

Huenda kukawa na sababu zinazofanana au tofauti kwa matukio mengine ya kihistoria yaliyoandikwa katika Biblia, ambayo manufaa yake tunaweza kuyaona hapo baadaye; matukio ambayo, kama kitabu hiki kisingekuwa ni historia bali andiko la mafundisho ya maadili tu, yangeweza kuachwa bila athari yoyote; ingawa hakuna mtu anayeweza kusema kwa mantiki kwamba Biblia inaridhia uchafu mahali popote. Ni vizuri, zaidi ya hayo, kukumbuka kwamba matukio hayohayo yanaweza kuelezwa kwa ulaini zaidi au kidogo katika lugha yoyote; na kwamba wakati watafsiri wa Biblia walikuwa, kwa usahihi, waangalifu mno kutoacha kumbukumbu yoyote, bado waliishi katika zama zisizokuwa na umakini sana katika kuchagua maneno ya staha kuliko zama zetu; na vivyo hivyo inaweza kudhaniwa kuhusu nyakati za zamani za Biblia na tabia za usemi. Hakika, hata mchambuzi makini zaidi hawezi kupata kipingamizi chochote kuhusu jambo hili katika andiko lolote la Agano Jipya.

**Vitabu vya Musa na Sheria Zilizotangazwa Ndani Yake**

Vitabu vitano vya kwanza vya Biblia vinajulikana kama Vitabu Vitano vya Musa, ingawa havimtaji popote jina lake kama mwandishi wake. Kwamba viliandikwa na Musa, au chini ya usimamizi wake, ni hitimisho la kimantiki; huku maelezo ya kifo na maziko yake yakiongezwa ipasavyo na mwandishi wake. Kuachwa kwa taarifa ya wazi kwamba vitabu hivi viliandikwa na Musa si uthibitisho dhidi ya wazo hilo; kwa maana kama mtu mwingine angeviandika ili kudanganya na kufanya udanganyifu, hakika angedai kwamba viliandikwa na kiongozi mkuu na mtawala wa Israeli, ili kufanikisha udanganyifu wake. (Tazama Kum. 31:9-27.) Kuhusu jambo moja tuna hakika, Musa aliliongoza taifa la Kiebrania kutoka Misri. Aliwapanga kama taifa chini ya sheria zilizoelezwa katika vitabu hivi; na taifa la Kiebrania, kwa makubaliano ya pamoja, kwa zaidi ya miaka elfu

tatu, limedai vitabu hivi kama zawadi kwao kutoka kwa Musa, na limeviheshimu kiasi kwamba hata nukta moja au alama ndogo haipaswi kubadilishwa—hivyo kutoa uhakikisho wa usafi wa maandishi.

Maandishi haya ya Musa yana historia pekee ya kuaminika iliyopo, ya kipindi inayokielezea. Historia ya Kichina inadai kuanza na uumbaji, ikieleza jinsi Mungu alivyokwenda juu ya maji kwa mashua ndogo, na, akichukua donge la udongo mkononi mwake, akalitupa majini. Donge hilo la udongo, inadai, likawa ulimwengu huu, n.k. Lakini hadithi nzima haina mantiki kiasi kwamba hata mtoto mdogo mwenye akili asingedanganywa nayo. Kinyume chake, maelezo yaliyotolewa katika Mwanzo yanaanza na dhana ya kimantiki kwamba Mungu, Muumba, Chanzo cha Kwanza chenye akili, tayari alikuwepo. Hayazungumzii Mungu kuwa na mwanzo, bali kazi yake na mwanzo wake na maendeleo yake yenye utaratibu na mpangilio—"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi." Kisha, ikaruka asili ya dunia bila maelezo ya kina au ufafanuzi, simulizi ya siku [vipindi] sita za kuiandaa kwa ajili ya mwanadamu linaendelea. Maelezo hayo yanathibitishwa kwa kiasi kikubwa na nuru inayoongezeka ya sayansi kwa miaka elfu nne; hivyo ni jambo la kimantiki zaidi kukubali dai kwamba mwandishi wake, Musa, alivuviwa na Mungu, kuliko kudhani kwamba akili ya mtu mmoja ilikuwa bora kuliko akili na utafiti wa pamoja wa jamii nzima iliyobaki katika miaka elfu tatu tangu wakati huo, ikisaidiwa na zana za kisasa na mamilioni ya fedha.

Tazama sasa mfumo wa sheria uliowekwa katika maandishi haya. Hakika sheria hizo zilikuwa za pekee, iwe ni katika nyakati zao au tangu wakati huo, hadi karne hii ya ishirini; na sheria za karne hii zimejengwa juu ya kanuni zilizowekwa katika Sheria ya Musa, na zilitungwa kwa kiasi kikubwa na watu waliokiri kuwa Sheria ya Musa ina asili ya Kimungu.

Amri Kumi ni muhtasari mfupi wa sheria yote. Amri hizo Kumi zinaagiza kanuni za ibada na maadili ambazo ni lazima zimvutie

kila mwanafunzi; na kama zisingekuwa zimejulikana hapo awali, na sasa zikapatikana miongoni mwa magofu na masalio ya Ugiriki, au Roma, au Babeli (mataifa yaliyoibuka na kuanguka tena, muda mrefu tangu sheria hizo zilipotolewa), zingeonekana kuwa za ajabu kama si za kimiujiza. Lakini kuzizoea na madai yake kumeleta hali ya kutojali, kiasi kwamba ukuu wake halisi hauonekani isipokuwa na wachache. Ni kweli, amri hizo hazifundishi juu ya Kristo; lakini zilitolewa, si kwa Wakristo, bali kwa Waebrania; si kufundisha imani katika fidia, bali kuwasadikisha wanadamu juu ya hali yao ya dhambi, na hitaji la fidia. Na kiini cha amri hizo kilifupishwa kwa ustadi na mwanzilishi mashuhuri wa Ukristo, kwa maneno haya: *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote";* na *"Mpende jirani yako kama nafsi yako." Marko 12:30,31*

Serikali iliyoanzishwa na Musa ilikuwa tofauti na nyingine zote, za kale na za kisasa, kwa kuwa ilidai kuwa ni ya Muumba mwenyewe, na watu waliwajibika kwake; sheria na taasisi zao, za kiraia na za kidini, zilidaiwa kutoka kwa Mungu, na, kama tutakavyoona punde, zilikuwa katika uwiano kamili na kile ambacho mantiki inatufundisha kuwa ndiyo tabia ya Mungu. Maskani, katikati ya kambi, ilikuwa na dhihirisho la uwepo wa Yehova kama Mfalme wao katika chumba chake cha "Patakatifu pa Patakatifu," ambapo kwa njia za kimiujiza walipokea maagizo kwa ajili ya usimamizi mzuri wa mambo yao kama taifa. Utaratibu wa makuhani ulianzishwa, ambao ulikuwa na usimamizi kamili wa Maskani, na kupitia wao pekee ndiyo iliruhusiwa kumkaribia na kuwasiliana na Yehova. Wazo la kwanza la wengine katika jambo hili labda lingekuwa: "Ah! Hapo ndipo tunapopata lengo la mpangilio wao: kwao, kama ilivyo kwa mataifa mengine, makuhani waliwatawala watu, wakitumia udhaifu wao wa kuamini na kuamsha hofu zao kwa ajili ya heshima na faida yao wenyewe." Lakini subiri, rafiki; tusifanye haraka kudhania jambo lolote. Pale ambapo kuna fursa nzuri kama hii ya kulijaribu jambo hili kwa kutumia ukweli,

haitakuwa busara kufikia hitimisho bila ukweli. Ushahidi usioweza kukanushwa unapingana na dhana kama hizo. Haki na fursa za makuhani zilikuwa na mipaka; hawakupewa mamlaka yoyote ya kiraia, na walikosa kabisa fursa ya kutumia ofisi yao kuingilia haki au dhamiri za watu; na mpangilio huu ulifanywa na Musa, mwanachama wa ukoo wa kikuhani.

Kama mwakilishi wa Mungu katika kuwatoa Israeli kutoka utumwa wa Misri, nguvu ya mazingira ilikuwa imeweka serikali mikononi mwake, na kumfanya Musa mpole awe na mamlaka na nguvu kamili, ingawa kutokana na upole wa tabia yake alikuwa kwa kweli mtumishi aliyelemewa na kazi za watu, ambaye maisha yake yalikuwa yakimalizwa na majukumu mazito ya cheo chake. Katika wakati huu mgumu serikali ya kiraia ilianzishwa, ambayo kwa kweli ilikuwa ni demokrasia. Tusieleweke vibaya: Ikitazamwa kama wasioamini wangeiona, serikali ya Israeli ilikuwa ni demokrasia, lakini ikitazamwa katika nuru ya madai yake yenyewe, ilikuwa ni **Teokrasia, yaani, serikali ya kimungu**; kwa maana sheria zilizotolewa na Mungu, kupitia Musa, hazikuruhusu marekebisho yoyote: hawakupaswa kuongeza wala kupunguza chochote kutoka kwenye kanuni zao za sheria. Ikionekana hivi, Serikali ya Israeli ilikuwa tofauti na Serikali nyingine yoyote ya kiraia, iwe ya kabla au ya baada. *"BWANA akamwambia Musa, Nikusanyie watu sabini, miongoni mwa wazee wa Israeli, unaowajua kuwa ni wazee wa watu, na maakida juu yao; nawe uwalete hata hema ya kukutania, wasimame huko pamoja nawe. Nami nitashuka niseme nawe huko; nami nitatwaa sehemu ya roho iliyo juu yako na kuiweka juu yao; nao watachukua mzigo wa watu pamoja nawe, ili usiuchukue wewe peke yako."* (*Hesabu. 11:16,17.* Tazama pia mistari 24 hadi 30 kwa mfano wa utawala wa kweli usio na hila na upole.) Musa, akielezea jambo hili, anasema: *"Basi nikawatwaa wakuu wa kabila zenu, watu wenye hekima, wanaojulikana [wenye ushawishi], nikawaweka wawe vichwa juu yenu, maakida ya maelfu, na maakida ya mamia, na maakida ya hamsini, na maakida ya makumi, na maafisa katika kabila zenu." Kum. 1:15; Kut. 18:13-26*

Hivyo inaonekana kwamba mtoa-sheria huyu mashuhuri, badala ya kutafuta kuendeleza au kuongeza mamlaka yake mwenyewe kwa kuweka Serikali ya watu chini ya udhibiti wa ndugu zake wa karibu, wa kabila la kikuhani, ili kutumia mamlaka yao ya kidini kufunga haki na uhuru wa watu, kinyume chake aliwaanzishia watu aina ya Serikali iliyokusudiwa kukuza roho ya uhuru. Historia za mataifa mengine na watawala hazionyeshi mfano kama huu. Katika kila kisa, mtawala ameutafuta ukuu wake mwenyewe na mamlaka makubwa zaidi. Hata katika visa ambapo watu kama hao wamesaidia kuanzisha jamhuri, imeonekana kutokana na matukio ya baadaye kwamba walifanya hivyo kwa Sera, ili kupata upendeleo kwa watu, na kuendeleza mamlaka yao wenyewe. Akiwa katika mazingira kama ya Musa, mtu yeyote mwenye tamaa, anayeongozwa na Sera na anayejaribu kuendeleza udanganyifu kwa watu, angefanya kazi kwa ajili ya kuimarisha mamlaka zaidi kwake mwenyewe na familia yake; hasa kwa kuwa hili lingeonekana kuwa kazi rahisi kutokana na mamlaka ya kidini kuwa tayari katika kabila hilo, na kutokana na dai la taifa hili la kutawaliwa na Mungu, kutoka Maskani. Wala haiwezekani kudhani kwamba mtu mwenye uwezo wa kutunga sheria kama hizo, na wa kuwatawala watu kama hao, angekuwa mjinga kiasi cha kutokuona mwelekeo wa mwenendo wake ungekuwa upi. Watu walipewa mamlaka kamili ya kujitawala. Hii inadhihirika wazi kiasi kwamba, ingawa kulikuwa na agizo kuwa mashauri mazito ambayo viongozi wao walishindwa kuyaamua yalipaswa kupelekwa kwa Musa, bado viongozi hao hao ndio walikuwa waamuzi wa mwisho kuhusu ni shauri lipi hasa lilikuwa 'zito' kiasi cha kumfikia. Musa mwenyewe aliwapa mamlaka hayo aliposema: "*na neno lo lote litakalowashinda, nileteeni mimi, nami nitalisikia.*" —Kumbukumbu la Torati 1:17.

Ikionekana hivi, Israeli ilikuwa jamhuri ambayo maafisa wake walitenda kazi chini ya agizo la Mungu. Na kwa aibu ya wale wanaodai kwa ujinga kwamba Biblia inaidhinisha utawala wa kifalme juu ya watu, badala ya "Serikali ya watu kwa ajili ya

watu," ikumbukwe kwamba aina hii ya serikali ya kiraia ya kijamhuri iliendelea kwa zaidi ya miaka mia nne. Na kisha ilibadilishwa na kuwa ya Ufalme kwa ombi la "Wazee," bila idhini ya Bwana, aliyemwambia Samweli, aliyekuwa akihudumu wakati huo kama Rais asiye rasmi, "*Isikilize sauti ya watu hawa katika yote watakayokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, nisije nikawatawala*." Kwa agizo la Mungu, Samweli aliwaeleza watu jinsi haki na uhuru wao vitakavyopuuzwa, na jinsi watakavyokuwa watumishi kwa mabadiliko kama hayo; lakini walikuwa wamevutiwa na wazo maarufu, lililoonyeshwa pande zote kuwazunguka katika Mataifa mengine. (*1 Sam. 8:6-22*) Katika kuzingatia maelezo haya ya *tamaa* yao ya kuwa na Mfalme, ni nani asiyevutiwa na wazo kwamba Musa angeweza kujiimarisha kwa urahisi katika uongozi wa dola kuu bila shida?

Ingawa Israeli kwa ujumla ilikuwa taifa moja, lakini mgawanyiko wa kikabila daima ulitambuliwa baada ya kifo cha Yakobo. Kila familia, au kabila, kwa makubaliano ya pamoja, ilichagua au kutambua baadhi ya washiriki kama wawakilishi, au machifu wake. Desturi hii iliendelezwa hata katika utumwa wao mrefu nchini Misri. Hawa waliitwa machifu au wazee, na ni kwa hawa ndio Musa alikabidhi heshima na mamlaka ya Serikali ya kiraia; ambapo, kama angetaka kuimarisha mamlaka kwake mwenyewe na familia yake, hawa wangekuwa watu wa mwisho kuwapa heshima ya mamlaka na ofisi.

Maagizo yaliyotolewa kwa wale walioteuliwa katika utawala wa kiraia kama kutoka kwa Mungu ni mfano wa unyenyekevu na usafi. Musa anawatangazia watu, wakiwa wanasikia majaji hawa: "*ikawaagiza wakati ule waamuzi wenu, nikawaambia, Sikizeni ninyi maneno kati ya ndugu zenu, mkaamue kwa haki kati ya mtu na nduguye, na mgeni[Msafiri] aliye pamoja naye. Msitazame nafsi za watu katika hukumu; mwasikize wadogo na wakubwa sawasawa; msiche uso wa mtu awaye yote; kwa kuwa hukumu ni ya Mungu; na lile neno liwashindalo mniletee mimi, nami nitalisikiza.*." (*Kum. 1:16,17*) Kesi ngumu kama hizo, baada ya kifo cha Musa,

zilipelekwa moja kwa moja kwa Bwana kupitia Kuhani Mkuu, jibu likiwa Ndiyo au Hapana, kwa Urimu na Thumimu.

Kwa kuzingatia *ukweli* huu, tuseme nini kuhusu nadharia inayopendekeza kwamba vitabu hivi viliandikwa na makuhani waongo ili kujipatia ushawishi na mamlaka juu ya watu? Je, watu kama hao, kwa lengo kama hilo, wangetunga kumbukumbu zinazoharibu malengo yale yale waliyotaka kuyaendeleza—kumbukumbu zinazothibitisha pasipo shaka kwamba Kiongozi mkuu wa Israeli, na mmoja wa kabila lao wenyewe, kwa agizo la Mungu, aliwatenga makuhani na mamlaka ya kiraia kwa kuweka mamlaka hayo mikononi mwa watu? Je, kuna yeyote anayeona hitimisho kama hilo kuwa la kimantiki?

Tena, ni jambo la kuzingatia kwamba sheria za ustaarabu uliopiga hatua zaidi, katika karne hii ya ishirini, hazijaweka utaratibu makini zaidi wa kuhakikisha kuwa tajiri na maskini wanakuwa katika daraja moja la uwajibikaji mbele ya sheria za nchi. Sheria za Musa hazikuweka ubaguzi wa aina yoyote ile. Na kuhusu kuwalinda watu dhidi ya hatari zinazotokana na wengine kuwa maskini sana na wengine kuwa matajiri na wenye nguvu kupita kiasi, hakuna sheria nyingine ya kitaifa iliyowahi kutungwa ambayo ililinda jambo hili kwa uangalifu kama hiyo. Sheria ya Musa iliandaa marejesho kila mwaka wa hamsini—mwaka wao wa Yubile. Sheria hii, kwa kuzuia uuzaji wa kudumu wa mali, hivyo ilizuia mkusanyiko wake mikononi mwa wachache. (Law. 25:9,13-23,27-30) Kwa hakika, walifundishwa kujiona kama ndugu, na kutenda ipasavyo; kusaidiana bila malipo, na kutochukuliana riba. Tazama Kut. 22:25; Law. 25:36,37; Hes. 26:52-56.

Sheria zote ziliwekwa wazi kwa umma, hivyo kuzuia watu wenye nia mbaya kufanikiwa kuchezea haki za watu. Sheria ziliwekwa wazi kwa namna ambayo yeyote aliyetaka angeweza kuzinakili; na, ili maskini zaidi na wasiojua kusoma na kuandika wasiwe wajinga kuzihusu, lilifanywa kuwa jukumu la makuhani kuwasomea watu katika sikukuu zao za kila baada ya miaka

saba. (Kum. 31:10-13) Je, ni jambo la kimantiki kudhani kwamba Sheria na mipango kama hiyo ilibuniwa na watu wabaya, au na watu waliopanga njama za kuwanyang'anya watu uhuru na furaha yao? Dhana kama hiyo haingekuwa ya kimantiki.

Katika kuheshimu haki na maslahi ya wageni, na ya maadui, Sheria ya Musa ilikuwa mbele ya nyakati zake kwa karne thelathini na mbili—kama siyo kwamba sheria za nchi zilizoendelea zaidi za leo zinafikia usawa na wema wake. Tunasoma:

> *"Mtakuwa na sheria moja tu, kwa huyo aliye mgeni[Msafiri], na kwa mzalia; kwa kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu." Kut. 12:49; Law. 24:22*
>
> *"Mgeni akaaye pamoja nawe atakuwa kama mzalia kwenu; mpende kama nafsi yako; kwa maana ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri; Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu. Msifanye yasiyo haki katika hukumu, wala katika kupima, wala katika mizani, wala katika cheo.." Law 19:33,34*
>
> *"wala usimpendelee mtu mnyonge katika neno lake. Ukimwona ng'ombe wa adui wako, au punda wake, amepotea, sharti umrudishie mwenyewe tena." Kut. 23:4,5*

Hata wanyama wasio na uwezo wa kusema hawakusahaulika. Ukatili kwa hawa pamoja na kwa wanadamu ulikatazwa vikali. Ng'ombe hakupaswa kufungwa mdomo anapopura nafaka; kwa sababu nzuri kwamba mfanyakazi yeyote anastahili chakula chake. Hata ng'ombe na punda hawakupaswa kulima pamoja, kwa sababu hawalingani kwa nguvu na hatua: ingekuwa ni ukatili. Mapumziko yao pia yaliandaliwa. *Kum. 25:4; 22:10; Kut. 23:12*

Ukuhani unaweza kudaiwa na wengine kuwa ulikuwa taasisi ya ubinafsi, kwa sababu kabila la Lawi lilitegemezwa na zaka, au fungu la kumi la kila mwaka, la mazao ya ndugu zao wa makabila mengine. Ukweli huu, ukielezwa hivi, ni uwasilishaji usio wa haki unaofanywa mara nyingi na wenye mashaka, ambao, yawezekana kwa ujinga, wanapotosha mojawapo ya ushahidi wa ajabu zaidi wa sehemu ya Mungu katika uanzishwaji wa

mfumo huo, na kwamba haikuwa kazi ya ukuhani wa ubinafsi na wenye hila. Hakika, mara nyingi huwakilishwa vibaya na ukuhani wa kisasa, unaohimiza mfumo kama huo sasa, wakitumia huo kama kielelezo, bila kutaja hali ya mambo ambayo ulijengwa juu yake, au njia yake ya malipo.

Kwa kweli, ulijengwa juu ya usawa mkali zaidi. Waisraeli walipomiliki nchi ya Kanaani, Walawi hakika walikuwa na haki sawa ya kupata sehemu ya nchi kama makabila mengine; lakini, kwa amri ya wazi ya Mungu, hawakupata chochote, isipokuwa miji au vijiji fulani vya makazi, vilivyotawanyika miongoni mwa makabila mbalimbali, ambayo walipaswa kuwahudumia katika mambo ya kidini. Marufuku hii imetolewa mara tisa, kabla ya mgawanyo wa ardhi. Badala ya kupewa aridhi, hakika walipaswa kuandaliwa kitu kingine sawa na hicho, hakika kwa hiyo zaka ilikuwa ndiyo riziki hii ya kimantiki na ya haki. Wala si hayo tu: zaka, ingawa, kama tulivyoona, ni deni la haki, haikulazimishwa kama kodi, bali ilipaswa kulipwa kama mchango wa hiari. Na hakuna tishio lililowafunga kutoa michango hiyo: yote yalitegemea dhamiri zao. Maonyo pekee kwa watu juu ya somo hili ni kama yafuatayo:

> *"Jilinde nafsi yako usimwache Mlawi siku zote uishizo katika nchi yako." (Kum. 12:19) "na Mlawi aliye ndani ya malango yako usimwache, kwani hana fungu wala urithi pamoja nawe." [katika nchi]. Kum. 14:27*

Tunauliza, je, ni jambo la kimantiki kudhani kwamba utaratibu huu wa mambo ungepangwa hivi na makuhani wa ubinafsi na wenye tamaa?—mpango wa kujinyima urithi wao wenyewe na kuwafanya wategemee ndugu zao kwa ajili ya riziki? Je, mantiki haitufundishi kinyume chake?

Kwa kupatana na hili, na isiyoelezeka kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kwa misingi inayodaiwa—kwamba Mungu ndiye mwandishi wa sheria hizo—ni ukweli kwamba hakuna mpango maalum uliowekwa kwa ajili ya kuwaheshimu makuhani. Katika jambo lolote, wadanganyifu wangekuwa waangalifu zaidi

kujipatia heshima na staha, na adhabu kali zaidi na laana kwa wale waliowatendea vibaya. Lakini hakuna kitu cha namna hiyo kinachoonekana: hakuna heshima maalum, au staha, au kinga dhidi ya unyanyasaji au matusi, iliyoandaliwa. Sheria ya kawaida, ambayo haikufanya tofauti kati ya matabaka, na haikupendelea watu, ndiyo ilikuwa ulinzi wao pekee. Hili ni la ajabu zaidi kwa sababu utunzaji wa watumishi, na wageni, na wazee, ulikuwa mada ya Sheria maalum. Kwa mfano: Usimdhulumu wala kumwonea *mgeni, au mjane, au yatima*; kwa maana wakinililia mimi [Mungu] hata kidogo, hakika nitasikia kilio chao; na hasira yangu itawaka, nami nitawaua ninyi kwa upanga, na wake zenu watakuwa wajane na watoto wenu mayatima. (*Kut. 22:21-24; 23:9; Law. 19:33,34*) *"Usimwonee mtumishi aliyeajiriwa* aliye maskini na mhitaji, awe wa ndugu zako, au wa wageni walio katika nchi yako, ndani ya malango yako. Siku yake utampa mshahara wake, wala jua lisichwe juu yake, kwa maana yeye ni maskini, na ameweka moyo wake juu yake; asije akamlilia Bwana juu yako na ikawa dhambi kwako." (*Law. 19:13; Kum. 24:14,15; Kut. 21:26,27*) *"wondokeeni mtu mwenye mvi; heshimuni uso wa mtu mzee; nawe mche Mungu wako, Mimi ndimi Bwana."* (*Law. 19:32.* Tazama pia *Law. 19:14*.) Yote haya, lakini hakuna kitu maalum kwa Makuhani, au Walawi, au zaka zao.

Mipangilio ya usafi ya sheria, iliyokuwa muhimu sana kwa watu masikini na waliokandamizwa kwa muda mrefu, pamoja na mipango na vikwazo kuhusu wanyama safi na wasio safi ambao wangeweza kuliwa au la, ni ya ajabu, na, pamoja na sifa nyingine, ingekuwa ya kuvutia kama nafasi ingeruhusu uchunguzi wake, kama inavyoonyesha Sheria hiyo ilikuwa sambamba na, kama si mbele ya, hitimisho la hivi karibuni la sayansi ya matibabu juu ya somo hilo. Sheria ya Musa pia ilikuwa na tabia ya mfano, ambayo ni lazima tuiache kwa ajili ya kuzingatiwa wakati ujao; lakini hata mtazamo wetu wa haraka umetoa ushahidi mwingi kwamba Sheria hii, ambayo inaunda mfumo wenyewe wa dini yote iliyofunuliwa, ambayo sehemu iliyobaki ya Biblia

inaifafanua, kwa kweli ni onyesho la ajabu la hekima na haki, hasa wakati tarehe yake inapozingatiwa.

Katika nuru ya Mantiki, wote ni lazima wakubali kwamba haina ushahidi wa kuwa ni kazi ya watu waovu, wenye hila, bali kwamba inalingana kikamilifu na kile ambacho maumbile yanafundisha kuwa ndiyo tabia ya Mungu. Inatoa ushahidi wa Hekima, Haki na Upendo wake. Na zaidi ya hayo, Musa, yule mtoa sheria ambaye dhahiri alikuwa mcha Mungu na mwenye heshima, anakana kuwa sheria hizo zilikuwa zake mwenyewe, na badala yake anazinasibisha kwa Mungu. (*Kut. 24:12; Kum. 9:9-11; Kut. 26:30; Law. 1:1*) Kwa kuzingatia tabia yake ya jumla, na amri zake kwa watu za kutoshuhudia uongo, na kuepuka unafiki na uongo, je, ni jambo la kimantiki kudhani kwamba mtu kama huyo alitoa ushahidi wa uongo na kuwasilisha maoni na sheria zake mwenyewe kama za Mungu? Ikumbukwe pia kwamba tunachunguza nakala za sasa za Biblia, na kwamba kwa hiyo uadilifu ambao unajulikana sana unawahusu vivyo hivyo warithi wa Musa; kwa maana ingawa watu wabaya walikuwa miongoni mwa warithi hao, ambao walitafuta mambo yao wenyewe na si mema ya watu, ni dhahiri kwamba hawakuchezea Maandiko Matakatifu, ambayo ni safi hadi leo.

### Manabii wa Biblia

Hebu sasa tuangalie tabia ya jumla ya manabii wa Biblia na shuhuda zao. Ukweli wa kushangaza ni kwamba manabii, isipokuwa wachache, hawakuwa wa tabaka la kikuhani; na kwamba katika siku zao unabii wao kwa ujumla ulikuwa wa kuchukiza kwa ukuhani uliokuwa ukidhoofika na kutafuta maslahi, na pia kwa watu waliokuwa na mwelekeo wa kuabudu sanamu. Ujumbe wao mkuu kutoka kwa Mungu kwenda kwa watu kwa ujumla ulikuwa ni karipio kwa ajili ya dhambi, pamoja na maonyo ya adhabu zilizokuwa zinakuja, ambapo ndani yake tunapata ahadi za mara kwa mara za baraka za wakati ujao, baada ya wao kusafishwa dhambi na kurudi katika upendeleo wa Bwana. Maisha yao, kwa sehemu kubwa, hayakuwa ya

kutamanika: kwa ujumla walitukanwa, wengi wao wakifungwa na kuuawa kikatili. Tazama *1 Wafalme 18:4,10,17,18; 19:10; Yer. 38:6; Ebr. 11:32-38.* Katika visa vingine ilipita miaka mingi baada ya vifo vyao kabla ya tabia yao ya kweli kama manabii wa Mungu kutambuliwa. Lakini tunazungumza hivi kuhusu waandishi wa kinabii ambao matamshi yao yanadai kuwa ni uvuvio wa moja kwa moja wa Yehova. Ni vema katika muktadha huu tukumbuke kwamba katika utoaji wa sheria kwa Israeli hapakuwa na uingiliaji wa kikuhani: ilitolewa na Mungu kwa watu kwa mkono wa Musa. (*Kut. 19:17-25; Kum. 5:1-5*) Na, zaidi ya hayo, lilifanywa kuwa jukumu la kila mtu aliyemwona mwingine akivunja sheria kumkemea mtenda dhambi. (*Law. 19:17*) Hivyo wote walikuwa na mamlaka ya kufundisha na kukemea; lakini kwa kuwa, kama ilivyo katika siku zetu, wengi walikuwa wamezama katika shughuli za biashara, na wakawa hawajali na wasio na dini, wachache ndio walitimiza agizo hili kwa kukemea dhambi na kuhimiza uchaji wa Mungu; na wahubiri hawa wanaitwa "manabii" katika Agano la Kale na Jipya. Neno nabii, kama linavyotumika kwa ujumla, linamaanisha **mwelezaji wa hadharani(public expaunder)**, na walimu wa hadharani wa ibada ya sanamu pia waliitwa hivyo; kwa mfano, "manabii wa Baali," n.k. Tazama *1 Kor. 14:1-6; 2 Pet. 2:1; Mt. 7:15; 14:5; Neh. 6:7; 1 Wafalme 18:40; Tito 1:12.*

Kutoa unabii, kwa maana ya kawaida ya kufundisha, baadaye kulijulikana sana miongoni mwa kundi fulani, na kukaporomoka na kuwa Ufarisayo—kufundisha, badala ya amri za Mungu, mapokeo ya wazee, na hivyo kuipinga kweli na kuwa manabii wa uongo, au walimu wa uongo. *Mt. 15:2-9*

Kutoka katika kundi kubwa lililoitwa manabii, Yehova kwa nyakati mbalimbali aliwachagua baadhi ambao aliwapa utume maalum wa kupeleka ujumbe, wakati mwingine ukihusu mambo ya wakati huo, na nyakati nyingine matukio ya baadaye. Ni kwa maandishi ya kundi hili, walionena na kuandika kama

walivyoongozwa na Roho mtakatifu, ndiyo tunayazingatia sasa. Wanaweza kuitwa kwa usahihi

**Manabii Waliotumwa na Mungu au Waonaji.**

Inapokumbukwa kwamba manabii hawa walikuwa hasa watu wa kawaida, wasiopokea msaada kutoka kwa zaka za kabila la kikuhani, na, kwa kuongezea hili, ni ukweli kwamba mara nyingi hawakuwa tu wakemeaji wa wafalme na waamuzi, bali pia wa makuhani (ingawa hawakukemea ofisi, bali dhambi za kibinafsi za watu walioishika), inakuwa dhahiri kwamba hatuwezi kuamua kimantiki kwamba manabii hawa walikuwa washirika katika muungano wowote wa makuhani, au wengine, wa kutunga uongo kwa jina la Mungu. Akili katika nuru ya ukweli inapingana na shaka kama hiyo.

Basi, ikiwa hatupati sababu ya kutilia shaka malengo ya waandishi mbalimbali wa Biblia, bali tunaona kwamba roho ya sehemu zake mbalimbali ni haki na kweli, hebu sasa tuendelee kuuliza kama kuna uhusiano wowote, au kifungo cha umoja, kati ya maandishi ya Musa, yale ya manabii wengine, na yale ya waandishi wa Agano Jipya. Kama tutapata mstari mmoja wa pamoja wa fikra uliofumwa katika Sheria yote na Manabii na maandishi ya Agano Jipya, yanayohusu kipindi cha miaka elfu moja na mia tano, hili, likichukuliwa pamoja na tabia ya waandishi, Itakuwa sababu nzuri ya kukubali dai lao—kwamba wamevuviwa na Mungu—hasa kama mada kuu kwa wote ni kuu na tukufu, inayopatana vizuri na kile ambacho akili timamu iliyotakaswa inafundisha kuhusu tabia na sifa za Mungu.

Hili ndilo tunalolipata: Mpango mmoja, roho moja, lengo moja na kusudi moja ndivyo vinavyotawala kitabu chote. Kurasa zake za mwanzo zinaandika uumbaji na anguko la mwanadamu; kurasa zake za mwisho zinaeleza urejesho wa mwanadamu kutoka katika anguko hilo; na kurasa zake za katikati zinaonyesha hatua zinazofuatana za mpango wa Mungu wa kutimiza kusudi hili. Uwiano, lakini pia utofauti, wa sura tatu za kwanza na tatu za

mwisho za Biblia unashangaza. Moja inaelezea uumbaji wa kwanza, nyingine uumbaji uliofanywa upya au kurejeshwa, huku dhambi na laana yake ya adhabu zikiwa zimeondolewa; moja inaonyesha Shetani na uovu vikiingia ulimwenguni ili kudanganya na kuharibu, nyingine inaonyesha kazi yake ikibatilishwa, walioharibiwa wakirejeshwa, uovu ukitokomezwa na Shetani akiharibiwa; moja inaonyesha mamlaka yaliyopotea na Adamu, nyingine inaonyesha yakirejeshwa na kuimarishwa milele na Kristo, na mapenzi ya Mungu yakifanyika duniani kama mbinguni; moja inaonyesha dhambi ikiwa ndiyo chanzo cha uharibifu, aibu na Mauti, nyingine inaonyesha thawabu ya haki kuwa ni utukufu, heshima na uzima.

Ingawa imeandikwa na waandishi wengi, kwa nyakati mbalimbali, chini ya mazingira tofauti, Biblia si mkusanyiko tu wa maagizo ya kimaadili, methali za hekima na maneno ya faraja. Ni zaidi ya hayo: ni maelezo ya kimantiki, ya kifalsafa na yenye uwiano ya vyanzo vya uovu wa sasa ulimwenguni, suluhisho lake pekee na matokeo ya mwisho kama yanavyoonekana na hekima ya Mungu, iliyouona mwisho wa mpango tangu kabla ya mwanzo wake, ikionyesha pia njia ya watu wa Mungu, na kuwategemeza na kuwaimarisha kwa ahadi kuu mno na za thamani zitakazotimizwa kwa wakati wake.

Fundisho la Mwanzo, kwamba mwanadamu alijaribiwa katika hali ya ukamilifu wa asili katika mwakilishi mmoja, kwamba alishindwa, na kwamba hali ya sasa ya kutokamilika, magonjwa na Mauti ni matokeo yake, lakini kwamba Mungu hajamwacha, na hatimaye atamkomboa kupitia mkombozi, aliyezaliwa na mwanamke (*Mwa. 3:15*), linaendelezwa na kufafanuliwa katika maandiko yote. Umuhimu wa kifo cha mkombozi kama dhabihu kwa ajili ya dhambi, na wa haki yake kama kifuniko cha dhambi zetu, unaonyeshwa katika mavazi ya ngozi kwa Adamu na Hawa; katika kukubaliwa kwa dhabihu za Abeli; katika Isaka juu ya madhabahu; katika vifo vya dhabihu mbalimbali ambazo kupitia hizo mababu walimkaribia Mungu, na za zile

zilizoanzishwa chini ya Sheria na kuendelezwa katika kipindi chote cha Kiyahudi. Manabii, ingawa wanaaminika kuelewa kidogo tu umuhimu wa baadhi ya matamshi yao (*1 Pet. 1:12*), wanataja kuwekwa kwa dhambi juu ya mtu badala ya mnyama asiye na akili, na katika njozi ya kinabii wanamwona yeye atakayekomboa na kuokoa jamii akiongozwa "kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni," kwamba "adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake," na kwamba "kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Walimwonyesha kama "aliyedharauliwa na kukataliwa na watu, mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko," na walitangaza kwamba "BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote." (*Isa. 53:3-6*) Walitaja mahali ambapo mkombozi huyu angezaliwa (*Mika 5:2*), na wakati ambapo angekufa, wakituhakikishia kwamba itakuwa "si kwa ajili yake mwenyewe." (*Dan. 9:26*) Wanataja sifa zake mbalimbali za kipekee—kwamba atakuwa 'mwenye haki,' asiye na 'udanganyifu' wala 'udhalimu,' na pasipo sababu yoyote ya haki ya kumpatia hukumu ya kifo.(*Isa. 53:8,9,11*); kwamba atasalitiwa kwa vipande thelathini vya fedha (*Zek. 11:12*); kwamba atahesabiwa pamoja na wakosaji katika kifo chake (*Isa. 53:12*); kwamba hakuna mfupa wake hata mmoja utakaovunjwa (*Zab. 34:20; Yoh. 19:36*); na kwamba ingawa angekufa na kuzikwa, mwili wake haungeharibika, wala asingebaki kaburini. *Zab. 16:10; Mdo. 2:31*

Waandishi wa Agano Jipya kwa uwazi na kwa nguvu, lakini kwa unyenyekevu, wanaandika utimilifu wa utabiri huu wote katika Yesu wa Nazareti, na kwa hoja za kimantiki wanaonyesha kwamba ***bei ya ukombozi*** kama ile aliyoitoa ilikuwa muhimu, kama ilivyotabiriwa tayari katika Sheria na Manabii, kabla ya dhambi za ulimwengu kuweza kufutwa. (*Isa. 1:18*) Wanaeleza mpango mzima kwa njia yenye mantiki na nguvu ya ushawishi. Hawalengi hisia za upendeleo wala mihemko ya wasikilizaji wao, bali wanazungumza na akili zao zilizopata nuru pekee. Kwa kufanya hivyo, wanawasilisha moja ya michanganuo yenye mantiki thabiti na mshikamano wa karibu zaidi kuwahi

kupatikana kuhusu mada yoyote.Tazama Warumi 5:17-19, na kuendelea hadi sura ya 12.

Musa, katika Sheria, hakuonyesha tu dhabihu, bali pia kufutwa kwa dhambi na kubarikiwa kwa watu chini ya mkombozi huyu mkuu, ambaye anatangaza kwamba nguvu na mamlaka yake vitazidi sana vyake mwenyewe, ingawa vitakuwa "kama" vyake. (*Kum. 18:15,19*) Mkombozi aliyeahidiwa atabariki si tu Israeli, bali kupitia Israeli "jamaa zote za dunia." (*Mwa. 12:3; 18:18; 22:18; 26:4*) Na licha ya hisia za upendeleo za watu wa Kiyahudi kinyume chake, manabii wanaendeleza mada hiyohiyo, wakitangaza kwamba Masihi atakuwa pia "nuru ya kuwaangazia Mataifa" (*Isa. 49:6; Luka 2:32*); kwamba Mataifa watamjia "kutoka miisho ya dunia" (*Yer. 16:19*); kwamba jina lake "litakuwa kuu kati ya Mataifa" (*Mal. 1:11*); na kwamba "utukufu wa BWANA utafunuliwa na wote wenye mwili watauona pamoja." *Isa. 40:5*. Tazama pia *Isa. 42:1-7.*

Waandishi wa Agano Jipya wanadai upako wa kimungu uliowawezesha kutambua utimilifu wa unabii kuhusu dhabihu ya Kristo. Wao, ingawa walikuwa na upendeleo kama Wayahudi wa kufikiria kila baraka kuwa ni kwa ajili ya watu wao pekee (*Mdo. 11:1-18*), waliwezeshwa kuona kwamba ingawa taifa lao lingebarikiwa, jamaa zote za dunia zingebarikiwa pia, pamoja nao na kupitia wao. Waliona pia kwamba, kabla ya kubarikiwa kwa Israeli au ulimwengu, uteuzi ungefanywa wa "*kundi dogo*" kutoka kwa Wayahudi na Wamataifa, ambao, wakijaribiwa, wangeonekana kuwa wanastahili kufanywa warithi-pamoja wa utukufu na heshima ya Mkombozi Mkuu, na washiriki pamoja naye wa heshima ya kubariki Israeli na mataifa yote. *Rum. 8:17*

Waandishi hawa wanaonyesha uwiano wa mtazamo huu na yale yaliyoandikwa katika Sheria na Manabii; na ukuu na upana wa mpango wanaouwasilisha unazidi hata dhana kuu zaidi ya kile unachodai kuwa—"*Habari njema ya furaha kuu, itakayokuwa kwa watu wote.*"

Wazo la Masihi kama mtawala si tu wa Israeli, bali pia wa ulimwengu, lililodokezwa katika vitabu vya Musa, ndiyo mada kuu ya manabii wote. Wazo la Ufalme lilikuwa kuu pia katika mafundisho ya mitume; na Yesu alifundisha kwamba tunapaswa kuomba, *"Ufalme wako uje,"* na akawaahidi sehemu katika Ufalme huo wale ambao kwanza wangeteseka kwa ajili ya kweli, na hivyo kujithibitisha kuwa wanastahili.

Tumaini hili la Ufalme mtukufu ujao liliwapa waaminifu wote ujasiri wa kustahimili mateso na kuvumilia shutuma, kunyimwa na kupoteza, hata hadi kifo. Na katika unabii mkuu wa mifano unaofunga Agano Jipya, "*Mwana-Kondoo aliyechinjwa*" anayestahili (*Ufu. 5:12*), "washindi" wanaostahili ambao atawafanya wafalme na makuhani katika Ufalme wake, na majaribu na vikwazo ambavyo ni lazima wavishinde ili wastahili kushiriki ufalme huo, yote yamechorwa kwa uaminifu. Kisha yanaonyeshwa maonyesho ya mfano ya baraka zitakazoupata ulimwengu chini ya utawala huo wa Milenia, wakati Shetani atakapofungwa na Mauti ya Adamu na huzuni vikafutwa, na wakati mataifa yote ya dunia yatakapotembea katika nuru ya Ufalme wa mbinguni—*Yerusalemu mpya*.

Biblia, tangu mwanzo hadi mwisho, inashikilia fundisho lisilopatikana mahali pengine popote, na linalopingana na nadharia za dini zote za kipagani—kwamba maisha yajayo kwa ajili ya wafu yatakuja kupitia UFUFUO WA WAFU. Waandishi wote walioongozwa na Mungu walieleza imani yao kwa mkombozi, na mmoja anatangaza kwamba "asubuhi," Mungu atakapowaita kutoka kaburini, nao watatoka, waovu hawatashika tena utawala wa dunia; kwa maana "Wanyofu watawatawala, asubuhi." (*Zab. 49:14*) Ufufuo wa wafu unafundishwa na manabii; na waandishi wa Agano Jipya wanajenga matumaini yao yote ya maisha yajayo na baraka juu yake. Paulo anaeleza hivi: *"Maana, kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuliwa; na kama Kristo hakufufuliwa, imani yenu ni bure;...nao walalao katika Kristo wamepotea. Lakini sasa Kristo amefufuliwa katika wafu, limbuko lao*

*waliolala;...kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, vivyo hivyo katika Kristo wote watahuishwa." 1 Kor. 15:13-22*

Kama saa, ambayo gurudumu zake nyingi mwanzoni zinaweza kuonekana kuwa si za lazima, lakini ambazo gurudumu zake zinazozunguka polepole zaidi ni muhimu, ndivyo ilivyo Biblia, iliyoundwa na sehemu nyingi, na iliyoandaliwa na waandishi wengi, ni kitu kimoja kamili na chenye uwiano. Hakuna sehemu hata moja isiyo ya lazima, na ingawa sehemu zingine zinachukua nafasi ya kazi zaidi na maarufu kuliko zingine, zote ni muhimu na za lazima. Imekuwa maarufu miongoni mwa wale wanaojiita "wenye fikra za juu" na "wanatheolojia wakuu" wa siku hizi kuyachukulia kirahisi, au kuyapuuza kama si kuyakana, mengi ya "miujiza" ya Agano la Kale, wakiyaita "hadithi za kizee." Miongoni mwa haya ni maelezo ya Yona na samaki mkubwa, Nuhu na safina, Hawa na nyoka, kusimama kwa jua kwa amri ya Yoshua, na punda anayezungumza wa Balaamu. Inaonekana watu hawa wenye hekima wanapuuza ukweli kwamba Biblia imefumwa na kuunganishwa sana katika sehemu zake mbalimbali kiasi kwamba kuiondoa miujiza hii, au kutoiamini, ni kuiharibu au kutoiamini yote. Kwa maana kama maelezo ya asili ni ya uongo, wale walioyarudia walikuwa waongo au walaghai, na katika hali yoyote ile, isingewezekana kwetu kukubali ushuhuda wao kama uliovuviwa na Mungu. Kuondoa katika Biblia miujiza iliyotajwa kungebatilisha ushuhuda wa waandishi wake wakuu, mbali na ule wa Bwana wetu Yesu. Hadithi ya anguko inathibitishwa na Paulo (*Rum. 5:17*); pia kudanganywa kwa Hawa na nyoka (*2 Kor. 11:3; 1 Tim. 2:14*). Tazama pia rejea ya Bwana wetu kwa hili la mwisho katika *Ufu. 12:9* na *20:2*. Tukio la kusimama kwa jua wakati wa kuangamizwa kwa Waamori, likiwa kama ushahidi wa uweza wa Bwana, lilikuwa dhahiri ni kivuli cha uweza utakaodhihirishwa hapo baadaye, katika 'siku ya Bwana,' mikononi mwa yule ambaye Yoshua alikuwa mfano wake. Hili linathibitishwa na manabii watatu. (*Isa. 28:21; Hab. 2:1-3,13,14* na *3:2-11; Zek. 14:1,6,7*) Maelezo ya punda anayezungumza yanathibitishwa na Yuda (mstari wa 11), na Petro (*2 Pet. 2:16*). Na

mwalimu mkuu, Yesu, anathibitisha masimulizi ya Yona na samaki mkubwa na ya Nuhu na gharika. (*Mt. 12:40; 24:38,39; Luka 17:26.* Tazama pia *1 Pet. 3:20.*) Kwa kweli hii si miujiza mikuu kuliko ile iliyofanywa na Yesu na mitume, kama vile kugeuza maji kuwa divai, kuponya magonjwa, n.k.; na kama muujiza, kuamka kwa wafu ndio wa ajabu zaidi ya yote.

Miujiza hii, isiyo ya kawaida katika maisha yetu, inapata mifano inayofanana nayo karibu nasi kila siku, ambayo, kwa kuwa ya kawaida zaidi, inapita bila kutambuliwa. Uzazi wa viumbe hai, iwe wanyama au mimea, ni *zaidi ya ufahamu wetu*, na pia zaidi ya uwezo wetu—hivyo ni muujiza. Tunaweza kuona utendaji wa kanuni ya uhai, lakini hatuwezi kuielewa wala kuizalisha. Tunapanda mbegu mbili kando kando; hali, hewa, maji, na udongo, ni sawa; *zinakua*, hatuwezi kusema jinsi gani, wala mwanafalsafa mwenye hekima zaidi hawezi kuelezea muujiza huu. Mbegu hizi zinakuza viumbe vyenye mwelekeo tofauti; moja inatambaa, nyingine inasimama wima; umbo, ua, rangi, kila kitu kinatofautiana, ingawa hali zilikuwa sawa. Miujiza kama hiyo inakuwa ya kawaida kwetu, nasi tunaacha kuikumbuka kama miujiza tunapoacha mshangao wa utotoni; lakini inadhihirisha nguvu iliyo zaidi yetu, na zaidi ya akili yetu yenye mipaka, kama vile miujiza michache iliyoandikwa katika Biblia kwa makusudi maalum, na kama vielelezo vilivyokusudiwa vya uweza usio na kikomo, na vya uwezo wa Muumba mkuu kushinda kila kikwazo na kutimiza mapenzi yake yote, hata hadi ufufuo wetu ulioahidiwa kutoka kwa wafu, kutokomezwa kwa uovu, na utawala wa mwisho wa haki ya milele.

Hapa tunahitimisha hoja yetu. Kila hatua imejaribiwa kwa Mantiki. Tumegundua kwamba Mungu yupo, Muumbaji mkuu, mwenye akili, ambaye ndani yake hekima, haki, upendo na nguvu vinapatikana katika uwiano mkamilifu. Tumegundua kuwa ni jambo la kimantiki kutarajia ufunuo wa mipango yake kwa viumbe vyake vyenye uwezo wa kuithamini na kuwa na shauku nayo. Tumeiona Biblia, inayodai kuwa ndiyo ufunuo

huo, kuwa inastahili kuzingatiwa. Tumewachunguza waandishi wake, na malengo yao yanayowezekana, katika nuru ya yale waliyoyafundisha; tumestaajabu; na *akili* yetu imetuambia kwamba hekima kama hiyo, ikiunganishwa na usafi kama huo wa lengo, haikuwa hila ya ujanja ya watu wenye hila kwa ajili ya malengo ya ubinafsi. Mantiki imesisitiza kwamba ni rahisi zaidi kuamini kwamba hisia na sheria za haki na wema kama hizo ni lazima ziwe za Mungu na si za wanadamu, na imesisitiza kwamba haziwezi kuwa kazi ya makuhani waongo. Tumeona uwiano wa ushuhuda kumhusu Yesu, dhabihu yake ya ukombozi, na ufufuo na baraka kwa wote kama matokeo, katika ufalme wake mtukufu ujao; na Mantiki imetuambia kwamba mpango mkuu na mpana kama huo, unaopita yote ambayo tungeweza kutarajia kimantiki, lakini uliojengwa juu ya hitimisho ya kimantiki kama hiyo, ni lazima uwe ndio mpango wa Mungu tunaoutafuta. Hauwezi kuwa ni ubunifu tu wa wanadamu, kwa maana hata unapofunuliwa, ni mkuu mno kiasi cha kutoweza kuaminiwa na wanadamu.

Columbus alipogundua mto Orinoco, mtu mmoja alisema alikuwa amegundua kisiwa. Alijibu: "Hakuna mto kama huo unaotiririka kutoka kisiwani. Mto huu mkuu ni lazima unakusanya maji ya bara zima." Hivyo ndivyo kina na nguvu na hekima na upana wa ushuhuda wa Biblia vinavyotusadikisha kwamba si mwanadamu, bali Mungu Mwenyezi, ndiye mwandishi wa mipango na mafunuo yake. Tumetazama kwa haraka tu madai ya juu juu ya Maandiko ya kuwa na asili ya kimungu, na tumeyaona kuwa ya kimantiki. Sura zinazofuata zitafunua sehemu mbalimbali za mpango wa Mungu, na, tunatumaini, zitatoa ushahidi wa kutosha kwa kila akili nyoofu kwamba Biblia ni ufunuo uliovuviwa na Mungu, na kwamba urefu na upana na kimo na kina cha mpango inaoufunua vinaakisi kwa utukufu tabia ya Mungu, ambayo hadi sasa ilieleweka kwa shida, lakini sasa inaonekana wazi zaidi katika nuru ya mapambazuko ya Siku ya Milenia.

*UKWELI WENYE THAMANI KUU*

*Kweli kuu hugharimu sana kuzipata. Ule ukweli wa kawaida, Ambao wanadamu hupeana siku kwa siku, Huja katika mwenendo wa kawaida wa maisha mepesi, Ukipeperushwa na upepo wa kizembe katika njia yetu.*

*Kweli kuu hupatikana kwa ushindi wa gharama; haziokotwi kwa bahati, Wala kuletwa na upepo wa ndoto za mchana; Bali hukamatwa katika pambano kuu la nafsi, Katika kushindana kigumu na upepo wa upinzani na mkondo wa maji.*

*Wakati mwingine, katikati ya mzozo, ghasia, hofu na huzuni, Wakati mkono wenye nguvu wa Mungu, ukinyooshwa kwa uweza, Unapolima udongo wa ndani wa moyo uliotuama, Huleta mbegu fulani za kweli zilizozikwa kwenye nuru.*

*Haupatikani sokoni, katikati ya ngano na divai; Wala katika biashara ya dhahabu na vito; Wala katika ukumbi wa dunia wa anasa za usiku wa manane, Wala katikati ya kung'aa kwa taji za kifalme;*

*Haupatikani katika mgongano wa imani za wanadamu, Wala katika biashara kati ya kanisa na dunia, Hazina safi ya ukweli haipatikani humo, katikati ya magugu na masuke; Wala bendera yake safi haikunjuliwi katikati yao.*

*Ukweli huchipuka kama mavuno kutoka mashamba yaliyolimwa vema, Ukituza kazi ya subira, na imani na juhudi. Kwa wale wanaoutafuta hivyo, siku zote hutoa Hazina zake tajiri zaidi kwa ustawi wao wa milele.*

## SOMO LA IV

# ENZI NA VIPINDI VILIVYOAINISHWA KATIKA MAENDELEO YA MPANGO WA MUNGU

MPANGO WA MUNGU NI DHAHIRI NA WENYE UTARATIBU — ENZI KUU TATU ZA HISTORIA YA ULIMWENGU — SIFA ZAKE MAHUSUSI — "DUNIA HUDUMU MILELE" — ULIMWENGU UJAO, MBINGU MPYA NA DUNIA MPYA — MIGAWANYO YA ENZI HIZI KUU — VIPENGELE MUHIMU VYA MPANGO WA MUNGU VINAVYOONEKANA HIVYO — UTARATIBU ULIOBAINIKA UNAFUNUA UWIANO — KULIGAWANYA SAWA NENO LA KWELI.

KAMA vile ambavyo wengine kwa ujinga wanahukumu vibaya ustadi na hekima ya msanifu majengo na mjenzi mkuu kwa kutazama kazi yake ambayo haijakamilika, ndivyo pia wengi katika ujinga wao sasa wanavyomhukumu Mungu vibaya kwa kutazama kazi yake ambayo haijakamilika; lakini baada ya muda, wakati jukwaa bovu la uovu, lililoruhusiwa kwa ajili ya nidhamu ya mwanadamu, na ambalo hatimaye litageuzwa kwa faida yake, litakapoondolewa, na vifusi kusafishwa, kazi ya Mungu *iliyokamilika* itatangaza kwa wote hekima na nguvu zake zisizo na kikomo; na mipango yake itaonekana kuwa inapatana na tabia yake tukufu.

> *Kwa kuwa Mungu anatuambia kwamba ana kusudi lililowekwa wazi, na kwamba makusudi yake yote yatatimizwa, inatupasa sisi, kama watoto wake, kuchunguza kwa bidii ni mipango gani hiyo, ili tuonekane kuwa tunapatana nayo. Ona jinsi Yehova anavyothibitisha kwa msisitizo uimara wa kusudi lake: "BWANA wa majeshi ameapa, akisema, Hakika yangu kama vile nilivyoazimia, ndivyo itakavyokuwa; na kama nilivyokusudia, ndivyo itakavyotokea." "BWANA wa majeshi amekusudia, naye ni nani atakayelibatili?" "Mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; Mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi,... Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote... Naam, nimenena, nami nitatekeleza; nimekusudia, nami nitafanya." (Isa. 14:24-27; 46:9-11)*

Kwa hiyo, hata kama matendo ya Mungu kwa wanadamu yanaweza kuonekana kuwa ya kubahatisha au ya fumbo, wale wanaoamini ushuhuda huu wa Neno lake ni lazima wakiri

kwamba mpango wake wa asili na usioweza kubadilika umekuwa, na bado unaendelea, kwa utaratibu hadi ukamilifu.

Wakati ambapo umati wa wanadamu, wakipapasa katika giza la ujinga, ni lazima wasubiri utekelezaji halisi wa mpango wa Mungu, kabla ya kuweza kuitambua tabia tukufu ya Msanifu Majengo wa Kimungu, ni fursa ya mtoto wa Mungu kuona kwa imani na kwa nuru ya taa yake utukufu uliotabiriwa wa wakati ujao, na hivyo kuthamini matendo ya zamani na ya sasa ambayo kwa vinginevyo yangekuwa ya fumbo. Kwa hiyo, tukiwa wana wa Mungu wenye shauku, na warithi wa urithi ulioahidiwa, tunaligeukia Neno la Baba yetu, ili tuweze kuyaelewa makusudi yake kutokana na mipango na maelezo yaliyotolewa humo. Humo tunajifunza kwamba mpango wa Mungu, kwa habari ya mwanadamu, unahusu vipindi vitatu vikuu vya wakati, kuanzia na uumbaji wa mwanadamu na kuendelea hadi katika wakati ujao usio na kikomo. Petro na Paulo wanaviita vipindi hivi "ULIMWENGU TATU," ambavyo tunaviwakilisha katika mchoro ufuatao.




Enzi hizi tatu kuu zinawakilisha maonyesho matatu tofauti ya majaliwa ya Mungu. Ya kwanza, kuanzia uumbaji hadi gharika, ilikuwa chini ya usimamizi wa malaika, na inaitwa na Petro "DUNIA ILIYOKUWAPO." *2 Pet. 3:6*

Enzi kuu ya pili, kuanzia gharika hadi kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu, uko chini ya udhibiti wa Shetani, "Mkuu wa ulimwengu huu," na kwa hiyo unaitwa "ULIMWENGU MWOVU WA SASA." *Gal. 1:4; 2 Pet. 3:7*

Enzi ya tatu itakuwa "ulimwengu usio na mwisho" (*Isa. 45:17*) chini ya utawala wa Mungu, Ufalme wa Mungu, na unaitwa "ULIMWENGU UJAO—ambamo haki Yakaa ndani yake." *Ebr. 2:5; 2 Pet. 3:13*

Kipindi cha kwanza kati ya hivi, au "Ulimwengu," chini ya usimamizi wa malaika, kilishindwa; cha pili, chini ya utawala wa Shetani, mnyang'anyi, kwa kweli kimekuwa "ulimwengu mbaya"; lakini cha tatu kitakuwa zama za haki na baraka kwa jamaa zote za dunia.

"Ulimwengu" mbili za mwisho kati ya hizi zimetajwa kwa undani zaidi, na kauli zinazozihusu ziko katika tofauti kubwa. Kipindi cha sasa, au cha pili, kinaitwa "ulimwengu mwovu wa sasa," si kwa sababu hakuna kitu kizuri ndani yake, bali kwa sababu ndani yake uovu unaruhusiwa kutawala. *"Na sasa twasema ya kwamba wenye kiburi ndio walio heri; naam, watendao uovu ndio wajengwao; naam, wamjaribuo Mungu ndio waponywao."* (*Mal. 3:15*) Ulimwengu wa tatu au wakati ujao umetajwa kama "ULIMWENGU UJAO—ambamo haki hukaa ndani yake," si kwa sababu hakutakuwa na uovu ndani yake, bali kwa sababu uovu hautatawala. Kufutwa kwa uovu kutakuwa hatua kwa hatua, kwa kipindi cha miaka elfu. Uovu hautatawala wakati huo; hautafanikiwa; hawatakuwa tena waovu watakaofanikiwa; bali "**wenye haki watastawi**" (*Zab. 72:7*), "wenye kutii watakula mema ya nchi" (*Isa. 1:19*), na "watenda mabaya watakatiliwa mbali." *Zab. 37:9*

Ikionekana hivi, kipindi kitakuwa tofauti sana kiasi cha kuwa kinyume kabisa cha kipindi cha sasa karibu katika kila jambo. Maneno ya Bwana wetu yanaonyesha kwa nini kutakuwa na tofauti kati ya kipindi cha sasa na cha wakati ujao. Ni kwa sababu

yeye atakuwa mkuu au mtawala wa ulimwengu ujao, ndiyo maana ndani yake haki na kweli vitafanikiwa; wakati ambapo, kwa sababu Shetani ndiye mkuu (mtawala) wa ulimwengu huu mbaya wa sasa, uovu unafanikiwa na waovu wanastawi. Ni kwa sababu, kama Yesu alivyosema, mkuu wa ulimwengu huu "hana kitu ndani yangu"—na kwa hiyo hana maslahi yoyote kwa wafuasi wake isipokuwa kuwapinga, kuwajaribu, kuwaudhi na kuwapiga (*Yn. 14:30; 2 Kor. 12:7*)—ndiyo maana katika ulimwengu huu mbaya wa sasa au wakati huu, yeyote atakaye kuishi maisha ya utauwa atateswa, huku waovu wakistawi kama mwerezi wa Lebanoni. *2 Tim. 3:12; Zab. 37:35*

Yesu alisema, "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu," na hadi zama au "ulimwengu ujao" *utakapofika*, Ufalme wa Kristo hautatawala dunia. Na kwa ajili ya hili tunafundishwa kutumaini na kuomba, "Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe duniani." Shetani ndiye "mkuu wa giza la ulimwengu huu," na kwa hiyo "giza linaifunika dunia na giza nene." Sasa anatawala na anafanya kazi katika mioyo ya watoto wa uasi. *Efe. 2:2; 6:12*

Ni lazima kuwe na sehemu muhimu sana ya mpango mkuu wa Msanifu Majengo kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu ambayo bado haijakamilika kikamilifu—la sivyo mkuu mpya na kipindi kipya vingekuwa vimeanzishwa zamani sana. Kwa nini iliahirishwa kwa wakati uliopangwa, na pia namna ya mabadiliko kutoka kwa utawala wa sasa wa uovu chini ya Shetani kwenda ule wa haki chini ya Kristo, ni mambo ya kuvutia ambayo yataonyeshwa kwa ukamilifu zaidi baadaye. Inatosha kusema sasa, kwamba falme za ulimwengu huu, ambazo sasa ziko chini ya Shetani, kwa wakati unaofaa zitakuwa falme za Bwana wetu na za Kristo wake. (*Ufu. 11:15*) Muktadha unaonyesha kwamba mabadiliko hayo yatatimizwa kupitia wakati wa dhiki kuu. Kuhusiana na hilo Yesu alisema, *"Hawezi mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu, na kuviteka vitu vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu; ndipo atakapoiteka nyumba yake." (Marko 3:22-27*) Hivyo tunafundishwa kwamba Shetani ni lazima

kwanza afungwe, azuiliwe na aondolewe mamlakani, kabla ya utawala wa Kristo wa haki na amani kuweza kuanzishwa. Kufungwa huku kwa Shetani kwa hiyo kunaonyeshwa kuwa ndiyo kazi ya kwanza ya kipindi kipya. *Ufu. 20:2*

Ikumbukwe kwamba dunia hii ndiyo msingi wa "Ulimwengu" hizi zote na vipindi hivi, na kwamba ingawa nyakati zinapita na vipindi vinabadilika, bado dunia inaendelea—"*nayo dunia hudumu daima.* (*Mhu. 1:4*) Akiendeleza mfano huohuo, Petro anakiita kila kimoja cha vipindi hivi **mbingu** na **nchi** tofauti. Hapa neno *mbingu* linaashiria mamlaka ya juu au ya kiroho yanayotawala, na *nchi* linaashiria serikali ya wanadamu na mipango ya kijamii. Hivyo, mbingu na nchi ya kwanza, au utaratibu na mpangilio wa mambo uliokuwepo wakati huo, baada ya kutimiza lengo lake, uliisha wakati wa gharika. Lakini mbingu halisi (anga na angahewa), na nchi halisi, havikupita: vilibaki. Vivyo hivyo, ulimwengu wa sasa (mbingu na nchi) utapita kwa kishindo kikuu, moto na kuyeyuka—fujo, taabu na kuvunjika. Mtu mwenye nguvu (Shetani), akifungwa, atapambana ili kubaki na mamlaka yake. Utaratibu au mpangilio wa sasa wa serikali na jamii, na si ule wa anga halisi na nchi halisi, ndio utakaopita. *Mbingu* za sasa (mamlaka ya utawala wa kiroho) ni lazima zipishe "mbingu mpya"—utawala wa kiroho wa Kristo. *Nchi* ya sasa (jamii ya wanadamu kama ilivyopangwa sasa chini ya utawala wa Shetani) ni lazima (kwa mfano) iyeyuke na ivunjwe, mwanzoni mwa "*Siku ya Bwana," ambayo "itawaka kama tanuru*." (*Mal. 4:1*) Itafuatiwa na "nchi mpya," yaani, jamii iliyopangwa upya kupatana na Mkuu mpya wa dunia—Kristo. Haki, amani na upendo vitatawala miongoni mwa wanadamu wakati mipango ya sasa itakapopisha ufalme mpya na bora, ambao msingi wake utakuwa ni haki iliyokamilika.

Paulo alipewa kuona kidogo kipindi kijacho, au, kama anavyokiita, "ulimwengu ujao." Anasema "alinyakuliwa" (kimwili au kiakili, au vyote viwili, hakuweza kusema, mambo yalikuwa halisi sana machoni pake) akisafirishwa katika

mkondo wa wakati hadi kwenye hali mpya ya mambo, "mbingu mpya," na hivyo "mbingu ya tatu." Hivyo aliona mambo kama yatakavyokuwa chini ya utawala wa kiroho wa Kristo, mambo ambayo hakuruhusiwa kuyafichua. (*2 Kor. 12:2-4*) Bila shaka haya yalikuwa ni mambo yaleyale ambayo Yohana aliyoyaona baadaye, na kuruhusiwa kuyaeleza kwa Kanisa kwa *mifano*, ambayo inaweza kueleweka tu inapowadia. Yohana, katika ufunuo aliopewa na Bwana wetu katika kisiwa cha Patmo, alichukuliwa katika njozi kupitia Kipindi hiki cha Kikristo na mabadiliko yake ya matukio ya kanisa na serikali, hadi mwisho wa ulimwengu huu mbaya wa sasa, au wakati huu, na huko katika njozi za kinabii alimwona Shetani amefungwa, Kristo anatawala, na mbingu mpya na nchi mpya zimeanzishwa; kwa maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zilikuwa zimepita. *Ufu. 21:1*

**Zama au Vipindi Maalum**

Sasa tunazungumzia zama ambazo nyakati hizi kuu zimegawanywa, kama inavyoonyeshwa katika mchoro ulio hapa chini.




Kipindi cha kwanza kati ya enzi hizi kuu za wakati ("Ulimwengu") hakikugawanywa katika sehemu ndogo. Njia ya Mungu ya kushughulika na wanadamu haikubadilika kwa wakati wote huo—kuanzia anguko la Adamu hadi Gharika.

Mungu alikuwa amempa mwanadamu sheria yake, iliyoandikwa katika asili yake; lakini baada ya kutenda dhambi, alimwacha kwa kiasi fulani afuate njia yake mwenyewe, ambayo **ilimpeleka kwenye uovu zaidi,** *"mawazo ya moyo wake ni mabaya tu siku zote."* Hii ilikuwa ili mwanadamu atambue upumbavu wake, na ili hekima ya Mungu katika kuamuru utii kamili iweze kudhihirishwa. Kipindi hicho cha mpango wa Mungu kiliisha kwa Gharika, iliyowaangamiza wote isipokuwa Nuhu

mwaminifu na familia yake. Hivyo, kipindi hicho cha kwanza hakikuonyesha tu athari za kutisha za dhambi, bali pia kilidhihirisha kwamba mwelekeo wa dhambi ni wa kumpeleka mtu kwenye uharibifu na taabu kubwa zaidi. Hii inathibitisha umuhimu wa kuingilia kati kwa Yehova, ikiwa urejesho wa 'kile kilichopotea'—yaani, hali ya kwanza ya mwanadamu—utawahi kutimizwa.

Wakati mkuu wa pili, au "ulimwengu wa sasa," unajumuisha zama tatu, kila moja ikiwa ni hatua katika mpango wa Mungu wa kuuangamiza uovu. Kila hatua ni ya juu kuliko ile iliyotangulia, na inausogeza mpango mbele na karibu zaidi na ukamilifu.

Enzi kuu ya tatu—"ulimwengu ujao"—ujao kuanzia ujio wa pili wa Kristo, unajumuisha Zama za Milenia, au "nyakati za marejesho"; na baada yake kuna "zama zijazo" nyingine, ambazo maelezo yake hayajafunuliwa. Mafunuo ya sasa yanahusu urejesho wa mwanadamu kutoka dhambini, na si juu ya umilele wa utukufu utakaofuata.

Zama za kwanza katika "ulimwengu wa sasa" tunaziita **ZAMA ZA MABABU WA IMANI**, au kipindi hicho, kwa sababu katika kipindi hicho Mungu alishughulika na kutoa upendeleo kwa watu wachache tu, huku wanadamu wengine wote wakipuuzwa kabisa. Hivyo Watu waliopendelewa walikuwa ni mababa wa imani Nuhu, Abrahamu, Isaka na Yakobo. Kila mmoja wao kwa zamu anaonekana kuwa aliyependelewa na Mungu. Wakati wa kifo cha Yakobo, zama hizo au utaratibu huo wa kushughulika uliisha. Wakati wa kifo cha Yakobo, wazao wake walianza kuitwa "kabila kumi na mbili za Israeli," na walitambuliwa pamoja na Mungu kama "watu wake wa pekee"; na kupitia dhabihu za mfano walikuwa mfano wa "taifa takatifu," lililotengwa na mataifa mengine kwa kusudi maalum, na kwa hiyo kupata fadhila fulani maalum. Wakati uliotengwa kwa ajili ya sehemu hii ya mpango wa Mungu, kuanzia hapa na kuishia wakati wa kifo cha Kristo, tunauita **ZAMA ZA KIYAHUDI**, au kipindi cha Sheria.

Katika zama hizo Mungu alilibariki taifa hilo kwa namna ya pekee. Aliwapa sheria yake; alifanya agano maalum nao; aliwapa Maskani, ambayo utukufu wake wa *shekina* katika Patakatifu pa Patakatifu uliwakilisha uwepo wa Yehova pamoja nao kama Kiongozi na Mfalme wao. Kwao aliwatuma manabii, na hatimaye Mwana wake. Yesu alifanya miujiza yake na kufundisha katikati yao, na hakwenda mwenyewe kwa wengine, wala hakuwaruhusu wanafunzi wake kwenda kwa mataifa yaliyowazunguka. Aliwatuma, akisema, *"Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie; afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli."* (*Mt. 10:5,6*) Na tena akasema, *"Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli."* (*Mt. 15:24*) Kwamba upendeleo huu wa kitaifa uliisha walipomkataa na kumsulubisha Yesu unaonyeshwa na maneno ya Yesu, alipotangaza, siku tano kabla ya kusulubishwa kwake, *"Tazama, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa." Mt. 23:38*

Hapo, wakati wa kifo cha Yesu, zama mpya zilianza—**ZAMA ZA KIKRISTO** au **KIPINDI CHA INJILI**, ambapo habari njema za kuhesabiwa haki zingetangazwa, si kwa Myahudi pekee, bali kwa mataifa yote; kwa maana Yesu Kristo, kwa neema ya Mungu, alionja Mauti kwa ajili ya kila mtu. Katika zama hizi za Injili pia kuna kundi linaloitwa kwa upendeleo maalum, ambalo limepewa ahadi maalum; yaani, wale ambao kwa imani wanamkubali Kristo Yesu kama Mkombozi na Bwana wao, wakifuata nyayo zake. Tangazo la injili limeenea huku na huko duniani kwa karibu miaka elfu moja na mia tisa, kiasi kwamba sasa inaweza kusemwa kuwa imehubiriwa kwa kiasi fulani katika *kila taifa*. Haijabadilisha mataifa—haikukusudiwa kufanya hivyo katika zama hizi; bali imechagua hapa na pale baadhi ya watu, kwa jumla "**kundi dogo**," kama Yesu alivyotabiri (*Luka 12:32*), ambalo ni furaha ya Baba kuwapa Ufalme katika zama zitakazofuata hizi. Kwa zama hizi "ulimwengu huu mbaya wa sasa" unaisha; na zingatia vizuri kwamba wakati Mungu amekuwa akiruhusu utawala na ukuu wa uovu, kwa kuonekana kuidhuru kazi yake, hata hivyo makusudi yake ya kina

yamekuwa yakiendelea kwa kasi kulingana na mpango uliowekwa na dhahiri, na kwa utaratibu kamili wa nyakati alizoziweka. Mwishoni mwa zama hizi, na mapambazuko ya zama zinazofuata, zama za Milenia, Shetani atafungwa na nguvu zake kupinduliwa, kama maandalizi ya kuanzishwa kwa ufalme wa Kristo na mwanzo wa "**ulimwengu ujao, ambamo haki yakaa ndani yake.**"

Milenia, ikimaanisha miaka elfu, kwa makubaliano ya pamoja inatumika kama jina la kipindi kilichotajwa katika *Ufu. 20:4*—miaka elfu ya utawala wa Kristo, zama za kwanza katika "ulimwengu ujao." Katika zama za Milenia, kutakuwa na urejesho wa vitu vyote vilivyopotea kupitia anguko la Adamu (*Mdo. 3:19-21*), na kabla ya kumalizika kwake machozi yote yatakuwa yamefutwa. Zaidi ya mipaka yake, katika zama za baraka zitakazofuata, hakutakuwa na Mauti tena, wala huzuni wala kilio; wala hakutakuwa na maumivu tena. Mambo ya kwanza yatakuwa yamepita. (*Ufu. 21:4*) Mafunuo ya Mungu hayaelezi zaidi, na hapo ndipo tunapoishia.

Hapa tumetazama kwa haraka tu muhtasari wa mpango huu wa zama. Kadiri tunavyouchunguza zaidi, ndivyo tutakavyogundua ndani yake uwiano mkamilifu, uzuri na mpamgilio. Kila zama ina sehemu yake ya kutimiza, muhimu kwa ajili ya ukamilifu wa mpango wa Mungu kwa ujumla. Mpango huu ni wa maendeleo, unaofunuliwa hatua kwa hatua kutoka zama hadi zama, ukipanda juu na kusonga mbele hadi kwenye utimilifu mkuu wa kusudi la asili la Msanifu Majengo wa Kimungu, "*ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake.*" (*Efe. 1:11*) Hakuna hata kimojawapo cha vipindi hivi vikuu kilicho kirefu mno au kifupi mno kwa saa moja kwa ajili ya kutimiza lengo lake. Mungu ni mchumi mwenye hekima wa wakati na njia, ingawa rasilimali zake hazina kikomo; na hakuna nguvu yoyote, hata iwe ya uovu kiasi gani, inayoweza kwa muda kuchelewesha au kuzuia makusudi yake. Mambo yote, mabaya na mema, chini

ya usimamizi na uongozi wa Mungu, yanafanya kazi pamoja kwa ajili ya kutimiza mapenzi yake.

Kwa akili isiyofundishwa na isiyo na nidhamu, ambayo inaweza kuona sehemu ndogo tu ya mfumo tata wa mpango wa Mungu, unaonekana kama fujo, mchafuko na kushindwa, kama vile ambavyo mashine tata nzima, au hata sehemu yake, ingeonekana kwa mtoto. Kwa akili yake changa na isiyofunzwa, haieleweki, na mzunguko tofauti wa magurudumu na mikanda yake ni fujo tu. Lakini ukomavu na uchunguzi vitaonyesha kwamba fujo inayoonekana ni uwiano mzuri, unaoleta matokeo mema. Hata hivyo, mashine hiyo ilikuwa na mafanikio sawa kabla ya mtoto kuelewa utendaji wake kama ilivyokuwa baada ya kuelewa. Vivyo hivyo, wakati mpango wa Mungu upo, na umekuwa kwa miaka mingi, ukiendelea kwa mafanikio, mwanadamu amekuwa akipokea nidhamu inayohitajika, si tu ili kumwezesha kuelewa utendaji wake tata, bali pia kupata uzoefu wa matokeo yake yenye baraka.

Tunapoendelea na funzo letu la mpango wa Mungu, ni muhimu tukumbuke zama hizi na sifa na malengo yake maalum; kwa maana *hakuna* zama *moja* mpango unaweza kuonekana, ***bali katika zote***, kama vile ambavyo kiungo kimoja si mnyororo, bali viungo kadhaa vikiunganishwa vinaunda mnyororo. Tunapata mawazo sahihi ya mpango mzima kwa kuzingatia sifa bainifu za kila sehemu, na hivyo tunawezeshwa kuligawa kwa usahihi neno la kweli.

Kauli ya Neno ambayo ni ya wakati mmoja, au kipindi kimoja, haipaswi kutumika kwa kingine, kwani mambo yaliyosemwa kuhusu zama moja si ya kweli kila wakati kuhusu zama nyingine. Kwa mfano, itakuwa ni uongo kusema kuhusu wakati wa sasa kwamba kumjua Bwana kunaijaza dunia yote, au kwamba hakuna haja ya kumwambia jirani yako, Mjue Bwana. (*Isa. 11:9; Yer. 31:34*) Hili si kweli katika zama hizi, na haliwezi kuwa kweli hadi Bwana, akiwa amekuja tena, atakapokuwa ameuanzisha ufalme wake; kwa maana katika zama hizi

kumekuwa na udanganyifu mwingi wa kupotosha, na tunaambiwa kwamba hata mwishoni kabisa mwa zama—"Siku za mwisho... watu waovu na wadanganyifu wataendelea, wakizidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganywa." (*2 Tim. 3:1,13*) Itakuwa ni matokeo ya utawala wa Masihi katika zama za Milenia ndipo maarifa na haki vitaifunika dunia kama maji yanavyoifunika bahari.

Kosa kama hilo, na la kawaida sana, ni kudhani kwamba ufalme wa Mungu sasa umeanzishwa na unatawala juu ya dunia, na kwamba mapenzi yake sasa yanafanyika miongoni mwa mataifa. Hili ni wazi kuwa liko mbali na ukweli, kwa maana falme za ulimwengu huu zinategemezwa na kutajirishwa kupitia ukandamizaji, udhalimu na udanganyifu, kwa kiwango kikubwa ambacho akili inayoongezeka ya watu itaruhusu. Shetani, "mkuu wa ulimwengu huu" wa sasa, bado ni lazima aondolewe, na falme hizi, ambazo sasa ziko chini ya udhibiti wake, ni lazima ziwe falme za Bwana wetu na za Mpakwa mafuta wake, atakapojitwalia mwenyewe nguvu zake kuu, na kutawala.

Kwa nuru ambayo sasa ni haki ya nyumba ya imani, tunatambua mfumo na utaratibu ule unaoainisha hatua tukufu za Mungu wetu katika zama zilizopita, nasi tunakumbushwa kwa nguvu juu ya mistari mizuri ya Cowper, iliyoongozwa na imani hai, ambayo ilitumaini mahali iliposhindwa kufuatilia nyayo za Yehova Mwenyezi:

***Ataifanya Iwe Wazi***

"*Mungu hutembea katika njia ya siri,*

*Ili kutenda maajabu yake:*

*Huweka nyayo zake baharini, Na kupanda juu ya dhoruba.*

"*Ndani ya migodi isiyochunguzika Ya ustadi usioshindwa kamwe,*
*Huweka hazina ya mipango yake miangavu, Na kutenda mapenzi yake ya enzi.*

*"Enyi watakatifu wenye hofu, twaeni ujasiri mpya; Mawingu mnayoyaogopa sana Yamejaa rehema, na yatapasuka Kwa baraka juu ya vichwa vyenu.*

*"Msimhukumu Bwana kwa hisia dhaifu, Bali mtumainini kwa neema yake. Nyuma ya majaliwa yenye sura ngumu Ameficha uso wenye tabasamu.*

*"Makusudi yake yataiva haraka, Yakifunuka kila saa. Chipukizi linaweza kuwa na ladha chungu, Lakini tamu itakuwa hiyo ua.*

*"Kutokuamini kwa kipofu hakika kutakosea, Na kuchunguza kazi yake bure. Mungu ndiye mkalimani wake mwenyewe, Na Yeye ataifanya iwe wazi."*

----------------------

*"Siijui njia iliyo mbele yangu, Furaha au huzuni itakazoleta; Ni mawingu gani yanatanda juu ya wakati ujao, Ni maua gani yanaweza kuchipuka kando ya njia. Lakini yupo Mmoja atakayesafiri nami, Hata katika raha au shida hataniacha; Na hii ndiyo faraja na tulizo langu, 'Yeye anaijua njia ninayoiendea.'"*

## SOMO LA V

## SIRI ILIYOFICHWA KWA ZAMA NA VIZAZI, LAKINI SASA IMEDHIHIRISHWA KWA WATAKATIFU WAKE" — Kol. 1:26

NURU HAFIFU YA AHADI YA KWANZA — AHADI KWA IBRAHIMU — KUCHELEWESHWA KWA TUMAINI — SIRI INAANZA KUFUMBULIWA WAKATI WA PENTEKOSTE — SIRI HIYO NI NINI — KWA NINI IMEWEKWA KUWA SIRI KWA MUDA MREFU HIVYO — BADO NI SIRI KWA ULIMWENGU — KUDHIHIRISHWA KWA WOTE KWA WAKATI WAKE — WAKATI SIRI ITAKAPO-KAMILIKA.

WAKATI wanadamu walipokuwa chini ya nidhamu ya uovu, na wasiweze kuelewa umuhimu wake, Mungu alieleza kusudi lake mara kwa mara la kuwarejesha na kuwabariki kupitia mkombozi ajaye. Lakini mkombozi huyo angekuwa nani ilikuwa ni siri kwa miaka elfu nne, na ilianza tu kufunuliwa wazi baada ya ufufuo wa Kristo, mwanzoni mwa zama za Kikristo au za Injili.

Tukitazama nyuma hadi wakati ambapo uzima na furaha ya Edeni vilipotezwa na wazazi wetu wa kwanza, tunawaona wakiwa chini ya adhabu ya haki ya dhambi, iliyojawa na huzuni, na bila chembe ya tumaini, isipokuwa ile iliyotokana na kauli isiyoeleweka kwamba uzao wa mwanamke ungeponda kichwa cha nyoka. Ingawa katika nuru ya maendeleo yaliyofuata kauli hii imejaa maana kwetu, kwao ilikuwa ni nuru hafifu tu. Karibu miaka elfu mbili ilipita bila ushahidi wowote wa utimilifu.

Yapata miaka elfu mbili baadaye, Mungu alimwita Abrahamu, na kumwahidi kwamba uzao wake utazibariki jamaa zote za dunia. Hili lilionekana kana kwamba Mungu alikuwa bado ana-shikilia kusudi lake alilolieleza hapo awali, na sasa alikuwa ka-ribu kulitimiza. Muda ulienda: nchi ya ahadi ya Kanaani ilikuwa bado si mali yao; walikuwa bado hawana mtoto, na Abrahamu na Sara walikuwa wakizeeka. Abrahamu alifikiri kwamba ilim-bidi amsaidie Mungu kutimiza ahadi yake; hivyo Ishmaeli aliza-liwa. Lakini msaada wake haukuhitajika, kwa maana kwa *wakati unaofaa* Isaka, mtoto wa tumaini na ahadi, alizaliwa. Wakati huo

ilionekana kana kwamba mtawala na mbariki wa mataifa aliyeahidiwa alikuwa amefika. Lakini la: miaka ilipita, na ilionekana kana kwamba ahadi ya Mungu ilikuwa haijatimizwa; kwa maana Isaka alikufa, na mrithi wake, Yakobo, pia. Lakini imani ya wachache bado ilishikilia ahadi hiyo kwa uthabiti, na ilitegemezwa na Mungu; kwa maana "agano alilofanya na Abrahamu" lilihakikishwa na "kiapo chake kwa Isaka, akamthibitishia Yakobo... na Israeli kuwa agano la milele." *1 Nya. 16:16,17*

Wakati wa kifo cha Yakobo, wazao wake walipoitwa kwa mara ya kwanza **KABILA KUMI NA MBILI ZA ISRAELI**, na kutambuliwa na Mungu kama "taifa teule" (*Mwa. 49:28; Kum. 26:5*), matarajio kwamba taifa hili kwa ujumla, kama uzao ulioahidiwa wa Abrahamu, lingemiliki Kanaani, na kutawala na kubariki ulimwengu, yalionekana kuwa karibu kutimia; kwa maana tayari, chini ya upendeleo wa Misri, walikuwa wakigeuka kuwa taifa lenye nguvu. Lakini tumaini lilikuwa karibu kuzimika na ahadi karibu kusahaulika wakati Wamisri, baada ya kuwatawala, walipowashikilia kama watumwa kwa kipindi kirefu.

Hakika ahadi za Mungu zilikuwa zimegubikwa na siri, na njia zake zilionekana kutoweza kuchunguzika. Hata hivyo, kwa wakati unaofaa alikuja Musa, mkombozi mkuu, ambaye kwa mkono wake Mungu aliwaongoza kutoka utumwani, akifanya miujiza mikuu kwa niaba yao. Kabla ya kuingia Kanaani mkombozi huyu mkuu alikufa; lakini kama msemaji wa Bwana alitangaza, *"Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi;.. ."* (*Kum. 18:15; Mdo. 3:22*) Hii ilitoa ufahamu zaidi katika mpango wa Mungu, ikionyesha kwamba si tu taifa lao, kwa ujumla, lingehusishwa kwa namna fulani na kazi ya wakati ujao ya kutawala na kubariki, bali kwamba mmoja atakayechaguliwa kutoka miongoni mwao angeongoza kwenye ushindi na utimilifu wa ahadi. Kisha Yoshua, ambaye jina lake linamaanisha mkombozi, au mwokozi, akawa kiongozi wao, na chini yake walipata ushindi mkuu, na kwa kweli wakaingia katika nchi iliyoahidiwa katika agano. Hakika

basi ilionekana kwamba kiongozi wa kweli alikuwa amefika, na kwamba ahadi ilikuwa karibu kupata utimilifu kamili.

Lakini Yoshua alikufa, nao hawakupata maendeleo kama taifa hadi Daudi, na kisha Sulemani, walipopewa kuwa Wafalme wao. Wakati huo walifikia kilele cha utukufu wao; lakini punde, badala ya kuona ahadi ikitimizwa, walinyang'anywa nguvu zao, na wakawa chini ya mataifa mengine. Hata hivyo, wengine walishikilia kwa uthabiti ahadi ya Mungu, na bado waliendelea kumtazamia mkombozi mkuu ambaye Musa, Yoshua, Daudi na Sulemani walikuwa ni mifano yake tu.

Wakati Yesu alipozaliwa, watu wote walikuwa wakimtarajia Masihi, mfalme ajaye wa Israeli na, kupitia Israeli, wa ulimwengu mzima.Lakini tumaini la Israeli la utukufu na heshima ya mfalme wao ajaye, lililochochewa na mifano na unabii wa ukuu na nguvu zake, liliwafanya wapuuze seti nyingine ya mifano na unabii, iliyoashiria kazi ya mateso na kifo, kama fidia kwa ajili ya wenye dhambi, iliyokuwa muhimu kabla ya baraka kuja. Hili lilionyeshwa kimfano katika Pasaka kabla ya kukombolewa kutoka Misri, katika kuchinjwa kwa wanyama wakati wa kutolewa kwa agano la sheria (*Ebr. 9:11-20; 10:8-18*), na katika dhabihu za Upatanisho zilizotolewa mwaka baada ya mwaka daima na ukuhani. Walipuuza, pia, kauli ya manabii, "waliotangulia kuyashuhudia *mateso* ya Kristo, na utukufu *utakaofuata*." (*1 Petro 1:11*) Hivyo, Yesu alipokuja kama dhabihu, hawakumtambua; hawakujua wakati wa kujiliwa kwao. (*Luka 19:44*) Hata wafuasi wake wa karibu walichanganyikiwa sana Yesu alipokufa; na kwa huzuni walisema, *"Nasi tulitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli."* (*Luka 24:21*) Ilionekana kana kwamba walikuwa wameweka matumaini yao mahali pasipofaa. Walishindwa kuona kwamba kifo cha kiongozi wao kilikuwa ni dhamana ya Agano Jipya ambalo chini yake baraka zingekuja, utimilifu wa sehemu ya agano la ahadi. Hata hivyo, walipogundua kwamba alikuwa amefufuka kutoka kaburini, matumaini yao yaliyonyauka yalianza kuchipua tena (*1 Petro 1:3*), na

alipokuwa karibu kuwaacha, waliuliza kuhusu tumaini lao la muda mrefu na lililocheleweshwa mara nyingi, wakisema, "Bwana, je, wakati huu ndipo utakapowarudishia Israeli ufalme?" Kwamba matumaini yao yalikuwa sahihi kwa kiasi kikubwa, ingawa hawakuweza kujua wakati ambapo yangetimizwa, ni dhahiri kutokana na jibu la Bwana wetu: *"Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, ambayo Baba ameyaweka katika uwezo wake mwenyewe." Mdo. 1:6,7*

Mpango wa Mungu sasa umechukua mkondo gani? lazima lilikuwa swali la wanafunzi wake Yesu alipopaa; kwa maana ni lazima tukumbuke kwamba mafundisho ya Bwana wetu kuhusu Ufalme yalikuwa hasa kwa mifano na maneno ya mafumbo. Alikuwa amewaambia, *"Hata bado ningali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa; lakini yeye, atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote." "Yeye atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia."* (*Yohana 16:12,13; 14:26*) Hivyo hawakuweza kuelewa kabla ya baraka ya Pentekoste kuja.

Hata wakati huo, ilichukua muda kabla ya kupata uelewa kamili na wazi wa kazi iliyokuwa ikifanyika, na uhusiano wake na agano halisi. (*Mdo. 11:9; Gal. 2:2,12,14*) Hata hivyo, inaonekana kwamba hata kabla ya kuelewa kikamilifu nakwa uwazi, walitumiwa kama vinywa vya Mungu, na maneno yao yaliyoongozwa na roho wa Mungu yawezekana yalikuwa ni maelezo ya kweli yaliyo wazi na ya kina zaidi kuliko walivyoelewa wao wenyewe.

> *Kwa mfano, soma hotuba ya Yakobo anaposema: "Simeoni ametueleza jinsi Mungu hapo kwanza alivyowaangalia Mataifa ili achague watu katika hao kwa ajili ya jina lake [bibi-arusi]. Na maneno ya manabii yapatana na hayo, kama ilivyoandikwa, Baada ya mambo haya [baada ya watu hawa kutoka kwa Mataifa kuwa wametolewa] nitarejea, Nami nitaijenga tena nyumba ya Daudi [utawala wa kidunia] iliyoanguka. Nitajenga tena maanguko yake, Nami nitaisimamisha; .'" Mdo. 15:14-16*

Yakobo alianza kusoma katika majaliwa ya Mungu, katika kupelekwa kwa Injili kupitia Petro kwa mwongofu wa kwanza wa Kimataifa na kupitia Paulo kwa Wamataifa kwa ujumla, kwamba katika zama hizi Wayahudi na Wamataifa wanaoamini wangependelewa sawasawa. Kisha alitafuta unabii na akakuta imeandikwa hivyo; na kwamba baada ya kazi ya zama hizi za Injili kukamilika, ndipo ahadi kwa Israeli wa kimwili zitatimizwa. Hatua kwa hatua ile siri kuu, iliyofichwa kwa muda mrefu, ilianza kueleweka na wachache—watakatifu, "rafiki" maalum wa Mungu.

Paulo anatangaza (*Kol. 1:27*) kwamba siri hii iliyofichwa tangu zama na vizazi, lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake, ni

**"Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu."**

Lakini kuna faida gani katika njia iliyofuatwa? Kwa nini wasipewe watu wote nafasi ya kibinafsi ya uzima sasa, mara moja, bila mchakato mrefu wa jaribio na hukumu ya Adamu, kushiriki kwa wazao wake katika hukumu yake, ukombozi wa wote kwa dhabihu ya Kristo, na toleo jipya kwa wote la uzima wa milele chini ya masharti ya Agano Jipya? Ikiwa uovu ni lazima uruhusiwe kwa sababu ya hiari ya kimadili ya mwanadamu, kwa nini kuondolewa kwake kunatimizwa kwa njia ya kipekee na ya mzunguko namna hii? Kwa nini kuruhusu taabu nyingi kiasi hicho iingilie kati, na kuwapata wengi ambao hatimaye watapokea zawadi ya uzima kama watoto watiifu wa Mungu?

"Aha! Hapo hasa ndipo penye kiini cha somo hili." Kama Mungu angepanga tofauti uenezaji wa jamii yetu, ili watoto wasishiriki matokeo ya dhambi za wazazi—udhaifu wa kiakili, kiadili na kimwili—na kama Muumba angepanga kwamba wote wawe na hali nzuri ya Edeni kwa ajili ya kujaribiwa kwao, na kwamba wakosaji pekee ndio wahukumiwe na “kukatiliwa mbali,” ni wangapi tunaoweza kudhania wangeonekana kuwa wanastahili, na wangapi wasiostahili uzima, chini ya hali zote hizo nzuri?

Ikiwa kisa kimoja cha Adamu kitachukuliwa kama kigezo (na hakika yeye alikuwa kwa kila namna mfano wa mwanadamu mkamilifu), hitimisho lingekuwa kwamba hakuna hata mmoja ambaye angeonekana kuwa mtiifu kikamilifu na anayestahili; kwa sababu hakuna ambaye angekuwa na ujuzi wa wazi na uzoefu na Mungu, ambao ungejenga ndani yao imani kamili katika sheria zake, zaidi ya hukumu yao binafsi. Tunahakikishiwa kwamba ni ujuzi wa Kristo kumhusu Baba ndio uliomwezesha kumtumaini na kumtii kikamilifu. (**Isaya 53:11**) Lakini hebu tuchukulie kwamba robo wangeupata

uzima; au hata zaidi, tuchukulie kwamba nusu wangeonekana kuwa wanastahili, na kwamba nusu nyingine wangepata mshahara wa dhambi—mauti. Basi nini kingefuata? Tuchukulie nusu nyingine, watiifu, hawakuwa wamepata uzoefu wala kushuhudia dhambi: je, wasingekuwa daima na udadisi juu ya mambo yaliyokatazwa, wakizuiliwa tu na hofu ya Mungu na ya adhabu? Utumishi wao usingeweza kuwa wa moyo wote kama ambavyo ungekuwa endapo wangejua mema na mabaya; na hivyo kuwa na uthamini kamili wa makusudi yenye wema ya Muumba katika kuweka sheria zinazoongoza mwenendo wake mwenyewe pamoja na ule wa viumbe vyake.

Halafu, pia, fikiria ile nusu ambayo ingeingia katika mauti kama matokeo ya dhambi yao wenyewe ya makusudi. Wangekatiliwa mbali na uzima kabisa, na tumaini lao pekee lingekuwa kwamba Mungu kwa upendo angewakumbuka kama viumbe vyake, kazi ya mikono yake, na kuwaandalia jaribio lingine. Lakini kwa nini afanye hivyo? Sababu pekee ingekuwa ni tumaini kwamba kama wangeamshwa na kujaribiwa tena, baadhi yao, kwa sababu ya **uzoefu** wao mkubwa zaidi, wangeweza kuchagua utii na kuishi.

Lakini hata kama mpango kama huo ungekuwa na matokeo mazuri kama ule ambao Mungu ameukubali, bado kungekuwa na mapingamizi makubwa dhidi yake.

Jinsi gani mpango wa Mungu unavyoonyesha hekima zaidi kwa kuuwekea uovu mipaka. Jinsi gani akili zetu zenye mipaka zinavyoweza kutambua kuwa ni bora zaidi, kuwa na sheria moja tu kamilifu na isiyo na upendeleo, inayotangaza kwamba mshahara wa dhambi ya makusudi ni mauti—uharibifu—kukatiliwa mbali na uzima. Hivyo Mungu anazuia uovu anaouruhusu, kwa kuandaa kwamba utawala wa Milenia wa Kristo utatimiza kutokomezwa kabisa kwa uovu na pia kwa watenda maovu wa makusudi, na kuleta

umilele wa haki, utakaotegemea ujuzi kamili na utii wa hiari kamilifu wa viumbe wakamilifu.

Lakini kuna mapingamizi mengine mawili kwa mpango uliopendekezwa, wa kumjaribu kila mtu peke yake mwanzoni. Mkombozi mmoja alitosha kabisa katika mpango ambao Mungu aliukubali, kwa sababu ni **mmoja** tu aliyetenda dhambi, na ni **mmoja** tu aliyekuwa amehukumiwa. (Wengine walishiriki hukumu **yake**.) Lakini kama jaribio la kwanza lingekuwa la mtu mmoja mmoja, na kama nusu ya jamii ya wanadamu wangetenda dhambi na kuhukumiwa kibinafsi, ingehitajika dhabihu ya mkombozi kwa kila mtu aliyehukumiwa. Uhai mmoja ambao haujapotezwa ungeweza kukomboa uhai mmoja uliopotezwa, lakini si zaidi. Mtu mmoja mkamilifu, *"mwanadamu Kristo Yesu,"* anayemkomboa Adamu aliyeanguka (na hasara zetu kupitia yeye), hakuweza kuwa *"ukombozi [bei sawasawa] kwa ajili ya WOTE"* chini ya hali nyingine zozote isipokuwa zile za mpango ambao Mungu aliuchagua.

Kama tungechukulia idadi ya wanadamu wote tangu Adamu kuwa ni bilioni mia moja, na kwamba ni nusu tu ya hawa walitenda dhambi, ingehitajika wanadamu wote bilioni hamsini watiifu, wakamilifu, wafe ili kutoa **ukombozi** [bei sawasawa] kwa ajili ya wakosaji wote bilioni hamsini; na hivyo kwa mpango huu pia mauti ingewapata wote. Na mpango kama huo ungehusisha mateso **yasiyo pungufu** kuliko yanayopatikana sasa.

Pingamizi lingine kwa mpango kama huo ni kwamba ungevuruga vibaya mipango ya Mungu inayohusiana na uteuzi na kuinuliwa kwenye asili ya kimungu kwa "kundi dogo," mwili wa Kristo, kundi ambalo Yesu ndiye Kichwa na Bwana wake.

Mungu hakuweza kwa haki **kuwaamuru** wana bilioni hamsini watiifu watoe haki zao, fursa zao na maisha yao kama ukombozi kwa ajili ya wenye dhambi; kwa maana chini ya sheria yake mwenyewe utii wao ungewapatia haki ya uzima wa kudumu. Kwa hiyo, kama watu

hao wakamilifu wangeombwa kuwa wakombozi wa walioanguka, ingekuwa ni mpango wa Mungu, kama ilivyokuwa kwa Bwana wetu Yesu, kuweka thawabu maalum mbele yao, ili wao, kwa furaha iliyowekwa mbele yao, wavumilie adhabu ya ndugu zao. Na kama wangepewa thawabu ileile aliyopewa Bwana wetu Yesu, yaani, kushiriki asili mpya, ya kimungu, na kuinuliwa juu sana kuliko malaika na falme na mamlaka, na kila jina litajwalo—akifuata Yehova (**Waefeso 1:20, 21**), basi kungekuwa na idadi kubwa mno katika daraja la kimungu, jambo ambalo hekima ya Mungu ni dhahiri haikukubaliana nalo. Zaidi ya hayo, hawa bilioni hamsini, chini ya hali kama hizo, wote wangekuwa katika **usawa**, na hakuna yeyote miongoni mwao angekuwa mkuu au kichwa, wakati mpango ambao Mungu **ameukubali** unahitaji Mkombozi mmoja tu, mmoja aliyeinuliwa sana kwenye asili ya kimungu, na kisha "kundi dogo" la wale aliowakomboa, na ambao "wanafuata nyayo zake" za mateso na kujikana, ili kushiriki jina lake, heshima yake, utukufu wake na asili yake, kama vile mke anavyoshiriki na mumewe.

Wale wanaoweza kuthamini sifa hii ya mpango wa Mungu, ambao, kwa kumhukumu kila mtu katika mwakilishi **mmoja**, ulifungua njia ya ukombozi na urejesho wa wote kwa Mkombozi **mmoja**, watapata ndani yake suluhisho la utata mwingi. Wataona kwamba hukumu ya **wote** katika mmoja ilikuwa kinyume cha jeraha: ilikuwa ni fadhila kubwa kwa **wote** ilipochukuliwa pamoja na mpango wa Mungu wa kuandaa kuhesabiwa haki kwa **wote** kupitia dhabihu ya mwingine.

Uovu utakomeshwa milele wakati kusudi la Mungu la kuuruhusu litakapotimizwa, na wakati manufaa ya ukombozi yatakapokuwa na upana sawa na adhabu ya dhambi. Hata hivyo, haiwezekani kuthamini ipasavyo sifa hii ya mpango wa Mungu bila utambuzi kamili wa ubaya wa dhambi, asili ya adhabu yake—mauti, umuhimu na thamani ya **ukombozi** ambao Bwana wetu Yesu aliutoa, na urejesho chanya na kamili wa mtu binafsi kwenye hali nzuri, hali ambazo chini yake atakuwa na jaribio kamili na la kutosha, kabla ya kuhukumiwa

kuwa anastahili thawabu (uzima wa kudumu), au adhabu (mauti ya kudumu).

Kwa mtazamo wa mpango mkuu wa ukombozi, na matokeo yake ya "urejesho wa vitu vyote," kupitia Kristo, tunaweza kuona kwamba baraka hutokana na kuruhusiwa kwa uovu, ambazo, pengine, zisingeweza kutambuliwa kikamilifu vinginevyo.

Si wanadamu tu wanaofaidika milele yote na uzoefu wanaoupata, na malaika kwa kuchunguza uzoefu wa mwanadamu, bali wote wanafaidika zaidi kwa kufahamiana kikamilifu na tabia ya Mungu kama inavyodhihirishwa katika mpango wake. Mpango wake utakapokamilika kikamilifu, wote wataweza kusoma waziwazi hekima, haki, upendo na nguvu zake. Wataiona haki ambayo haikuweza kukiuka amri ya kimungu, wala kuiokoa jamii iliyohukumiwa kwa haki bila kuondolewa kwa adhabu yao na mkombozi aliyejitolea. Watauona upendo ulioandaa dhabihu hii adhimu na uliomwinua sana Mkombozi kwenye mkono wa kuume wa Mungu mwenyewe, ukimpa nguvu na mamlaka ya kuwarejesha kwenye uzima wale aliowanunua kwa damu yake ya thamani. Wataziona pia nguvu na hekima zilizoweza kuandaa hatima tukufu kwa viumbe vyake, na kuviongoza kila mvuto unaopinga kiasi cha kuwafanya wawe watendaji wa hiari au wasio wa hiari kwa ajili ya kuendeleza na kukamilisha makusudi yake makuu. Kama uovu usingeruhusiwa na hivyo kuongozwa na majaliwa ya kimungu, hatuwezi kuona jinsi matokeo haya yangeweza kupatikana. Kuruhusiwa kwa uovu kwa muda miongoni mwa wanadamu hivi kunaonyesha hekima inayoona mbali, iliyoelewa mazingira yote yaliyoambatana, ikabuni suluhisho, na kuweka alama ya matokeo ya mwisho kupitia nguvu na neema yake.

Wakati wa kipindi cha Injili, dhambi na maovu yanayoambatana nayo vimetumika zaidi kwa ajili ya nidhamu na maandalizi ya Kanisa. Kama dhambi isingeruhusiwa, dhabihu ya Bwana wetu Yesu na ya

Kanisa lake, ambayo thawabu yake ni asili ya kimungu, isingewezekana.

Inaonekana wazi kwamba kimsingi sheria ileile ya Mungu iliyo juu ya wanadamu sasa, ambayo utii kwake una thawabu ya uzima, na uasi una adhabu ya mauti, ni lazima hatimaye itawale viumbe wote wenye akili wa Mungu; na sheria hiyo, kama Bwana wetu alivyoifafanua, inaeleweka kwa ufupi katika neno moja, **Upendo**.

> *"'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.'" (**Luka 10:27**)*

Hatimaye, makusudi ya Mungu yatakapotimizwa, utukufu wa tabia ya kimungu utadhihirishwa kwa viumbe wote wenye akili, na kuruhusiwa kwa uovu kwa muda kutaonekana na wote kuwa lilikuwa jambo la hekima katika sera ya kimungu. Sasa, hili linaweza kuonekana tu kwa jicho la imani, likitazama mbele kupitia Neno la Mungu kwenye mambo yaliyonenwa na vinywa vya manabii wote watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu—urejesho wa vitu vyote.

# SOMO LA VIII
# SIKU YA HUKUMU

MTAZAMO WA JUMLA JUU YA SIKU YA HUKUMU — JE, NI WA KIMAANDIKO? — KUFAFANULIWA KWA MANENO: HUKUMU NA SIKU — SIKU KADHAA ZA HUKUMU ZILIZOTAJWA KATIKA MAANDIKO — SIKU YA KWANZA YA HUKUMU NA MATOKEO YAKE — SIKU NYINGINE IMEWEKWA — HAKIMU — TABIA YA HUKUMU IJAYO — KUFANANA NA KUTOFANANA KWA SIKU YA KWANZA NA YA PILI YA HUKUMU — KUWAJIBIKA KWA SASA KWA ULIMWENGU — HUKUMU MBILI ZA KATIKATI NA KUSUDI LAKE — MITAZAMO TOFAUTI SANA JUU YA HUKUMU IJAYO — JINSI MANABII NA MITUME WALIVYOITAZAMA.

> *"Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua"—"Yesu Kristo, mwenye haki." "Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote."* —***Matendo 17:31; 1 Yohana 2:1; Yohana 5:22***

KUNA wazo lisilo wazi na lisiloeleweka vizuri kuhusu siku ya hukumu. Mtazamo unaoaminiwa na wengi ni kwamba Kristo atakuja duniani, akiwa ameketi juu ya kiti kikuu cheupe cha enzi. Kisha, atawaita watakatifu na wenye dhambi wajipange mbele zake ili wahukumiwe, huku kukiwa na misukosuko mikuu ya asili—matetemeko ya ardhi, makaburi yakifunguka, miamba ikipasuka na milima ikianguka. Wazo hili linasema kwamba wenye dhambi watatetemeka wakitolewa kutoka kwenye mateso ya milele ili wasikie dhambi zao zikitajwa, na kisha warudishwe tena kwenye adhabu ya milele isiyo na huruma. Wakati huohuo, watakatifu watatolewa mbinguni ili washuhudie mateso na kukata tamaa kwa waliohukumiwa, wasikie tena uamuzi wa kesi zao wenyewe, na kisha warudi walikotoka. Kulingana na nadharia hii maarufu, kila mtu anapokea hukumu na thawabu yake anapokufa; na hii inayoitwa hukumu ya jumla ni marudio tu ya ile hukumu ya kwanza, lakini bila kusudi lolote linaloeleweka, kwa kuwa wanadai kwamba uamuzi wa mwisho na usioweza kubadilika hutolewa wakati wa kifo.

Muda wote unaodhaniwa kutengwa kwa ajili ya kazi hii kubwa ya kuhukumu mabilioni ya watu unasemekana kuwa ni siku moja ya saa ishirini na nne. Hotuba iliyotolewa hivi karibuni kwa kutaniko moja la Brooklyn ilielezea mtazamo huu wa kawaida. Ilidai kutoa maelezo ya kina ya kazi ya Siku ya Hukumu, ikionyesha kuwa ilikamilika ndani ya mipaka ya siku moja halisi.

Hii ni dhana duni sana, na haipatani kabisa na Neno lililovuviwa. Inatokana na tafsiri ya kiharisi mno ya ule mfano wa Bwana wetu wa kondoo na mbuzi. (Mat. 25:31-46) Hii inaonyesha upuuzi wa kujaribu kulazimisha tafsiri ya neno kwa neno kwenye lugha ya picha. Mfano kamwe si maelezo halisi, bali ni kielelezo tu cha ukweli fulani kwa kutumia kitu ambacho kwa namna nyingi kinafanana nao. Kama mfano huu ungekuwa maelezo halisi ya jinsi hukumu itakavyoendeshwa, ungehusu kondoo na mbuzi halisi, kama unavyosomeka, na si wanadamu hata kidogo. Sasa hebu tuangalie mtazamo unaopatana zaidi na Maandiko na pia wenye mantiki zaidi kuhusu kazi na matokeo ya Siku kuu ya Hukumu ambayo Mungu ameiweka, ambayo hitimisho zote zenye mantiki na za Kimaandiko, pamoja na mifano na picha zote, zinapaswa na kwa kweli zinakubaliana nayo.

Neno **hukumu** linamaanisha zaidi ya kutoa uamuzi. Linajumuisha wazo la kesi au jaribio, pamoja na uamuzi unaotegemea jaribio hilo. Na hili ni kweli si tu kwa neno la Kiingereza *judgment*, bali pia kwa neno la Kigiriki linalotafsiriwa.

Neno **siku**, katika Maandiko na katika matumizi ya kawaida, ingawa mara nyingi hutumika kuwakilisha kipindi cha saa kumi na mbili au ishirini na nne, kwa kweli linamaanisha kipindi chochote maalumu cha wakati. Kwa mfano, tunazungumza kuhusu siku za Nuhu, siku za Luther, siku za Washington; na vivyo hivyo katika Biblia wakati wote wa uumbaji unaitwa siku, tunaposoma juu ya *"siku ile Bwana Mungu alipozifanya mbingu na nchi"* (**Mwanzo 2:4**)—kipindi kirefu, maalum. Kisha tunasoma kuhusu *"siku ya kujaribiwa, jangwani"*—miaka arobaini (**Waebrania 3:8,**

**9**); *"siku ya wokovu"* (**2 Wakorintho 6:2**); pia "siku ya kisasi," "siku ya ghadhabu" na "siku ya taabu"—maneno yanayotumika kwa kipindi cha miaka arobaini mwishoni mwa zama za Kiyahudi, na kwa kipindi kama hicho cha taabu mwishoni mwa Zama za Injili.

Kisha tena tunasoma kuhusu "siku ya Kristo," "siku ya hukumu," na "siku yake"—maneno yanayotumika kwa Zama za Milenia, ambazo ndani yake Masihi atatawala, na kuuhukumu ulimwengu kwa haki, akitoa jaribio pamoja na kutoa hukumu. Na kuhusu kipindi hicho imeandikwa: Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na katika siku yake ataonyesha ni nani aliye Mbarikiwa, Mwenye uwezo pekee, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana. (**Matendo 17:31; 1 Timotheo 6:15**) Kwa nini mtu yeyote adhani siku hii ya hukumu ni ya saa kumi na mbili au ishirini na nne tu, huku akitambua maana pana ya neno **siku** katika visa vingine vinavyofanana, ni jambo lisiloeleweka, isipokuwa kwa dhana kwamba wameathiriwa na mapokeo, bila ushahidi au uchunguzi unaofaa.

Wale watakaochunguza kwa makini konkodansi kamili ya Biblia kuhusiana na Siku ya Hukumu, na kuona aina na kiasi cha kazi itakayotimizwa ndani ya kipindi hicho, watatambua upesi upuuzi wa mtazamo wa kawaida, na uhitaji wa kulipa neno **siku** maana yake pana zaidi.

Wakati Maandiko yanapozungumza juu ya siku kuu ya hukumu au jaribio ijayo, na kuonyesha kwamba umati wa wanadamu utapata jaribio lao kamili na hukumu ya mwisho katika siku hiyo, pia yanafundisha kwamba kumekuwepo na siku nyingine za hukumu, ambazo ndani yake **makundi** fulani teule yamekuwa yakijaribiwa.

Hukumu kuu ya kwanza [jaribio na hukumu] ilikuwa mwanzoni, katika Edeni, wakati jamii nzima ya wanadamu, ikiwakilishwa na kichwa chake, Adamu, iliposimama kujaribiwa mbele za Mungu. Matokeo ya jaribio hilo yalikuwa uamuzi—Mwenye hatia, asiye mtiifu, asiyestahili uzima; na adhabu

iliyotolewa ilikuwa kifo—*"Hakika utakufa."* (**Mwanzo 2:17**, maelezo ya pembeni) Na hivyo *"katika Adamu wote hufa."* Wakati huo wa jaribio katika Edeni ulikuwa siku ya kwanza ya hukumu ya ulimwengu, na uamuzi wa Mwamuzi (Yehova) umekuwa ukitekelezwa tangu wakati huo.

*"Kwa maana ghadhabu ya Mungu* ***imefunuliwa*** *kutoka mbinguni juu ya uasi wote."* Inaweza kuonekana katika kila msafara wa mazishi. Kila kaburi ni shahidi wake. Inasikika katika kila maumivu na uchungu tunaoupata—yote hayo ni matokeo ya jaribio na hukumu ya kwanza—hukumu ya haki ya Mungu, kwamba hatustahili uzima na baraka zilizokuwa zimeandaliwa kwa mwanadamu mwanzoni alipokuwa mtiifu na kwa mfano wa Mungu. Lakini wanadamu watarejeshwa kutoka katika hukumu ya jaribio hilo la kwanza kwa dhabihu moja kwa ajili ya wote, ambayo Mkombozi mkuu anaiandaa. Wote wataokolewa kutoka kaburini na kutoka katika hukumu ya kifo—uharibifu—ambayo kwa mtazamo wa ukombozi huu haichukuliwi tena kama kifo kwa maana kamili, ya milele ya neno, bali kama usingizi wa muda; kwa sababu katika asubuhi ya Milenia wote wataamshwa na Mtoa-Uhai aliyewakomboa wote.

Ni Kanisa la waamini katika Kristo pekee ambalo kwa namna fulani limeachiliwa au *"limeepuka"* hukumu na adhabu hii ya asili; na kuepuka kwao bado si **halisi**, bali ni kwa kuhesabiwa tu kwa imani. *"Tumeokolewa* ***kwa tumaini****"* tu. Kuachiliwa kwetu halisi kutoka katika adhabu hii ya kifo (tuliyoipata katika Adamu na kuiepuka kwa kuingia katika Kristo) hakutatimizwa kikamilifu hadi asubuhi ya ufufuo, tutakaporidhika kuamka katika mfano wa Mkombozi wetu.

Lakini ukweli kwamba sisi ambao tumefikia ujuzi wa mpango wa neema wa Mungu katika Kristo *"****tumeokoka na uharibifu*** *ulio ulimwenguni"* [bado], badala ya kuthibitisha kwamba wengine hawatakuwa na tumaini la wakati ujao la kuepuka, unathibitisha kinyume chake; kwa maana sisi ni malimbuko kwa Mungu kati ya viumbe vyake. Kuepuka kwetu kifo katika Adamu na kuingia

katika uzima katika Kristo ni kionjo tu cha ukombozi wa yeyote atakayetaka kukombolewa kutoka katika utumwa wa uharibifu [mauti] na kuingia katika uhuru wa uzima unaowafaa wote ambao Mungu atawatambua kama wana. Wote watakaotaka wanaweza kukombolewa kutoka mauti na kuingia uzimani, bila kujali tofauti za asili ambazo Mungu ameziandaa kwa ajili ya wana wake katika viwango tofauti vya uwepo. Zama za Injili ni siku ya jaribio la uzima au mauti kwa wale walioitwa kwenye asili takatifu ya Mungu.

Lakini Mungu ameweka siku, atakayowahukumu walimwengu. Hili linawezekanaje? Je, Mungu amebadili nia yake? Je, ameona kwamba uamuzi wake katika jaribio la mtu wa kwanza na hukumu ya jumla haukuwa wa haki, ulikuwa mkali mno, na sasa anahitimisha kuuhukumu ulimwengu kila mtu mmoja mmoja? La; kama ingekuwa hivyo, tusingekuwa na hakikisho bora zaidi la uamuzi wa haki katika jaribio la wakati ujao kuliko la wakati uliopita. Si kwamba Mungu anauchukulia uamuzi wake katika hukumu ya kwanza kuwa si wa haki, bali ni kwamba ameandaa **ukombozi** kutoka katika adhabu ya hukumu ya kwanza, ili aweze kutoa hukumu nyingine (jaribio) chini ya masharti bora zaidi kwa jamii nzima ya wanadamu—wote wakiwa wamekwisha pata uzoefu wa dhambi na matokeo yake. Mungu hajabadilika hata chembe kutoka katika kusudi lake la asili, alilolifanya kabla ya kuwepo ulimwengu. Anatujulisha waziwazi kwamba yeye habadiliki, na kwamba hatamhesabia kamwe mwenye hatia kuwa hana hatia. Atadai adhabu kamili aliyoitamka kwa haki.

Na adhabu hiyo kamili imetolewa na Mkombozi au mbadala ambaye Mungu mwenyewe alimwandaa—Yesu Kristo, ambaye, *"kwa neema ya Mungu, alionja mauti kwa ajili ya kila mtu."* Kwa kuwa Bwana wetu ametoa fidia kwa ajili ya jamii ya Adamu, kwa uhai wake mwenyewe, anaweza kwa haki kuwapa wote toleo jipya la uzima. Toleo hili kwa Kanisa liko chini ya Agano la dhabihu (**Zaburi 50:5; Warumi 12:1**): kwa ulimwengu litakuwa

chini ya Agano Jipya. —**Warumi 14:9; Waebrania 10:16; Yeremia 31:31**

Tunaelezwa zaidi kwamba Mungu atakapoupa ulimwengu jaribio hili la mtu mmoja mmoja, litakuwa chini ya Kristo kama Mwamuzi, ambaye Yehova atamheshimu hivyo kwa sababu ya utii wake hata mauti kwa ajili ya ukombozi wetu. Mungu amemwinua sana, hata kwenye asili ya kimungu, ili awe Mkuu na Mwokozi (**Matendo 5:31**), ili aweze kuwarejesha kutoka katika mauti na kuwapa hukumu wote aliowanunua kwa damu yake ya thamani. Mungu amemkabidhi Mwana hukumu yote, na amempa mamlaka yote mbinguni na duniani. —**Yohana 5:22**

Basi, ni yule Kristo aliyetukuzwa na kuinuliwa sana, yeye aliyeupenda ulimwengu kiasi cha kutoa maisha yake kuwa bei ya fidia, ndiye atakayekuwa Hakimu wa ulimwengu katika jaribio lake la wakati ujao lililoahidiwa. Na ni Yehova mwenyewe ndiye amemteua kwa kazi hiyo, kwa kusudi hilohilo. Kwa kuwa haya ndiyo maelezo ya wazi ya Maandiko, hakuna chochote cha kuogopa. Kinyume chake, kuna sababu kubwa ya kufurahi kwa watu wote wanapoitazamia Siku ya Hukumu. Tabia ya Hakimu mwenyewe ni uhakikisho tosha kwamba hukumu itakuwa ya haki na rehema, na itazingatia ipasavyo udhaifu wa wote. Hukumu hiyo itaendelea hadi wale walio radhi na watiifu watakaporejeshwa kwenye ule ukamilifu wa asili uliopotea Edeni.

Mwamuzi, katika nyakati za zamani, alikuwa ni mtu aliyetekeleza haki na kuwaokoa wanaoonewa. Angalia, kwa mfano, jinsi, walipokuwa chini ya ukandamizaji wa adui zao kwa sababu ya makosa dhidi ya Bwana, Israeli walivyookolewa na kubarikiwa mara kwa mara kwa kuinuliwa kwa waamuzi. Hivyo tunasoma, *"Wana wa Israeli walipomlilia Bwana, Bwana akawainulia* ***mwokozi****,... Othnieli. Roho ya Bwana ikawa juu yake, naye* ***akawa mwamuzi*** *wa Israeli, akatoka aende vitani, akashinda, nayo nchi ikawa na amani miaka arobaini."* (**Waamuzi 3:9-11**)

Hivyo, ingawa ulimwengu umekuwa kwa muda mrefu chini ya mamlaka na ukandamizaji wa adui, Shetani, bado hivi karibuni yeye anayelipia dhambi za wote kwa damu yake ya thamani atachukua uwezo wake mkuu na kutawala. **Atawaokoa** na **kuwahukumu** wale aliowapenda kiasi cha kuwakomboa. Na maandiko yote ya kinabii yanakubaliana na hitimisho hili. Imeandikwa: *"Atauhukumu ulimwengu kwa haki, Na mataifa kwa adili."* —**Zaburi 98:9.**

Hukumu hii ijayo itakuwa kwenye kanuni zilezile kama ya kwanza. Sheria ileile ya utii itawasilishwa, ikiwa na thawabu ileile ya uzima, na adhabu ileile ya mauti. Na kama jaribio la kwanza lilivyokuwa na mwanzo, likaendelea, na kufikia kilele kwa hukumu, ndivyo litakavyokuwa la pili; na hukumu itakuwa ni uzima kwa wenye haki, na mauti kwa wasio haki. Jaribio la pili litakuwa na afadhali zaidi kuliko la kwanza, kwa sababu ya uzoefu uliopatikana chini ya matokeo ya jaribio la kwanza. Tofauti na jaribio la kwanza, jaribio la pili litakuwa ni lile ambalo kila mtu atasimama katika jaribio kwa ajili yake mwenyewe peke yake, na si kwa ajili ya mwingine.

Hakuna atakayekufa wakati huo kwa sababu ya dhambi ya Adamu, au kwa sababu ya kutokamilika kulikorithiwa. Hakutasemwa tena, *"Baba za watu wamekula zabibu mbichi, na meno ya watoto wao yametiwa ganzi; bali* ***yeye alaye zabibu mbichi, meno yake yatatiwa ganzi****." "Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa."* (**Ezekieli 18:4; Yeremia 31:29, 30**) Na itakuwa kweli kwa ulimwengu wakati huo, kama ilivyo kwa Kanisa sasa, kwamba mtu hatahukumiwa kulingana na kile asicho nacho, bali kulingana na kile alicho nacho. (**2 Wakorintho 8:12**) Chini ya utawala wa Kristo, wanadamu wataelimishwa, kufunzwa na kutiwa nidhamu hatua kwa hatua hadi wafikie ukamilifu. Na watakapokuwa wamefikia ukamilifu, upatano kamili na Mungu utatakiwa, na yeyote atakayepungukiwa na utii mkamilifu wakati huo atakatiliwa mbali, akihukumiwa kuwa hastahili uzima.

Dhambi iliyoleta mauti kwa jamii ya wanadamu kupitia Adamu ilikuwa kitendo kimoja tu cha uasi; lakini kwa kitendo hicho alianguka kutoka katika ukamilifu wake. Mungu alikuwa na haki ya kudai utii mkamilifu kutoka kwake, kwa kuwa aliumbwa mkamilifu; naye atadai vivyo hivyo kwa watu wote wakati kazi kuu ya kuwarejesha itakapokamilika. Hakuna atakayeruhusiwa kuwa na uzima wa milele ambaye wakati huo atapungukiwa na ukamilifu hata kwa kiwango kidogo kabisa. Kupungukiwa na ukamilifu, wakati huo, itakuwa ni kutenda dhambi kwa makusudi dhidi ya nuru kamili na uwezo kamili.

Yeyote atakayekusudia kutenda dhambi kwa makusudi, akiwa na nuru kamili na uwezo wa kuelewa, atapotea katika mauti ya pili. Na ikiwa mtu yeyote, katika ile enzi ya majaribio, chini ya mwangaza kamili wa kweli, atakataa neema zinazotolewa na asifanye maendeleo kuelekea ukamilifu kwa muda wa miaka mia moja, atahesabiwa kuwa hastahili uzima, na atakatiliwa mbali—ingawa kwa miaka hiyo mia atahesabiwa kama mtoto mdogo. Hivyo imeandikwa juu ya siku hiyo: *"Mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mwenye dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa."* (**Isaya 65:20**) Hivyo wote ni lazima wapate angalau miaka mia moja ya jaribio; na, kama hawatakuwa wakaidi kiasi cha kukataa kufanya maendeleo, jaribio lao litaendelea katika siku yote ya Kristo, na kufikia kilele tu mwishoni mwake.

Mwisho wa hukumu ijayo ya ulimwengu inaonyeshwa wazi katika mfano wa kondoo na mbuzi (**Mathayo 25:31-46**), katika **Ufunuo 20:15; 21:8** na katika **1 Wakorintho 15:25**. Maandiko haya na mengine yanaonyesha kwamba mwishoni mwake makundi mawili yatakuwa yametenganishwa kabisa—watiifu na wasio watiifu; wale walio katika upatano na andiko na Roho ya sheria ya Mungu, na wale wasio katika upatano nayo. Wanaingia katika uzima wa milele, na wengine wanahukumiwa kifo, kutoweka ("mauti ya pili"), hukumu ileile kama katika hukumu ya kwanza, ambayo walikuwa wameachiliwa kutoka kwayo kwa kuhesabiwa na Kristo ambaye alipata haki ya kuwaachilia kwa

kutoa fidia yao—kwa kifo chake. Hii itakuwa mauti yao ya pili. Hakuna fidia itakayotolewa kwa ajili yao, na hakutakuwa na kuachiliwa wala ufufuo kwa ajili yao, dhambi yao ikiwa ni dhambi ya makusudi, ya kibinafsi dhidi ya nuru kamili na fursa kamili, chini ya jaribio la kibinafsi lenye fadhila nyingi zaidi.

Hatutaki kueleweka kana kwamba tunapuuza wajibu wa sasa wa ulimwengu, ambao kila mtu anao, kulingana na kiasi cha nuru anachofurahia, iwe ni nyingi au kidogo, iwe ni nuru ya asili au ya ufunuo. *"Macho ya Bwana yako kila mahali, yakichunguza waovu na wema,"* na *"kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya."* (**Mithali 15:3; Mhubiri 12:14**) Matendo mema na mabaya ya wakati huu yatapokea thawabu ya **haki** iwe sasa au baadaye. *"Dhambi za watu wengine zi dhahiri, zatangulia kwenda hukumuni; na za wengine zawafuata."* (**1 Timotheo 5:24**) Hakuna wengine isipokuwa "kundi dogo" la Bwana lililopendelewa ambao hadi sasa wana nuru ya kutosha kuwapata adhabu ya mwisho, yaani, mauti ya pili. Hapa tunagusia tu mada ya uwajibikaji wa ulimwengu kwa sasa, tukiacha maelezo ya kina kwa ajili ya kuzingatiwa baadaye.

Kipindi cha takriban miaka elfu sita kinapita kati ya siku ya kwanza na ya pili ya hukumu ya ulimwengu, na katika kipindi hiki kirefu Mungu amekuwa akichagua makundi mawili maalum kutoka miongoni mwa wanadamu, na kuwajaribu, kuwatia nidhamu na kuwafunza kipekee ili wawe vyombo vyake vya heshima katika kipindi au siku ya hukumu ya ulimwengu.

Makundi haya mawili yametajwa na Paulo (**Waebrania 3:5, 6**) kama nyumba ya wana na nyumba ya watumishi, lile la kwanza likiundwa na wale washindi waliojaribiwa na kuonekana waaminifu wakati wa kipindi cha Kikristo, na lile la pili likiundwa na washindi waaminifu waliotangulia kipindi cha Kikristo. Uteuzi huu maalum hauathiri kwa vyovyote ile hukumu au jaribio lililoahidiwa kwa ulimwengu wa wanadamu katika zama zitakazofuata Kipindi hiki cha Injili. Wale watakaofaulu jaribio la mojawapo ya makundi haya maalum

hawataingia hukumuni pamoja na ulimwengu, bali wataingia katika thawabu yao wakati ulimwengu unapokuja hukumuni. Watakuwa watendaji wa Mungu katika kuubariki ulimwengu—katika kuwapa wanadamu maelekezo na mafunzo muhimu kwa ajili ya jaribio na hukumu yao ya mwisho. *"Au hamjui ya kuwa watakatifu watauhukumu ulimwengu?"* **—1 Wakorintho 6:2**

Makundi haya yaliyochaguliwa kipekee, kama wanadamu wengine wote, hapo awali yalikuwa chini ya hukumu ya Adamu, lakini yakawa washiriki kwa imani katika manufaa ya kifo cha Kristo. Baada ya kuhesabiwa haki kwanza kwa kuamini ahadi za Mungu, na kisha kutimiza yale masharti yaliyofuata ya wito wao mbalimbali, wanahesabiwa kuwa wanastahili kutukuzwa juu sana kwenye nafasi za heshima na mamlaka.

Jaribio au hukumu ya makundi yote haya mawili imekuwa kali zaidi kuliko jaribio la ulimwengu litakavyokuwa katika siku yake ya hukumu; kwa sababu hawa wamelazimika kumpinga Shetani, mkuu wa ulimwengu huu, na hila zake zote na mitego yake, ilhali katika siku ya hukumu ya ulimwengengu, Kristo atakuwa akitawala, na Shetani atakuwa amefungwa, ili asiyadanganye mataifa. (**Ufunuo 20:3**) Hawa wamepata mateso kwa ajili ya uadilifu, wakati ambapo watu wa wakati ule watapewa thawabu kwa ajili ya uadilifu, na kuadhibiwa tu kwa ajili ya ukosefu wa uadilifu. Hawa wamekuwa na vikwazo vikubwa na mitego njiani mwao, vitu ambavyo vitaondolewa wakati ulimwengu utakapowekwa chini ya jaribio. Lakini ingawa jaribio la makundi haya mawili maalum limekuwa kali zaidi kuliko litakavyokuwa jaribio la ulimwengu, thawabu zao nazo ni kubwa zaidi vivyo hivyo.

Shetani, yule mdanganyifu mkuu, ametumia hoja zake potofu na kufanikiwa kuunyang'anya ulimwengu pamoja na lile Kanisa la jina tu, ule uhakika wenye baraka wa wakati ujao wa hukumu ya haki. Ingawa wanajua Biblia inasema kutakuwa na siku ya hukumu, wao huiwazia tu kwa hofu na woga mkubwa. Ndiyo maana, hakuna habari wanayoichukia kama ile inayosema, "Siku

ya Bwana imekaribia." Hujaribu kulisahau wazo hilo na hawapendi hata kulisikia likitajwa.

Hawana wazo lolote la baraka zilizoandaliwa kwa ajili ya ulimwengu chini ya utawala huo mtukufu wa yeye ambaye Mungu amemchagua kuuhukumu ulimwengu kwa haki. Miongoni mwa mvuto mkuu zaidi wa kupofusha ambao Shetani ameubuni ili kuwaweka wanadamu katika ujinga kuhusu ukweli wa siku ya hukumu, ni makosa yaliyoingia katika kanuni za imani na vitabu vya nyimbo vya madhehebu mbalimbali ya kidini. Wengi wamekuja kuyaheshimu makosa haya kuwa ya umuhimu mkuu kuliko Neno la Mungu.

Jinsi gani manabii na mitume walivyoiona tofauti siku hiyo ya hukumu iliyoahidiwa! Angalia tamko la kinabii lenye shangwe kuu la Daudi (**1 Mambo ya Nyakati 16:31-34**). Anasema:

> *"Mbingu na zifurahi, nchi na ishangilie; Na waseme katika mataifa, Bwana ametamalaki; Bahari na ivume na vyote viijazavyo; Mashamba na yashangilie na vyote vilivyomo; Ndipo miti yote ya mwituni iimbe kwa furaha, Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema; Kwa maana fadhili zake ni za milele."*

Mtume pia anaielekezea siku hiyo hiyo, akituhakikishia kwamba itakuwa siku tukufu na ya kutamanika, na kwamba kwa ajili yake viumbe vyote vinaugua na kuwa na utungu pamoja—vikimngojea Mwamuzi mkuu aokoe na kuubariki ulimwengu, na pia kuliinua na kulitukuza Kanisa. —**Warumi 8:21, 22.**

Katika Yohana 5:28, 29, ahadi ya thamani kwa ajili ya ulimwengu ya jaribio la hukumu ijayo la kupata uzima wa milele, imegeuzwa, kwa tafsiri isiyo sahihi, kuwa laana ya kutisha. Kulingana na Kigiriki, wale waliotenda mabaya—wale waliokosa kibali cha Mungu—watatoka kwa ajili ya ufufuo [kuinuliwa hadi ukamilifu] kwa njia ya hukumu, "mapigo," na nidhamu.

### ***Baadaye***

*"Njia za Mungu ni sawa: dhoruba au shwari, Majira ya hatari na ya pumziko, Mshale unaoumiza, zeri iponyayo, Vyote vimegawanywa inavyofaa. Katika hukumu zisizoeleweka, Kwa njia za siri na fiche, Hutoa mema yadumuyo toka uovuni, Na kuhakikisha furaha ya mwisho. Wakati Haki ikishika mkondo kwa nguvu, Upendo wakuza imani na tumaini: Ataipa dunia iliyorudiwa hatimaye Amani yake ya baadaye.*

*"Wakati nguvu za kutisha za upepo Zikitimiza makusudi yake makali, Na ujuzi wa mtu haufai kitu Dhidi ya ghadhabu ya dhoruba, Mioyo ipendayo imtumaini bado, Kwenye njia ya giza na tatanishi; Nani angepinga mapenzi yake mema, Yaongozayo toka usiku hadi furaha? Tulia chini ya utunzaji wake, Maana ataikomesha dhoruba, Na kuleta toka maumivu haya Amani ya baadaye.*

*"Tazama juu, Ee Dunia; dhoruba haidumu Kupita mipaka Mungu aliyoweka. Kazi yake iliyopangwa ikisha, Kwa furaha utasahau huzuni. Palipopita jembe la huzuni, Maua yako mazuri yatachipuka, Maana Mungu atakupa uzima upya, Na magofu yako yatacheka na kuimba. Mtumaini yeye; mpango wake kwako Utaishia ushindi na uhuru. Usiogope, maana hakika utaiona Amani yake ya baadaye."*

## SOMO LA IX

# FIDIA NA UREJESHO

UREJESHO ULIOHAKIKISHWA KWA FIDIA — SI UZIMA WA MILELE, BALI KUJARIBIWA KWA AJILI YAKE, KULIKOPATIKANA KWA FIDIA — MASHARTI NA MANUFAA YA KUJARIBIWA HUKO — DHABIHU YA KRISTO ILIKUWA YA LAZIMA — JINSI JAMII ILIVYOWEZA NA ILIVYOKOMBOLEWA KWA KIFO CHA MMOJA — IMANI NA MATENDO BADO NI VYA LAZIMA — MSHAHARA WA DHAMBI YA MAKUSUDI NI HAKIKA — JE, KUTAKUWA NA NAFASI DUNIANI KWA AJILI YA MAMILIONI WATAKAOFUFULIWA? — UREJESHO DHIDI YA MAGEUZI.

KUTOKANA na muhtasari wa mpango wa Mungu uliofunuliwa, kama ilivyoainishwa mpaka sasa, ni dhahiri kwamba kusudi lake kwa wanadamu ni urejesho au kurudishwa kwenye ukamilifu na utukufu uliopotea Edeni. Ushahidi wenye nguvu zaidi, na wa kuhitimisha, juu ya suala hili unaonekana wazi zaidi wakati ukubwa na asili ya fidia inapoeleweka na kuthaminiwa kikamilifu. Urejesho uliotabiriwa na mitume na manabii lazima ufuate fidia kama mtiririko wa haki na wa kimantiki. Kulingana na mpangilio wa Mungu katika kutoa fidia, wanadamu wote, isipokuwa kama wataipinga kwa makusudi nguvu ya kuokoa ya Mkombozi Mkuu, lazima wawekwe huru kutoka katika ile adhabu ya asili, '*utumwa wa uharibifu*,' **yaani mauti**, la sivyo fidia hiyo haitafaa kwa ajili ya wote.

Hoja ya Paulo juu ya somo hili iko wazi sana na ina msisitizo. Anasema (**Warumi 14:9**), *"Kwa maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, anawamiliki [ mtawala, msimamizi] waliokufa na walio hai pia."* Yaani, lengo la kifo na ufufuo wa Bwana wetu halikuwa tu kuwabariki, kuwatawala na kuwarejesha walio hai, bali kumpa mamlaka juu ya, au udhibiti kamili wa, waliokufa na walio hai pia, na hivyo kuhakikisha manufaa ya fidia yake yanawafikia wote kwa usawa. Ali * *"jitoa mwenyewe kuwa fidia [bei*

* *Tunaweza kutambua ipasavyo maana ya ziada na pana zaidi katika maneno ya Mtume; yaani, kwamba familia nzima ya wanadamu ilijumuishwa katika usemi "waliokufa." Kwa mtazamo wa Mungu, jamii nzima ya wanadamu, ikiwa chini ya hukumu ya kifo, inahesabiwa kana kwamba imekufa tayari (**Mathayo 8:22**); kwa hiyo usemi "walio hai" ungehusisha viumbe wengine nje ya familia ya wanadamu ambao maisha yao hayakupotezwa – yaani, malaika*

*sawasawa] kwa ajili ya wote,"* ili aweze kuwabariki wote, na kumpa kila mwanadamu jaribio la mtu binafsi la kupata uzima. Kudai kwamba alijitoa *"kuwa fidia kwa ajili ya* ***wote,"*** na wakati huohuo kudai kwamba ni wachache tu miongoni mwa waliokombolewa watakaowahi kupata manufaa yoyote kutoka kwayo, ni upuuzi. Madai kama hayo yangeashiria mojawapo ya mambo mawili: aidha Mungu aliikubali bei ya fidia kisha kwa dhuluma akakataa kuwaachilia huru waliokombolewa, au Bwana, baada ya kuwakomboa wote, hakuwa na uwezo au nia ya kutekeleza lile kusudi la awali lenye wema. Ukweli kwamba mipango ya Mungu haibadiliki, pamoja na ukamilifu wa haki na upendo wake, unapingana na wazo kama hilo na unalifutilia mbali. Hii inatupa hakikisho kwamba mpango wa asili na wa wema, ambao msingi wake ulikuwa "**fidia kwa ajili ya wote,"** utatekelezwa kikamilifu katika "**wakati ufaao**" wa Mungu. Mpango huo utawaletea waamini waaminifu baraka ya kuachiliwa kutoka katika hukumu ya Adamu na fursa ya kurudi kwenye haki na uhuru wa wana wa Mungu, kama ilivyokuwa kabla ya dhambi na laana.

### Si Uzima wa Milele, bali Jaribio la Kuupata, Linalohakikishwa na Fidia

Manufaa na matokeo halisi ya fidia yanapoeleweka wazi, mapingamizi yote juu ya matumizi yake kwa wote lazima yatoweke. "Fidia kwa ajili ya wote" iliyotolewa na "mwanadamu Kristo Yesu" haimpi wala haimhakikishii mwanadamu yeyote uzima wa milele au baraka; lakini inamhakikishia kila mwanadamu **fursa nyingine au jaribio** la kupata uzima wa milele.

Jaribio la kwanza la mwanadamu, lililosababisha kupotea kwa baraka alizopewa mwanzoni, kwa kweli linageuzwa kuwa baraka ya uzoefu kwa wale wenye mioyo ya uaminifu, kwa sababu ya **fidia** ambayo Mungu ameiandaa. Lakini ukweli kwamba wanadamu wamekombolewa kutoka katika adhabu ya kwanza hakuondoi uwezekano wa wao kushindwa kutoa ule

utii, ambao bila huo hakuna atakayeruhusiwa kuishi milele, watakapojaribiwa mmoja mmoja kwa ajili ya uzima wa milele.

Mwanadamu, kwa sababu ya uzoefu wa sasa wa dhambi na adhabu yake chungu, ataonywa kikamilifu; na atakapopewa jaribio lingine, la mtu binafsi, kama matokeo ya fidia, chini ya uangalizi na usimamizi wa yeye aliyempenda kiasi cha kutoa maisha yake kwa ajili yake, na ambaye hataki yeyote apotee, bali wote wamgeukie Mungu na kuishi, tunaweza kuwa na hakika kwamba ni wasiotii kwa makusudi tu ndio watakaopokea adhabu ya jaribio la pili. Adhabu hiyo itakuwa ni **mauti ya pili**, ambayo hakutakuwa na fidia, wala ukombozi, kwa sababu kusingekuwa na lengo la fidia nyingine au jaribio zaidi. Wote watakuwa wameona na kuonja kikamilifu mema na mabaya; watakuwa wameshuhudia na kuhisi wema na upendo wa Mungu; na kila mmoja atakuwa amepata jaribio lake kamili na la haki kwa ajili ya uzima, chini ya mazingira yenye neema zaidi. Hakuna zaidi kinachoweza kuombwa, na wala hakuna zaidi kitakachotolewa. Jaribio hilo litaamua milele ni nani angekuwa mwenye haki na mtakatifu hata katika majaribio elfu; na litaamua pia ni nani angekuwa dhalimu, asiye mtakatifu na mwenye kuendelea kuwa mchafu, hata katika majaribio elfu.

### Masharti na Faida za Jaribio

Haitakuwa na faida kutoa jaribio lingine la uzima chini ya hali zilezile. Ingawa hali za wale watakaojaribiwa zitakuwa tofauti, yaani, zenye fadhila zaidi, vigezo au masharti ya jaribio lao la mtu mmoja mmoja la kupata uzima vitakuwa vilevile kama katika jaribio la Adamu. Sheria ya Mungu itabaki ileile—haibadiliki. Bado itasema, *"Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa"*; na hali ya mwanadamu, kwa upande wa mazingira, haitakuwa bora zaidi kuliko hali na mazingira ya Edeni.

Lakini tofauti kubwa itakuwa ni **maarifa yaliyoongozeka**. **Uzoefu** wa uovu, ukilinganishwa na uzoefu wa wema, ambao kila mmoja ataupata wakati wa jaribio katika zama zijazo, ndio

utakaokuwa faida ambayo kwayo matokeo ya jaribio la pili yatatofautiana sana na matokeo ya la kwanza. Na ni kwa sababu hii ndiyo Hekima na Upendo wa kimungu viliandaa "fidia kwa ajili ya wote," na hivyo kuwahakikishia wote baraka ya jaribio jipya. Hakuna jaribio bora zaidi, hakuna sheria bora zaidi, hakuna masharti au hali bora zaidi zinazoweza kufikiriwa kama sababu za fidia nyingine au jaribio zaidi kwa yeyote baada ya Zama za Milenia.

Fidia iliyotolewa haitoi kisingizio cha dhambi kwa yeyote; haikusudii **kuwahesabu** wenye dhambi kama watakatifu, na hivyo kuwaingiza katika raha ya milele. Inamwachilia tu mwenye dhambi anayeikubali kutoka katika hukumu ya kwanza na matokeo yake, ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja, na kumweka tena kwenye jaribio la kupata uzima. Katika jaribio hilo, utii wake wa makusudi au uasi wake wa makusudi ndio utakao amua kama atapata uzima wa milele au la.

Wala isidhaniwe, kama wengi wanavyoonekana kupenda kudhani, kwamba wote wanaoishi katika hali ya ustaarabu, na kuiona au kumiliki Biblia, wamekwisha pata fursa kamili au jaribio la uzima. Lazima ikumbukwe kwamba anguko halijawaathiri watoto wote wa Adamu kwa usawa. Wengine wamekuja ulimwenguni wakiwa dhaifu na potovu kiasi cha kupofushwa kwa urahisi na mungu wa dunia hii, Shetani, na kuchukuliwa mateka na dhambi inayowazunguka na kuwavamia. Na wote, kwa kiwango fulani, wako chini ya ushawishi huu, kiasi kwamba, hata wanapotaka kutenda mema, uovu upo na una nguvu zaidi kupitia mazingira, n.k., na mema wanayotaka kuyatenda karibu hayawezekani, huku maovu wasiyotaka kuyatenda karibu hayaepukiki.

Ni wachache mno wale ambao kwa wakati huu wanajifunza kweli na kwa uzoefu juu ya uhuru ambao Kristo huwaweka huru wale wanaoikubali fidia yake, na kujiweka chini ya usimamizi wake kwa ajili ya mwongozo wa wakati ujao. Hata hivyo, ni wachache hawa tu, yaani, Kanisa, walioitwa na kujaribiwa kabla

ya wakati kwa kusudi maalum la kuwa wafanyakazi pamoja na Mungu katika kuubariki ulimwengu—wakitoa ushahidi sasa, na kuutawala, kuubariki na kuuhukumu ulimwengu katika zama zake za jaribio—ndio wanaofurahia kwa kiasi chochote manufaa ya fidia, au wako **sasa** kwenye jaribio la kupata uzima.

Wachache hawa **wanahesabiwa** (na wanapokea **kwa imani**) baraka zote za urejesho ambazo zitaandaliwa kwa ajili ya ulimwengu katika zama zijazo. Hawa, ingawa si wakamilifu, wala hawajarejeshwa kihalisi katika hali ya Adamu, wanatendewa kwa namna inayofidia tofauti hiyo. Kupitia imani katika Kristo **wanahesabiwa** kuwa wakamilifu, na hivyo wanarejeshwa kwenye ukamilifu na upendeleo wa kimungu, kana kwamba si wenye dhambi tena. Kutokamilika kwao na udhaifu wao usioweza kuepukika, vikifidiwa na fidia, havihesabiwi kwao, bali vinafunikwa na ukamilifu wa Mkombozi. Kwa hiyo, jaribio la Kanisa, kwa sababu ya hadhi yake ya kuhesabiwa katika Kristo, ni la haki kama lile ambalo ulimwengu utakuwa nalo katika wakati wake wa jaribio. Ulimwengu wote utaletwa kwenye ujuzi kamili wa kweli, na kila mmoja, anapokubali maandalizi na masharti yake, hatatendewa tena kama mwenye dhambi, bali kama mwana, ambaye baraka zote za urejesho zimekusudiwa kwake.

Tofauti moja kati ya uzoefu wa ulimwengu chini ya jaribio na uzoefu wa Kanisa wakati wa jaribio lake itakuwa kwamba watiifu wa ulimwengu wataanza mara moja kupokea baraka za urejesho kwa kuondolewa taratibu kwa udhaifu wao—wa kiakili na kimwili; ilhali Kanisa la Injili, lililowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi wa Bwana hata mauti, linaingia katika mauti na kupata ukamilifu wake mara moja katika ufufuo wa kwanza. Tofauti nyingine kati ya majaribio hayo mawili ni katika mazingira bora zaidi ya zama zijazo ikilinganishwa na hizi, kwa kuwa wakati huo jamii, serikali, n.k., vitapendelea haki, vikitunuku imani na utii, na kuadhibu dhambi; ilhali sasa, chini ya mkuu wa ulimwengu huu, jaribio la Kanisa liko chini ya hali zisizopendelea haki, imani, n.k. Lakini hili, kama tulivyoona, litafidiwa kwa tuzo

ya utukufu na heshima ya asili ya kimungu inayotolewa kwa Kanisa, pamoja na zawadi ya uzima wa milele.

### Ulazima wa Dhabihu ya Kristo

Kifo cha Adamu kilikuwa cha uhakika, ingawa kilifikiwa kwa miaka mia tisa thelathini ya kufa. Kwa kuwa yeye mwenyewe alikuwa akifa, watoto wake wote walizaliwa katika hali hiyo hiyo ya kufa na bila haki ya uzima; na, kama wazazi wao, wote hufa baada ya mchakato mrefu au mfupi. Ikumbukwe, hata hivyo, kwamba si maumivu na mateso katika kufa, bali ni kifo—**kutoweka kwa uhai**—ambako ndiko kilele cha kufa, ndiyo adhabu ya dhambi. Mateso ni sehemu ya ziada tu, na adhabu huwapata wengi ikiwa na mateso kidogo au bila mateso kabisa. Ikumbukwe zaidi kwamba Adamu alipopoteza uhai, aliupoteza milele; na hakuna hata mmoja wa wazao wake aliyewahi kuweza kufidia hatia yake au kurejesha ule urithi uliopotea.

Kizazi chote kimekufa au kiko katika hali ya kufa. Na ikiwa hawakuweza kufuta hatia yao kabla ya kufa, hakika hawawezi kufanya hivyo wakiwa wamekufa—yaani, wakiwa hawapo tena. Adhabu ya dhambi haikuwa kufa tu, huku kukiwa na upendeleo na haki ya kurudi kwenye uzima baadaye. Katika adhabu iliyotamkwa, hakukuwa na dokezo lolote la kuachiliwa huru. (Mwa. 2:17) Hivyo, Urejesho ni tendo la neema ya bure au hisani kwa upande wa Mungu. Na mara tu adhabu ilipoingia, hata wakati ilipokuwa ikitamkwa, hisani ya bure ya Mungu ilidokezwa, ambayo, itakapotimizwa, itatangaza upendo wake kikamilifu sana.

### Jinsi Jamii ya Wanadamu Ilivyoweza Kukombolewa na Ilivyokombolewa kwa Kifo cha Mmoja

Kama isingekuwa kwa mwanga wa tumaini, uliotolewa na kauli kwamba uzao wa mwanamke ungeponda kichwa cha nyoka, jamii ya wanadamu ingekuwa katika hali ya kukata tamaa kabisa;

lakini ahadi hii ilionyesha kwamba Mungu alikuwa na mpango fulani kwa manufaa yao. Mungu alipomwapia Ibrahimu kwamba katika uzao wake jamaa zote za dunia zitabarikiwa, ilimaanisha ufufuo au urejesho wa wote; kwa maana wengi walikuwa wamekufa wakati huo, na wengine wamekufa tangu wakati huo, bila kubarikiwa. Hata hivyo, ahadi bado ni ya hakika: wote watabarikiwa *"nyakati za kuburudishwa"* zitakapokuja. (**Matendo 3:19**) Zaidi ya hayo, kwa kuwa baraka inaashiria upendeleo, na kwa kuwa upendeleo wa Mungu uliondolewa na laana yake ikaja badala yake kwa sababu ya dhambi, ahadi hii ya baraka ya wakati ujao ilimaanisha kuondolewa kwa laana, na hivyo kurudi kwenye upendeleo wake. Pia ilimaanisha kwamba ama Mungu angelegeza msimamo, kubadili hukumu yake na kuiondolea hatia jamii hiyo, au la sivyo alikuwa na mpango fulani ambao ungewezesha ikombolewe, kwa adhabu ya mwanadamu kulipwa na mwingine.

Mungu hakumwacha Ibrahimu katika mashaka kuhusu upi ulikuwa mpango wake, bali alionyesha, kwa dhabihu mbalimbali za mfano ambazo wote waliomkaribia ilibidi wazilete, kwamba hakuweza na hakulegeza msimamo, wala kuisamehe dhambi; na kwamba njia pekee ya kuifuta na kuiondoa adhabu yake ingekuwa ni kwa dhabihu ya kutosha kulipia adhabu hiyo. Jambo hili lilionyeshwa kwa Abrahamu kupitia kielelezo muhimu sana: Mwanawe, ambaye alikuwa kitovu cha ile baraka ya ahadi, alipaswa kwanza kutolewa kama dhabihu kabla ya yeye kuweza kubariki. Na kwa njia ya mfano, Abrahamu alimpokea tena kutoka kwa wafu. (**Waebrania 11:19**) Katika mfano huo Isaka aliwakilisha uzao wa kweli, Kristo Yesu, aliyekufa ili kuwakomboa wanadamu, ili waliokombolewa wote waweze kupokea baraka iliyoahidiwa. Kama Ibrahimu angefikiri kwamba Bwana angesamehe na kumwachilia mwenye hatia, angehisi kwamba Mungu alikuwa anabadilika, na kwa hiyo asingeweza kuwa na imani kamili katika ahadi aliyopewa. Angeweza kusema, Ikiwa Mungu amebadili nia yake mara moja,

kwa nini asibadili tena? Ikiwa atalegeza msimamo kuhusu laana ya kifo, je, hawezi kulegeza tena kuhusu fadhila na baraka aliyoahidi? Lakini Mungu hatuachi katika hali kama hiyo ya kutokuwa na uhakika. Anatupa hakikisho la kutosha la haki yake na kutobadilika kwake. Hakuweza kumwachilia mwenye hatia, ingawa aliwapenda sana kiasi kwamba *"hakumwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa [kwa mauti] kwa ajili yetu sote."*

Kama vile jamii nzima ya wanadamu ilivyokuwa ndani ya Adamu alipohukumiwa, na kupoteza uhai kupitia yeye, ndivyo Yesu alipojitoa *"kuwa fidia kwa ajili ya wote,"* kifo chake kilihusisha uwezekano wa jamii isiyozaliwa iliyokuwa katika viuno vyake. Malipo kamili, au bei sawasawa, kwa ajili ya wanadamu wote hivi yaliwekwa mikononi mwa Haki—ili yatumike "kwa wakati ufaao," na yeye ambaye hivyo **aliwanunua wote** ana mamlaka kamili ya kuwarejesha wote wanaomjia Mungu kupitia yeye.

> *"Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki." (**Warumi 5:18, 19**)*

Hoja iko wazi: Wengi kadiri walivyoshiriki mauti kwa sababu ya dhambi ya Adamu, watapewa fursa za uzima na Bwana wetu Yesu, aliyekufa kwa ajili yao na kwa kujitoa dhabihu akawa **mbadala wa Adamu** mbele ya sheria iliyovunjwa, na hivyo *"akajitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote."* Alikufa, *"mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili atulete kwa Mungu."* (**1 Petro 3:18**) Hata hivyo, isisahaulike kamwe kwamba maandalizi yote ya Mungu kwa ajili ya jamii yetu yanatambua utashi wa mwanadamu kama jambo muhimu katika kupata fadhila za kimungu zilizoandaliwa kwa wingi. Wengine wamepuuza sifa hii walipokuwa wakichunguza andiko lililotajwa —Warumi 5:18, 19. Hata hivyo, kauli ya Mtume ni kwamba, kama vile hukumu ya adhabu ilivyowafikia uzao wote wa Adamu, vivyo hivyo, kupitia

utii wa Bwana wetu Yesu Kristo kwa mpango wa Baba, kwa kujitoa dhabihu kwa niaba yetu, karama ya bure inatolewa kwa wote—karama ya msamaha, ambayo, ikikubaliwa, itaunda msingi wa kuhesabiwa haki kupata uzima wa milele. Na *"kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi **waliingizwa** katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi **wataingizwa** [si **waliingizwa**] katika hali ya wenye haki."* Kama fidia pekee, bila sisi kuikubali, ingetufanya wenye haki, basi ingesomeka, kwa kutii kwake mmoja watu wengi **waliingizwa** katika hali ya wenye haki.

Lakini ingawa bei ya fidia imetolewa na Mkombozi, ni wachache tu katika Zama za Injili waliofanywa wenye haki—waliohesabiwa haki—*"kwa imani katika damu yake."* Hata hivyo, kwa kuwa Kristo ndiye upatanisho (malipo ya kuridhisha) kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote, watu wote wanaweza kwa sababu hii kusamehewa na kuachiliwa kutoka katika adhabu ya dhambi ya Adamu na yeye—chini ya Agano Jipya.

Kabla ya kuichunguza njia hii, hatari zake na magumu yake, hebu tuangalie mwisho wake ni—**uzima.** Kama tulivyokwishaona, uzima unaweza kufurahiwa katika viwango mbalimbali vya uwepo, vya juu na vya chini kuliko vya kibinadamu. Uzima ni neno pana na lenye maana nyingi, lakini hapa Bwana wetu analitumia kurejelea aina ile ya juu zaidi ya uzima, inayohusiana na asili ya kimungu—**kutokufa**—tuzo ambayo alitualika kuikimbilia.

Uzima ni nini? Sisi si tu kwamba tunauhisi ndani yetu, bali tunaona utendaji wake kwa wanyama wa chini, na hata katika mimea, na tunaambiwa juu ya uwepo wake katika aina za juu zaidi, za kimalaika na za kimungu. Tutawezaje kulifafanua neno lenye maana pana kiasi hiki?

Ingawa hatuwezi kugundua chanzo halisi cha uhai katika kila kiumbe, tunaweza kusema kwa uhakika kwamba Mungu Mwenyewe, Yehova, ndiye chemchemi kuu ya uhai wote, na vyanzo vingine vyote vinatokana nayeye. Vitu vyote vilivyo hai vinatokana nayeye na vinamtegemea yeye ili viendelee kuwa hai.

Uhai wote, uwe ule ulio ndani ya Mungu au ule ulio katika viumbe vyake, ni uleule: ni **kanuni inayohuisha** (inayotia nguvu), na si kitu kinachoonekana au kushikika. Ni kanuni ambayo ni sehemu ya asili ya Mungu mwenyewe, lakini kwa viumbe vyake,

uhai unatokana na taratibu fulani alizoziweka Mungu. Hivyo basi, yeye ndiye chanzo, mtunzi na chemchemi ya uhai huo. Hivyo, kiumbe si sehemu ya dhati ya Muumba wala si uzao wa asili yake, kama wengine wanavyofikiri; bali ni kazi ya mikono ya Mungu iliyotiwa uhai.

Tukitambua ukweli kwamba ni katika asili ya Uungu pekee ndimo uhai unajitegemea, hauna kikomo, hauishi, unaendelea daima na hauzalishwi wala kuongozwa na mazingira, tunaona kwamba kwa ulazima Yehova yuko juu ya sheria za kimwili na mahitaji aliyoyaweka kwa ajili ya kuwategemeza viumbe vyake. Ni sifa hii, inayohusiana na asili ya Uungu pekee, ndiyo inayoelezewa kwa neno **kutokufa**. Kama ilivyoonyeshwa katika sura iliyotangulia, **asiyekufa** humaanisha asiyeweza kufa, na hivyo pia asiyeweza kupata magonjwa na maumivu. Kwa kweli, **kutokufa** kunaweza kutumika kama neno lenye maana sawa na **uungu**. Kutoka katika chemchemi ya kimungu, isiyokufa, hutiririka uhai na baraka zote, kila kipawa chema na kikamilifu, kama vile dunia inavyopokea nuru na nguvu zake kutoka kwenye Jua.

Jua ndiyo chemchemi kuu ya nuru kwa dunia, likiangaza vitu vyote, likizalisha aina nyingi za rangi na vivuli vya nuru, kulingana na asili ya kitu kinachoangaziwa. Mwangaza uleule wa jua ukiangaza juu ya almasi, juu ya tofali, na juu ya aina mbalimbali za vioo, huleta athari tofauti sana. Nuru ni ileile, lakini vitu vinavyoangaziwa vinatofautiana katika uwezo wao wa kuipokea na kuipitisha. Ndivyo ilivyo na uzima: wote hutiririka kutoka katika chemchemi moja isiyokwisha. Chaza ana uhai, lakini mwili wake umeumbwa kiasi kwamba hauwezi kutumia uhai mwingi, kama vile tofali lisivyoweza kuakisi nuru nyingi ya jua. Ndivyo ilivyo na kila onyesho la juu la uhai, katika mnyama, samaki na ndege. Kama aina mbalimbali za vioo chini ya mwangaza wa jua, ndivyo viumbe hawa mbalimbali wanavyoonyesha tofauti mbalimbali za nguvu za miili yao, wakati uhai unapoihuisha.

Almasi iliyong'arishwa imeumbwa kwa ajili ya nuru kiasi kwamba inaonekana kana kwamba ina nuru ndani yake yenyewe, na ni jua dogo. Ndivyo ilivyo kwa mwanadamu, mojawapo ya kazi bora za uumbaji wa Mungu, aliyefanywa tu *"mdogo punde kuliko malaika."* Aliumbwa kwa ustadi mkuu kiasi cha kuweza kupokea na kuhifadhi uzima kwa kutumia njia ambazo Mungu aliziandaa, na kamwe asififie. Hivyo ndivyo Adamu alivyokuwa kabla ya kuanguka, mkuu kuliko kiumbe mwingine yeyote wa duniani, si kwa sababu ya tofauti yoyote katika **kanuni ya uhai** iliyopandikizwa, bali kwa sababu ya **mwili bora zaidi**.

Hata hivyo, tukumbuke kwamba kama vile almasi isivyoweza kuakisi nuru isipokuwa jua linaimulika, ndivyo mwanadamu anavyoweza kuwa na uhai na kuufurahia pale tu anapoendelea kupewa uhai huo. Mwanadamu hana uhai ambao ni sehemu ya asili yake; yeye si chemchemi ya uhai, kama vile almasi isivyo chemchemi ya nuru.

Na moja ya uthibitisho imara zaidi unaoonyesha kwamba hatuna akiba isiyoisha ya uhai ndani yetu—au kwa maneno mengine, kwamba sisi si viumbe visivyoweza kufa—ni huu: tangu dhambi ilipoingia, mauti imewapata wanadamu wote.

Mungu alikuwa amepanga kwamba mwanadamu katika Edeni aweze kufikia miti yenye kuendeleza uhai, na paradiso alimowekwa ilikuwa na miti mingi ya *"kila [aina ya] mti"* mzuri kwa chakula au kwa pambo. (**Mwanzo 2:9, 16, 17**) Miongoni ile miti ya uzima iliyokuwa mizuri kwa chakula, kulikuwa na mmoja uliokatazwa. Ingawa kwa muda alikatazwa kula mti wa ujuzi, aliruhusiwa kula kwa uhuru ile miti ambayo iliutegemeza uhai kwa ukamilifu; na alitenganishwa nayo tu baada ya kosa, ili kwa njia hiyo ile adhabu ya mauti ianze kufanya kazi. —**Mwanzo 3:22**

Hivyo, utukufu na uzuri wa mwanadamu unaonekana kutegemea kuendelea kupewa uhai, kama vile uzuri wa almasi unavyotegemea kuendelea kumulikwa na jua. Dhambi

ilipomnyang'anya mwanadamu haki ya kuishi na akaacha kupewa uhai huo, papo hapo kito hicho (mwanadamu) kilianza kupoteza mng'ao na uzuri wake, na mwishowe anapoteza chembe ya mwisho ya uzuri wake kaburini.

*"Ukimrudi mtu kwa kumkemea kwa uovu wake, Watowesha uzuri wake kama nondo."* (Zab. 39:11) Kama vile almasi inavyopoteza uzuri na mng'ao wake nuru inapoondolewa, ndivyo mwanadamu anavyopoteza uhai Mungu anapomnyima uhai huo. *"Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia; Naam, mwanadamu hutoa roho, naye yupo wapi?"* (Ayu. 14:10) *"Wanawe hufikilia heshima, wala yeye hajui; Kisha wao huaibishwa, lakini yeye hana habari zao."* (Ayu. 14:21) *"kwa maana hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe."* (Mhu. 9:10) Lakini kwa kuwa fidia imepatikana, na kwa kuwa adhabu ya kifo imelipwa na Mkombozi, kito hicho kitarejeshewa uzuri wake. Kitaakisi tena kikamilifu sura ya Muumba, hapo *"jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake."* (Mal. 4:2) Ni kwa sababu ya dhabihu ya dhambi, yaani dhabihu ya Kristo, ndiyo maana *"watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka."* Kutakuwa na urejesho wa vitu vyote; kwanza, kutakuwa na fursa ya urejesho kwa wote, na hatimaye wote watakaomtii Mkombozi watafikia ukamilifu wa kibinadamu.

Hata hivyo, hii siyo thawabu anayoirejelea Yesu kama mwisho wa njia nyembamba. Kutoka katika maandiko mengine tunajifunza kwamba thawabu iliyoahidiwa kwa wale wanaotembea katika njia nyembamba ni "**asili ya Uungu**"—uhai wa asili, uhai katika kiwango kile cha juu kabisa ambacho ni asili ya kimungu pekee inayoweza kuwa nacho—yaani, **kutokufa**. Ni tumaini kubwa kama nini! Je, tunathubutu kutamani kilele cha utukufu kama hicho? Hakika si bila mwaliko wa wazi na wa moja kwa moja ndipo yeyote angepewa haki ya kutamani hivyo.

Kutoka **1 Timotheo 6:14-16**, tunajifunza kwamba asili ya kutokufa, yaani Asili ya Mungu, mwanzoni ilikuwa ni sifa ya Mungu pekee. Tunasoma sehemu ya aya hizo ikisema:

*"...[Yesu] kwa majira yake [Enzi ya Milenia] atakudhihirisha, yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona."*

Viumbe wengine wote, kama vile malaika, wanadamu, wanyama, ndege, samaki, n.k., ni kama vyombo tu, ambavyo kila kimoja kimepewa kiasi chake cha uhai. Na vyote vinatofautiana kwa tabia, uwezo, na ubora, kulingana na umbo ambalo Muumba amependa kumpa kila mmoja.

Zaidi ya hayo, tunajifunza kwamba Yehova, ambaye peke yake ndiye aliyekuwa na hali ya kutokufa mwanzoni, amemwinua sana Mwanawe, Bwana wetu Yesu, kwenye asili ileile ya kimungu, isiyoweza kufa; kwa hiyo sasa yeye ndiye chapa kamili ya nafsi ya Baba. (**Waebrania 1:3**) Hivyo tunasoma, *"Kama vile Baba alivyo na **UZIMA NDANI YAKE MWENYEWE** [ufafanuzi wa Mungu wa "kutokufa" – uzima ndani yake mwenyewe – usiotokana na vyanzo vingine, wala kutegemea mazingira, bali uzima unaojitegemea, wa asili], **vivyo hivyo** alimpa na Mwana kuwa na **UZIMA NDANI YAKE MWENYEWE**."* (**Yohana 5:26**)

Basi, tangu ufufuo wa Bwana Yesu, viumbe wawili hawawezi kufa; na, ni neema ya ajabu kama nini! toleo lilelile linatolewa kwa Bibi-arusi wa Mwana-Kondoo, anayechaguliwa wakati wa Zama za Injili. Hata hivyo, si wote wa kundi kubwa la watu ambao ni wa Kanisa kwa jina tu watakaopokea tuzo hii kuu, bali ni lile "**kundi dogo**" tu la washindi wanaokimbia ili kuipata; wanaofuata kwa karibu nyayo za Bwana wao; ambao, kama yeye, wanatembea katika njia nyembamba ya dhabihu, hata mauti.

Hawa, watakapozaliwa upya kutoka kwa wafu katika ufufuo, watakuwa na Asili ya Mungu na umbo la Mungu. Huku kutokufa, yaani ile Asili ya uungu ya kujitegemea na isiyotegemea kingine kuwepo, ndio uhai ambao ile "njia nyembamba"inaelekea.

Kundi hili halitafufuliwa kutoka kaburini likiwa na miili ya kibinadamu; kwa maana Mtume anatuhakikishia kwamba, ingawa *"hupandwa mwili wa asili,"* utafufuliwa ukiwa *"mwili wa roho."* Hawa wote *"watabadilishwa,"* na kama vile walivyoichukua sura ya yule wa duniani, yaani asili ya kibinadamu, ndivyo watakavyoichukua sura ya yule wa mbinguni. Lakini *"haijadhihirika bado tutakavyokuwa"*—yaani, jinsi mwili wa kiroho ulivyo; lakini *"twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye,"* na tutashiriki katika *"utukufu ule utakaofunuliwa."*—**1 Yohana 3:2; Wakolosai 1:27; 2 Wakorintho 4:17; Yohana 17:22; 1 Petro 5:10; 2 Wathesalonike 2:14**

Si tu kwamba wito huu mkuu wa **mabadiliko ya asili** umetengwa kwa ajili tu ya Zama za Injili, bali ndilo toleo pekee la zama hizi. Kwa hiyo maneno ya Bwana wetu yaliyonukuliwa mwanzoni mwa sura hii yanawajumuisha katika njia pana iendayo upotevuni wote wasio katika njia iendayo kwenye tuzo pekee **inayotolewa sasa**. Wengine wote bado wako kwenye njia pana—ni hawa pekee ndio hadi sasa wameepuka hukumu iliyo juu ya ulimwengu. Hii, njia pekee ya uzima iliyo wazi sasa, kwa sababu ya ugumu wake, inapata wachache wanaojali kutembea ndani yake. Umati wa wanadamu katika udhaifu wao wanapendelea njia pana, rahisi ya kujifurahisha.

Njia nyembamba, ingawa inaishia katika uzima, katika kutokufa, inaweza kuitwa njia ya mauti, kwa kuwa tuzo yake inapatikana kupitia dhabihu ya asili ya kibinadamu hata mauti. Ni njia nyembamba **ya** mauti **iendayo** uzimani. Wakiwa wamehesabiwa kuwa huru kutokana na hatia ya Adamu na adhabu ya kifo, waliojiweka wakfu wanajitoa kwa hiari au **kutoa dhabihu** haki zile za kibinadamu, zilizohesabiwa kuwa zao, ambazo kwa wakati ufaao wao, pamoja na ulimwengu kwa ujumla, wangezipokea katika uhalisia.

Kama vile yule **"mwanadamu Kristo Yesu"** alivyoutoa uhai wake dhabihu kwa ajili ya ulimwengu, ndivyo hawa nao wanavyokuwa washiriki pamoja naye katika kujitoa dhabihu. Si

kwamba dhabihu yake haikutosha na kwamba nyingine **zilihitajika**; bali ingawa yake inatosheleza kabisa, hawa wanaruhusiwa kutumika na kuteseka pamoja naye ili waweze kuwa bibi-arusi wake na warithi pamoja naye. Basi, wakati ulimwengu uko chini ya hukumu ya kifo, na unakufa **pamoja na** Adamu, "kundi dogo" hili, kupitia mchakato wa kuhesabiwa kwa imani na dhabihu, uliokwishaelezwa, wanasemekana kufa **pamoja na** Kristo. Wanajitoa dhabihu na kufa **pamoja naye** kama wanadamu, ili waweze kuwa washiriki wa asili ya Uungu na utukufu **pamoja naye**; kwa maana tunaamini kwamba kama tukifa **pamoja naye**, tutaishi pia **pamoja naye**. Kama tukiteseka **pamoja naye**, tutatukuzwa pia **pamoja**. **—Warumi 8:17 na 2 Timotheo 2:11, 12**

Mwanzoni mwa Zama za Milenia, wale ambao sasa wanatembea katika njia nyembamba watakuwa wamepata tuzo kuu waliyokuwa wakiikimbilia, yaani, kutokufa; na wakiwa wamevikwa asili ya Uungu na nguvu, watakuwa tayari kwa ajili ya kazi kuu ya kuurejesha na kuubariki ulimwengu katika zama hizo.

Kufikia mwisho wa Zama ya Injili, ile njia nyembamba iendayo kwenye hali ya kutokufa itafungwa, kwa sababu lile **'kundi dogo'** teule ambalo njia hiyo ilikusudiwa kulijaribu na kulithibitisha litakuwa limekamilika. *"Sasa ndio wakati uliokubalika"*— Sasa ndio wakati uliokubalika [Kigiriki, dektos, unaokubalika au wa kupokelewa]'—huo ndio wakati ambapo wale wanaotoa dhabihu, wakija kwa njia ya stahili za Yesu na kufanyika wafu pamoja naye, wanakubalika kwa Mungu—dhabihu ya harufu nzuri. Mauti, kama adhabu ya Adamu, haitaruhusiwa milele; itaondolewa wakati wa Zama za Milenia; Lakini, yakiwa kama dhabihu, yatakubaliwa na **kupewa thawabu** katika enzi ya Injili pekee.

Ni wakiwa kama 'viumbe vipya' tu ndipo watakatifu wa zama hii wako katika njia iendayo uzimani; na ni wakiwa kama wanadamu tu ndipo tumewekwa wakfu ili kuharibiwa, kama dhabihu. Ikiwa, tukiwa viumbe wa kibinadamu, tumekufa

pamoja na Kristo, *basi tukiwa viumbe wapya wa kiroho, tutaishi pamoja naye*. (Rum. 6:8) Nia ya Mungu ndani yetu, ile nia iliyogeuzwa, ndicho kiini cha hiyo asili mpya.

Uzima huo mpya unaweza kudhoofishwa kwa urahisi; na Paulo anatuhakikishia kwamba tunapozaliwa kwa roho kupitia kweli, kama tukiishi kwa kufuata mwili, tutakufa (tutapoteza uzima wetu), lakini kama, kupitia roho, tukiyaua matendo ya mwili (mwelekeo wa asili ya kibinadamu), sisi (kama viumbe vipya) tutaishi; kwa maana wana wa Mungu ni wale wanaoongozwa na roho ya Mungu. (**Warumi 8:13, 14**)

Hili ni wazo la muhimu mno kwa wote waliowekwa wakfu; kwa maana ikiwa tumefanya agano na Mungu la kutoa asili ya kibinadamu kuwa dhabihu, na ikiwa dhabihu hiyo ilikubaliwa naye, ni kazi bure kujaribu kuitwaa tena. Kwa Mungu, ubinadamu huo unahesabiwa kuwa umekufa sasa, na lazima ufe hasa, bila kurejeshwa tena kamwe. Basi, yote yanayoweza kupatikana kwa kurudi nyuma na kuishi kwa kufuata mwili, ni kujiridhisha kidogo kwa kibinadamu kwa gharama ya kupoteza ile asili mpya ya kiroho.

Hata hivyo, kuna wengi waliojiweka wakfu wanaotamani **tuzo**, na ambao wamezaliwa na roho, ambao kwa kiasi fulani wanashindwa na vishawishi vya ulimwengu, tamaa za mwili, au hila za ibilisi. Kwa kiasi fulani wanapoteza mtazamo wa tuzo ililowekwa mbele yetu, na kujaribu kutembea katika njia ya kati—kujaribu kuweka fadhila ya Mungu na fadhila ya ulimwengu, wakisahau kwamba *"urafiki wa ulimwengu ni uadui kwa Mungu"* (**Yakobo 4:4**), na kwamba maelekezo kwa wale wanaokimbia katika mbio za tuzo ni, Msiupende ulimwengu, na, Msitafute heshima ninyi kwa ninyi, bali ile heshima itokayo kwa Mungu pekee. **—1 Yohana 2:15; Yohana 5:44**

Hawa, wanaoipenda dunia ya sasa, lakini ambao hawajamwacha Bwana kabisa na kulidharau agano lao, wanapokea adhabu ya kuchapwa na kusafishwa kwa moto wa mateso. Kama Mtume

anavyoeleza, wanakabidhiwa kwa Shetani kwa ajili ya kuangamizwa kwa mwili, ili roho (asili mpya iliyozaliwa) iweze kuokolewa katika siku ya Bwana Yesu. (**1 Wakorintho 5:5**)

Na kama wakitiwa nidhamu ipasavyo, hatimaye watapokelewa katika hali ya kiroho. Watakuwa na uzima wa milele wa kiroho kama malaika walivyo, lakini watapoteza tuzo la kutokufa. Watamtumikia Mungu katika hekalu lake, na kusimama **mbele ya** kiti cha enzi, wakiwa na matawi ya mitende mikononi mwao (**Ufunuo 7:9-17**); lakini ingawa hiyo itakuwa tukufu, haitakuwa tukufu kama nafasi ya lile "kundi dogo" la washindi, watakaokuwa wafalme na makuhani wa Mungu, walioketi pamoja na Yesu **katika kiti cha enzi** kama bibi-arusi wake na mrithi pamoja naye, na pamoja naye kuvikwa taji ya kutokufa.

Njia yetu ni ngumu, yenye mwinuko na nyembamba, na kama isingekuwa kwamba tunapewa nguvu kwa kila hatua ya safari, tusingeweza kamwe kufikia lengo. Lakini neno la Nahodha wetu linatia moyo:

*"Jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu"; "Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu."* (**Yohana 16:33; 2 Wakorintho 12:9**)

Magumu ya njia hii yamekusudiwa kutumika kama kanuni ya kutenganisha ili kuwatakasa na kuwasafisha *"watu wa pekee"* ili wawe *"warithi wa Mungu, na warithi pamoja na Yesu Kristo."* Kwa mtazamo wa mambo haya, *"na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji,"* huku tukipiga vita vizuri vya imani na kuishikilia *"taji ya utukufu"*—kutokufa, asili ya Uungu. —**2 Timotheo 4:8; 1 Petro 5:4.**

**Njia Kuu ya Utakatifu**

Wakati tumaini maalum la Zama za Injili ni la utukufu upitao kiasi, na njia iendayo kwake ni ngumu vivyo hivyo—nyembamba, yenye kuzungukwa na magumu na hatari kila hatua—

kiasi kwamba ni wachache wanaoiona, na kupata tuzo kuu mwishoni mwake, utaratibu mpya wa mambo katika zama zijazo utakuwa tofauti kabisa.

Kama vile tumaini tofauti linavyotolewa, ndivyo pia **njia** tofauti inavyoelekea kwake. Njia iendayo kwenye kutokufa imekuwa ni njia iliyohitaji dhabihu ya matumaini, malengo na tamaa ambazo vinginevyo zingekuwa halali na sahihi—dhabihu ya milele ya asili ya kibinadamu. Lakini njia iendayo kwenye ukamilifu wa kibinadamu, yaani, urejesho, tumaini la ulimwengu, inahitaji tu kuweka dhambi kando: si dhabihu ya haki na fursa za kibinadamu, bali matumizi yake sahihi. Itaongoza kwenye utakaso wa kibinafsi na kurejeshwa kwenye mfano wa Mungu kama ilivyofurahiwa na Adamu kabla ya dhambi kuingia ulimwenguni.

Njia ya kurudi kwenye ukamilifu halisi wa kibinadamu itafanywa kuwa wazi sana na rahisi; wazi kiasi kwamba hakuna atakayeweza kuikosea njia; wazi kiasi kwamba *"wasafirio, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo"* (**Isaya 35:8--Lesser**); wazi kiasi kwamba hakuna atakayehitaji kumfundisha jirani yake, akisema, Mjue Bwana, kwa maana wote watamjua Bwana tangu aliye mdogo hata aliye mkuu. (**Yeremia 31:34**)

Badala ya kuwa njia nyembamba ambayo wachache wanaweza kuiona, inaitwa "njia kuu," barabara ya umma—si njia ya pembeni nyembamba, yenye mwinuko, ngumu, na iliyozungukwa na vizuizi, bali ni njia iliyoandaliwa maalum kwa ajili ya safari **rahisi**—iliyopangwa maalum kwa ajili ya urahisi na faraja ya wasafiri.

Mistari ya 8 na 9 inaonyesha kwamba ni barabara ya umma, iliyo wazi kwa wote waliokombolewa—kila mwanadamu. Kila mwanadamu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake, atakayetambua na kutumia fursa na baraka zilizonunuliwa kwa damu ya thamani, anaweza kupita juu ya Njia hii Kuu ya Utakatifu kuelekea lengo

kuu la urejesho kamili kwenye ukamilifu wa kibinadamu na uzima wa milele.

Wala hawa **hawahesabiwi** kuwa wenye haki na kupewa hadhi ya kuhesabiwa ya utakatifu na ukamilifu machoni pa Mungu; watakapoanza safari katika njia hii kuu ya utakatifu wanaweza kupanda juu yake hadi kufikia ukamilifu **halisi**, kama matokeo ya jitihada na utii, ambapo mambo yote yatafanywa kuwa rahisi kwao na Mkombozi wao, atakayekuwa akitawala kwa nguvu wakati huo. Kila mtu, kulingana na mahitaji yake, atasaidiwa na utawala wenye hekima na mkamilifu wa ufalme mpya.

Hili, kama wengine watakavyofikiri, ndilo matokeo halali ya fidia. Kwa kuwa Bwana wetu, mwanadamu Kristo Yesu, alijitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote, na anatamani wote wafikie ujuzi wa kweli, na hivyo kufikia ukamilifu halisi, kwa nini hafanyi mara moja njia kuu nzuri na pana kwa ajili ya wote? Kwa nini haondoi vizuizi, mawe ya kukwaza, mashimo na mitego? Kwa nini asimsaidie mwenye dhambi arudi kwenye upatano kamili na Mungu, badala ya kuifanya njia iwe nyembamba, ngumu, yenye miiba, vigumu kuiona, na vigumu zaidi kuitembea?

Kushindwa kulitumia kwa halali Neno la kweli, na kuona kwamba njia ya sasa nyembamba inaelekea kwenye tuzo maalum, na ni kwa ajili ya jaribio na uteuzi wa kundi dogo la warithi-pamoja, mwili wa Kristo, ambalo, litakapochaguliwa na kuinuliwa pamoja na Kichwa chao, litabariki mataifa yote, kumewafanya wengine wawe na mawazo mkanganyiko juu ya somo hili.

Wakishindwa kuona mpango wa Mungu, wengi hujaribu kuhubiri njia kuu ya utakatifu, njia rahisi ya uzima, katika zama hizi, wakati hakuna njia kama hiyo, nao wanachanganya na kulegeza msimamo ili kupatanisha ukweli na Maandiko na nadharia zao potofu. Katika njia kuu itakayofunguliwa hivi karibuni, ni mambo ya dhambi tu yatakayokatazwa, ilhali wale wanaosafiri katika njia nyembamba ni lazima wajikane wenyewe

na kutoa dhabihu mambo mengi yasiyo ya dhambi, na pia kupigana vita daima dhidi ya dhambi zinazowazingira. Hii ni njia ya dhabihu, kama vile ile ya zama zijazo itakavyokuwa njia kuu ya haki.

Kuhusu njia hiyo kuu, imeelezwa kwa lugha ya ishara kwamba *"Hapo hapatakuwa na simba, wala mnyama mkali hatapanda juu yake; hawataonekana hapo."* (**Isaya 35:9**)

Ni simba wangapi wa kutisha walio katika njia ya wale ambao wangefurahi kuacha njia za dhambi, na kufuata haki sasa! Yupo simba wa maoni potofu ya umma, ambayo huwazuia wengi wasithubutu kutii maamrisho ya dhamiri katika mambo ya maisha ya kila siku—mavazi, nyumba, na mipango ya biashara, n.k. Simba wa jaribu la kileo huwazuia maelfu ambao wangefurahi kuliona likiondolewa.

Wapiga marufuku pombe na watetezi wa kiasi sasa wana kazi ngumu mno mikononi mwao, ambayo ni mamlaka na nguvu za zama zijazo pekee ndizo zinaweza kuiondoa; na vivyo hivyo inaweza kusemwa juu ya juhudi nyingine za kustahili za mabadiliko ya maadili. *"Wala mnyama mkali hatapanda juu yake."* Hakuna mashirika makubwa, yaliyoandaliwa kuendeleza maslahi ya ubinafsi, ya mtu mmoja mmoja kwa gharama ya wema wa jumla, yatakayovumiliwa. *" Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu;"* (ufalme) asema Bwana. (**Isaya 11:9**)

Ingawa kutakuwa na magumu ya kupambana nayo katika kushinda mielekeo ya uovu, n.k., bado, ikilinganishwa na njia nyembamba ya zama hizi, hiyo itakuwa njia rahisi. *"Mawe [mawe ya kukwaza] yatatolewa njiani,"* na bendera ya kweli itainuliwa kwa ajili ya watu. (**Isaya 62:10**)

Ujinga na ushirikina vitakuwa mambo ya zamani, na haki itapokea thawabu yake inayostahili, huku uovu ukipewa adhabu yake ya haki. (**Malaki 3:15, 18**) Kwa adhabu zenye manufaa, himizo linalofaa na maelekezo ya wazi, kama wana wapotevu

waliorejea, wanadamu watafunzwa na kutiwa nidhamu hadi kufikia ukamilifu mkuu ambao baba Adamu alianguka kutoka kwake. Hivyo *"waliokombolewa na Bwana* ***watarudi*** *[kutoka uharibifuni, kwa njia kuu ya utakatifu]... wakiwa na nyimbo na furaha ya milele juu ya vichwa vyao; watapata furaha na shangwe, na huzuni na kuugua kutakimbia."* (**Isaya 35:10**)

Bwana wetu alirejelea njia mbili tu kati ya hizi, kwa sababu ya tatu ilikuwa bado haijafika wakati wake wa kufunguliwa—kama vile alipokuwa akitangaza habari njema, alisema, *"Andiko hili limetimia masikioni mwenu,"* lakini aliacha kutaja *"siku ya kisasi,"* kwa sababu ilikuwa bado haijafika wakati wake. (Linganisha **Luka 4:19** na **Isaya 61:2**.) Sasa, hata hivyo, kadiri njia nyembamba inavyokaribia mwisho, njia kuu ya haki inaanza kuonekana wazi zaidi na zaidi, katika nuru ya siku inayopambazuka.

Hivyo, tumegundua **"Njia Pana,"** ambayo kwa sasa umati wa wanadamu unasafiri, wakidanganywa na "mkuu wa ulimwengu huu," na kuongozwa na ladha zilizopotoka. Tumegundua kwamba ilifunguliwa na kwamba jamii yetu ilianzishwa katika mwendo wake wa kasi juu yake kwa *"kuasi kwake mtu mmoja."* Tumegundua kwamba **"Njia Kuu ya Utakatifu"** itafunguliwa na Bwana wetu, aliyejitoa kuwa fidia kwa ajili ya wote na anawakomboa **wote** kutoka katika upotevu ambao "Njia Pana" inaelekea, na kwamba, kwa wakati ufaao, itakuwa rahisi kupitika kwa ajili ya wote waliokombolewa aliowanunua kwa damu yake ya thamani.

Tumegundua, zaidi ya hayo, kwamba **"Njia Nyembamba"** ya sasa, iliyofunguliwa kwa kustahili wa damu hiyohiyo ya thamani, ni njia maalum inayoongoza kwenye tuzo maalum, na imefanywa kuwa nyembamba na ngumu maalum kama **jaribio** na nidhamu kwa wale wanaochaguliwa sasa ili wafanywe washiriki wa asili ya **Uungu** na warithi-pamoja na Bwana wetu Yesu katika Ufalme wa utukufu utakaofunuliwa hivi karibuni kwa ajili ya baraka za wote. Wale walio na **tumaini** hili—wanaiona tuzo hii—wanaweza kuhesabu matumaini mengine

yote kuwa ni hasara na takataka kwa kulinganisha. **—Wafilipi 3:8-15**

## SOMO LA XII

# UFAFANUZI WA CHATI INAYOWAKILISHA MPANGO WA ZAMA

ZAMA—MAVUNO—NGAZI ZA NAFASI HALISI NA YA KUHESABIWA—SAFARI YA BWANA WETU YESU—SAFARI YA WAFUASI WAKE—MAKUNDI MATATU KATIKA KANISA LA JINA—UTENGANISHO KATIKA MAVUNO—KUNDI LA WATIWA-MAFUTA LIKIWA LIMETUKUZWA—KUNDI LA DHIKI KUU—MAGUGU YANACHOMWA—ULIMWENGU UNABARIKIWA—MATOKEO MATUKUFU.

NYUMA ya kitabu hiki, kuna chati inaoonyesha mpango wa Mungu wa wokovu kwa ulimwengu. Lengo la chati hii ni kukusaidia uelewe kwa urahisi (kwa njia ya kuona) jinsi mpango wa Mungu unavyoendelea hatua kwa hatua. Vilevile, unaonyesha hatua ambazo kila mtu anapaswa kuzifuata ili apate yale "mabadiliko" kamili kutoka katika asili ya kibinadamu kwenda kwenye asili tukufu ya Mungu.

Kwanza, tuna muhtasari wa vipindi vikuu vitatu, **A**, **B**, **C**—cha kwanza kati ya hivi, **A**, kinaanzia uumbaji wa mwanadamu hadi Gharika; cha pili, **B**, kinaanzia Gharika hadi mwanzo wa utawala wa Milenia wa Kristo, wakati wa kurudi kwake mara ya pili; na cha tatu, au **"Kipindi cha Utimilifu wa Nyakati,"** **C**, kinaanzia mwanzo wa utawala wa Kristo kwa "zama zijazo." (*Waefeso 1:10; 2:7*) Vipindi hivi vikuu vitatu mara nyingi vinarejelewa katika Maandiko: **A** kinaitwa "ulimwengu uliokuwako"; **B** na Bwana wetu Yesu kinaitwa "ulimwengu huu," na Paulo "ulimwengu huu wa mwovu wa sasa," na Petro "ulimwengu wa sasa." **C** kinaitwa "ulimwengu ujao, ambao ndani yake haki inakaa," tofauti na ulimwengu huu wa uovu wa sasa. Sasa uovu ndio unatawala na wenye haki wanateseka, ilhali katika ulimwengu ujao utaratibu huu utageuzwa: haki itatawala na watenda maovu watateseka, na hatimaye uovu wote utaangamizwa.

Katika kila kimoja cha vipindi hivi vikuu vitatu, au "**ulimwengu,"** mpango wa Mungu kuhusu wanadamu una muhtasari tofauti na wa pekee; lakini kila kimoja ni sehemu tu ya mpango mmoja mkuu ambao, utakapokamilika, utaonyesha hekima ya

Mungu—ingawa sehemu hizi zikichukuliwa peke yake zinashindwa kuonyesha kusudi lake la kina.

Kwa kuwa "ulimwengu" wa kwanza ("mbingu na nchi," au utaratibu huo wa mambo) ulipita wakati wa Gharika, inafuata kwamba ni lazima uwe ulikuwa utaratibu tofauti na "ulimwengu huu wa uovu," ambao Bwana wetu alisema Shetani ndiye mkuu wake; hivyo mkuu wa ulimwengu huu wa uovu hakuwa mkuu wa ulimwengu uliokuwako kabla ya Gharika, ingawa hakuwa pasipo ushawishi wakati huo.

Maandiko kadhaa yanaangazia matendo ya Mungu wakati huo, na hivyo yanatupa ufahamu wa wazi wa mpango wake kwa ujumla. Wazo linalodokezwa na haya ni kwamba "ulimwengu" wa kwanza, au kipindi cha kabla ya Gharika, ulikuwa chini ya usimamizi na huduma maalum ya malaika, walioruhusiwa kujaribu kile walichoweza kufanya ili kuirejesha jamii iliyoanguka na iliyopotoka. Bila shaka, kwa ruhusa ya Mungu, walikuwa na shauku ya kujaribu; kwa maana shauku yao ilidhihirishwa walipoimba na kupiga kelele za furaha juu ya kazi za uumbaji. (*Ayubu 38:7*) Kwamba malaika walikuwa watawala walioruhusiwa, ingawa hawakufanikiwa, kwa kipindi hicho cha kwanza, si tu kwamba inaonyeshwa na marejeo yote ya kipindi hicho, bali pia inaweza kufikiriwa kimantiki kutokana na kauli ya Mtume wakati, akilinganisha kipindi cha sasa na cha zamani na cha baadaye, anaposema (*Waebrania 2:5*), *"Kwa maana hakuuweka chini ya malaika ulimwengu ule ujao."*

La; ulimwengu huo utakuwa chini ya udhibiti wa Bwana Yesu na warithi-pamoja naye; na hivyo si tu kwamba utakuwa utawala wa haki zaidi kuliko ule wa "ulimwengu huu wa uovu," bali pia utafanikiwa zaidi kuliko ule wa ulimwengu wa kwanza au kipindi cha kwanza chini ya "huduma ya malaika," ambao kutoweza kwao kuirejesha jamii ya wanadamu kunadhihirishwa na ukweli kwamba uovu wa mwanadamu ulikuwa mkuu kiasi kwamba Mungu kwa ghadhabu na hasira yake ya haki

aliangamiza kwa gharika jamii yote iliyokuwa hai wakati huo isipokuwa watu wanane. —*Mwanzo 7:13*

Wakati wa "ulimwengu huu wa uovu," mwanadamu anaruhusiwa kujaribu kujitawala mwenyewe; lakini kwa sababu ya anguko yuko chini ya udhibiti wa Shetani, **"mkuu wa ulimwengu huu**," ambaye hila na njama zake za siri amepambana nazo bure katika jitihada zake za kujitawala katika kipindi kirefu tangu Gharika hadi sasa. Utawala huu wa mwanadamu chini ya Shetani unaelekea kumalizika katika kipindi cha dhiki kuu ambacho ulimwengu haujawahi kukijua. Na hivyo itakuwa imethibitishwa ubatili, si tu wa nguvu za malaika katika kuiokoa jamii ya wanadamu, bali pia wa jitihada za mwanadamu mwenyewe kufikia hali za kuridhisha.

Kipindi cha pili kati ya vile vipindi vikuu, yaani **B,** kinaundwa na zama tatu mahususi; na kila moja, ikiwa ni hatua ya maendeleo, inaongoza kwenda juu na mbele katika mpango wa Mungu..

**Zama D** zilikuwa ni zile ambazo Mungu alishughulika kipekee na mababu wa imani kama vile Ibrahimu, Isaka na Yakobo.

**Zama E** ni Zama za Kiyahudi, au kipindi kilichofuata baada ya kifo cha Yakobo, ambapo wazao wake wote walichukuliwa na Mungu kama watu wake maalum. Kwa hawa alionyesha fadhila za kipekee, na akatangaza, *"Ni ninyi tu niliowajua (niliowatambua kwa fadhila) katika jamaa zote za dunia."* (*Amosi 3:2*)

Hawa, kama taifa, walikuwa mfano wa Kanisa la Kikristo, "taifa takatifu, watu wa pekee." Ahadi walizopewa zilikuwa mfano wa "ahadi zilizo bora" tulizopewa sisi. Safari yao kupitia jangwani hadi nchi ya ahadi ilikuwa mfano wa safari yetu kupitia jangwa la dhambi hadi Kanaani ya mbinguni. Dhabihu zao ziliwahesabia haki kwa mfano, na sio katika uhalisia; kwa maana *"haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi."* (*Waebrania 10:4*)

Lakini katika **Zama za Injili, F**, tuna "dhabihu zilizo bora," zinazofanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote. Tuna "ukuhani wa kifalme," unaoundwa na wote wanaojitoa kwa Mungu kama "dhabihu zilizo hai," takatifu na zenye kukubalika, kupitia Yesu Kristo, ambaye ndiye Mkuu au *"Kuhani Mkuu wa ungamo letu."* (*Waebrania 3:1*) Katika Zama za Injili tunapata uhalisi wa mambo ambayo Zama za Kiyahudi na huduma na maagizo yake vilikuwa vivuli vyake. —*Waebrania 10:1*

**Zama za Injili, F**, ni kipindi ambacho mwili wa Kristo unaitwa kutoka ulimwenguni, na kuonyeshwa kwa imani taji ya uzima, na ahadi zilizo kuu mno, za thamani, ambazo kwayo (kwa kutii wito na matakwa yake) wanaweza kuwa washiriki wa asili ya Uungu. (*2 Petro 1:4*) Bado Mungu anaruhusu uovu utawale duniani, na kuna sababu muhimu sana ya yeye kufanya hivyo. Lengo ni kuwajaribu watu wake kupitia mapambano yao na uovu. Jaribu lenyewe ni hili: kuona kama wako tayari, kwa hiari yao wenyewe, kuachilia mbali asili yao ya kibinadamu pamoja na baraka na mapendeleo yote yanayoambatana nayo. Ili kufaulu, wanapaswa kujitoa wenyewe kama dhabihu iliyo hai, wakikubali kufananishwa na kifo cha Yesu. Hapo ndipo watahesabiwa kuwa wanastahili kufanana naye katika ufufuo. **(Zaburi 17:15)**

Kipindi kikuu cha tatu, **C**, kitaundwa na zama nyingi—"Zama Zijazo." Ya kwanza kati ya hizi, **Zama za Milenia, G**, ndiyo pekee tunayo habari dhahiri kuihusu. Ni ile miaka elfu ambayo Kristo atatawala na hivyo kuzibariki jamaa zote za dunia, akitimiza "urejesho wa vitu vyote, alivyonena Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu." (*Matendo 3:19-21*) Katika zama hizo, dhambi na mauti vitafutwa milele; kwa maana *"ni lazima amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake... Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti"*—mauti ya Adamu. (*1 Wakorintho 15:25, 26*) Hicho kitakuwa kipindi kikuu cha ujenzi upya. Watakaoshirikiana na Kristo Yesu katika utawala huo watakuwa ni Kanisa, bibi-arusi wake, mwili wake, kama vile alivyohaidi, akisema, *"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika*

*kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi." —Ufunuo 3:21*

"Zama Zijazo," **H**, zinazofuata kipindi kikuu cha ujenzi upya, zitakuwa ni zama za ukamilifu, baraka na furaha, ambapo Maandiko hayazungumzii kazi zake. Inatosha kujua, tukiwa mbali hivi, kwamba zitakuwa ni zama za utukufu na baraka chini ya fadhila ya kimungu.

Kila kimoja cha vipindi hivi kina majira yake maalum ya kuanza na kuendeleza kazi yake, na kila kimoja kinamalizika kwa mavuno yanayoonyesha matunda yake.

Mavuno ya mwisho wa Zama za Kiyahudi yalikuwa ni kipindi cha miaka arobaini, kuanzia mwanzo wa huduma ya Yesu, alipo**pakwa mafuta** na Mungu kwa Roho (*Matendo 10:37, 38*), mwaka 29 BK, hadi kuangamizwa kwa Yerusalemu, mwaka 70 BK. Katika mavuno haya Zama za Kiyahudi ziliisha na Zama za Injili zikaanza. Kulikuwa na kupishana kwa vipindi hivi, kama inavyoonyeshwa kwenye chati.

Zama za Kiyahudi ziliisha kwa kiasi fulani wakati, mwishoni mwa huduma yake ya miaka mitatu na nusu, Bwana alipolikataa taifa hilo, akisema, *"Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa."* (*Mathayo 23:38*) Hata hivyo, walionyeshwa fadhila kwa miaka mitatu na nusu baada ya hapo, kwa kuendelea kupewa wito wa Injili wao pekee, kwa kupatana na tangazo la nabii (*Danieli 9:24-27*) kuhusu majuma sabini (ya miaka) ya fadhila kwao. Katikati ya juma la mwisho, Masihi angekatiliwa mbali (kufa), lakini si kwa ajili yake mwenyewe. *"Kristo alikufa [si kwa ajili yake, bali] kwa ajili ya dhambi zetu,"* na hivyo akasababisha dhabihu na sadaka zikome katikati ya juma—miaka mitatu na nusu kabla ya kumalizika kwa majuma sabini ya agano la fadhila kwa Wayahudi. Dhabihu ya kweli ilipokuwa imetolewa, bila shaka zile za mfano hazingeweza tena kutambuliwa na Yehova.

Kulikuwa, basi, na maana kamili zaidi ambapo Zama hizo za Kiyahudi ziliisha mwishoni mwa juma la sabini, yaani, miaka

mitatu na nusu baada ya msalaba—ambapo baada ya hapo Injili ilihubiriwa kwa watu Wamataifa pia, kuanzia na Kornelio. (*Matendo 10:45*) Hili lilimaliza zama zao kwa upande wa fadhila na utambuzi wa Mungu kwa kanisa la Kiyahudi; uwepo wao kama taifa ulikoma katika wakati mkuu wa taabu uliofuata.

Enzi ya Injili ilianza katika kipindi cha mavuno ya Wayahudi. Lengo kuu la enzi hii ni kuwaita, kuwakuza, na kuwajaribu wale wanaounda **"Kristo wa Mungu"**—yaani, Kichwa (Yesu) na Mwili wake (Kanisa). Kipindi hiki kinaitwa pia kipindi cha Roho Mtakatifu. Hivyo basi, ni sahihi kusema kwamba Enzi ya Injili ilianza pale Yesu alipotiwa mafuta **"kwa Roho Mtakatifu na nguvu"** wakati wa ubatizo wake **(Matendo 10:38; Luka 3:22; 4:1, 18)**. Hata hivyo, kwa upande wa Kanisa (ambalo ni mwili wake), enzi hii ilianza miaka mitatu na nusu baadaye.

“**Mavuno**” yanaunda pia kipindi cha mwisho cha Zama za Injili, ambapo tena kuna kupishana kwa zama mbili—Zama za Injili zikiisha, na Zama za Urejesho au Milenia zikianza. Zama za Injili zinaisha kwa hatua, kama kielelezo au “kivuli” chake, Zama za Kiyahudi. Kama vile ambavyo miaka saba ya kwanza ya mavuno huko ilitolewa kwa maana maalum kwa ajili ya kazi ndani na kwa ajili ya Israeli wa kimwili, na ilikuwa miaka ya fadhila, ndivyo tunavyoona miaka saba kama hiyo ikionyeshwa hapa kuwa na umuhimu uleule kwa Kanisa la Injili, ikifuatwa na kipindi cha taabu (“moto”) juu ya ulimwengu, kama adhabu ya uovu, na kama maandalizi ya utawala wa haki—tutazungumzia hili zaidi baadaye.

### Njia Iendayo Kwenye Utukufu

**K, L, M, N, P, R**, kila moja inawakilisha daraja tofauti. **N** ni daraja la **asili kamilifu ya kibinadamu**. Adamu alikuwa katika daraja hili kabla ya kutenda dhambi; lakini tangu wakati wa uasi alianguka hadi kwenye daraja la upotovu au dhambi, **R**, ambamo

wazao wake wote wanazaliwa. Hili linalingana na "Njia Pana" iendayo upotevuni.

**P** inawakilisha daraja la kuhesabiwa haki kwa mfano, lililohesabiwa kuwa limetokana na dhabihu za Torati. Haikuwa ukamilifu halisi, kwa maana *"Torati haikukamilisha neno lo lote."* — *Waebrania 7:19*

**N** inawakilisha si tu daraja la ukamilifu wa kibinadamu, kama lile alilokuwapo mwanadamu mkamilifu, Adamu, bali pia hadhi ya watu wote waliohesabiwa haki. *"Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko,"* na matokeo yake waamini wote katika Kristo—wote wanaoikubali kazi yake kamilifu na iliyokamilika kama muhesabishaji haki wao—wanahesabiwa na Mungu, kwa njia ya imani, kama wenye haki, kana kwamba ni watu wakamilifu, kana kwamba hawajawahi kuwa wenye dhambi. Machoni pa Mungu, basi, wote wanaomkubali Kristo kama Mkombozi wao wako, kwa kuhesabiwa, katika daraja la ukamilifu wa kibinadamu, **N**. Hii ndiyo hadhi pekee ambayo kwayo mwanadamu anaweza kumkaribia Mungu, au kuwa na ushirika wowote naye. Wote walio katika daraja hili Mungu anawaita wana—wana wa kibinadamu. Adamu alikuwa mwana hivyo (*Luka 3:38*), alikuwa na ushirika kabla ya kuwa mkosefu mbele za Mungu. Wote wanaoikubali kazi ya fidia iliyokamilika ya Bwana wetu Yesu **wanahesabiwa** kama waliorejeshwa kwenye usafi wa asili; na matokeo yake wanapata ushirika na Mungu.

Katika Zama za Injili, Mungu ametoa toleo maalum kwa wanadamu waliohesabiwa haki, akiwaambia kwamba chini ya masharti fulani wanaweza kupata mabadiliko ya asili, ili waache kuwa viumbe wa Duniani, wa kibinadamu, na wawe viumbe wa Mbinguni, wa kiroho, kama Kristo, Mkombozi wao. Baadhi ya waamini—watu waliohesabiwa haki—wanaridhika na furaha na amani walizo nazo kwa kuamini katika msamaha wa dhambi zao, na hivyo hawaisikilizi sauti inayowaita wapande juu zaidi. Wengine, wakiguswa na upendo wa Mungu kama

ulivyoonyeshwa katika ukombozi wao kutoka dhambini, na wakihisi kwamba wao si mali yao wenyewe, wakiwa wamenunuliwa kwa bei, husema, "Bwana, wataka nifanye nini?"

Watu kama hao wana jibu la Bwana kupitia Paulo, anayesema, *"Basi, **ndugu zangu**, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe **dhabihu** iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."* (**Warumi 12:1**) Mtume anamaanisha nini anapohimiza hivi utoaji wa miili yetu kama dhabihu zilizo hai? Anamaanisha kwamba tunapaswa kuweka wakfu kwa ajili ya utumishi wa Mungu kila nguvu na kipawa tulicho nacho, ili tangu sasa tusiishi kwa ajili yetu wenyewe, wala kwa ajili ya marafiki, wala familia, wala ulimwengu, wala kwa ajili ya kitu kingine chochote isipokuwa kwa ajili ya, na katika utumishi mtiifu wa, yeye aliyetununua kwa damu yake ya thamani.

Lakini kwa kuwa Mungu hakukubali dhabihu za mfano zenye dosari, na kwa kuwa sisi sote tulifanyika wenye dhambi kupitia Adamu, je, tunaweza kuwa dhabihu zinazokubalika? Paulo anaonyesha kwamba ni kwa sababu tu sisi ni watakatifu ndiyo tunakuwa dhabihu zinazokubalika.

Sisi si watakatifu kama Yesu, asiyejua dhambi, kwa maana sisi ni wa jamii iliyohukumiwa; wala si kwa sababu tumefanikiwa kikamilifu kufikia ukamilifu wa mwenendo, kwa maana hatuhesabu kuwa tumefikia ukamilifu ule tulioitiwa; bali tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo (dhaifu na vinavyovuja), ili utukufu wa ukamilifu wetu wa mwisho uonekane kuwa ni wa fadhila ya Mungu, na si wa uwezo wetu wenyewe. Lakini utakatifu wetu, na kukubalika kwetu mbele za Mungu kama dhabihu, kunatokana na ukweli kwamba Mungu ametuhesabia haki bure kutoka dhambi zote, kupitia imani yetu katika dhabihu ya Kristo kwa niaba yetu.

Wengi kadiri wanavyothamini na kutii wito huu wanafurahi kuhesabiwa kuwa wanastahili kustahimili shutuma kwa ajili ya

jina la Kristo, na hawaangalii vitu vinavyoonekana, bali vile visivyoonekana—wanaangalia "taji ya uzima"—"thawabu ya wito wetu mkuu katika Kristo Yesu" na "utukufu utakaofunuliwa ndani yetu."

Hawa, tangu wakati wa kujiweka wakfu kwa Mungu, hawahesabiwi tena kama wanadamu, bali kama waliozaliwa na Mungu kupitia neno la kweli—si tena wa kibinadamu, bali tangu hapo ni watoto wa kiroho. Sasa wako hatua moja karibu na tuzo kuliko walipoamini mara ya kwanza. Lakini uwepo wao wa kiroho bado si mkamilifu: wao **wametungwa tu kwa roho** (begotten), bado **hawajazaliwa** (born) na Roho. Wao ni watoto wa kiroho walio katika hatua ya **kiinitete**, kwenye daraja **M**—daraja la kiumbe kipya.

Kwa sababu wamezaliwa na Roho, hawahesabiwi tena kama wanadamu, bali kama wa kiroho; kwa maana asili ya kibinadamu, iliyokuwa yao hapo awali, iliyohesabiwa haki, sasa wameiacha au kuihesabu kuwa imekufa—dhabihu iliyo hai, takatifu, yenye kukubalika na iliyokubaliwa na Mungu. Sasa wao ni viumbe vipya katika Kristo Yesu: mambo ya kale (matumaini ya kibinadamu, utashi na malengo) yamepita, na mambo yote yamekuwa mapya; *"Lakini ninyi hamfuati mwili, bali mwaifuata roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu."* (**2 Wakorintho 5:17; Warumi 8:9**) Kama mmezaliwa na Roho, *"Kwa maana mlikufa (kama wanadamu), na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.."* —**Wakolosai 3:3**

**Daraja L** linawakilisha hali ya kiumbe **mkamilifu wa kiroho**; lakini kabla ya daraja **L** kufikiwa, masharti ya agano letu ni lazima yatekelezwe. Ni jambo moja kuweka agano na Mungu kwamba tutakuwa tumekufa kwa mambo yote ya kibinadamu, na ni jambo lingine kutekeleza agano hilo katika maisha yetu yote ya kidunia—*"nikiutawala mwili wangu"* (ukiwa umekufa), nikiuweka utashi wangu mbali, na kutekeleza tu mapenzi ya Bwana.

Kuingia kwenye daraja **L** kunaitwa kuzaliwa, au kuingia kikamilifu katika uzima kama kiumbe wa kiroho. Kanisa zima litaingia kwenye daraja hili litakapokusanywa (kuchaguliwa) kutoka ulimwenguni katika "mavuno" au mwisho wa Zama za Injili. *"Waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza."* Kisha sisi, tulio hai na tuliosalia, tutabadilishwa kwa dakika moja—na kufanywa viumbe wakamilifu wa kiroho wenye miili kama mwili mtukufu wa Kristo (kwa maana *"ni lazima huu wenye kufa uvae kutokufa"*). Kisha, kile kilicho kikamilifu kitakapokuja, kile kilicho cha sehemu (hali ya kuzaliwa kiroho na vikwazo mbalimbali vya mwili tunavyokabiliana navyo sasa) kitaondolewa.

Lakini kuna hatua nyingine zaidi ya kuchukua baada ya ukamilifu wa kiumbe wa kiroho, yaani, kuelekea "utukufu utakaofuata"—**Daraja K**. Hapa haturejelei utukufu wa nafsi, bali utukufu wa mamlaka au cheo. Kufikia **daraja L** huleta utukufu kamili wa mmoja mmoja; yaani, kiumbe mtukufu, anayefanana na Kristo. Lakini baada ya kukamilishwa hivi, na kufanywa kufanana kabisa na Bwana na Kichwa chetu, tutashirikiana naye katika "utukufu" wa mamlaka na cheo—kuketi pamoja naye katika kiti chake cha enzi, kama yeye, baada ya kukamilishwa wakati wa ufufuo wake, alivyoinuliwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu aliye juu. Hivyo tutaingia katika utukufu wa milele, **Daraja K**.

Sasa hebu tuisome chati kwa makini na tuangalie vielelezo vyake vya sifa mbalimbali za mpango wa Mungu. Katika vielelezo hivi tunatumia umbo la piramidi kuwakilisha ukamilifu, kwa sababu ya kufaa kwake na kwa sababu ya marejeo ya wazi kwake katika Maandiko.

Adamu alikuwa kiumbe mkamilifu, **piramidi a**. Angalia nafasi yake—kwenye **daraja N**, linalowakilisha ukamilifu wa kibinadamu. Kwenye **daraja R**, daraja la dhambi na kutokamilika au daraja la upotovu, **piramidi b** isiyo na kilele, umbo lisilo kamilifu, inawakilisha Adamu aliyeanguka na wazao wake—waliopotoka, wenye dhambi na waliohukumiwa.

Ibrahimu na wengine wa siku hizo, waliohesabiwa haki kupata ushirika na Mungu kwa sababu ya imani, wanawakilishwa na **piramidi c** kwenye **daraja N**. Ibrahimu alikuwa mshiriki wa familia ya wanadamu iliyopotoka na kwa asili alikuwa pamoja na wengine kwenye **daraja R**; lakini Paulo anatuambia kwamba Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani; yaani, alihesabiwa na Mungu kuwa mtu asiye na dhambi na mkamilifu kwa sababu ya imani yake. Hili, katika makadirio ya Mungu, lilimwinua juu ya ulimwengu wa wanadamu waliopotoka wenye dhambi hadi **daraja N**; na ingawa kiuhalisia bado hakuwa mkamilifu, alipokelewa katika fadhila ambayo Adamu alikuwa ameipoteza, yaani, ushirika na Mungu kama "rafiki." (**Yakobo 2:23**) Wote walio katika **daraja N** kamilifu (lisilo na dhambi) ni marafiki wa Mungu, naye ni rafiki yao; lakini wenye dhambi (kwenye **daraja R**) wako katika uadui na Mungu—"**maadui kwa matendo maovu."**

Ulimwengu wa wanadamu baada ya Gharika, unaowakilishwa na **umbo d**, bado ulikuwa kwenye **daraja R**—bado katika uadui, ambapo unaendelea hadi Kanisa la Injili litakapochaguliwa na Zama za Milenia kuanza.

Israeli kwa namna ya mwili, wakati wa Zama za Kiyahudi, walipotakaswa kwa dhabihu za mfano za mafahali na mbuzi (si uhalisia, bali kwa mfano, *"kwa maana Torati haikukamilisha neno lo lote"*—**Waebrania 7:19**), walihesabiwa haki kwa mfano. Hivyo wao (**e**) wako kwenye **daraja P**, daraja la kuhesabiwa haki kwa mfano, lililodumu tangu kutolewa kwa Torati katika Mlima Sinai hadi Yesu alipoikomesha Torati, akiigongomea msalabani. Hapo ndipo kuhesabiwa haki kwa mfano kulipokoma kwa kuanzishwa kwa "dhabihu zilizo bora" kuliko zile za mfano za Kiyahudi, zile ambazo kihalisia *"huondoa dhambi ya ulimwengu"* na *"kuwakamilisha [kihalisia] wale wakaribiao."* —**Waebrania 10:1**

Moto wa jaribu na taabu ambao Israeli wa kimwili walipitia, Yesu alipokuwepo, ukiwachuja na kutoa ngano, yaani, "Waisraeli kweli kweli," kutoka katika kanisa lao la jina, na hasa

alipochoma makapi [sehemu isiyofaa ya mfumo huo] kwa moto usiozimika" baada ya kutenganisha ngano, unaonyeshwa kwa **umbo f**. Ulikuwa ni wakati wa taabu ambao hawakuwa na uwezo wa kuuepuka. Tazama **Luka 3:17, 21, 22; 1 Wathesalonike 2:16**.

Yesu, akiwa na umri wa miaka thelathini, alikuwa mwanadamu mkamilifu, aliyekomaa (**g**), akiwa ameacha utukufu wa hali ya kiroho na kuwa **mwanadamu** ili yeye (kwa neema ya Mungu) aonje mauti kwa ajili ya kila mtu. Haki ya sheria ya Mungu ni kamili: jicho kwa jicho, jino kwa jino na uhai kwa uhai. Ilikuwa ni lazima **mwanadamu** mkamilifu afe kwa ajili ya wanadamu, kwa sababu madai ya haki hayangeweza kutimizwa kwa njia nyingine yoyote. Kifo cha malaika hakingeweza kulipia adhabu na kumwachilia mwanadamu kama vile ambavyo kifo cha "mafahali na mbuzi, ambacho hakiwezi kamwe kuondoa dhambi" hakingeweza. Kwa hiyo, yeye anayeitwa "Mwanzo wa uumbaji wa Mungu" alifanyika **mwanadamu**, *"alifanyika mwili,"* ili aweze kutoa fidia hiyo (bei sawasawa) ambayo ingewakomboa wanadamu.

Ilimbidi awe mwanadamu mkamilifu, la sivyo asingeweza kufanya zaidi ya mshiriki yeyote wa jamii iliyoanguka ili kulipa gharama. Alikuwa *"mtakatifu, asiye na madhara, asiye na waa, aliyetengwa na wenye dhambi."* Alitwaa umbo au mfano uleule walio nao wenye dhambi—"mfano wa mwili wa dhambi"—mfano wa kibinadamu. Lakini aliuchukua mfano huo katika ukamilifu wake: hakushiriki dhambi yake wala hakushiriki kutokamilika kwake, isipokuwa aliposhiriki kwa hiari huzuni na maumivu ya wengine wakati wa huduma yake, akichukua maumivu na udhaifu wao alipowapa nguvu na afya yake. Imeandikwa kwamba *"Yeye mwenyewe **alichukua** udhaifu wetu na kubeba magonjwa yetu"* (**Isaya 53:4**), na *"nguvu [uhai, nguvu] zilimtoka zikawaponya wote."* —**Marko 5:30; Luka 6:19; Mathayo 8:16, 17**

Akiwa katika umbo la mwanadamu (mkamilifu), alijinyenyekeza na akawa mtiifu hata mauti. Alijitoa kwa Mungu,

akisema, *"Tazama, nimekuja (katika gombo la chuo imeandikwa habari zangu) kufanya mapenzi yako, Ee Mungu"* — na akaashiria kujiweka wakfu huku kwa ubatizo wa maji. Alipojitoa hivi, akiweka wakfu uwepo wake, sadaka yake ilikuwa takatifu (safi) na yenye kukubalika kwa Mungu, ambaye alionyesha kukubali kwake kwa kumjaza Roho na nguvu yake—Roho mtakatifu alipomshukia, na hivyo kumpaka mafuta.

Kujazwa huku kwa Roho kulikuwa ni **kutungwa kwa roho** katika asili mpya—ya kimungu—ambayo ingekua kikamilifu au kuzaliwa (born) atakapokuwa amekamilisha kikamilifu utoaji—dhabihu ya asili ya kibinadamu. Kutungwa(beggoten) huku kiroho kulikuwa ni hatua ya kupanda kutoka hali za kibinadamu, na kunaonyeshwa kwa **piramidi h**, kwenye **daraja M**, daraja la kutungwa kiroho. Katika daraja hili Yesu alikaa kwa miaka mitatu na nusu ya maisha yake—hadi uwepo wake wa kibinadamu ulipokoma msalabani. Kisha, baada ya kuwa amekufa kwa siku tatu, alifufuliwa kwenye uzima—kwenye ukamilifu wa kiumbe wa kiroho (**i, daraja L**), akiwa amezaliwa kwa Roho—"mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu." *"Kilichoz**aliwa** kwa Roho ni roho."* Kwa hiyo Yesu, wakati na baada ya ufufuo wake, alikuwa roho—kiumbe wa kiroho, na si tena kiumbe mwanadamu kwa maana yoyote.

Ni kweli, baada ya ufufuo wake alikuwa na uwezo wa kutokea, na alitokea, kama mwanadamu, ili aweze kuwafundisha wanafunzi wake na kuwathibitishia kwamba hakuwa amekufa tena; lakini hakuwa mwanadamu, na hakuwa tena akiongozwa na hali za kibinadamu, bali aliweza kutoweka na kuonekana kama upepo (hata milango ilipokuwa imefungwa), na hakuna aliyeweza kujua alikotoka wala alikokwenda. *"Ndivyo alivyo kila mtu aliyezaliwa kwa Roho."* (Linganisha **Yohana 3:8; 20:19, 26**).

Tangu wakati wa kujiweka kwake wakfu kwa ajili ya dhabihu, wakati wa ubatizo wake, ubinadamu ulikuwa umehesabiwa umekufa—na hapo ndipo asili mpya ilipohesabiwa kuanza,

ambayo ilikamilishwa wakati wa ufufuo, alipofikia daraja kamilifu la kiroho, **L**—akafufuliwa akiwa na mwili wa kiroho.

Siku arobaini baada ya ufufuo wake, Yesu alipaa kwenda kwa Mwenyezi aliye juu—daraja la utukufu wa kimungu, **K** (**piramidi k**). Wakati wote wa Zama za Injili amekuwa katika utukufu (**l**), *"ameketi pamoja na Baba katika kiti chake cha enzi,"* na ni Kichwa juu ya Kanisa lake duniani—Mkurugenzi na Kiongozi wake. Katika Zama hizi zote za Injili, Kanisa limekuwa katika mchakato wa kukua, kutiwa nidhamu na kujaribiwa, kwa kusudi kwamba mwishoni au katika mavuno ya zama hizi liweze kuwa bibi-arusi wake na mrithi-pamoja naye. Kwa hiyo lina ushirika katika mateso yake, ili liweze pia kutukuzwa pamoja naye (kwenye **daraja K**), wakati unaofaa utakapofika.

Hatua za Kanisa kuelekea utukufu ni zilezile kama za Kiongozi na Bwana wake, ambaye *"ametuachia kielelezo, ili tufuate nyayo zake"*—isipokuwa kwamba Kanisa linaanzia katika daraja la chini. Bwana wetu, kama tulivyoona, alikuja ulimwenguni akiwa katika daraja la ukamilifu wa kibinadamu, **N**, ilhali sisi sote wa jamii ya Adamu tuko katika daraja la chini zaidi, **R**—daraja la dhambi, kutokamilika na uadui na Mungu. Kitu cha kwanza muhimu kwetu, basi, ni **kuhesabiwa haki**, na hivyo kufikia **daraja N**.

Hili linatimizwaje? "Je, jambo hili linawezekanaje? Je, ni kwa njia ya matendo mema? Jibu ni la hasha, kwa sababu wenye dhambi hawawezi kufanya matendo yaliyo mema. Tusingeweza kamwe kujifanya tukubalike mbele za Mungu.", kwa hiyo *"Mungu aonyesha pendo lake kwetu, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."* (**Warumi 5:8**) Basi, sharti ambalo kwalo tunafika kwenye daraja la kuhesabiwa haki au ukamilifu wa kibinadamu ni kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, akatukomboa na kutuinua, *"kwa imani katika damu yake,"* hadi kwenye daraja kamilifu, ambalo, katika Adamu, tulianguka kutoka kwake.

*"Tunahesabiwa haki [tunainuliwa hadi daraja **N**] kwa imani."* Na *"basi, tukiisha **kuhesabiwa haki** itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu"* (**Warumi 5:1**), na hatuhesabiwi tena na Mungu kama maadui, bali kama wana wa kibinadamu waliohesabiwa haki, katika daraja lilelile kama Adamu na Bwana wetu Yesu, isipokuwa kwamba wao walikuwa wakamilifu kiuhalisia, ilhali sisi tunahesabiwa tu kuwa hivyo na Mungu.

Uhesabiwaji huu wa haki tunautambua kupitia imani katika Neno la Mungu, linalosema, "*Mmenunuliwa," "mmekombolewa," "mmehesabiwa haki bure kutoka katika mambo yote*." Tunasimama mbele za Mungu tukiwa hatuna lawama, hatuna doa na ni watakatifu katika mavazi ya haki ya Kristo tuliyovikwa kwa kuhesabiwa kwa imani. Yeye alikubali dhambi zetu **zihesabiwe** kwake, ili aweze kubeba adhabu yetu kwa ajili yetu; naye alikufa kwa niaba yetu, kana kwamba yeye ndiye alikuwa mwenye dhambi. Haki yake, kwa hiyo, **inahesabiwa** kwa wote wanaoikubali fidia yake, na inaleta pamoja nayo haki na baraka zote zilizokuwa za asili kabla ya dhambi kuingia. Inaturejesha kwenye uzima na kwenye ushirika na Mungu. Ushirika huu tunaweza kuwa nao mara moja kwa kutumia imani, na uzima na ushirika kamili zaidi na furaha vimehakikishwa—katika "**wakati ufaao"** wa Mungu.

Lakini kumbuka kwamba ingawa kuhesabiwa haki ni jambo lililobarikiwa, hakubadili asili yetu:* sisi bado ni wanadamu.

Tumeokolewa kutoka katika hali duni ya dhambi na kutengwa na Mungu, na badala ya kuwa wenye dhambi wa kibinadamu, sisi ni wana wa kibinadamu; na sasa, kwa sababu sisi ni wana, Mungu anazungumza nasi kama watu wa hadhi hiyo. Katika Zama za Injili amekuwa akiliita "kundi dogo" la "warithi-pamoja," akisema, *"Mwanangu, nipe moyo wako"*—yaani, jitoe wewe mwenyewe, nguvu zako zote za kidunia, utashi wako, talanta zako, kila kitu chako, kwangu, kama vile Yesu alivyowawekea mfano; nami nitakufanya mwana katika daraja la juu kuliko la kibinadamu. Nitakufanya mwana wa kiroho, mwenye mwili wa kiroho kama wa Yesu aliyefufuka—**"chapa kamili ya nafsi ya Baba**." Kama utayaacha matumaini yote ya kidunia, malengo, na madhumuni, n.k., ukiweka wakfu asili ya kibinadamu kikamilifu, na kuitumia yote katika utumishi wangu, nitakupa asili ya juu kuliko jamii yako yote; nitakufanya *"mshiriki wa asili ya uungu"—"mrithi wa Mungu, na mrithi-pamoja na Yesu Kristo, **ikiwa tunateseka pamoja naye, ili tuweze pia kutukuzwa pamoja**."*

Wale wanaothamini ipasavyo tuzo hii iliyowekwa mbele yao katika injili, huweka kando kwa furaha kila mzigo na kupiga mbio kwa saburi katika mashindano yaliyowekwa, ili waweze kulipata. Matendo yetu hayakuhitajika ili kupata kuhesabiwa haki: Bwana wetu Yesu alifanya kazi yote iliyoweza kufanywa kwa ajili hiyo, na tulipokubali kwa imani kazi yake iliyokamilika, tulihesabiwa haki, tukainuliwa hadi **daraja N**.

---

* *Neno **asili** hutumika kwa maana isiyo rasmi inaposemwa kuhusu mtu kwamba ana tabia mbaya. Kwa maana halisi, hakuna mwanadamu aliye mwovu kwa asili. Asili ya kibinadamu ni "njema sana," mfano wa kidunia wa asili ya kimungu. Hivyo kila mwanadamu ana asili njema, ugumu ukiwa ni kwamba asili hii njema imepotoka. Basi, si jambo la asili kwa mwanadamu kuwa mwovu, mkatili, n.k., na ni jambo la asili kwake kuwa kama Mungu. Ni katika maana hii ya msingi ndivyo tunavyotumia neno **asili**, hapo juu. Tumehesabiwa haki na Kristo ili turejee kikamilifu kwenye fursa na baraka zote za asili yetu ya kibinadamu – mfano wa kidunia wa Mungu.*

Lakini sasa, kama tunataka kwenda mbele zaidi, hatuwezi kwenda bila matendo. Ni kweli, hatupaswi kupoteza imani yetu, la sivyo tutapoteza kuhesabiwa haki; lakini tukiwa tumehesabiwa haki, na tukiendelea katika imani, tunaweza (kupitia neema tuliyopewa kwa kutungwa kwetu na Roho) kufanya matendo, kuzaa matunda yanayokubalika kwa Mungu. Na Mungu anataka hivi; kwa maana ndiyo dhabihu tuliyoweka agano kuitoa. Mungu anataka tuonyeshe uthamini wetu wa tuzo hii kuu kwa kutoa vyote tulivyo navyo na tulivyo kwa ajili yake; si kwa wanadamu, bali kwa Mungu—dhabihu takatifu na, kupitia Kristo, yenye kukubalika kwake—utumishi wetu wenye maana.

Tunapotoa vitu hivi vyote, tunasema: Bwana, unatakaje niitoe hii, dhabihu yangu, wakati wangu, talanta, ushawishi, n.k., kwako? Kisha, tukichunguza Neno la Mungu kwa jibu, tunasikia sauti yake ikituelekeza tutoe **vyote** vyetu kwake kama Bwana wetu Yesu alivyofanya, kwa kuwatendea mema watu wote kadiri tupatavyo fursa, hasa wale wa nyumba ya imani—tukiwahudumia kwa chakula cha kiroho au cha kimwili, tukiwavika haki ya Kristo au mavazi ya kidunia, kulingana na uwezo wetu, au kulingana na mahitaji yao. Tukiisha weka wakfu **vyote**, tunatungwa na Roho, tumefikia **daraja M**; na sasa, kupitia nguvu tuliyopewa, kama tukiitumia, tutaweza kutimiza agano letu lote, na kutoka tukiwa washindi, na zaidi ya washindi, kupitia (nguvu au Roho ya) yeye aliyetupenda na kutununua kwa damu yake ya thamani. Lakini, tukitembea hivyo katika nyayo za Yesu,

*Kamwe usifikiri ushindi umepatikana, Wala usiketi chini kupumzika.*
*Kazi yako ngumu haitakuwa imekwisha, Hadi utakapokuwa umeipata taji yako.*

Taji itapatikana tutakapokuwa, kama ndugu yetu mwaminifu Paulo, tumepiga vita vizuri na kumaliza mwendo, lakini si kabla ya hapo. Hadi wakati huo, mwali na uvumba wa dhabihu yetu ya kazi na huduma lazima upae kila siku—dhabihu ya harufu

nzuri kwa Mungu, inayokubalika kupitia Yesu Kristo, Bwana wetu.

Wale wa kundi hili linaloshinda ambao “wanalala” watafufuliwa wakiwa viumbe wa kiroho, **daraja L**, na wale wa kundi lilelile watakaokuwa hai na kusalia hadi kuja kwa Bwana “watabadilishwa” na kuingia katika daraja lilelile la viumbe wa kiroho, nao “hawatalala” hata kwa dakika moja, ingawa “mabadiliko” hayo yatahitaji kuyeyushwa kwa chombo cha udongo. Wakiwa si tena viumbe dhaifu, wa kidunia, wenye kufa, na wenye kuharibika, hawa watakuwa wamezaliwa kikamilifu na Roho—viumbe wa mbinguni, wa kiroho, wasioharibika, wasioweza kufa. —**1 Wakorintho 15:44, 52**

**Hatujui** itachukua muda gani baada ya “mabadiliko” yao, au kukamilishwa kwao kama viumbe wa kiroho (**daraja L**), kabla ya wao, kama kundi kamili, kutukuzwa (**daraja K**) pamoja na Bwana, wakiunganishwa naye katika mamlaka na utukufu mkuu. Kuunganishwa huku na kutukuzwa kikamilifu kwa mwili mzima wa Kristo na Kichwa chake, tunaelewa kuwa ndiyo “arusi ya Mwana-Kondoo” kwa Bibi-arusi wake, atakapoingia kikamilifu katika furaha za Bwana wake.

Angalia tena kwenye chati—**n, m, p, q** ni makundi manne tofauti ambayo kwa pamoja yanawakilisha Kanisa la Injili la jina tu kwa ujumla, linalodai kuwa mwili wa Kristo. Makundi yote ya **n** na **m** yako kwenye daraja la kutungwa kwa roho, **M**. Makundi haya mawili yamekuwepo pamoja katika Zama zote za Injili; yote yaliweka agano na Mungu la kuwa dhabihu zilizo hai; yote “yalikubaliwa katika mpendwa” na kutungwa kwa Roho kama “viumbe vipya.” Tofauti kati yao ni hii: **n** inawakilisha wale wanaotimiza agano lao na wamekufa pamoja na Kristo kwa mapenzi, malengo na tamaa za kidunia, ilhali **m** inawakilisha kundi kubwa zaidi la watoto walotungwa-kiroho ambao wameweka agano, lakini, ole wao! wanasitasita kutekeleza agano lao.

Kundi la **n** linajumuisha washindi watakaokuwa Bibi-arusi wa Kristo, watakaoketi na Bwana katika kiti chake cha enzi katika utukufu—**daraja K**. Hili ndilo "kundi dogo" ambalo ni furaha ya Baba kuwapa Ufalme. (**Luka 12:32**) Wale wa kundi la **m** wanasita kukabili kifo cha utashi wa kibinadamu, lakini Mungu bado anawapenda, na kwa hiyo atawapitisha katika njia ya dhiki na taabu hadi **daraja L**, daraja kamilifu la kiroho. Lakini watakuwa wamepoteza haki ya kufikia **daraja K**, kiti cha enzi cha utukufu, kwa sababu hawakuwa washindi.

Ikiwa tunathamini upendo wa Baba yetu, ikiwa tunatamani kibali cha Bwana wetu, ikiwa tunatamani kuwa washiriki wa mwili wake, Bibi-arusi wake, na kuketi katika kiti chake cha enzi, ni lazima tulitimize agano letu la dhabihu kwa uaminifu na kwa hiari.

Wengi wa Kanisa la **jina tu** wanawakilishwa na sehemu **p**. Angalia kwamba hawako kwenye **daraja M**, bali kwenye **daraja N**. Wamehesabiwa haki lakini hawajatakaswa. Hawajawekwa wakfu kikamilifu kwa Mungu, na hivyo, hawajatungwa kama viumbe wa kiroho. Hata hivyo, wako juu kuliko ulimwengu, kwa sababu wanamkubali Yesu kama fidia yao kutoka dhambini; lakini hawajaukubali wito mkuu wa zama hizi wa kuwa sehemu ya familia ya kiroho ya Mungu. Kama wakiendelea katika imani na kujinyenyekeza kikamilifu chini ya sheria za haki za Ufalme wa Kristo, katika Nyakati za Urejesho, hatimaye watafikia mfano wa mwanadamu mkamilifu wa kidunia, Adamu. Watarejeshewa kikamilifu yote yaliyopotea kupitia yeye. Watafikia ukamilifu uleule wa kibinadamu, wa kiakili, kiadili na kimwili, na watakuwa tena katika mfano wa Mungu, kama Adamu alivyokuwa; kwa maana walikombolewa kwa ajili ya yote haya.

Na nafasi yao ya kuhesabiwa haki, **daraja N**, kama wale waliosikia na kuamini katika wokovu kupitia Kristo, ni baraka maalum wanayoifurahia kwa imani mapema zaidi kuliko ulimwengu wote (kwa maana wote wataletwa kwenye ujuzi sahihi

wa Kweli, katika Zama za Milenia). Hawa, hata hivyo, watakuwa na faida ya kuanza mapema na maendeleo fulani katika mwelekeo sahihi.

Lakini kundi **p** linashindwa kutumia manufaa halisi ya kuhesabiwa haki kwa imani huku kwa wakati huu. Imetolewa sasa kwa kusudi maalum la kuwawezesha wengine kutoa dhabihu inayokubalika, na kuwa kundi la **n** kama washiriki wa "mwili wa Kristo." Wale wa kundi **p** wanaipokea fadhila ya Mungu [kuhesabiwa haki] "bure" (**2 Wakorintho 6:1**): wanashindwa kuitumia ili wasonge mbele na kujitoa wenyewe kama dhabihu zinazokubalika, katika wakati huu ambapo dhabihu zinakubalika kwa Mungu. Wale wa kundi hili, ingawa si "watakatifu," si washiriki wa "mwili" uliojiweka wakfu, wanaitwa "ndugu" na Mtume. (**Warumi 12:1**) Kwa maana hiyohiyo jamii nzima ya wanadamu, itakaporejeshwa, milele watakuwa ndugu za Kristo, na watoto wa Mungu, ingawa wa asili tofauti. Mungu ni Baba wa **wote** walio katika upatano naye, katika kila daraja na la kila asili.

Kundi lingine linalohusishwa na Kanisa la jina tu, ambalo halikuwahi kamwe kumwamini Yesu kama dhabihu ya dhambi zake, na ambalo kwa hiyo halijahesabiwa haki—haliko kwenye **daraja N**—linawakilishwa chini ya **daraja N**, kwa sehemu **q**. Hawa ni **"mbwa mwitu waliovaa ngozi ya kondoo"**; lakini bado wanajiita Wakristo na wanatambuliwa kama washiriki wa lile Kanisa la jina tu. Ukweli ni kwamba, wao si waamini wa kweli wanaomkubali Kristo kama Mkombozi wao. Wao wako katika daraja **R**; ni sehemu ya ulimwengu, na hawana nafasi ya kweli ndani ya Kanisa, bali wanaliletea madhara makubwa

Katika hali hii ya mchanganyiko, na makundi haya mbalimbali, **n, m, p,** na **q**, yakichanganyikana pamoja na yote yakijiita Wakristo, ndivyo Kanisa limekuwepo katika Zama zote za Injili. Kama Bwana wetu alivyotabiri, ufalme wa mbinguni wa jina tu (Kanisa la jina tu) unafanana na shamba lililopandwa ngano na magugu. Naye akasema "viache vyote vikue pamoja hata wakati

wa mavuno" mwishoni mwa zama. Wakati wa mavuno atawaambia wavunaji ("malaika"—wajumbe), *"Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita ili yateketezwe; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu."* —**Mathayo 13:38, 41, 49**

Maneno haya ya Bwana wetu yanatuonyesha kwamba ingawa alikusudia vyote vikue pamoja wakati wa zama hizi, na vitambuliwe kama washiriki wa Kanisa la jina tu, alikusudia pia kwamba kutakuja wakati wa utengano kati ya vitu hivi tofauti, ambapo wale ambao ni Kanisa la kweli, watakatifu wake (**n**) waliokubaliwa na kumilikiwa na Mungu, watadhihirishwa. —**Mathayo 13:39**

Wakati wa Zama za Injili, mbegu njema imekuwa ikikua, na magugu au waigaji pia. *"Mbegu njema ni wana wa ufalme,"* watoto wa kiroho, yaani, makundi **n** na **m**, ilhali *"magugu ni wana wa yule mwovu."* Kwa hiyo, wote wa kundi **q**, na wengi wa kundi **p**, ni "magugu"; kwa maana *"hakuna awezaye kuwatumikia mabwana wawili,"* na *"ninyi ni watumishi wake yeye mnayemtii."* Kwa kuwa wale walio katika kundi **p** hawatoi wakfu utumishi na talanta zao kwa Bwana aliyewanunua—utumishi wenye maana—bila shaka wanatoa muda wao mwingi na talanta zao katika kumpinga Mungu, na hivyo katika kumtumikia adui.

Sasa angalia kwenye chati, mavuno au mwisho wa Zama za Injili; angalia sehemu mbili inamogawanywa—miaka saba na miaka thelathini na tatu, mfano halisi wa mavuno ya Zama za Kiyahudi. Mavuno haya, kama yale ya Kiyahudi, kwanza yatakuwa wakati wa jaribu na kupepeta juu ya Kanisa, na baadaye wakati wa ghadhabu au kumwagwa kwa "**mapigo saba ya mwisho"** juu ya ulimwengu, likijumuisha Kanisa la jina tu. Kanisa la Kiyahudi lilikuwa ndicho 'kivuli' au kielelezo katika daraja la kimwili cha yote yale ambayo Kanisa la Injili linayafurahia katika daraja la kiroho. Kile kilichomjaribu Israeli wa kimwili katika mavuno ya zama zao ilikuwa ni KWELI iliyowasilishwa kwao wakati huo. Kweli ya wakati huo ilikuwa ndiyo mundu, nao uliwatenganisha "Waisraeli kweli kweli" kutoka kwa Kanisa la Kiyahudi la jina

tu; na katika ngano ya kweli kulikuwa na sehemu ndogo tu ikilinganishwa na waliokiri imani. Ndivyo ilivyo pia na mavuno ya zama hizi.

Mavuno ya Zama za Injili, kama yale ya Zama za Kiyahudi, yako chini ya usimamizi wa mvunaji mkuu, Bwana wetu Yesu, ambaye lazima awepo wakati huo. (**Ufunuo 14:14**) Kazi ya kwanza ya Bwana wetu katika mavuno ya zama hizi itakuwa ni kutenganisha walio wa kweli na walio wa uongo. Kanisa la jina tu, kwa sababu ya hali yake ya mchanganyiko, Bwana analiita "Babeli"—machafuko; na mavuno ni wakati wa kutenganisha makundi tofauti katika Kanisa la jina tu, na kwa ajili ya kukomaza na kukamilisha kundi la **n**. Ngano itatenganishwa na magugu, ngano iliyoiva na isiyoiva, n.k. Wale walio katika kundi **n** ni "malimbuko" ya ngano, na baada ya kutenganishwa, kwa wakati ufaao, watakuwa Bibi-arusi wa Kristo, na watakuwa pamoja na Bwana wao na kufanana naye milele.

Kutenganishwa kwa kundi hili dogo kutoka Babeli kunaonyeshwa kwa **umbo s**. Liko njiani kuwa **mmoja** na Bwana, na kubeba jina lake na kushiriki utukufu wake. Kristo aliyetukuzwa, Kichwa na mwili, anaonyeshwa kwa **umbo w**.

**Maumbo t, u,** na **v** yanawakilisha Babiloni—yaani, Kanisa la jina tu—likianguka na kusambaratika wakati wa **"kipindi cha taabu"** katika **"siku ya Bwana wetu."** Ingawa tukio hili linaweza kuonekana kuwa la kutisha, kwa uhalisia litakuwa la faida kubwa sana kwa ngano yote halisi (waamini wa kweli).

Babiloni inaanguka kwa sababu hali yake halisi ni tofauti na inavyojidai kuwa. Ndani ya Kanisa la jina tu kuna wanafiki wengi. Wamejiunga nalo kwa sababu ya heshima inayopata machoni pa ulimwengu. Lakini, kwa mwenendo wao, wanafanya Babiloni liwe chukizo kubwa mbele ya ulimwengu.

Bwana amekuwa akizijua tabia zao halisi siku zote, lakini kulingana na kusudi lake, anawavumilia hadi utakapofika wakati wa mavuno., atakapo *"wakusanya kutoka katika ufalme wake [Kanisa la*

*kweli, na kuwafunga matita] mambo yote ya kukwaza, na hao watendao maovu, na kuwatupa katika tanuru la moto [taabu,* ***inayoharibu*** *mfumo wao wa jina na ungamo lao la uongo]... Ndipo wenye haki [kundi* ***n****] watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao."* (**Mathayo 13:41-43**)

Taabu itakayolipata Kanisa itasababishwa kwa kiasi kikubwa na kukua kwa Kutokuamini na Kuwasiliana na Mizimu, kwa namna mbalimbali, mambo ambayo yatakuwa ni majaribu makali kwa sababu Babeli inashikilia mafundisho mengi yaliyo kinyume na Neno la Mungu. Kama ilivyokuwa katika mavuno ya Zama za Kiyahudi ambapo **msalaba** wa Kristo ulikuwa kwa Myahudi, aliyetarajia utukufu na mamlaka, jiwe la kujikwaa, na kwa Mgiriki mwenye hekima ya kidunia, upumbavu, ndivyo itakavyokuwa katika mavuno ya Zama za Injili ambapo litakuwa tena jiwe la kujikwaa na mwamba wa kukwaza.

Kila mtu aliyejenga juu ya Kristo kitu kingine chochote isipokuwa dhahabu, fedha na mawe ya thamani ya kweli, na tabia inayopatana nayo, atajikuta akisumbuliwa sana wakati wa ghadhabu ("moto"); kwa maana miti, majani na mabua yote ya mafundisho na matendo yatateketezwa. Wale waliojenga ipasavyo, na ambao matokeo yake wana tabia iliyokubaliwa, wanawakilishwa na **umbo s**, ilhali **t** inawakilisha "mkutano mkubwa sana," waliozaliwa kwa Roho, lakini waliojenga kwa miti, majani na mabua—ngano, lakini isiyoiva kikamilifu wakati wa kukusanywa kwa malimbuko (**s**). Wao (**t**) wanapoteza tuzo la kiti cha enzi na asili ya Uungu, lakini hatimaye watafikia kuzaliwa kama viumbe wa kiroho wa daraja la chini kuliko asili ya Uungu.

Ingawa hawa wamejiweka wakfu kweli, wanashindwa na roho ya kidunia kiasi kwamba wanashindwa kutoa maisha yao dhabihu. Hata katika "mavuno," wakati washiriki walio hai wa Bibi-arusi wanatenganishwa na wengine kwa **kweli**, masikio ya wengine, likiwemo kundi **t**, yatakuwa mazito kusikia.

Watakuwa wazito kuamini na wazito kutenda katika wakati huo wa utengano.

Bila shaka, watashtuka sana watakapotambua baadaye kwamba Bibi-arusi amekamilika na kuunganishwa na Bwana, na kwamba wao, kwa sababu walikuwa wazembe na waliolemewa, wamepoteza tuzo hiyo kuu; lakini uzuri wa mpango wa Mungu, ambao wataanza kuutambua kama wa upendo, kwa ajili yao na kwa ajili ya ulimwengu wote wa wanadamu, utaishinda kabisa huzuni yao, nao watapiga kelele, *"Haleluya! kwa kuwa Bwana Mungu Mwenyezi anamiliki. Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari."* (**Ufunuo 19:6, 7**)

Angalia, pia, maandalizi tele ya Bwana: ujumbe unatumwa kwao—Ingawa ninyi si Bibi-arusi wa Mwana-Kondoo, mnaweza kuwepo kwenye karamu ya arusi — *"Heri walioalikwa **karamuni ya arusi ya Mwana-Kondoo**."* (**Mstari wa 9**) Kundi hili, kwa wakati ufaao, kupitia adhabu za Bwana za kuwaadibisha, litakuja katika upatano kamili naye na mpango wake, na watafua mavazi yao, ili hatimaye waweze kufikia nafasi karibu na Bibi-arusi—**y**, kwenye daraja la kiroho, **L**. —**Ufunuo 7:14, 15**

Wakati wa taabu, utakavyouathiri ulimwengu, utakuwa ni baada ya Babeli kuanza kuanguka na kusambaratika. Utakuwa ni kupinduliwa kwa jamii yote ya kibinadamu na serikali zote, ukiandaa ulimwengu kwa ajili ya utawala wa haki. Wakati wa taabu, Israeli wa kimwili (**e**), aliyetupwa kando hadi utimilifu wa Wamataifa uingie, atarejeshwa kwenye fadhila ya Mungu, na Kanisa la Injili, au Israeli wa kiroho, litakamilishwa na kutukuzwa. Wakati wa zama ya Milenia (yaani, Utawala wa Miaka Elfu), taifa la Israeli litakuwa ndilo taifa kuu na kiongozi duniani. Watu wote watakaokuwa watiifu wataongozwa hatua kwa hatua ili kuungana na Israeli katika hali ya umoja na upatano.

Kurejeshwa kwao kwenye asili kamilifu ya kibinadamu, na pia kwa ulimwengu kwa ujumla, kutakuwa ni kazi ya taratibu,

itakayohitaji Zama zote za Milenia kwa ajili ya utimilifu wake kamili. Katika utawala huo wa miaka elfu wa Kristo, matokeo ya kifo cha Adamu yatakomeshwa au kuangamizwa hatua kwa hatua. Hatua zake mbalimbali—ugonjwa, maumivu na udhaifu, na pia kaburi—vitatii mamlaka ya Mrejeshi Mkuu, hadi mwisho wa zama hizo piramidi kuu la chati yetu litakapokuwa limekamilika.

Kristo (**x**) atakuwa kichwa cha vitu vyote—cha mkutano mkuu, cha malaika, na cha wanadamu—akifuata Baba; anayefuata katika daraja au cheo watakuwa ni mkutano mkuu, viumbe wa kiroho (**y**), na kisha, malaika; kisha Israeli wa kimwili (**z**), likijumuisha tu Waisraeli kweli kweli, wakiwa kichwa cha mataifa ya kidunia; kisha ulimwengu wa wanadamu (**w**), ukiwa umerejeshwa kwenye ukamilifu wa uwepo, kama kichwa cha jamii ya wanadamu, Adamu, kabla ya kutenda dhambi. Urejesho huu utatimizwa hatua kwa hatua wakati wa Zama za Milenia—"nyakati za urejesho." (**Matendo 3:21**)

Hata hivyo, wengine wataangamizwa kutoka miongoni mwa watu: kwanza, wote ambao, chini ya nuru kamili na fursa, kwa miaka mia moja watakataa kufanya maendeleo kuelekea haki na ukamilifu (**Isaya 65:20**); na pili, wale ambao, baada ya kufikia ukamilifu, katika jaribio la mwisho mwishoni mwa Milenia watathibitika kuwa si waaminifu. (**Ufunuo 20:9**) Watu kama hao wanakufa mauti ya pili, ambayo hakuna ufufuo wala urejesho ulioahidiwa kutoka kwayo. Ni jaribio moja tu kamili la mtu binafsi linalotolewa. Ni fidia moja tu itakayotolewa. **Kristo hafi tena.**

Tunapouangalia mpango mkuu wa Baba yetu wa kulitukuza Kanisa na kubariki kupitia kwake Israeli na jamaa zote za dunia kwa urejesho wa vitu vyote, unatukumbusha wimbo wa malaika:

*"Utukufu kwa Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani, kwa watu aliowaridhia!"*

Huo ndio utakuwa utimilifu wa mpango wa Mungu—"kuvijumlisha vitu vyote katika Kristo." Nani basi atasema kwamba mpango wa Mungu umeshindwa? Nani basi atasema kwamba hakuongoza uovu kwa ajili ya wema, na kuifanya ghadhabu ya wanadamu na mashetani imsifu?

Umbo la piramidi si tu kwamba linasaidia vizuri kusudi la kuwaonyesha viumbe wakamilifu, bali linaendelea kutimiza kusudi la kielelezo katika kuwakilisha umoja wa uumbaji wote, kama vile katika utimilifu wa mpango wa Mungu utakapokuwa **mmoja**, ambapo upatano na ukamilifu wa vitu vyote utafikiwa chini ya kichwa cha Kristo, aliye Kichwa, si tu cha Kanisa ambalo ni mwili wake, bali pia cha vitu vyote mbinguni na duniani. —*Waefeso 1:10*

Kristo Yesu alikuwa "mwanzo," "kichwa," "jiwe la kilele," "jiwe kuu la pembeni (la juu)" la jengo hili kuu, ambalo hadi sasa limeanzishwa tu; na kila jiwe la chini ni lazima lijengwe kwa kupatana na mistari na pembe za jiwe la kilele. Haijalishi ni aina ngapi za mawe zitakazokuwa katika jengo hili, haijalishi ni asili ngapi tofauti zitakazokuwepo miongoni mwa wana wa Mungu, wa duniani na wa mbinguni, wote, ili wakubalike kwake milele, ni lazima wafananishwe na sura ya Mwana wake. Wote watakaokuwa sehemu ya jengo hili ni lazima washiriki roho ya utii kwa Mungu, na ya upendo kwake na kwa viumbe vyake vyote (kama ilivyoonyeshwa kwa wingi katika Yesu), utimilifu wa sheria—*Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, akili, nafsi na nguvu zako zote, na jirani yako kama nafsi yako.*

Katika mchakato huu (kama Neno la Mungu linavyoueleza wa kuvikusanya pamoja vitu vyote, vya mbinguni na vya duniani, chini ya kichwa kimoja), Kristo Yesu, aliye Kichwa, alichaguliwa kwanza; pili, Kanisa, ambalo ni mwili wake. Malaika na makundi mengine ya kiroho watafuata katika cheo; kisha waadilifu wa Israeli na wa ulimwengu. Kuanzia walio juu zaidi, mpangilio utaendelea hadi wote **watakaokubali** watakapoletwa katika upatano na umoja.

Jambo la kipekee ni kwamba hili jiwe la kilele, la pembeni, lililojaribiwa, linawekwa kwanza na kuitwa jiwe la **msingi**. Hivi ndivyo inavyoonyeshwa kwamba msingi wa matumaini yote kwa Mungu na haki umewekwa, si duniani, bali mbinguni. Na wale wanaojengwa chini yake na kuunganishwa na msingi huu wa kimbingu wanashikiliwa kwake na mvuto na sheria za kimbingu. Na ingawa mpangilio huu ni kinyume kabisa na jengo la kidunia, jinsi gani inavyofaa kwamba jiwe ambalo mfano wake jengo zima linapaswa kuwa, liwekwe kwanza. Na jinsi gani inavyofaa pia kugundua kwamba msingi wetu unawekwa **kuelekea juu**, si **kuelekea chini**; na kwamba sisi, kama mawe yaliyo hai, *"tunajengwa **ndani yake** katika mambo yote."*

Hivyo kazi itaendelea wakati wa Zama za Milenia, hadi kila kiumbe, kwa kila asili, mbinguni na duniani, kitakapokuwa kikimsifu na kumtumikia Mungu kwa kupatana na mistari ya utiifu mkamilifu. Ulimwengu basi utakuwa safi; kwa maana katika siku hiyo *"itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo, ataangamizwa na kutengwa na watu wake"*—katika mauti ya pili. —*Matendo 3:22, 23*

**Hema ya Kukutania ya Jangwani**

Somo lile lile linaloonyeshwa katika ile Chati ya Zama linafundishwa hapa katika mfano huu uliopangwa na Mungu, ambapo masomo yake yatachunguzwa kwa kina zaidi hapo baadaye.

Tunaiweka [picha ya Hema] kando yake, ili madaraja au hatua tofauti za kuelekea Patakatifu pa Patakatifu ziweze kuonekana au kuthaminiwa ipasavyo, zikifundisha hatua zilezile ambazo tayari zimechunguzwa kwa kina. Nje ya uwanja wa hema kuna ulimwengu mzima ukiwa katika dhambi, kwenye daraja lililopotoka, **R.** Tukiingia kupitia 'lango' hadi ndani ya 'uwanja,' tunakuwa waumini au watu waliohesabiwa haki, kwenye daraja la **N**. Wale wanaosonga mbele katika kujiweka wakfu wanasogea hadi mlangoni mwa Hema, na, wakiingia ndani (daraja la **M**),

wanakuwa makuhani. Wanatiwa nguvu na 'mikate ya wonyesho,' wanaangazwa na 'kinara cha taa' na kuwezeshwa kutoa uvumba unaokubalika kwa Mungu kupitia Yesu Kristo kwenye **'Madhabahu ya Dhahabu**.' Hatimaye, katika ufufuo wa kwanza, wanaingia katika hali kamilifu ya kiroho, au **'Patakatifu pa Patakatifu' (daraja la L),** na kisha wanashirikiana na Yesu katika utukufu wa Ufalme, daraja la **K.**

***Tumaini Lenye Baraka***

*Bado kitambo, vita vya dunia vitakwisha; Bado kitambo, machozi yake yatafutwa; Bado kitambo, uweza wake Yehova Utageuza giza hili kuwa Siku ya Milenia.*

*"Bado kitambo, taabu zinazowaelemea sasa Zitabaki tu kuwa kumbukumbu za kale; Bado kitambo, upendo ule uliowakomboa Utageuza kilio chao kuwa wimbo wa shukrani.*

*"Bado kitambo! Inazidi kukaribia — Mapambazuko angavu ya siku hiyo tukufu. Sifa kwa Mungu, nuru inazidi kung'aa, Ikiangaza zaidi na zaidi hata mchana mkamilifu.*

## SOMO LA XIII

# FALME ZA ULIMWENGU HUU

MAMLAKA YA KWANZA—KUPOTEZWA KWAKE—KUKOMBOLEWA NA KUREJESHWA KWAKE—UFALME WA MUNGU ULIO MFANO—MNYANG'ANYI—SURA MBILI ZA MAMLAKA YA SASA—MAMLAKA ZILIZOPO, ZIMEAMRIWA NA MUNGU—MTAZAMO WA NEBUKADNEZA KUZIHUSU—MTAZAMO WA DANIELI NA TAFSIRI YAKE—FALME ZA ULIMWENGU HUU ZIKITAZAMWA KUTOKA MTAZAMO MWINGINE—UHUSIANO SAHIHI WA KANISA NA SERIKALI ZA SASA—HAKI YA KIMUNGU YA WAFALME IKICHUNGUZWA KWA UFUPI—MADAI YA UKRISTO WA JINA NI YA UONGO—TUMAINI BORA KATIKA UFALME WA TANO WA ULIMWENGU.

KATIKA sura ya kwanza ya Ufunuo wa Mungu, Mungu anatangaza kusudi lake kuhusu uumbaji wake wa kidunia na serikali yake:

> *"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi."*

Hivyo, utawala wa dunia uliwekwa mikononi mwa jamii ya wanadamu, ikiwakilishwa na mtu wa kwanza Adamu, aliyekuwa mkamilifu, na kwa hiyo aliyestahili kikamilifu kuwa bwana, mtawala au mfalme wa dunia. Agizo hili la kuzaa, kuijaza, kuitiisha, na kutawala dunia halikuwa kwa Adamu peke yake, bali kwa wanadamu wote: *"**Wao** wakatawale,"* n.k. Kama jamii ya wanadamu ingebaki kamilifu na isiyo na dhambi, utawala huu haungetoka kamwe mikononi mwake.

Ikumbukwe kwamba katika agizo hili hakuna mwanadamu anayepewa utawala au mamlaka juu ya wanadamu wenzake, bali jamii nzima inapewa utawala juu ya dunia, ili kuilima na kutumia mazao yake kwa ajili ya wema wa wote. Si tu utajiri wake wa mimea na madini unaowekwa chini ya amri ya mwanadamu,

bali pia aina zake zote za viumbe hai ziko chini yake na kwa ajili ya utumishi wake. Kama jamii ya wanadamu ingebaki kamilifu na kutekeleza mpango huu wa asili wa Muumba, kadiri idadi yao ilivyoongezeka ingekuwa muhimu kwa watu kushauriana pamoja, na kupanga juhudi zao kimfumo, na kubuni njia na mbinu za usambazaji wa haki na wenye hekima wa baraka za pamoja. Na kwa kuwa, baada ya muda, isingewezekana, kwa sababu ya idadi yao kubwa, kukutana na kushauriana pamoja, ingekuwa muhimu kwa makundi mbalimbali ya watu kuchagua baadhi yao ili wawawakilishe, watamke hisia zao za pamoja, na kuwatendea kazi. Na kama watu wote wangekuwa wakamilifu, kiakili, kimwili na kiadili; kama kila mtu angempenda Mungu na kanuni zake kwa moyo wote, na jirani yake kama nafsi yake, kusingekuwa na msuguano wowote katika mpango kama huo.

Kwa kuona hivi, mpango wa asili wa Muumba kwa ajili ya serikali ya dunia ulikuwa wa mfumo wa **Jamhuri**, serikali ambayo kila mtu angeshiriki; ambamo kila mwanadamu angekuwa mtawala mkuu, aliyestahili kikamilifu katika kila jambo kutekeleza majukumu ya ofisi yake kwa ajili ya wema wake mwenyewe na wa wote.

Utawala huu wa dunia aliopewa mwanadamu ulikuwa na sharti moja tu ambalo mwendelezo wake wa milele ulitegemea; nalo ni kwamba utawala huu uliotolewa na Mungu daima utekelezwe kwa upatano na Mtawala Mkuu wa ulimwengu, ambaye sheria yake moja, ikielezwa kwa ufupi, ni Upendo. *"Upendo ndio utimilifu wa sheria." "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote;... na mpende jirani yako kama nafsi yako."* —**Warumi 13:10; Mathayo 22:37-40.**

Kuhusu fadhila hii kuu aliyopewa mwanadamu, Daudi, akimsifu Mungu, anasema: *"Umemfanya mdogo punde kuliko malaika; Umemvika taji ya utukufu na heshima; Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako."* (**Zaburi 8:5, 6**) Utawala huu waliopewa wanadamu katika nafsi ya Adamu ulikuwa ndio uanzishwaji wa kwanza wa Ufalme wa Mungu duniani. Hivyo, mwanadamu alitumia

utawala kama mwakilishi wa Mungu. Lakini kutotii kwa mwanadamu kwa Mtawala Mkuu kulimfanya apoteze si tu uhai wake, bali pia haki na fursa zake zote kama mtawala mwakilishi wa Mungu duniani.

Tangu hapo akawa muasi, aliyevuliwa ufalme na kuhukumiwa kifo. Ndipo kwa haraka ufalme wa Mungu duniani ukakoma, na haujaanzishwa tena tangu wakati huo, isipokuwa kwa muda mfupi, kwa namna ya mfano, katika Israeli. Ingawa katika Edeni mwanadamu alipoteza haki yake ya uzima na utawala, hakunyang'anywa vitu hivyo ghafla; na maadamu uhai uliohukumiwa unaendelea, mwanadamu anaruhusiwa kutumia utawala wa dunia kulingana na mawazo na uwezo wake mwenyewe, hadi utakapofika wakati ufaao wa Mungu kwa ajili ya yeye aliye na haki ya kuchukua utawala aliounuua.

Kifo cha Bwana wetu kilikomboa au kununua si tu mwanadamu, bali pia urithi wake wote wa asili, ukijumuisha utawala wa dunia. Akiwa ameuununua, sasa anamiliki hati yake: yeye sasa ndiye mrithi halali, na kwa wakati ufaao, na hivi karibuni, atachukua milki ya ununuzi wake. (**Waefeso 1:14**) Lakini kama alivyomnunua mwanadamu si kwa ajili ya kumshikilia kama mtumwa wake, bali ili amrejeshe katika hali yake ya zamani, ndivyo ilivyo kwa utawala wa dunia: aliununua pamoja na baraka zote za asili za mwanadamu kwa kusudi la kuzirejesha wakati mwanadamu atakapokuwa tena na uwezo wa kuzitumia kwa upatano na mapenzi ya Mungu.

Kwa hiyo, utawala wa Masihi duniani hautakuwa wa milele. Utaendelea tu mpaka, kwa utawala wake thabiti wa chuma, atakapokuwa amezima uasi na ukaidi wote, na kuirejesha jamii iliyoanguka kwenye ukamilifu wa asili, watakapokuwa na uwezo kamili wa kutumia ipasavyo utawala wa dunia kama ilivyokusudiwa mwanzoni. Watakaporejeshwa hivyo, utakuwa tena ni Ufalme wa Mungu duniani, chini ya mwanadamu, mwakilishi aliyeteuliwa na Mungu.

Wakati wa Zama za Kiyahudi, Mungu aliwaandaa watu wa Israeli kama ufalme wake, chini ya Musa na Waamuzi—aina fulani ya Jamhuri—lakini ulikuwa wa mfano tu. Na utawala wa kimabavu zaidi ulioanzishwa baadaye, hasa chini ya Daudi na Sulemani, ulikuwa kwa namna fulani mfano wa ufalme ulioahidiwa, Masihi atakapotawala. Tofauti na mataifa yaliyowazunguka, Israeli walikuwa na Yehova kama Mfalme wao, na watawala wao walitumika chini yake kwa jina tu, kama tunavyojifunza kutoka **Zaburi 78:70, 71**. Hili limeelezwa kwa uwazi kabisa katika **2 Mambo ya Nyakati 13:8** na **1 Mambo ya Nyakati 29:23**, ambapo Israeli unaitwa "Ufalme wa Bwana," na ambapo inasemwa kwamba Sulemani *"akaketi katika kiti cha enzi cha BWANA, badala ya Daudi baba yake,"* ambaye alikikalia au kutumia utawala wa kiti hichohicho cha enzi kwa miaka arobaini iliyotangulia, akimfuata Sauli, mfalme wa kwanza.

Watu wa Israeli walipomkosea Bwana, aliwaadhibu mara kwa mara, hatimaye akauondoa ufalme wao kabisa. Katika siku za Sedekia, wa mwisho aliyetawala katika ukoo wa Daudi, fimbo ya enzi ya kifalme iliondolewa. Hapo ndipo ufalme wa mfano wa Mungu ulipopinduliwa.

Uamuzi wa Mungu kuhusu jambo hili unaelezwa katika maneno haya,

> *"Na wewe, Ewe mtu mwovu, uliyetiwa jeraha kiasi cha kukuua, mkuu wa Israeli, ambaye siku yako imekuja, katika wakati wa uovu wa mwisho; Bwana MUNGU asema hivi; Kiondoe kilemba, ivue taji; haya hayatakuwa tena kama yalivyo; kikweze kilicho chini, kakishushe kilichoinuka. Nitakipindua, nitakipindua, nitakipindua; hiki nacho hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake; nami nitampa." (**Ezekieli 21:25-27**)*

Katika utimilifu wa unabii huu mfalme wa Babeli aliinuka dhidi ya Israeli, akawachukua watu mateka na kumwondoa mfalme wao. Ingawa baadaye walirejeshwa na kuwa taifa tena na Koreshi Mwajemi, walikuwa chini ya himaya na waliolipa kodi kwa falme zilizofuata za Umedi-Uajemi, Ugiriki, na Roma, hadi

kuangamizwa kabisa kwa utaifa wao, mwaka 70 BK, na tangu wakati huo wakatawanywa miongoni mwa mataifa yote.

Ufalme wa Israeli ndio pekee, tangu anguko, ambao Mungu aliwahi kuutambua kuwa kwa namna yoyote unawakilisha serikali yake, sheria zake, n.k. Kulikuwa na mataifa mengi kabla yao, lakini hakuna lingine ambalo lingeweza kwa haki kudai kwamba Mungu ndiye mwanzilishi wake, au kwamba watawala wake walikuwa wawakilishi wa Mungu. Kilemba kilipoondolewa kwa Sedekia na ufalme wa Israeli kupinduliwa, iliamriwa kwamba ubaki umepinduliwa hadi Kristo, mrithi halali wa ulimwengu, atakapokuja kuudai.

Hivyo, kwa kumaanisha, falme nyingine zote zilizokuwa madarakani hadi kuanzishwa upya kwa ufalme wa Mungu zinaitwa "**falme za ulimwengu huu**," chini ya "**mkuu wa ulimwengu huu**"; na hivyo madai yoyote yanayotolewa na yeyote kati yao ya kuwa ni falme za Mungu ni ya uongo. Wala Ufalme huu wa Mungu hauku **"SIMAMISHWA**" wakati wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza. (**Luka 19:12**) Kuanzia wakati huo na kuendelea, Mungu amekuwa akichagua kutoka ulimwenguni wale watakaohesabiwa kuwa wamestahili kutawala pamoja na Kristo kama warithi pamoja naye wa kiti hicho cha enzi. Ni mpaka wakati wa kuja kwake kwa mara ya pili ndipo Kristo atautwaa ufalme, uweza na utukufu, na kutawala akiwa Bwana wa wote.

Falme nyingine zote isipokuwa ile ya Israeli Kimaandiko zinaitwa falme za kipagani au za Wamataifa—"falme za ulimwengu huu," chini ya "mkuu wa ulimwengu huu"—**Shetani**. Kuondolewa kwa ufalme wa Mungu katika siku za Sedekia kuliacha ulimwengu bila serikali yoyote ambayo Mungu angeweza kuikubali, au ambayo sheria na mambo yake aliyaelekeza kipekee. Serikali za Wamataifa Mungu alizitambua isivyo moja kwa moja, kwa kuwa anatangaza hadharani amri yake (**Luka 21:24**) kwamba katika kipindi cha mpito, udhibiti wa Yerusalemu na ulimwengu ungefanywa na serikali za Wamataifa.

Kipindi hiki cha mpito, au muda wa katikati, kati ya kuondolewa kwa fimbo ya enzi na serikali ya Mungu na kurejeshwa kwake katika nguvu na utukufu mkuu zaidi katika Kristo, Kimaandiko kinaitwa **"Nyakati za mataifa."** Na "nyakati" hizi au miaka, ambapo "falme za ulimwengu huu" zinaruhusiwa kutawala, zimewekwa na zina mipaka, na wakati wa kuanzishwa upya kwa Ufalme wa Mungu chini ya Masihi umewekwa na kuonyeshwa vivyo hivyo katika Maandiko.

Ingawa serikali hizi za mataifa zimekuwa mbovu, ziliruhusiwa au "kuwekwa na Mungu" kwa kusudi la hekima. (**Warumi 13:1**) Ukosefu wao wa ukamilifu na utawala mbaya ni sehemu ya somo la jumla juu ya ubaya mwingi wa dhambi, na vinathibitisha kutoweza kwa mwanadamu aliyeanguka kujitawala mwenyewe, hata kwa namna inayomridhisha. Mungu anaziruhusu, kwa sehemu kubwa, zitekeleze makusudi yao wenyewe kadiri ziwezavyo, akiziingilia tu zinapotaka kuvuruga mipango yake. Anakusudia kwamba hatimaye yote yatafanya kazi kwa wema, na kwamba hatimaye hata *"Maana hasira ya binadamu itakusifu,..."* Mabaki yake, ambayo hayangeleta wema, hayangetumikia kusudi lolote au kufundisha somo lolote, huyazuia. — **Zaburi 76:10**

Kutoweza kwa mwanadamu kuanzisha serikali kamilifu kunatokana na udhaifu wake mwenyewe katika hali yake ya anguko, na ya upotovu. Udhaifu huu, ambao wenyewe ungetatiza juhudi za kibinadamu za kuleta serikali kamilifu, pia umetumiwa na Shetani, ambaye kwanza alimjaribu mwanadamu asiwe mwaminifu kwa Mtawala Mkuu. Shetani ameendelea kutumia udhaifu wa mwanadamu, akafanya mema yaonekane mabaya, na mabaya yaonekane mema; naye amepotosha tabia na mipango ya Mungu na kuwapofusha wanadamu wasione ukweli. Akifanya kazi hivyo katika mioyo ya wana wa uasi (**Waefeso 2:2**), amewachukua mateka kama apendavyo na kujifanya kile ambacho Bwana wetu na mitume wanamwita—mkuu au mtawala wa ulimwengu huu. (**Yohana 14:30; 12:31**) Yeye si mkuu wa

ulimwengu huu kwa haki, bali kwa unyang'anyi; kupitia udanganyifu, ulaghai na kuwatawala wanadamu walioanguka. Ni kwa sababu yeye ni mnyang'anyi ndiyo maana ataondolewa madarakani kwa ghafla. Kama angekuwa na haki halisi kama mkuu wa ulimwengu huu, asingeshughulikiwa hivyo.

Hivyo itaonekana kwamba utawala wa dunia, kama unavyotumiwa sasa, una pande mbili, **usioonekana na unaoonekana**. Ule wa kwanza ni wa kiroho, na wa pili ni wa kibinadamu—falme zinazoonekana za kidunia zikiwa kwa kiasi fulani chini ya udhibiti wa mkuu wa anga, Shetani. Ni kwa sababu Shetani alikuwa na udhibiti kama huo ndiyo maana aliweza kujitolea kumfanya Bwana wetu awe mfalme mkuu anayeonekana wa dunia chini ya uongozi wake. (**Mathayo 4:9**) Nyakati za mataifa zitakapoisha, pande zote mbili za utawala wa sasa zitakoma: Shetani atafungwa na falme za ulimwengu huu zitapinduliwa.

Uumbaji ulioanguka, uliopofushwa, na unaougua umesonga mbele kwa shida katika njia yake ya uchovu kwa karne nyingi, ukishindwa katika kila hatua, hata juhudi zake bora zikithibitika kuwa hazina matunda, lakini daima ukitumaini kwamba zama za dhahabu zilizotamaniwa na wanafalsafa wake zilikuwa karibu. Haujui kwamba ukombozi mkuu zaidi kuliko ule unaoutumaini na kuuugulia utakuja kupitia Mnazarayo aliyedharauliwa na wafuasi wake, ambao kama Wana wa Mungu watadhihirishwa hivi karibuni katika nguvu za ufalme kwa ajili ya ukombozi wake. —**Warumi 8:22, 19**

Ili watoto wake wasiwe gizani kuhusiana na kuruhusu kwake serikali mbovu za sasa na kuhusu kusudi lake la mwisho la kuleta serikali bora wakati falme hizi, chini ya majaliwa yake yanayoongoza, zitakapokuwa zimetimiza kusudi ambalo ziliruhusiwa, Mungu ametupa, kupitia manabii wake, maono kadhaa makuu ya kimtazamo ya "falme za ulimwengu huu," kila mara akionyesha, kwa ajili ya kututia moyo, kupinduliwa kwake na kuanzishwa kwa ufalme wake wa haki na wa milele chini ya Masihi, Mfalme wa Amani.

Kwamba juhudi za sasa za mwanadamu za kutumia utawala si katika kukaidi kwa mafanikio mapenzi na nguvu za Yehova, bali ni kwa ruhusa yake, inaonyeshwa na ujumbe wa Mungu kwa Nebukadreza, ambapo Mungu anatoa **ruhusa** ya kutawala, hadi wakati wa kusimamishwa kwa ufalme wa Kristo, kwa falme nne kuu, Babeli, Umedi-Uajemi, Ugiriki na Roma. (**Danieli 2:37-43**) Hii inaonyesha ni wapi kipindi hiki cha utawala wa muda kitaishia.

Tunapoangalia sasa maono haya ya kinabii, hebu tukumbuke kwamba yanaanza na Babeli wakati wa kupinduliwa kwa ufalme wa Israeli, ufalme wa mfano wa Bwana.

### Ndoto ya Nebukadneza Kuhusu Serikali za Dunia

Miongoni mwa mambo "yaliyoandikwa zamani kwa ajili ya mafundisho yetu," ili sisi, tulioamriwa kuzitii mamlaka zilizopo, tuweze kuwa na tumaini kwa saburi na faraja ya Maandiko (**Warumi 15:4; 13:1**), ni ndoto ya Nebukadneza na tafsiri yake ya kimungu kupitia Nabii. —**Danieli 2:31-45**

Danieli aliifafanua ndoto hiyo, akisema:

> *"Wewe, Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana. Sanamu hii, iliyokuwa kubwa sana, na mwangaza wake mwingi sana, ilisimama mbele yako; na umbo lake lilikuwa lenye kutisha.Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba;miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo.Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila kazi ya mikono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa milima mikubwa, likaijaza dunia yote. Hii ndiyo ile ndoto, nasi tutaihubiri tafsiri yake mbele ya mfalme. Wewe, Ee mfalme, u mfalme wa wafalme[hapo ndipo falme za Wamataifa, au mamlaka zilizopo, ziliwekwa na Mungu], na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme, na uwezo, na nguvu, na*

*utukufu; na kila mahali wakaapo wanadamu, wanyama wa kondeni na ndege wa angani amewatia mkononi mwako, naye amekumilikisha juu ya hao wote; wewe u kichwa kile cha dhahabu. Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe; na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utakaoitawala dunia yote. Na ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja na kuseta. Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika; lakini ndani yake zitakuwako nguvu za chuma, kama vile ulivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope. Na kama vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu, na nusu yake umevunjika. Na kama vile ulivyokiona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo. Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele. Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunja-vunja kile chuma, na ile shaba na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti."*

Mwanafunzi wa historia anaweza kwa urahisi kuzitambua, miongoni mwa falme nyingi ndogo za dunia zilizoibuka, zile nne zilizoelezwa hapo juu na Danieli. Hizi zinaitwa **FALME ZA ULIMWENGU WOTE**—Babeli, ya kwanza, kichwa cha dhahabu (mstari wa 38); Umedi-Uajemi, mshindi wa Babeli, ya pili, kifua cha fedha; Ugiriki, mshindi wa Umedi-Uajemi, ya tatu, tumbo la shaba; na Roma, ya nne, ufalme wenye nguvu, miguu ya chuma na nyayo zilizochanganyika na udongo. Falme tatu kati ya hizi zilikuwa zimepita, na ya nne, ya Roma, ilishikilia utawala wa ulimwengu wote, wakati wa kuzaliwa kwa Bwana wetu, kama tunavyosoma, " *Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari*

*Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu* ***wote wa ulimwengu****."* —**Luka 2:1**

Ufalme wa chuma, Rumi, ulikuwa na nguvu zaidi, na ulidumu kwa muda mrefu kuliko walioutangulia. Kwa kweli, Dola ya Kirumi bado inaendelea, ikiwakilishwa na mataifa ya Ulaya. Mgawanyiko huu unawakilishwa katika vidole kumi vya sanamu.

Kipengele cha udongo kilichochanganyika na chuma katika nyayo za miguu kinawakilisha mchanganyiko wa kanisa na serikali. Mchanganyiko huu katika Maandiko unaitwa **"Babeli"**—machafuko. Kama tutakavyoona hivi karibuni, **jiwe** ni ishara ya Ufalme wa kweli wa Mungu, na Babeli aliweka mwigo wa jiwe—udongo—ambao ameuunganisha na mabaki yaliyogawanyika ya Dola ya Kirumi [ya chuma].

Na mfumo huu wa mchanganyiko—kanisa na serikali—Kanisa la jina tu lililofunga ndoa na falme za ulimwengu huu, ambalo Bwana analiita Babeli, machafuko, linajidai kujiita Jumuiya ya Wakristo—Ufalme wa Kristo. Danieli anafafanua:

> *"Na kama vile ulivyoona chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao na wanadamu [kanisa na ulimwengu vinachanganyikana – Babeli], lakini hawataambatana, kama vile chuma kisivyochanganyika na udongo." Hawawezi kuchanganyikana kabisa. "Na katika siku za wafalme hao [falme zinazowakilishwa na vidole vya miguu, zile zinazoitwa 'falme za Kikristo' au 'Jumuiya ya Wakristo'] Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele; wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote na kuziharibu, nao utasimama milele."* — ***Danieli 2:43, 44***

Danieli hapa hataji wakati wa mwisho wa serikali hizi za mataifa: hilo tunalipata mahali pengine; lakini kila hali iliyotabiriwa inaonyesha kwamba leo mwisho umekaribia, naam, upo mlangoni. Mfumo wa Upapa kwa muda mrefu umedai kwamba ndio ufalme ambao Mungu wa mbinguni aliahidi kuusimamisha, na

kwamba, katika utimilifu wa unabii huu, ulizivunja vipande vipande na kuziharibu falme nyingine zote.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba, Kanisa la jina tu liliungana na falme za kidunia kama udongo na chuma, na kwamba Upapa haukuwa kamwe Ufalme wa kweli wa Mungu, bali ulikuwa bandia tu. Mojawapo ya ushahidi bora zaidi kwamba Upapa haukuziharibu na kuziteketeza falme hizi za kidunia ni kwamba bado zipo. Na sasa kwa kuwa udongo wa matope umekauka na kuwa "mwepesi kuvunjika," unapoteza nguvu yake ya kushikamana, na chuma na udongo vinaonyesha dalili za kusambaratika, na vitaporomoka haraka vitakapopigwa na "jiwe," Ufalme wa kweli.

Akiendelea na tafsiri yake, Danieli anasema:

> *" Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunja-vunja kile chuma, na ile shaba na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti."* —***Mstari wa* 45**

Jiwe lililochongwa mlimani bila kazi ya mikono, linalopiga na kuzitawanya mamlaka za mataifa, linawakilisha Kanisa la kweli, Ufalme wa Mungu. Wakati wa Zama za Injili ufalme huu wa "jiwe" unaumbwa, "unachongwa," na kupewa umbo kwa ajili ya nafasi yake ya baadaye na ukuu wake—si kwa mikono ya wanadamu, bali kwa nguvu au roho ya kweli, nguvu isiyoonekana ya Yehova. Utakapokamilika, utakapochongwa kabisa, utazipiga na kuziharibu falme za ulimwengu huu. Si watu, bali serikali, ndizo zinazoashiriwa na ile sanamu, na hizi ndizo zitakazoharibiwa ili watu waweze kukombolewa. Bwana wetu Yesu hakuja kuharibu maisha ya watu, bali kuwaokoa. —**Yohana 3:17**

**Jiwe**, wakati wa maandalizi yake, linapokuwa linachongwa, linaweza kuitwa mlima kiinitete, kwa mtazamo wa hatima yake ya baadaye; vivyo hivyo, Kanisa linaweza kuitwa, na wakati mwingine linaitwa, Ufalme wa Mungu. Hata hivyo, kwa kweli, jiwe haliwi mlima hadi litakapoipiga sanamu; na hivyo Kanisa,

kwa maana kamili, litakuwa Ufalme wa kuijaza dunia yote wakati wa"siku ya Bwana," "siku ya hasira juu ya mataifa" au "wakati wa taabu," utakapokuwa umekwisha, na utakapokuwa umesimamishwa imara na falme nyingine zote kuwa tiifu kwake.

Kumbukeni sasa ahadi aliyoitoa Bwana wetu kwa washindi wa Kanisa la Kikristo:

> *"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi" – "Na yeye ashindaye, na kuyashika matendo yangu hata mwisho, nitampa amri juu ya mataifa; naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, na kama vyombo vya mfinyanzi watavunjwa vipande vipande; kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu." (**Ufunuo 3:21; 2:26, 27; Zaburi 2:8-12**)*

Fimbo ya chuma itakapokuwa imekamilisha kazi ya uharibifu, ndipo mkono uliopiga utakapogeuka na kuponya, na **watu** watamrudia Bwana, naye atawaponya (**Isaya 19:22; Yeremia 3:22, 23; Hosea 6:1; 14:4; Isaya 2:3**), akiwapa uzuri badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, na vazi la sifa badala ya roho nzito.

### Ndoto ya Danieli Kuhusu Serikali za Kidunia.

Katika ndoto ya Nebukadneza tunaona falme za dunia, kama zinavyotazamwa kutoka kwa mtazamo wa ulimwengu, kuwa ni maonyesho ya utukufu, ukuu, na nguvu za kibinadamu; ingawa ndani yake tunaona pia dokezo la kuchakaa na kuangamizwa kwake mwishoni, kama inavyoelezwa katika kufifia kutoka dhahabu hadi chuma na udongo.

Lile **Kundi la jiwe**, ambalo ndilo Kanisa la kweli, katika kipindi chote cha kuchaguliwa kwake kutoka ulimwenguni (kinachofananishwa na "mlima"), limekuwa likionekana na ulimwengu kama kitu kisicho na thamani. Limedharauliwa na kukataliwa na wanadamu. Hawakuona uzuri wowote ndani yake wa kuwafanya walitamani.

Ulimwengu unawapenda, unawastaajabia, unawasifu na kuwatetea watawala na serikali zinazowakilishwa katika sanamu hii kuu, ingawa umeendelea kukatishwa tamaa, kudanganywa, kujeruhiwa na kukandamizwa nao. Ulimwengu unawasifu kwa shamrashamra, katika maandishi na mashairi, watu wakuu na waliofanikiwa wa sanamu hii, akina Alexander, Kaisari, Bonaparte na wengine, ambao ukuu wao ulionekana katika mauaji ya wanadamu wenzao, na ambao, katika tamaa yao ya madaraka, walisababisha mamilioni ya wajane na yatima. Na ndivyo ilivyo bado roho iliyopo katika "vidole kumi" vya sanamu, kama tunavyoiona ikionyeshwa leo katika majeshi yao yaliyopangwa ya zaidi ya watu milioni kumi na mbili waliojihami kwa kila kifaa cha kishetani cha ubunifu wa kisasa, ili kuuana kwa amri ya "**mamlaka zilizopo**."

*" Na sasa twasema ya kwamba wenye kiburi ndio walio heri; naam, watendao uovu ndio wajengwao; naam, wamjaribuo Mungu ndio waponywao."* (**Malaki 3:15**). Je, hatuwezi kuona, basi, kwamba kuangamizwa kwa sanamu hii kuu kwa kupigwa na lile jiwe, na kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu, kunamaanisha ukombozi wa wanaokandamizwa na baraka kwa wote? Ingawa kwa muda mabadiliko hayo yatasababisha maafa na taabu, hatimaye yatatoa matunda ya haki yenye amani.

Lakini sasa, tukikumbuka tofauti ya mtazamo, hebu tuziangalie falme zilezile nne za ulimwengu wote za dunia kutoka kwa mtazamo wa Mungu na wale walio katika upatano naye, kama zilivyoonyeshwa katika ndoto kwa nabii mpendwa Danieli. Kama kwetu falme hizi zinavyoonekana kuwa zisizo na utukufu na za kinyama, ndivyo kwake falme hizi nne za ulimwengu wote zilionyeshwa kama wanyama-mwitu wanne wakubwa na wakali. Na kwa mtazamo wake, Ufalme ujao wa Mungu (lile jiwe) ulikuwa mkuu zaidi kuliko ulivyoonekana na Nebukadneza. Danieli anasema:

> *"Danieli akanena, akisema, Naliona katika maono yangu wakati wa usiku; na tazama, hizo pepo nne za mbinguni zilivuma kwa nguvu*

*juu ya bahari kubwa. Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini, wote wa namna mbalimbali. Wa kwanza alikuwa kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai; nikatazama, hata mabawa yake yakafutuka manyoya, akainuliwa katika nchi, akasimamishwa juu kwa miguu miwili kama mwanadamu; naye akapewa moyo wa kibinadamu. Na tazama, mnyama mwingine, wa pili, kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake; wakamwambia mnyama huyo hivi, Inuka, ule nyama tele. Kisha nikatazama, na kumbe! Mnyama mwingine, kama chui, naye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege; mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne; akapewa mamlaka. Baadaye nikaona katika njozi ya usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi, naye alikuwa na meno ya chuma, makubwa sana; alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; na umbo lake lilikuwa mbali kabisa na wale wa kwanza, naye alikuwa na pembe kumi" –* ***Danieli 7:2-7***

Maelezo ya kina yanayohusu wanyama watatu wa kwanza (Babeli simba, Umedi-Uajemi dubu, na Ugiriki chui), pamoja na vichwa vyao, miguu, mabawa, n.k., ambayo yote ni ya mfano, tunayaacha, kwa kuwa si muhimu sana katika uchunguzi wetu wa sasa kuliko maelezo ya kina ya mnyama wa nne, Rumi.

Kuhusu mnyama wa nne, Rumi, Danieli anasema:

*"Baadaye nikaona katika njozi ya usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi, naye alikuwa na meno ya chuma, makubwa sana; alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; na umbo lake lilikuwa mbali kabisa na wale wa kwanza, naye alikuwa na pembe kumi. Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu.." –* ***Danieli 7:7, 8***

Hapa Dola ya Kirumi inaonyeshwa; na migawanyiko ya mamlaka yake inaonyeshwa katika zile pembe kumi, pembe ikiwa ni ishara ya **mamlaka**. Ile pembe ndogo iliyoinuka miongoni mwa hizi, na ambayo ilijinyakulia mamlaka ya tatu kati yazo, na

kutawala miongoni mwa zile nyingine, inawakilisha mwanzo mdogo na kuinuka taratibu kwa mamlaka ya Kanisa la Roma, yaani, mamlaka ya **Kipapa**. Lilipokuwa likiinuka katika ushawishi, migawanyiko mitatu, pembe au mamlaka za Dola ya Kirumi (Heruli, Uwakilishi wa Mashariki na Ostrogoth) ziling'olewa ili kutoa nafasi kwa ajili ya kuanzishwa kwake kama mamlaka ya kiraia. Pembe hii ya mwisho yenye sifa maalum, yaani Upapa, inajulikana kwa macho yake, yanayowakilisha akili, na kwa kinywa chake—matamshi yake, madai yake, n.k.

Kwa mnyama huyu wa nne, anayewakilisha Rumi, Danieli hamtoi jina la kumwelezea. Wakati wengine wanaelezwa kuwa kama simba, kama dubu na kama chui, wa nne alikuwa mkali na wa kutisha kiasi kwamba hakuna mnyama yeyote wa duniani aliyeweza kulinganishwa naye.

Yohana , akimwona mnyama huyu wa mfano (serikali) katika njozi, pia alikosa jina la kumwelezea, na hatimaye alimpa majina kadhaa. Miongoni mwa mengine, alimwita "Ibilisi." (**Ufunuo 12:9**) Hakika alichagua jina linalofaa; kwa maana Roma, inapotazamwa kwa kuzingatia mateso yake ya umwagaji damu, hakika imekuwa ya kishetani zaidi kati ya serikali zote za kidunia. Hata katika mabadiliko yake kutoka Rumi ya Kipagani kwenda Roma ya Kipapa ilionyesha mojawapo ya sifa kuu za Shetani; kwa maana yeye pia hujigeuza aonekane kama **malaika wa nuru** (**2 Wakorintho 11:14**), kama vile Rumi ilivyojigeuza kutoka katika upagani na kudai kuwa ya Kikristo—**Ufalme wa Kristo**.*

Baada ya kutoa maelezo kadhaa kuhusu mnyama huyu wa mwisho au wa Kirumi, na hasa kuhusu pembe yake ya kipekee ya

---

* *Ukweli kwamba Roma inaitwa "Ibilisi" haukanushi kamwe kuwepo kwa Ibilisi wa kiuhalisia: bali ni kinyume chake. Ni kwa sababu kuna wanyama kama simba, dubu, na chui, wenye tabia zinazojulikana, ndiyo maana serikali zilifananishwa nao; na vivyo hivyo, ni kwa sababu yupo Ibilisi, mwenye tabia zinazojulikana, ndiyo maana ufalme wa nne unafananishwa naye.*

Kipapa, Nabii anasema kwamba hukumu dhidi ya pembe hii ingetolewa, na ingeanza kupoteza mamlaka yake, ambayo **ingeteketezwa** kwa mchakato wa taratibu hadi **mnyama** atakapoangamizwa.

Mnyama huyu au Dola ya Kirumi katika pembe zake au migawanyiko yake bado ipo, na itauawa na kuinuka kwa umati wa watu, na kupinduliwa kwa serikali, katika "Siku ya Bwana," kama maandalizi ya kutambuliwa kwa utawala wa kimbingu. Hili linaonyeshwa wazi kutoka katika maandiko mengine ambayo bado hayajachunguzwa. Hata hivyo, **kuteketezwa** kwa pembe ya Kipapa huja kwanza. Nguvu na ushawishi wake vilianza kuteketezwa wakati Napoleon alipomchukua Papa mateka kwenda Ufaransa. Kisha, wakati laana za Mapapa wala sala zao hazikuwaokoa kutoka kwa mamlaka ya Bonaparte, ikawa dhahiri kwa mataifa kwamba mamlaka ya kimungu na nguvu zilizodaiwa na Upapa hazikuwa na msingi. Baada ya hapo, mamlaka ya kidunia ya Upapa yalififia haraka hadi, mnamo Septemba, 1870, ilipopoteza chembe ya mwisho ya mamlaka yake ya kidunia mikononi mwa **Victor Emmanuel.**

Hata hivyo, katika kipindi chote hicho ambacho ilikuwa "ikiteketezwa," iliendelea kutoa maneno yake makuu ya makufuru, tamko lake kuu la mwisho likiwa mwaka 1870, ambapo, miezi michache tu kabla ya kupinduliwa kwake, ilitoa tamko la **kutokosea** kwa Mapapa. Yote haya yanaelezwa katika unabii:

> *"Nikatazama **wakati huo** [yaani, **baada** ya amri dhidi ya 'pembe' hii, baada ya kuteketezwa kwake kuanza] kwa sababu ya sauti ya yale **MANENO MAKUU** iliyoyanena ile pembe."* – ***Danieli 7:11***

Hivyo, katika historia tumefikishwa mpaka siku zetu wenyewe, na kuonyeshwa kwamba jambo linalopaswa kutazamiwa, kwa kadiri falme za dunia zinavyohusika, ni kuangamizwa kwake kabisa. Jambo linalofuata linaelezwa kwa maneno, *"Nikatazama*

*hata mnyama yule akauawa, na mwili wake ukaharibiwa, ukatolewa apate kuteketezwa kwa moto."*

Kuuawa na kuchomwa ni ishara, kama vile mnyama mwenyewe alivyo ishara, na vinamaanisha kuangamizwa kabisa na bila tumaini kwa serikali zilizopangwa za sasa. Katika mstari wa 12 nabii anaona tofauti kati ya mwisho wa mnyama huyu wa nne na watangulizi wake. Wale watatu kwa mfululizo (Babeli, Uajemi na Ugiriki) **mamlaka** yao yaliondolewa; waliacha kushikilia mamlaka ya kutawala dunia; lakini maisha yao kama mataifa hayakukoma mara moja. Ugiriki na Uajemi bado vina uhai kiasi, ingawa ni karne nyingi zimepita tangu mamlaka ya ulimwengu wote ilipoondoka mikononi mwao. Hata hivyo, haitakuwa hivyo kwa Dola ya Rumi, yule mnyama wa nne na wa mwisho kati ya hawa. Yeye atapoteza mamlaka na uhai kwa mpigo mmoja, na kuingia katika maangamizi kamili; na pamoja naye, wale wengine watatoweka pia —**Danieli 2:35**

Haijalishi ni njia gani au chombo gani kitakachotumiwa, **sababu** ya anguko hili itakuwa ni kuanzishwa kwa Ufalme wa Tano wa Ulimwengu Wote wa dunia, Ufalme wa Mungu, chini ya Kristo, ambaye ana haki ya kuchukua utawala. Uhamisho wa ufalme kutoka kwa mnyama wa nne, ambaye kwa wakati wake uliopangwa "aliwekwa na Mungu," kwenda kwenye ufalme wa tano, chini ya Masihi, wakati majira yake yaliyopangwa yatakapofika, unaelezwa na Nabii kwa maneno haya:

> *"Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye [Kristo—kichwa na mwili wakiwa wamekamilika] akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie. Mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa." Hili malaika alilifasiri kumaanisha kwamba "ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu nzima, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ambao ufalme wao ni ufalme wa milele, na mamlaka zote zitamtumikia na kumtii."* —***Danieli 7:13, 27***

Kwa kuona hivi, utawala wa dunia utawekwa mikononi mwa Kristo na Yehova ("Mzee wa Siku"), atakaye *"vitia vitu vyote chini ya miguu yake."* (**1 Wakorintho 15:27**) Hivyo, akiwa ametawazwa juu ya ufalme wa Mungu, lazima atawale mpaka atakapokwisha kukomesha kila mamlaka na nguvu inayopingana na mapenzi na sheria ya Yehova. Ili kutimiza utume huu mkuu, kupinduliwa kwa serikali hizi za mataifa ni muhimu kwanza; kwa maana "falme za ulimwengu huu," kama "mkuu wa ulimwengu huu," hazitajisalimisha kwa amani, bali ni lazima zifungwe na kuzuiliwa kwa nguvu. Na ndivyo ilivyoandikwa, *"Kuwafunga wafalme wao kwa minyororo, Na wakuu wao kwa pingu za chuma; Kuwatendea hukumu iliyoandikwa, Heshima hii wanayo watakatifu wake wote."* —**Zaburi 149:8, 9**

Tunapoziangalia hivi serikali za sasa kutoka kwa mtazamo wa Bwana wetu na wa Nabii Danieli, na kutambua tabia zake za kinyama, za uharibifu, na za ubinafsi, mioyo yetu inatamani mwisho wa serikali za mataifa na inatazamia kwa furaha wakati huo uliobarikiwa ambapo washindi wa zama hizi wataketishwa enzi pamoja na Kichwa chao, ili kutawala, kubariki na kuurejesha uumbaji unaougua. Hakika watoto wote wa Mungu wanaweza kusali kwa moyo wote pamoja na Bwana wao—"**UFALME WAKO UJE**, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni."

Kila moja ya serikali hizi zilizowakilishwa katika ile sanamu na wale wanyama ilikuwepo kabla ya kupata mamlaka kama ufalme wa ulimwengu wote. Ndivyo ilivyo pia na Ufalme wa kweli wa Mungu: umekuwepo kwa muda mrefu ukiwa umetengana na ulimwengu, usijaribu kutawala, bali ukingoja wakati wake—wakati uliopangwa na Mzee wa Siku. Na, kama zile nyingine, ni lazima upokee uteuzi wake na uingie katika mamlaka au "kusimamishwa" **kabla** ya kuweza kutumia nguvu zake katika kuipiga na kuiua falme iliyotangulia.

Hapo ndipo panapofaa kauli, *"Na katika siku za wafalme hao [wakati bado wana mamlaka] Mungu wa mbinguni atausimamisha*

*[kuuweka imara katika nguvu na mamlaka] ufalme."* Na baada ya kusimamishwa, *"utavunja falme hizi zote na kuziharibu, nao utasimama milele."* (**Danieli 2:44**) Kwa hiyo, hata tuutazamie vipi, ni lazima tutarajie Ufalme wa Mungu uzinduliwe **kabla** ya kuanguka kwa falme za ulimwengu huu, na kwamba nguvu na pigo lake ndivyo vitaleta kupinduliwa kwao.

### Serikali za Sasa Kutoka Mtazamo Mwingine

Haki na mamlaka kuu ya kuutawala ulimwengu daima zitakuwa mikononi mwa Muumba, Yehova, haijalishi ni nani anayeruhusu au anayempa idhini ya kuwa na udhibiti wa chini yake. Kutokana na udhaifu na kasoro zilizotokana na uasi wake kwa Mfalme wa wafalme, Adamu alianza kudhoofika na kukosa msaada. Kama mtawala, alianza kupoteza nguvu alizokuwa nazo mwanzoni, ambazo zilimwezesha kuamuru na kudhibiti utii wa wanyama wa chini kwa nguvu ya utashi wake. Alipoteza pia udhibiti wake mwenyewe, kiasi kwamba alipotaka kufanya mema, udhaifu wake uliingilia kati na uovu ulikuwa pamoja naye. Hivyo, mema aliyotaka kufanya hakuyatenda, na uovu aliokuwa hataki kuufanya, aliufanya.

Kwa hiyo, ingawa hatujaribu kuitetea jamii yetu ya waasi, tunaweza kuhurumia juhudi zake za bure za kujitawala na kujipangia ustawi wake. Na kuna kitu kinaweza kusemwa kuhusu mafanikio ya ulimwengu katika mwelekeo huu; kwa maana, huku tukitambua tabia halisi ya serikali hizi za kinyama, ingawa zimekuwa fisadi, zimekuwa bora zaidi kuliko kutokuwepo kabisa—bora zaidi kuliko hali ya kutokuwa na sheria na machafuko. Ingawa machafuko pengine yangekubalika kabisa kwa "mkuu wa ulimwengu huu," haikuwa hivyo kwa raia zake, na mamlaka yake si kamili: yana mipaka kulingana na uwezo wake wa kutenda kazi kupitia wanadamu; na sera yake lazima kwa kiasi kikubwa ifanane na mawazo, tamaa, na chuki za wanadamu.

Wazo la mwanadamu lilikuwa ni kujitawala bila kumtegemea Mungu; na Mungu alipomruhusu ajaribu, Shetani alichukua

fursa hiyo kupanua ushawishi na mamlaka yake. Hivyo, ilikuwa ni kwa kutaka kumsahau Mungu **(Warumi 1:28)** ndipo mwanadamu alipojiweka wazi kwa ushawishi wa adui huyu mjanja na mwenye nguvu, ingawa haonekani; na hivyo, tangu wakati huo, amelazimika kupambana na hila za Shetani, pamoja na udhaifu wake mwenyewe.

Kwa kuwa hali iko hivi, hebu tuziangalie tena falme za ulimwengu huu, tukiziona sasa kama juhudi za wanadamu walioanguka kujitawala bila kumtegemea Mungu. Ingawa ufisadi na ubinafsi wa mtu mmoja mmoja umepotosha mkondo wa haki, kiasi kwamba haki kamili ni mara chache imetolewa kwa yeyote chini ya falme za ulimwengu huu, lengo la dhahiri la serikali zote zilizowahi kuundwa miongoni mwa wanadamu limekuwa ni kukuza haki na ustawi wa watu wote.

Kwa kiwango gani lengo hilo limefikiwa ni swali lingine; lakini hayo yamekuwa madai ya serikali zote, na ndilo limekuwa lengo la watu wanaotawaliwa katika kujinyenyekeza na kuziunga mkono. Na pale ambapo malengo ya haki yamepuuzwa sana, aidha umati umepofushwa na kudanganywa, au vita, vurugu na mapinduzi vimekuwa ndio matokeo.

Matendo ya giza ya watawala waovu, waliopata nafasi za mamlaka katika serikali za ulimwengu, hayakuwakilisha sheria na taasisi za serikali hizo, bali katika kunyang'anya mamlaka na kuyatumia kwa malengo maovu waliupa serikali hizo tabia yao ya kinyama.

Kila serikali imekuwa na sheria nyingi za hekima, za haki na nzuri—sheria za kulinda maisha na mali, za kulinda maslahi ya nyumbani na kibiashara, za kuadhibu uhalifu, n.k. Pia zimekuwa na mahakama za rufaa katika masuala ya migogoro, ambapo haki hutolewa kwa kiasi fulani, angalau; na ingawa walio madarakani wanaweza kuwa wasio wakamilifu, manufaa na umuhimu wa taasisi kama hizo ni dhahiri. Jinsi zilivyokuwa duni serikali hizi, bila zenyewe kundi la watu waovu zaidi katika

jamii, kwa nguvu ya idadi yao, lingelishinda kundi la watu waadilifu na bora zaidi.

Kwa hiyo, ingawa tunatambua tabia ya kinyama ya serikali hizi, kama ilivyofanywa hivyo na kuinuliwa madarakani kwa watawala wengi wasio waadilifu, kupitia hila na udanganyifu wa Shetani, akitumia udhaifu na mawazo yaliyopotoka ya mwanadamu, bado tunazitambua kama juhudi bora zaidi za wanadamu maskini, walioanguka, katika kujitawala. Karne baada ya karne Mungu amewaruhusu wafanye juhudi, na waone matokeo.

Lakini baada ya karne nyingi za majaribio, matokeo hayaridhishi leo kama ilivyokuwa katika kipindi kingine chochote cha historia ya ulimwengu. Kwa kweli, kutoridhika kumeenea zaidi na ni kwa jumla kuliko wakati mwingine wowote; si kwa sababu kuna ukandamizaji na dhuluma zaidi kuliko hapo awali, bali kwa sababu, chini ya mpango wa Mungu, macho ya watu yanafunguliwa na ongezeko la maarifa.

Serikali mbalimbali ambazo zimeanzishwa mara kwa mara zimeonyesha **uwezo wa wastani** wa watu wanaowakilishwa nazo wa kujitawala. Hata pale ambapo serikali za kimabavu zimekuwepo, ukweli ni kwamba zimevumiliwa na umati umethibitisha kwamba kama watu hawakuwa na uwezo wa kuanzisha na kuunga mkono serikali bora zaidi, ingawa watu wengi bila shaka daima walikuwa mbele sana kuliko hadhi ya wastani.

Tunapolinganisha hali ya ulimwengu leo na hali yake katika kipindi kingine chochote cha zamani, tunapata tofauti kubwa katika hisia za umati. Roho ya uhuru sasa imeenea, na watu hawafungwi macho, kudanganywa na kuongozwa na watawala na wanasiasa kwa urahisi, na kwa hiyo hawatajinyenyekeza chini ya nira za siku za zamani.

Mabadiliko haya ya maoni ya umma hayajawa ya taratibu tangu mwanzo kabisa wa juhudi za mwanadamu za kujitawala, bali yanaonekana wazi tu kuanzia karne ya kumi na sita; na maendeleo yake yamekuwa ya haraka zaidi katika miaka hamsini iliyopita.

Mabadiliko haya, kwa hiyo, si matokeo ya uzoefu wa zama zilizopita, bali ni matokeo ya asili ya ongezeko la hivi karibuni na usambazaji mkuu wa maarifa miongoni mwa umati wa wanadamu. Maandalizi ya usambazaji huu mkuu wa maarifa yalianza na uvumbuzi wa uchapishaji, karibu mwaka 1440 BK, na matokeo yake kuongezeka kwa vitabu na magazeti.

Ushawishi wa uvumbuzi huu katika kuelimisha umma kwa jumla ulianza kuonekana karibu karne ya kumi na sita; na hatua za maendeleo tangu wakati huo zinajulikana na wote. Elimu ya jumla kwa umati imekuwa maarufu, na uvumbuzi na ugunduzi vinakuwa matukio ya kila siku. Ongezeko hili la maarifa miongoni mwa wanadamu, ambalo ni la agizo la Mungu, na linatokea kwa wakati wake ufaao, ni mojawapo ya mvuto mkuu unaofanya kazi sasa wa kumfunga Shetani—kupunguza ushawishi wake na kuwekea mipaka nguvu zake katika "Siku hii ya **Maandalizi**" kwa ajili ya kusimamishwa kwa ufalme wa Mungu duniani.

Ongezeko la maarifa katika kila upande linaamsha hisia ya kujiheshimu miongoni mwa watu, na utambuzi wa haki zao za asili na zisizoweza kuondolewa, ambazo hawataruhusu kwa muda mrefu zipuuzwe au kudharauliwa; badala yake, watakwenda kwenye upande mwingine uliokithiri. Angalia nyuma katika karne zilizopita na uone jinsi mataifa yalivyoandika historia ya kutoridhika kwao kwa damu.

Na manabii wanatangaza kwamba kwa sababu ya ongezeko la maarifa, kutoridhika kwingine kwa jumla na kumeenea zaidi hatimaye kutajionyesha katika mapinduzi ya dunia nzima, katika kupinduliwa kwa sheria na utaratibu wote; kwamba machafuko na dhiki kwa matabaka yote vitakuwa ndio matokeo; lakini kwamba katikati ya machafuko haya Mungu wa mbinguni ATAUSIMAMISHA Ufalme wake, ambao utatosheleza tamaa za mataifa yote. Wakiwa wamechoka na kuvunjika moyo na kushindwa kwao wenyewe, na wakiona juhudi zao za mwisho na kubwa zaidi zikileta machafuko, watu watakaribisha kwa

furaha na kuinama mbele ya mamlaka ya Mbinguni, na kuitambua serikali yake yenye nguvu na ya haki. Hivyo, mwisho wa uwezo wa mwanadamu utakuwa fursa ya Mungu, na *" vitu vinavyotamaniwa na mataifa yote vitakuja;"*—Ufalme wa Mungu, katika nguvu na utukufu mkuu. —**Hagai 2:7**

Wakijua hili kuwa ndilo kusudi la Mungu, Yesu wala mitume hawakuingilia watawala wa kidunia kwa namna yoyote. Kinyume chake, walifundisha Kanisa kujinyenyekeza chini ya mamlaka hizi, ingawa mara nyingi waliteseka chini ya matumizi yao mabaya ya madaraka. Walifundisha Kanisa kutii sheria, na kuwaheshimu wenye mamlaka kwa sababu ya ofisi zao, hata kama wao binafsi hawakustahili heshima; kulipa kodi zao zilizowekwa, na, isipokuwa pale zilipopingana na sheria za Mungu (**Matendo 4:19; 5:29**), wasitoe upinzani wowote kwa sheria yoyote iliyowekwa. (**Warumi 13:1-7; Mathayo 22:21**) Bwana Yesu na mitume na Kanisa la awali wote walitii sheria, ingawa walikuwa wametengana na, na hawakushiriki katika, serikali za ulimwengu huu.

Ingawa mamlaka zilizopo, serikali za ulimwengu huu, ziliwekwa au kupangwa na Mungu, ili wanadamu wapate uzoefu unaohitajika chini yao, bado Kanisa, waliojiweka wakfu wanaotamani vyeo katika Ufalme ujao wa Mungu, hawapaswi kutamani heshima na mapato ya ofisi katika falme za ulimwengu huu, wala hawapaswi kupinga mamlaka hizi. Wao ni raia wenza na warithi wa ufalme wa mbinguni (**Waefeso 2:19**), na kwa hivyo wanapaswa kudai tu haki na fursa kama zile wanazopewa **wageni** chini ya falme za ulimwengu huu.

Ujumbe wao si kuusaidia ulimwengu kuboresha hali yake ya sasa, wala kujihusisha na mambo yake kwa sasa. Kujaribu kufanya hivyo itakuwa ni kupoteza juhudi tu; kwa maana mwendo wa ulimwengu na mwisho wake vyote vimeelezwa wazi katika Maandiko na viko chini ya udhibiti kamili wa yeye ambaye kwa wakati wake mwenyewe **atatupa** sisi ufalme.

Ushawishi wa Kanisa la **kweli** sasa na daima umekuwa mdogo—mdogo kiasi cha kutohesabika kisiasa; lakini hata ungeonekana kuwa mkuu kiasi gani, tunapaswa kufuata mfano na fundisho la Bwana wetu na mitume. Wakijua kwamba kusudi la Mungu ni kuuacha ulimwengu ujaribu kikamilifu uwezo wake wa kujitawala, Kanisa la kweli halipaswi, likiwa ndani yake, kuwa **la** ulimwengu. Watakatifu wanaweza kuushawishi ulimwengu tu kwa kujitenga nao, kwa kuacha **nuru yao** iangaze; na hivyo kupitia maisha yao roho ya kweli INAUKEMEA ulimwengu. Hivyo—kama watiifu wa amani, wenye utaratibu na wasifiaji wa kila sheria ya haki, wakemeaji wa uasi na dhambi, na waelekezaji mbele kwenye Ufalme ulioahidiwa wa Mungu na baraka zitakazotarajiwa chini yake, na si kwa njia inayotumiwa na wengi ya kujichanganya katika siasa na kufanya njama na ulimwengu kwa ajili ya mamlaka, na hivyo kuvutwa katika vita na dhambi na uharibifu wa jumla—katika usafi mtukufu ndivyo Bibi-arusi mtarajiwa wa Mfalme wa Amani anapaswa kuwa nguvu ya wema, kama mwakilishi wa Bwana wake ulimwenguni.

Kanisa la Mungu linapaswa kutoa **uangalifu** na juhudi zake **zote** katika kuhubiri Ufalme wa Mungu, na katika kuendeleza maslahi ya Ufalme huo kulingana na mpango uliowekwa katika Maandiko. Kama hili likifanywa kwa uaminifu, hakutakuwa na wakati wala mwelekeo wa kujihusisha katika siasa za serikali za sasa. Bwana hakuwa na wakati wa kufanya hivyo; mitume hawakuwa na wakati wa kufanya hivyo; wala watakatifu wowote wanaofuata mfano wao.

Kanisa la awali, muda mfupi baada ya kifo cha mitume, liliangukia mtego wa jaribu hili hili. Kuhubiri juu ya Ufalme wa Mungu unaokuja, ambao ungeondoa falme zote za kidunia, na juu ya Kristo aliyesulibiwa kama mrithi wa Ufalme huo, haukupendwa, na uliandamana na mateso, dhihaka na kudharauliwa. Lakini baadhi walifikiri kuboresha mpango wa Mungu, na, badala ya kuteseka, kuliweka Kanisa katika nafasi ya

kupata kibali kwa ulimwengu. Kwa kuungana na mamlaka za kidunia walifanikiwa. Matokeo yake, Upapa uliibuka, na baada ya muda ukawa bibi na malkia wa mataifa. —**Ufunuo 17:3-5; 18:7**

Kwa sera hii kila kitu kilibadilika: badala ya mateso, ikaja heshima; badala ya unyenyekevu, kikaja kiburi; badala ya ukweli, ukaja uongo; na badala ya kuteswa, yeye akawa mtesi wa wote waliolaani heshima zake mpya na haramu. Punde alianza kubuni nadharia mpya na hoja za udanganyifu ili kuhalalisha mwenendo wake, kwanza akijidanganya mwenyewe, na kisha mataifa, katika imani kwamba utawala wa milenia ulioahidiwa wa Kristo ULIKUWA UMEKUJA, na kwamba Kristo Mfalme aliwakilishwa na mapapa wake, waliotawala juu ya wafalme wa dunia kama makaimu wake.

Madai yake yalifanikiwa kuudanganya ulimwengu wote. *"Akawanywesha mataifa yote"* kwa mafundisho yake potofu (**Ufunuo 17:2**), akiwatia hofu kwa kufundisha kwamba mateso ya milele yaliwangoja wote waliopinga madai yake. Punde wafalme wa Ulaya walivikwa taji au kuondolewa madarakani kwa amri yake, na chini ya mamlaka yake yaliyodhaniwa.

Hivyo ndivyo ilivyo kwamba falme za Ulaya leo zinadai kuwa falme za Kikristo, na zinatangaza kwamba watawala wanatawala "kwa neema ya Mungu," yaani, kupitia uteuzi wa ama Upapa au baadhi ya madhehebu ya Kiprotestanti. Kwa maana ingawa Wanamatengenezo waliyatupilia mbali madai mengi ya Upapa kuhusu mamlaka ya kikanisa, na kadhalika, bado waliishikilia heshima hii ambayo wafalme wa dunia walikuwa wameiambatanisha na Ukristo.

Na hivyo Wanamatengenezo waliangukia katika kosa lilelile, na kutumia mamlaka ya wafalme katika kuteua na kuidhinisha serikali na wafalme, na kuzitaja kama "falme za Kikristo," au falme za Kristo. Hivyo tunasikia mengi leo kuhusu fumbo lile la ajabu, "Ulimwengu wa Kikristo"—fumbo kweli, linapotazamwa kwa kuzingatia kanuni za kweli za Injili. Bwana wetu alisema juu

ya wanafunzi wake, *"Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu."* Na Paulo anatuonya, akisema, *"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii."* —**Yohana 17:16; Warumi 12:2**

Mungu hakuwahi kuridhia kuziita falme hizi kwa jina la Kristo. Zikiwa zimedanganywa na Kanisa la jina, mataifa haya yanapeperusha bendera ya uongo, yakidai kuwa kile ambacho hasa sio. Haki yao pekee ya umiliki, mbali na kura za wananchi, iko katika kile kibali cha Mungu chenye ukomo, kilichotajwa kwa Nebukadneza—hadi atakapokuja yeye aliye na haki ya utawala.

Madai kwamba falme hizi zisizo kamilifu, zenye sheria zake zisizo kamilifu na mara nyingi watawala wabinafsi na waovu, ndizo "falme za Bwana wetu na Masihi wake" ni kashfa kubwa dhidi ya Ufalme wa kweli wa Kristo, ambao mbele yake lazima zianguke hivi karibuni, na dhidi ya "Mfalme wa Amani" wake na watawala waadilifu. —**Isaya 32:1**

Jeraha jingine zito linalotokana na kosa hilo ni kwamba kwa njia hiyo uangalifu wa watoto wa Mungu umevutwa mbali na ufalme wa Mbinguni ulioahidiwa; nao wameongozwa kwenye utambuzi usiofaa na urafiki wa karibu na falme za kidunia, na kwenye majaribio yasiyo na matunda ya kupandikiza neema na maadili ya Kikristo kwenye mashina haya ya mwitu, ya kidunia, na kuiacha injili inayohusu Ufalme wa kweli na matumaini yaliyojikita ndani yake.

Chini ya udanganyifu huu, wengine kwa sasa wana hangaiko kubwa kwamba jina la Mungu liingizwe katika Katiba ya Marekani, ili **kwa njia hiyo** hili liweze kuwa taifa la Kikristo. Wapresbiteri Waliofanyiwa Marekebisho kwa miaka mingi wamekataa kupiga kura au kushika wadhifa chini ya serikali hii, **kwa sababu** si Ufalme wa Kristo. Hivyo wanatambua kutofaa kwa Wakristo kushiriki katika serikali nyingine yoyote. Tuna huruma kubwa na hisia hii, lakini si na hitimisho, kwamba kama **jina** la Mungu lingetajwa katika Katiba, ukweli huo ungeigeuza serikali

hii kutoka ufalme wa ulimwengu huu na kuwa ufalme wa Kristo, na kuwapa uhuru wa kupiga kura na kushika wadhifa chini yake. Lo, jinsi ulivyo upumbavu! Jinsi ulivyo mkuu udanganyifu ambao kwake “Mama wa makahaba” ameyalewesha mataifa yote (**Ufunuo 17:2**); kwa maana kwa namna hiyohiyo inadaiwa kwamba falme za Ulaya zilihamishwa kutoka kwa Shetani kwenda kwa Kristo, na kuwa “mataifa ya Kikristo.

Na ionekane wazi kwamba mataifa bora na mabaya zaidi ya dunia ni “falme za ulimwengu huu,” ambao kibali chao cha kutawala kutoka kwa Mungu sasa **kinakaribia** kwisha, ili zipate kumpisha mrithi wake aliyewekwa rasmi, Ufalme wa Masihi, Ufalme wa Tano wa Ulimwengu Wote wa dunia (**Danieli 2:44; 7:14, 17, 27**)—mtazamo huu utasaidia sana kuimarisha ukweli na kupindua uongo.

Lakini kama ilivyo, matendo ya Upapa katika suala hili, yaliyoidhinishwa na Wanamatengenezo wa Kiprotestanti, hayahojiwi miongoni mwa watu wa Kikristo. Na kwa kuwa wanapaswa kuunga mkono Ufalme wa Kristo, wanajiona wamelazimika kuzitetea falme za sasa zinazoanguka za ile inayoitwa Jumuiya ya Wakristo, ambazo wakati wake unakwisha kwa kasi; na hivyo huruma zao mara nyingi zinalazimishwa kuwa upande wa ukandamizaji, badala ya upande wa haki na uhuru—upande wa falme za ulimwengu huu, na mkuu wa ulimwengu huu, badala ya upande wa Ufalme wa kweli ujao wa Kristo. —**Ufunuo 17:14; 19:11-19**

Ulimwengu unakaribia kwa kasi kutambua kwamba “falme za ulimwengu huu” si kama za Kristo, na kwamba dai lao la kuwa zimeteuliwa na Kristo linaweza kuhojiwa. Watu wanaanza kutumia nguvu zao za kufikiri juu ya hili na maswali yanayofanana; nao watatenda kulingana na misimamo yao kwa nguvu zaidi, watakapotambua kwamba udanganyifu umefanywa juu yao kwa jina la Mungu wa Haki na Mfalme wa Amani. Kwa kweli, mwelekeo wa wengi ni kuhitimisha kwamba Ukristo wenyewe ni ulaghai usio na msingi, na kwamba, ukiwa

umeungana na watawala wa kiraia, lengo lake ni kuzuia tu uhuru wa umati.

Laiti watu wangekuwa na hekima, wangeelekeza mioyo yao kuelewa kazi na mpango wa Bwana! Ndipo falme za sasa zingeyeyuka taratibu—mageuzi yangefuata mageuzi kwa kasi, na uhuru ungefuata uhuru, na haki na kweli vingeshinda hadi haki itakapoimarishwa duniani. Lakini hawatafanya hivi, wala hawawezi katika hali yao ya sasa ya anguko; na hivyo, wakiwa wamejihami kwa ubinafsi, kila mmoja atashindania mamlaka, na falme za ulimwengu huu zitapita kwa wakati mkuu wa taabu, ambao haujawahi kutokea tangu lilipoanza kuwako taifa. Kuhusu wale watakaojaribu bure kung'ang'ania mamlaka ambayo muda wake umekwisha, wakati mamlaka hayo yatakapokabidhiwa kwa yule ambaye ni haki yake, Bwana anasema, akisisitiza kwamba wanapigana naye—pambano ambalo bila shaka watashindwa. Anasema:

> *"Mbona mataifa wanafanya ghasia, Na makabila wanatafakari ubatili? Wafalme wa dunia wanajipanga, Na watawala wanafanya shauri pamoja, Juu ya BWANA, na juu ya Masihi wake, wakisema, Na tuvipasue vifungo vyao, Na kuzitupia mbali nasi kamba zao. Yeye aketiye mbinguni anacheka; Bwana anawafanyia dhihaka. Ndipo atakaposema nao kwa hasira yake, Na kuwafadhaisha kwa ghadhabu yake, [akisema], **Nami nimemweka mfalme wangu** Juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu... Na sasa, enyi wafalme, fanyeni akili, Enyi waamuzi wa dunia, mwadibiwe. Mtumikieni Bwana kwa kicho, Shangilieni kwa kutetemeka. Shikeni yaliyo bora. Mbusuni [fanyeni urafiki na] Mwana, asije akaghadhibika, Nanyi mkapotea njiani; Kwa maana hasira yake itawaka upesi. Heri wote wanaomkimbilia." —* ***Zaburi 2:1-6, 10-12***

***Ufalme U Karibu***

*"Mlinzi, tupe habari za usiku — Ishara zake za ahadi ni zipi? Msafiri, juu ya kilele cha mlima ule, Tazama ile nyota ing'aayo utukufu! Mlinzi, je, mwali wake maridadi Unatabiri tumaini au furaha yoyote? Msafiri, ndiyo, inaleta mchana — Siku ya ahadi ya Israeli.*

*"Mlinzi, tupe habari za usiku — Nyota ile inazidi kupanda juu. Msafiri, baraka na nuru, Amani na kweli mwendo wake unaashiria. Mlinzi, je, mionzi yake pekee Itang'arisha tu pale ilipozaliwa? Msafiri, zama zote ni zake; Tazama, utukufu wake waijaza dunia.*

*"Mlinzi, tuambie, je, asubuhi Ya utukufu wa Sayuni inapambazuka? Je, ishara zinazoashiria kuja kwake Zimeshamulika kwenye njia yako? Msafiri, ndiyo: inuka! tazama kote! Nuru inachomoza angani! Jifunge mavazi yako ya harusi! Kunakucha! inuka! inuka!"*

## SOMO LA XIV

# UFALME WA MUNGU

UMUHIMU WA SOMO HILI—TABIA YA UFALME—UFALME WAKATI WA ZAMA YA INJILI—MITAZAMO YA UONGO IKISAHIHISHWA NA PAULO—MATOKEO YA MAWAZO YA UONGO JUU YA UFALME—SURA MBILI ZA UFALME WA MUNGU—SURA YA KIROHO NA KAZI YAKE—SURA YA KIDUNIA NA KAZI YAKE—UTENDAJI WAO WA PAMOJA KWA UWIANO—UTUKUFU WA SURA YA KIDUNIA—UTUKUFU WA SURA YA MBINGUNI—MZIZI WA AGANO AMBAKO MATAWI HAYA HUOTEA—SURA YA KIDUNIA YA UFALME, YA KIISRAELI—MAKABILA YALIYOPOTEA—YERUSALEMU WA MBINGUNI—ISRAELI WATU WA MFANO—KUPOTEZWA NA KUREJESHWA KWA ISRAELI—MADARAJA YA WATEULE—WARITHI WA UFALME—UTAWALA WA CHUMA—KIELELEZO CHA LENGO LA UTAWALA WA MIAKA ELFU—UFALME UKIKABIDHIWA KWA BABA—KUSUDI LA ASILI LA MUNGU LIKIKAMILISHWA KIKAMILIFU.

YEYOTE ambaye hajalichunguza somo hili kwa makini, akiwa na konkodansi na Biblia mkononi, atashangaa, atakapofanya hivyo, kuona jinsi lilivyopewa nafasi kubwa katika Maandiko. Agano la Kale limejaa tele ahadi na unabii ambamo Ufalme wa Mungu na Mfalme wake, Masihi, ndio kiini hasa. Lilikuwa ni tumaini la kila Mwisraeli (**Luka 3:15**) kwamba, kama watu wake, Mungu angelitukuza taifa lao chini ya Masihi; na Bwana alipokuja kwao, alikuja kama Mfalme wao, ili kuusimamisha ule Ufalme wa Mungu ulioahidiwa tangu zamani juu ya dunia.

Yohana, mtangulizi na mpiga mbiu wa Bwana wetu Yesu, alianza kazi yake kwa tangazo, '*Tubuni; kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia.*' **(Mathayo. 3:2).** Bwana alianza huduma yake kwa tangazo hilo hilo sawasawa (**Mathayo. 4:17**); na mitume walitumwa kuhubiri ujumbe huo huo. (**Mathayo. 10:7; Luka 9:2).** Sio tu kwamba ufalme ulikuwa ndiyo mada ambayo Bwana alianza nayo huduma yake ya hadhara, bali kwa kweli ndiyo ilikuwa mada kuu ya mahubiri yake yote (**Luka 8:1; 4:43; 19:11),** masomo mengine yakitajwa tu kuhusiana na au kwa ajili ya kufafanua somo hili moja. Sehemu kubwa ya mifano yake ilikuwa vielelezo vya ufalme kutoka mitazamo mbalimbali, na katika sura tofauti, au ilitumika kuonyesha kwamba kujitoa wakfu kikamilifu kwa Mungu ni muhimu ili kupata sehemu

katika ufalme huo, na kurekebisha dhana potofu ya Wayahudi kwamba walikuwa na uhakika wa ufalme kwa sababu walikuwa watoto wa asili wa Ibrahimu, na hivyo warithi wa asili wa ahadi.

Bwana wetu Yesu, katika mazungumzo yake na wafuasi wake, aliimarisha na kutia moyo matarajio yao ya ufalme ujao, aki-waambia: '*Nami nawawekea ninyi ufalme, kama vile Baba yangu alivyoniwekea mimi; mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu; na kuketi katika viti vya enzi, huku mkiyahukumu [mkiyatawala] kabila kumi na mbili za Israeli.*' (**Luka 22:29,30).** Na tena, '*Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule ufalme.*' (**Luka 12:32).**

Na wakati ambapo, badala ya kuvikwa taji na kutawazwa kwenye kiti cha enzi, mfalme wao waliyemtambua alisulubiwa, wanafunzi wake walivunjika moyo sana. Kama vile wawili wao walivyomweleza yule waliyemdhania kuwa mgeni njiani kuele-kea Emau baada ya kufufuka kwake, walikuwa '*wakitarajia ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli*' —akiwatoa katika nira ya Rumi, na kuifanya Israeli kuwa Ufalme wa Mungu katika nguvu na utukufu. Lakini walikatishwa tamaa vibaya na mabadiliko ya mambo ya siku chache zilizopita. Ndipo Yesu akazifungua akili zao kwa kuwaonyesha kutoka katika Maandiko kwamba dhabihu yake ilipaswa kutolewa kwanza kabla ya ufalme huo kusimamishwa. **Luka 24:21, 25-27**.

Mungu angeweza kumpa Yesu mamlaka ya dunia bila kumkom-boa mwanadamu; kwa maana '*Aliye Juu anamiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye.*' (**Danieli 4:32**). Lakini Mungu alikuwa na kusudi kuu zaidi kuliko lile ambalo lingeweza kutimizwa kwa mpango wa namna hiyo. Ufalme kama huo un-geweza kuleta baraka ambazo, hata kama ni nzuri, zingekuwa za muda tu, kwa sababu wanadamu wote walikuwa chini ya hukumu ya kifo. Ili kufanya baraka za ufalme wake ziwe za milele na kamilifu, ilibidi jamii ya wanadamu ikombolewe kwanza kutoka katika mauti na hivyo kuachiliwa kisheria kutoka katika ile hukumu iliyowafikia wote katika Adamu.

Kwamba katika kufafanua unabii Yesu alifufua tumaini la wanafunzi la ufalme ujao ni dhahiri kutokana na ukweli kwamba baadaye, alipokuwa akiwaacha, waliuliza, *"Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?"* Jibu lake, ingawa halikuwa la moja kwa moja, halikupinga matumaini yao. Alisema, *"Si kazi **yenu** kujua **nyakati wala majira**, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe"'* **Matendo ya Mitume** 1:6,7.

Ni kweli, wanafunzi hapo awali, sawa na taifa zima la Wayahudi, walikuwa na uelewa usio mkamilifu juu ya Ufalme wa Mungu kwa kudhani kuwa ungekuwa ufalme wa kidunia pekee, kama vile wengi leo wanavyokosea katika uelekeo ulio kinyume kwa kudhani kuwa ni ufalme wa mbinguni pekee. Na mengi ya mafumbo na maneno mazito ya Bwana wetu Yesu yalikusudiwa kwa wakati wake kurekebisha dhana hizi potofu. Lakini siku zote alishikilia lile wazo la ufalme, serikali, itakayosimamishwa **katika dunia** na kutawala kati ya wanadamu. Na si tu kwamba alijenga ndani yao tumaini la kupata sehemu katika ufalme huo, bali aliwafundisha pia kuomba kwa ajili ya kusimamishwa kwake— *"Ufalme wako **uje**; mapenzi yako yatimizwe DUNIANI kama huko mbinguni."*

Kwa wale wenye hekima ya kidunia miongoni mwa Wayahudi, Bwana wetu alionekana kama mzushi na mshupavu; na waliwachukulia wanafunzi wake kama watu waliohadaika tu. Hekima na busara yake, pamoja na miujiza yake, hawakuweza kuipinga wala kuielezea kwa mantiki; lakini, kutokana na mtazamo wao wa kutokuamini, dai lake kwamba yeye ndiye mrithi wa ulimwengu, na kwamba angeusimamisha ufalme ulioahidiwa ambao ungetawala dunia, na kwamba wafuasi wake, ambao wote walitoka katika tabaka la chini la maisha, wangekuwa watawala pamoja naye katika ufalme huo, yalionekana kuwa ya kipuuzi mno hata kufikiriwa.

Rumi, ikiwa na wapiganaji wake wenye nidhamu, majemadari wake hodari na utajiri mwingi, ndiyo ilikuwa bwana wa dunia, na ilikuwa inazidi kupata nguvu siku baada ya siku. Basi, huyu

Mnazareti alikuwa nani? na hawa wavuvi walikuwa nani, wasio na fedha wala ushawishi, na wakiwa na kundi dogo tu la wafuasi miongoni mwa watu wa kawaida? Hawa walikuwa nani hata wazungumzie kuusimamisha ufalme ulioahidiwa tangu zamani kuwa ndio ufalme mtukufu na wenye nguvu zaidi ambao dunia imewahi kuujua?

Mafarisayo, wakitumaini kuweka wazi ule udhaifu waliodhani upo katika madai ya Bwana wetu, na kwa njia hiyo **kuwazindua** wafuasi wake, walimhoji—Ni lini ufalme huu unaouhubiri utaanza kuonekana?—askari wako watafika lini?—Ufalme huu wa Mungu utatokea lini? (**Luka 17:20-30**). Jibu la Bwana wetu lingewapa wazo jipya kama wasingekuwa na chuki dhidi yake na kupofushwa na hiyo hekima yao ya kudhani. Alijibu kwamba ufalme wake haungeonekana kamwe kwa namna ile waliyoitarajia. Ufalme aliouhubiri, na ambao aliwaalika wafuasi wake kuwa warithi pamoja naye, ulikuwa ni ufalme usioonekana, na hawakupaswa kutarajia kuuona. "*Akawajibu, akasema, Ufalme wa Mungu hauji kwa kuonekana [kudhihirika kwa nje]; wala hawatasema, Tazama huku! au, kule! kwa kuwa tazama, ufalme wa Mungu umo [utakuwa] ndani yenu [katikati mwenu].*"* Kwa kifupi, alionyesha kwamba ufalme wake utakapokuja, ungekuwapo kila mahali na wenye nguvu kila mahali, ilhali hauonekani mahali popote.

Hivyo aliwapa wazo la ufalme wa kiroho aliouhubiri; lakini hawakuwa wamejiandaa nao wala hawakuupokea. Kulikuwa na kiasi fulani cha ukweli katika matarajio ya Wayahudi kuhusu ufalme ulioahidiwa, ambayo yatatimilika kwa wakati wake, kama itakavyoonyeshwa; lakini rejea ya Bwana wetu hapa inahusu ile sura ya kiroho ya ufalme, ambayo haitaonekana. Na kwa kuwa sura hii ya ufalme ndiyo itakayoanza kusimamishwa

---

* *Tafsiri ya Diaglott na ile ya Rotherham zinatafsiri neno hili kama "miongoni mwenu," ambayo ni sawa na kusema "katikati yenu." Hakika, haileti maana yoyote kusisitiza kwamba ufalme ule ambao Yesu alidai anataka kuusimamisha ungekuwa ndani ya mioyo ya Mafarisayo, watu ambao aliwaita wanafiki na makaburi yaliyopakwa chokaa. Bali ufalme huu, utakaposimamishwa, utakuwa "katikati ya" au "miongoni mwa" madaraja yote, ukitawala na kuhukumu wote*

kwanza, kuwapo kwake hakutaonekana, na kwa muda hautafahamika.

Haki ya urithi katika sura hii ya kiroho ya Ufalme wa Mungu ndiyo iliyokuwa ofa pekee iliyotolewa wakati huo, na imekuwa ndilo tumaini la wito wetu katika kipindi chote cha Zama ya Injili, iliyoanza wakati huo. Hivyo Yesu alikuwa akiirejelea hiyo pekee. (**Luka 16:16).** Hili litaonekana wazi zaidi tunapoendelea.

Pengine ni kwa sababu ya mtazamo huu hasi wa watu, hasa miongoni mwa Mafarisayo, ndiyo maana Nikodemo alimwendea Yesu usiku, akiwa na shauku ya kufumbua fumbo hilo, lakini akionekana kuona aibu kukiri hadharani kwamba madai hayo yalikuwa na uzito wowote akilini mwake. Mazungumzo kati ya Bwana na Nikodemo (**Yohana** 3), ingawa yameandikwa kwa sehemu tu, yanatoa mwangaza zaidi kuhusu tabia ya Ufalme wa Mungu. Ni dhahiri kwamba hoja kuu za mazungumzo hayo zimetajwa ili kutokana na hizo tuweze kupata picha kamili ya yote yaliyozungumzwa, ambayo tunaweza kuyafafanua kwa maneno yetu wenyewe kama ifuatavyo:

Nikodemo—"*Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*" Hata hivyo, baadhi ya kauli zako zinaonekana kupingana sana kwangu, nami nimekuja kuomba ufafanuzi. Kwa mfano, wewe na wanafunzi wako mnazunguka mkitangaza, "*Ufalme wa mbinguni umekaribia*"; lakini huna jeshi, wala utajiri, wala ushawishi, na kwa jinsi inavyoonekana dai hili si la kweli; na katika hili unaonekana kuwadanganya watu.

Mafarisayo kwa ujumla wanakuona kama mzushi, lakini mimi nina hakika lazima kuna ukweli fulani katika mafundisho yako, "*...kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*" Lengo la ziara yangu ni kutaka kujua ufalme huu unaoutangaza ni wa namna gani,

utakuja lini na unatoka wapi? na utasimamishwa lini na kwa jinsi gani?

**Yesu**—Ombi lako la kutaka kuwa na ufahamu kamili kuhusu ufalme wa mbinguni haliwezi kujibiwa sasa ukaridhika; si kwamba mimi siujui kikamilifu, bali ni kwamba katika hali yako ya sasa hungeuridhia wala kuuelewa, endapo ningekufafanulia kikamilifu. "*...Mtu asipo**zaliwa*** *kutoka juu, hawezi kuuona [Kiyunani, eidon*†, *kuujua, au kufahamiana nao] ufalme wa Mungu...*"

Hata wanafunzi wangu bado wana mawazo yasiyo wazi sana juu ya tabia ya ufalme wanaoutangaza. Siwezi kuwaambia, kwa sababu ile ile inayonizuia nisiweze kukuambia wewe; na wao hawakuweza kuelewa, kwa sababu hiyo hiyo. Lakini, Nikodemo, utaratibu mmoja wa pekee katika matendo ya Mungu ni kwamba anahitaji utii kwa nuru ambayo mtu anayo tayari kabla ya kumpa nuru zaidi; na katika uteuzi wa wale watakaohesabiwa kuwa wanastahili kuushiriki ufalme, dhihirisho la imani linahitajika. Lazima wawe watu walio tayari kufuata uongozi wa Mungu, hatua kwa hatua, mara nyingi wakiona wazi hatua moja tu iliyo mbele yao. Wanaenenda kwa imani na si kwa kuona.

---

* *Neno la Kiyunani gennao na maneno yanayotokana nalo, ambalo wakati mwingine hutafsiriwa **kutungwa** na wakati mwingine **kuzaliwa**, kwa kweli linabeba mawazo yote mawili, na linapaswa kutafsiriwa kwa mojawapo ya maneno haya mawili, kulingana na maana ya fungu ambamo linatokea. Mawazo haya mawili, kutungwa mimba na kuzaliwa, siku zote yamo ndani ya neno hilo, kiasi kwamba moja likitajwa, lingine linadokezwa siku zote, kwani kuzaliwa ni matokeo ya asili ya kutungwa, na kutungwa ni hatua ya awali ya asili kabla ya kuzaliwa.*
*Wakati mtendaji anayehusishwa na neno gennao ni mwanaume, linapaswa kutafsiriwa **kutungwa**; na likihusishwa na mwanamke, linapaswa kutafsiriwa **kuzaliwa**. Hivyo, katika **1 Yohana** 2:29; 3:9; 4:7; 5:1,18, gennao linapaswa kuwa **kutungwa**, kwa sababu Mungu (kiume) ndiye mtendaji.*
*Hata hivyo, wakati mwingine tafsiri hutegemea asili ya tendo hilo, kama ni la kiume au la kike. Hivyo, likitumika pamoja na neno ek, likimaanisha kutoka au nje ya, linapaswa kutafsiriwa **kuzaliwa**. Hivyo katika **Yohana** 3:5,6, gennao linapaswa kutafsiriwa **kuzaliwa**, kama inavyoonyeshwa na neno ek – "kwa [kutoka] maji," "kwa [kutoka] mwili," "kwa [kutoka] roho."*

† *Neno hili hili la Kiyunani limetafsiriwa fikiri katika **Matendo ya Mitume** 15:6. "...Mitume na wazee wakakusanyika wapate kulifikiri [kujua au kuelewa] neno hilo..." Neno hilo hilo limetafsiriwa tazama katika **Warumi** 11:22. "...Tazama [fikiri, elewa], basi, wema na ukali wa Mungu..."; pia katika **1 Yohana** 3:1 – "...Tazameni [fikirini, jueni, eleweni], ni pendo la namna gani alilotupa Baba..."*

**Nikodemo**—Lakini sikuelewi. Unamaanisha nini? "*...Awezaje mtu kutungwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili, akazaliwa?...*" Au unamaanisha kwamba ile toba iliyohubiriwa na "Yohana Mbatizaji," na kuashiriwa na ubatizo wa maji, ni aina fulani ya kuzaliwa kwa mfano? Nimeona kuwa wanafunzi wako wanahubiri na kubatiza vivyo hivyo. Je, huku ndiko kuzaliwa upya kunakohitajika kwa wale wanaotaka kuuona au kuuingia ufalme wako?

**Yesu**—Taifa letu ni taifa lililowekwa wakfu, watu wa agano. Wote walibatizwa wawe wa Musa katika bahari na katika wingu walipoondoka Misri. Mungu aliwakubali ndani ya Musa, mpatanishi wa agano lao, pale Sinai; lakini wamelisahau agano lao, baadhi wanaishi waziwazi kama watoza ushuru na wenye dhambi, na wengine wengi ni wanafiki wanaojiona kuwa wenye haki; hivyo mahubiri ya Yohana na yale ya wanafunzi wangu ni toba—kumrudia Mungu na kulitambua agano lililofanywa; na ubatizo wa Yohana huashiria toba hii na mabadiliko ya moyo na maisha, na **sio** kuzaliwa upya.

Lakini usipokuwa na zaidi ya hili hutauona Ufalme kamwe. Isipokuwa ukipokea **kutungwa** na kuzaliwa kwa roho kama nyongeza ya yale mabadiliko yaliyoashiriwa na ubatizo wa Yohana, huwezi kuuona Ufalme wangu. Toba itakurudisha kwenye hali ya kuhesabiwa haki; katika hali hiyo utaweza kwa urahisi kunitambua mimi kama Masihi, mtimilifu wa mfano wa Musa; na hivyo kwa kujitoa wakfu kwangu **utatungwa** na Baba kwenye uzima mpya na asili ya uungu, ambayo, ikikua na kuhuishwa, itahakikisha **unazaliwa** kiumbe kipya, kiumbe wa kiroho, katika ufufuo wa kwanza; na ukiwa hivyo hutauona tu bali utaushiriki Ufalme.

Mabadiliko yatakayoletwa na kuzaliwa huku kupya kwa Roho ni makubwa kweli, Nikodemo; kwa maana "*...kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho...*" Basi, usistaajabie kauli yangu ya kwanza, kwamba lazima **utungwe** kutoka juu kabla ya kuweza kuelewa, kujua na kuthamini

mambo unayoyaulizia. "*...Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili...*" Tofauti kati ya hali yako ya sasa, ukiwa umezaliwa kwa mwili, na hali ya wale waliozaliwa kwa Roho, watakaoingia au kuunda ufalme ninaouhubiri, ni kubwa sana.

Acha nikupe kielelezo ambacho kwacho utapata wazo fulani juu ya viumbe ambao, wakizaliwa kwa Roho, watauunda ufalme huu: "*...Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na kila mtu aliyezaliwa kwa Roho...*" Kama vile upepo unavyovuma huku na kule, huwezi kuuona, ingawa unaleta ushawishi kukuzunguka kote. Hujui unakotoka wala unakoenda. Hiki ndicho kielelezo kizuri zaidi ninachoweza kukupa kuhusu wale waliozaliwa kwa Roho katika ufufuo, wale watakao "ingia" au kuunda huo Ufalme ninaouhubiri sasa. Wote watakuwa hawaonekani kama upepo, na wanadamu, wasiozaliwa kwa Roho, hawatajua walikotoka wala wanakokwenda.

**Nikodemo**—Haya yawezekanaje?—viumbe wasioonekana!

**Yesu**— "*...Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyajui?...*"— kwamba viumbe vya roho wanaweza kuwapo, na bado wasionekane? Je, wewe, unayejaribu kufundisha wengine, hujapata kusoma habari za Elisha na mtumishi wake, au habari za punda wa Balaamu? na matukio mengi katika Maandiko yanayodhihirisha kanuni hii, kwamba viumbe vya roho wanaweza kuwapo miongoni mwa wanadamu, ilhali hawaonekani?

Zaidi ya hayo, wewe ni wa dhehebu la Mafarisayo, ambao mnakiri kuamini malaika kama viumbe vya roho. Lakini hili linadhihirisha kile nilichokuambia mwanzoni: Mtu asipozaliwa kutoka juu, hawezi kuuona [kuujua, kufahamiana nao, au kuuelewa kuwa wenye mantiki] Ufalme wa Mungu na mambo mbalimbali yanayohusiana nao.

Kama ungetaka kuingia na kuwa mrithi pamoja nami wa ufalme huo ninaoutangaza, lazima uifuate nuru, hatua kwa hatua.

Unapofanya hivyo, nuru zaidi itakuja, na itakuja haraka kulingana na jinsi utakavyokuwa tayari kuipokea. Nimekuwa nikihubiri mambo haya yanayofaa sasa ambayo unaweza kuyaelewa, na kufanya miujiza, nawe unanikiri kuwa mwalimu niliyetoka kwa Mungu, lakini hujaitendea kazi imani yako na kuwa mwanafunzi na mfuasi wangu waziwazi. Usitarajie kuona zaidi, mpaka utakapoishi kulingana na yote unayoyaona; ndipo Mungu atakapokupa nuru zaidi na ushahidi kwa ajili ya hatua inayofuata. "*...Amin, amin, nakuambia, tunanena tuyajuayo, na kushuhudia tuliyoyaona, wala [ninyi Mafarisayo] hamkubali ushuhuda wetu. Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, nanyi hamwamini, mtaamini je! nikiwaambia mambo ya mbinguni?...*"

Ingekuwa kazi bure kwangu kujaribu kukueleza mambo ya mbinguni, kwa maana hungeshawishika na mahubiri yangu yangeonekana ya kipumbavu zaidi kwako. Ikiwa yale niliyofundisha, ambayo yamekuwa ya asili ya kidunia, au kufafanuliwa kwa mambo ya kidunia, ambayo unaweza kuyaelewa na unayaelewa, hayajaleta ushawishi wa kutosha akilini mwako kukuongoza waziwazi kuwa mwanafunzi na mfuasi wangu, isingekuwa na ushawishi zaidi kwako kama ningekuambia mambo ya mbinguni, ambayo huyajui kabisa; kwa maana hakuna mtu aliyepata kupaa mbinguni, hivyo hakuna ambaye angeweza kuuthibitisha ushuhuda wangu. Mimi, niliyeshuka kutoka mbinguni, pekee ndiye ninayeyaelewa mambo ya mbinguni. "*...Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adamu* * " Ujuzi wa mambo ya mbinguni unaweza kupokelewa tu baada ya kutungwa kwa Roho; na yale mambo ya mbinguni yenyewe, hupatikana wakati wa kuzaliwa kwa roho, na kuwa viumbe vya roho.

Hivyo ilihitaji uvumilivu kwa upande wa Bwana, katika kutangaza asili ya ufalme kwa wale ambao mitazamo yao hasi na elimu yao ilizuia wasione chochote isipokuwa mitazamo

---

* *Maneno "aliye mbinguni" (mstari wa 13) hayapatikani katika Miswada ya kale na ya kuaminika zaidi.*

iliyopotoka ya upande wa kidunia wa ufalme huo. Hata hivyo uteuzi wa daraja linalofaa kushiriki ufalme wa Masihi uliendelea, ingawa ni wachache tu walichaguliwa kutoka Israeli, ambao walitolewa ofa hiyo pekee kwa miaka saba. Kama Mungu alivyojua tangu awali, kutokana na kutokuwa tayari kwao, na kushindwa kwao kuelewa na kutimiza masharti yaliyowekwa, ile haki ya kushiriki katika ufalme wa Masihi iliondolewa kwao kama taifa, ambapo ni mabaki tu miongoni mwao waliipokea, na ikaja kwa Mataifa ili kuchukua pia kutoka kwao "*...watu kwa ajili ya jina lake...*" Na miongoni mwa hawa pia ni mabaki tu, "*...kundi dogo,*" wanaothamini haki hiyo na kuhesabiwa kuwa wanastahili urithi wa pamoja katika ufalme wake na utukufu.

Kosa kubwa limeingizwa katika Kanisa la Kikristo la jina tu, ambalo hutafsiri vibaya ufalme huu ulioahidiwa kuwa unamaanisha tu Kanisa la jina tu katika hali yake ya sasa, na kazi yake kuwa ni kazi ya neema tu ndani ya mioyo ya waamini; na kosa hili limepelekwa mbali mno kiasi kwamba muungano wa sasa usio mtakatifu na utawala wa Kanisa la jina tu pamoja na ulimwengu unaaminiwa na wengi kuwa ndio utawala wa Ufalme wa Mungu duniani. Ni kweli, kuna maana ambayo kwayo Kanisa sasa ni Ufalme wa Mungu, na kazi ya neema sasa inaendelea ndani ya mioyo ya waamini; lakini kuchukulia hili kuwa ndilo jambo pekee, na kukataa Ufalme wa Mungu halisi ujao ambao bado utasimamishwa chini ya mbingu yote, ambamo mapenzi ya Mungu yatatimizwa kama huko mbinguni, ni kubatilisha na kufanya zisizokuwa na maana ahadi zenye nguvu na za wazi zaidi zilizoandikwa na Bwana wetu na mitume na manabii, kwa ajili ya kututia moyo na kutusaidia kuushinda ulimwengu.

Katika mifano ya Bwana wetu, mara nyingi Kanisa linaitwa ufalme; na Mtume analisema kuwa ni ufalme ambao Kristo anautawala sasa, akisema kwamba Mungu "*...ametuhamisha kutoka katika ufalme wa giza na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake.*" Sisi tunaomkubali Kristo sasa tunatambua haki yake ya kutawala aliyoinunua, na tunampa utii wa shukrani na

wa hiari kabla hajausimamisha ufalme huo kwa nguvu ulimwenguni.

Tunatambua tofauti kati ya sheria za haki, ambazo atazisimamia, na ufalme wa giza unaoungwa mkono na yule mvamizi, ambaye kwa sasa ni mkuu wa ulimwengu huu. Hivyo, imani katika ahadi za Mungu hubadili utiifu wetu, nasi tunajihesabu kuwa raia wa mkuu huyo mpya, na, kwa hisani yake, warithi pamoja naye katika ufalme huo ambao bado utasimamishwa kwa nguvu na utukufu mkuu.

Lakini ukweli huu haubatilishi kamwe ahadi kwamba hatimaye ufalme wa Kristo utakuwa "*...toka bahari hata bahari, na toka mto hata miisho ya dunia...*" (**Zaburi 72:8);** kwamba mataifa yote yatamtumikia na kumtii; na kwamba kila goti litapigwa mbele zake, la vitu vya mbinguni na vya duniani. (**Danieli 7:27**; Wafilipi 2:10). Bali, kinyume chake, kuteuliwa kwa "*...kundi dogo...*" sasa kunathibitisha ahadi hizo.

Mifano ya Bwana wetu ikichunguzwa kwa makini, itaonekana kwamba inafundisha wazi kuwa kuja au kusimamishwa kwa Ufalme wa Mungu katika nguvu ni jambo la wakati ujao; na, kama jambo lililo wazi, halitatokea mpaka Mfalme atakapokuja. Hivyo mfano wa yule mtu kabaila aliyekwenda nchi ya mbali ili ajipatie ufalme na kurudi, na kadhalika (**Luka** 19:11-15), unaweka wazi kuwa kusimamishwa kwa Ufalme kutafanyika wakati wa kurudi kwa Kristo. Na ujumbe uliotumwa na Bwana kwa Kanisa miaka mingi baadaye ulikuwa, "*...Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima...*" (**Ufunuo 2:10**). Kutokana na hili ni dhahiri kwamba wafalme watakaotawala pamoja naye hawatavikwa taji wala kutawala kama wafalme katika maisha haya.

Kwa hiyo, Kanisa kwa sasa si Ufalme wa Mungu uliosimamishwa katika nguvu na utukufu, bali liko katika hali yake ya awali, ya kiinitete. Na hivyo, kwa hakika, ndivyo yanavyofundisha maneno yote ya Agano Jipya yanayolirejelea.

Ufalme wa mbinguni sasa unateseka kwa jeuri mikononi mwa ulimwengu; Mfalme alitendewa vibaya na kusulubiwa; na yeyote atakayefuata nyayo zake atapata mateso na jeuri kwa namna fulani. Hili, itajulikana, ni kweli kwa Kanisa *halisi* tu, na si lile la jina tu. Lakini ahadi imetolewa kwamba ikiwa sasa sisi (Kanisa, ufalme ulio katika kiinitete) tunateseka pamoja na Kristo, sisi pia, kwa wakati wake, atakapotwaa uweza wake mkuu na kutawala, tutatukuzwa na tutatawala pamoja naye.

**Yakobo (2:5**), kwa upatano na mafundisho ya Bwana wetu, anatuambia kwamba Mungu amewachagua maskini na waliodharauliwa kwa viwango vya ulimwengu huu, si kutawala sasa, bali kama "*...warithi wa ufalme ule aliouahidi...*" Bwana anasema, "*...Jinsi itakavyokuwa vigumu kwa wenye mali kuuingia ufalme wa Mungu!...*" (**Marko 10:23**). Ni dhahiri kwamba hamaanishi Kanisa la jina tu, ambalo sasa linatawala pamoja na ulimwengu; maana matajiri wanashinikizwa kuingia humo. Petro anawahimiza warithi wa ufalme kuwa na saburi, uvumilivu, wema na imani, akisema: "*...Ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe; maana hivi mtawezeshwa kwa wingi kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo...*" **2 Petro 1:10,11**.

Kauli ya Paulo katika **Warumi** 14:17 inadhaniwa na baadhi ya watu kurejelea ufalme wa *mfano*; lakini inapochunguzwa kwa mwanga wa muktadha, ni dhahiri kwamba fungu hilo linamaanisha hivi tu: Sisi, ndugu, tuliohamishwa sasa na kuingia katika ufalme wa Mwana wa pendo la Mungu, tuna uhuru fulani kuhusu chakula chetu, na kadhalika, ambao hatukuwa nao kama Wayahudi chini ya sheria (mstari 14); lakini tusiutumie uhuru huu ikiwa utasababisha ndugu ambao bado hawajatambua hilo kujikwaa na kukiuka dhamiri zao. Tusimharibu ndugu yetu ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake kwa sababu ya uhuru wetu wa chakula; bali tukumbuke kwamba haki za ufalme, sasa na wakati ujao, zinajumuisha baraka kuu zaidi kuliko uhuru wa chakula; yaani, katika uhuru wetu wa kutenda haki, amani yetu kwa Mungu kupitia Kristo, na furaha yetu katika kushiriki Roho

mtakatifu wa Mungu. Uhuru huu wa ufalme (sasa na hata milele) ni mkuu sana kiasi kwamba ule uhuru mdogo wa chakula unaweza kabisa kutolewa dhabihu, kwa sasa, kwa ajili ya mema ya ndugu yetu.

Hivyo, haijalishi tunatazama kutoka mtazamo gani wa kimaandiko, wazo la kwamba ahadi za ufalme ni udanganyifu wa kihadithi, au kwamba hali zetu za sasa zinatimiza ahadi hizi, linapingwa.

Kwa Kanisa la kwanza, ahadi za heshima ya ufalme na urithi wa pamoja na Bwana zilikuwa vichocheo vikali vya uaminifu chini ya majaribu na mateso ya sasa, ambayo walikuwa wameonywa tangu awali kuyatarajia; na katika maneno yote ya faraja na kutia moyo katika Apokalipsi (Ufunuo), yaliyotolewa kwa makanisa saba, hakuna yanayong'aa kwa uwazi zaidi na kwa nguvu kuliko yale yanayotangaza, "*...Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi...*"; na, "*...Na yeye ashindaye... nitampa mamlaka juu ya mataifa.*"

Lakini asili ya kibinadamu hutafuta kukwepa mateso na siku zote iko tayari kung'ang'ania heshima na mamlaka; hivyo tunaona kwamba hata katika siku za mitume baadhi ya watu Kanisani walikuwa na mwelekeo wa kujitwalia ahadi za heshima na mamlaka ya wakati ujao kwa ajili ya maisha ya sasa, na walikuwa wakianza kutenda kana kwamba walidhani wakati ulikuwa umewadia kwa ulimwengu kuliheshimu na hata kulitii Kanisa. Mtume Paulo anaandika, akirekebisha kosa hili, akijua kwamba mawazo kama hayo yangeleta madhara kwa Kanisa kwa kusitawisha kiburi na kuwaondoa katika njia ya dhabihu.

Anawaambia, **kwa dhihaka**, "*...Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmemiliki pasipo sisi...*" Na kisha anaongeza, kwa dhati, "*...Na laiti mngemiliki, ili sisi [mitume tunaoteswa] nasi tumiliki pamoja nanyi.*" **1 Wakorintho** 4:8. Walikuwa wakifurahia Ukristo wao kwa kujaribu kupata heshima nyingi iwezekanavyo

ndani yake na kupitia huo; na Mtume alijua vyema kwamba kama wangekuwa *waaminifu* kama wafuasi wa Bwana wasingekuwa katika hali hiyo. Hivyo anawakumbusha kwamba ikiwa kweli ule utawala uliotarajiwa kwa muda mrefu ungalikuwa umeanza, yeye naye angekuwa akitawala pasipo kupungua kwao, na ukweli kwamba yeye kwa uaminifu alikuwa mteswaji kwa ajili ya kweli, ulikuwa uthibitisho kwamba *utawala wao* ulikuwa wa kabla ya wakati, na ulikuwa mtego badala ya kuwa utukufu.

Kisha, kwa mguso wa **dhihaka**, anaongeza, "*...Sisi [mitume na watumishi waaminifu] tu wapumbavu kwa ajili ya Kristo, lakini ninyi ni wenye akili katika Kristo; sisi tu dhaifu, lakini ninyi mna nguvu; ninyi mna utukufu, lakini sisi hatuna heshima.*" Siandiki mambo haya ili kuwatahayarisha tu: nina kusudi bora na tukufu zaidi—KUWAONYA; maana njia ya heshima ya sasa haielekei kwenye utukufu na heshima *itakayofunuliwa*; bali mateso ya sasa na kujikana nafsi ndiyo njia nyembamba iendayo kwenye utukufu, heshima, kutokufa na urithi wa pamoja katika ufalme. Kwa hiyo, nawasihi, "*...mnifuate mimi...*" Tesekeni na kutukanwa na kuudhiwa sasa, ili mpate kushiriki nami ile taji ya uzima, "*...ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.*" **1 Wakorintho** 4:10-17; **2 Timotheo** 4:8.

Lakini, baada ya mateso mengi kuvumiliwa kwa uaminifu na Kanisa la kwanza, nadharia zilianza kuenea zikisema kwamba utume wa Kanisa ulikuwa ni kuuteka ulimwengu, kusimamisha ufalme wa mbinguni duniani na kutawala mataifa **kabla ya Kuja kwake Bwana mara ya pili**. Hili liliweka msingi wa hila za kidunia, fahari na kiburi, maonyesho ya kujigamba na sherehe katika Kanisa, ambazo zilikusudiwa kuushangaza, kuuteka na kuutia hofu ulimwengu, na ambazo ziliongoza hatua kwa hatua kwenye madai makubwa ya Upapa kwamba kama Ufalme wa Mungu duniani, ulikuwa na haki ya kuamuru heshima na utii kwa sheria zake na maofisa wake kutoka kwa kila jamaa, taifa, na watu.

Chini ya dai hili la uongo (na inaonekana walijidanganya wenyewe pamoja na wengine), Upapa kwa muda uliwatawaza na kuwazulu wafalme wa Ulaya, na bado unadai mamlaka ambayo kwa sasa hauwezi kuyatekeleza kwa nguvu

Wazo hili hili kupitia Upapa limeshuka hadi kwenye Uprotestanti, ambao pia unadai, ingawa kwa utata zaidi, kwamba kwa namna fulani *utawala* wa Kanisa unaendelea; na kama Wakorintho, wafuasi wake "wameshiba" na ni "matajiri," na wanamiliki "kama wafalme," kama ilivyoelezwa wazi na Bwana wetu. (**Ufunuo** 3:17,18). Hivyo imetokea kwamba washiriki wa jina tu wa Kanisa—wale ambao hawajaongoka kikweli, ambao si ngano halisi, bali magugu, waigaji tu wa ngano—wanapita sana idadi ya wanafunzi wa kweli wa Kristo. Na hawa wanapinga sana kila dhabihu ya kweli na kujikana nafsi, hawateswi kwa ajili ya haki [kweli], na zaidi wanashikilia tu desturi za kufunga, na kadhalika, badala yake. Kwa kweli wanamiliki pamoja na ulimwengu na hawako katika mstari wa maandalizi kwa ajili ya kushiriki katika ufalme halisi utakaoanzishwa na Bwana wetu wakati wa kuwapo kwake kwa mara ya pili.

Kwa mchunguzi makini yeyote, kuna kutokubaliana kwa dhahiri kati ya mtazamo huu na mafundisho ya Yesu na mitume. Walifundisha kwamba hapawezi kuwa na ufalme mpaka Mfalme atakapokuja. (**Ufunuo** 20:6; 3:21; **2 Timotheo** 2:12). Kwa hiyo, ufalme wa mbinguni **hauna budi** kutendewa jeuri mpaka wakati huo, utakaposimamishwa katika utukufu na nguvu.

### Sehemu Mbili za Ufalme wa Mungu

Ingawa ni kweli, kama ilivyosemwa na Bwana wetu, kwamba Ufalme wa Mungu hauji kwa namna ya kuonekana—yaani, hauanzi kwa kuonekana kwa nje—bado kwa wakati wake utadhihirishwa kwa wote kwa ishara za nje, zinazoonekana na zisizo na shaka. Utakaposimamishwa kikamilifu, Ufalme wa Mungu utakuwa na sehemu mbili, sehemu ya kiroho au ya mbinguni na sehemu ya kidunia au ya kibinadamu.

Sehemu hiyo ya kiroho haitaonekana kwa wanadamu siku zote, kwa kuwa wale wanaoifanyiza watakuwa na asili ya uungu, ya kiroho, ambayo hakuna mwanadamu aliyepata kuiona wala awezaye kuiona (**1 Timotheo** 6:16; **Yohana** 1:18); hata hivyo kuwapo kwake na nguvu zake zitadhihirishwa kwa uweza mkuu, hasa kupitia wawakilishi wake wa kibinadamu, ambao watauunda ule upande wa kidunia wa Ufalme wa Mungu.

Wale watakaounda sehemu ya kiroho ya ufalme ni watakatifu washindao wa enzi ya Injili—yaani Kristo, kichwa na mwili—wakiwa wametukuzwa. Kufufuliwa kwao na kuinuliwa kwao kwenye mamlaka hutangulia kule kwa wengine wote, kwa sababu kupitia kundi hili wengine wote watabarikiwa. (**Waebrania** 11:39,40).

Ufufuo wao ndio ule ufufuo wa kwanza. (**Ufunuo** 20:5*).Kazi kuu iliyo mbele ya kundi hili tukufu lililotiwa mafuta—yaani Kristo—**inalazimu wainuliwe** kwenye asili ya uungu: hakuna nguvu nyingine isipokuwa uweza wa kiungu inayoweza kuitimiza kazi hiyo. Kazi yao haihusu ulimwengu huu pekee, bali inahusu vitu vyote mbinguni na duniani—miongoni mwa viumbe vya roho na vilevile miongoni mwa wanadamu. **Mathayo 28:18; Wakolosai 1:20; Waefeso 1:10; Wafilipi 2:10; 1 Wakorintho 6:3**. Kazi ya awamu ya kidunia ya Ufalme wa Mungu itahusishwa na dunia hii na wanadamu. Na wale watakaoheshimiwa sana kiasi cha kushiriki katika kazi hiyo watakuwa ni watu waliotukuzwa na kuheshimiwa zaidi na Mungu miongoni mwa wanadamu. Hawa ndio kundi lililotajwa katika Sura ya

---

* *Katika mstari huu maneno "Lakini wafu waliosalia hawakuwa hai tena hata itimie ile miaka elfu" si halisi. Hayapatikani katika Miswada ya kale na ya kuaminika zaidi ya Kigiriki, yaani Sinaitic, Vatican Na. 1209 na 1160, wala Mswada wa Kisyria. Lazima tukumbuke kwamba vifungu vingi vinavyopatikana katika nakala za kisasa ni nyongeza ambazo hazipaswi kuwapo katika Biblia. Kwa kuwa tumeamriwa tusiongeze neno la Mungu, ni wajibu wetu kukataa nyongeza kama hizo mara tu ubatili wake unapothibitishwa. Maneno yaliyoainishwa pengine yaliingia katika maandishi kwa bahati mbaya, katika karne ya tano; kwa maana hakuna Mswada wa tarehe ya awali (wa Kigiriki au Kisyria) ulio na sehemu hii. Pengine mwanzoni yalikuwa maoni tu ya pembezoni yaliyotolewa na msomaji, yakieleza wazo lake juu ya andiko hilo, na yakanakiliwa na kuingizwa ndani ya andiko lenyewe na mwandishi wa baadaye ambaye alishindwa kutofautisha kati ya andiko na maoni hayo. Hata hivyo, kukataliwa kwa sehemu hii si jambo la lazima kwa "Mpango" kama ulivyoelezwa hapa; kwa maana wafu waliosalia – ulimwengu kwa ujumla – hawatakuwa hai tena katika maana kamili, katika maana kamilifu ambayo Adamu aliishi kabla ya kutenda dhambi na kuingia chini ya hukumu "kufa utakufa." Uzima mkamilifu usio na udhaifu au kufa ndiyo maana pekee ambayo Mungu analitambua neno uzima. Kwa mtazamo wake ulimwengu wote tayari umepoteza uzima, unakufa, na sasa unaweza kusemwa kwa usahihi zaidi kuwa umekufa kuliko kuwa hai.* ***2 Wakorintho 5:14; Mathayo 8:22****.*

*Neno ufufuo (Kigiriki, anastasis) humaanisha kuinua. Likihusishwa na mwanadamu, linamaanisha kumwinua mwanadamu kwenye ile hali ambayo alianguka kutoka kwayo, kwenye ukamilifu kamili wa kibinadamu – jambo lililopotea kupitia Adamu. Ukamilifu ambamo jamii yetu ilianguka ndio ukamilifu ambao watauinukia hatua kwa hatua, wakati wa* ***Zama za Milenia*** *za urejesho au ufufuo (kuinua).* ***Zama za Milenia*** *si tu* ***zama*** *za majaribu, bali pia ni* ***zama*** *za baraka, na kupitia ufufuo au urejesho wa uzima yote yaliyopotea yatarejeshwa kwa wote ambao, watakapojua na kupata fursa, watatii kwa furaha. Mchakato wa ufufuo utakuwa wa hatua kwa hatua, ukihitaji* ***zama*** *yote hiyo ili kukamilika kwake kikamilifu; ingawa kuamshwa tu kwenye kiasi fulani cha uzima na fahamu, kama inavyofurahiwa sasa, bila shaka itakuwa kazi ya mara moja. Hivyo haitakuwa mpaka miaka elfu itakapokwisha ndipo jamii ya wanadamu itakuwa imepata kikamilifu kipimo kamili cha uzima uliopotea katika Adamu. Na kwa kuwa chochote kilichopungua uzima mkamilifu ni hali ya kifo cha sehemu, inafuata kwamba, ingawa maneno hayo hapo juu si sehemu ya kumbukumbu iliyoongozwa na roho, lingekuwa jambo la kweli kabisa kusema kwamba wafu waliosalia hawatakuwa hai tena (hawatapata tena utimilifu wa uzima uliopotea) mpaka ile miaka elfu ya urejesho na baraka itakapoisha.*

Nane, ambao siku yao ya hukumu ilikuwa kabla ya zama za Injili. Baada ya kujaribiwa na kuonekana kuwa waaminifu, katika kuamshwa kwao hawataletwa tena katika hukumu, bali mara moja watapokea thawabu ya uaminifu wao, yaani ufufuo wa papo hapo hadi ukamilifu kama wanadamu. Wengine, tofauti na hawa na kundi la kiroho, watafikia ukamilifu hatua kwa hatua katika kipindi chote cha zama za Milenia.

Hivyo basi, kundi hili litakuwa tayari mara moja kwa ajili ya kazi kubwa iliyo mbele yao, kama mawakala wa kibinadamu wa Kristo katika kuwarejesha na kuwabariki wanadamu wengine wote. Kama vile asili ya kiroho ilivyo ya lazima kwa ajili ya kutekeleza kazi ya Kristo, vivyo hivyo asili kamilifu ya kibinadamu inafaa kwa ajili ya kutimiza kazi itakayofanywa miongoni mwa wanadamu. Watu hawa watatumikia katikati ya wanadamu na wataonekana na wanadamu, na utukufu wa ukamilifu wao utakuwa mfano wa kudumu na kichocheo kwa wanadamu wengine kujitahidi kufikia ukamilifu huo huo.

Kwamba hawa waheshimiwa wa kale watakuwa katika awamu ya kibinadamu ya Ufalme na wataonekana na wanadamu kunathibitishwa kikamilifu na maneno ya Yesu kwa Wayahudi wasioamini waliokuwa wakimkataa. Alisema kwamba watawaona Abrahamu, Isaka, na Yakobo, pamoja na manabii wote, katika Ufalme wa Mungu. Inapaswa pia kutambuliwa kwamba Bwana hakusema kuwa yeye au mitume wangekuwa wanaonekana pamoja na Abrahamu. Kwa kweli, wanadamu watawaona na kushirikiana na awamu ya kidunia ya Ufalme, ilhali awamu ya kiroho haitakuwa ikionekana kwa macho ya kibinadamu; na baadhi yao bila shaka watahuzunika sana watakapogundua kwamba walikataa heshima kubwa namna hiyo.

Hatupewi maelezo ya wazi kuhusu namna halisi ambayo awamu hizi mbili za Ufalme wa mbinguni zitakavyofanya kazi pamoja kwa upatanifu; hata hivyo, tuna mfano wa jinsi zinavyoweza kufanya kazi, katika jinsi Mungu alivyoshughulika na Israeli kupitia wawakilishi wao, Musa, Haruni, Yoshua,

manabii, n.k. — ingawa udhihirisho ujao wa nguvu za Mungu utazidi sana ule wa zama hizo za mfano; kwa kuwa kazi ya zama ijayo inajumuisha kufufuliwa kwa wafu wote na kurejeshwa kwa watiifu katika ukamilifu.

Kazi hii italazimu kuanzishwa kwa serikali kamilifu miongoni mwa wanadamu, ikiwa na watu wakamilifu katika nafasi za uongozi, ili waweze kuyaongoza kwa haki mambo ya serikali. Pia italazimu kuanzishwa kwa mifumo sahihi ya elimu ya kila aina, pamoja na hatua mbalimbali za hisani. Na kazi hii tukufu ya kuinua jamii ya wanadamu kwa hatua za hakika na thabiti (chini ya uongozi wa washiriki wa kiroho wasioonekana wa Ufalme huohuo) ndiyo heshima kuu ambayo Mababu wa Imani wamewekewa, na kwa ajili yake watatokea wakiwa tayari muda mfupi baada ya kuanguka kabisa kwa falme za ulimwengu huu na kufungwa kwa Shetani, mkuu wao. Na kama wawakilishi waliotukuzwa na Mungu wa Ufalme wa mbinguni, watapokea kwa haraka heshima na ushirikiano kutoka kwa wanadamu wote.

Kupata nafasi katika sehemu ya kidunia ya Ufalme wa Mungu itakuwa ni kupata kutoshelezwa kwa kila tamaa na shauku ya moyo wa kibinadamu ulio mkamilifu. Itakuwa ni fungu tukufu na la kuridhisha tangu mwanzo kabisa wa kuingia humo, na bado utukufu huo utazidi kuongezeka kadiri muda unavyo-songa na ile kazi iliyobarikiwa inavyoendelea.

Na wakati, mwishoni mwa ile miaka elfu, ile kazi kuu ya urejesho itakapokamilishwa na Kristo (kwa kiasi kikubwa kupitia utendaji wa wafanyakazi wenzao hawa wa kibinadamu walio bora); wakati jamii yote ya wanadamu (isipokuwa wale wasioweza kurekebishika --**Mathayo 25:46; Ufunuo 20:9**) itaka-posimama ikiwa imekubaliwa, pasipo waa, wala kunyanzi, wala lolote kama hayo, mbele za Yehova, hawa waliofanyika nyenzo katika kazi hiyo watang'aa miongoni mwa wanadamu wenzao na mbele za Mungu na Kristo na malaika, kama "*nyota milele na milele.*" (**Danieli 12:3**). Kazi yao na taabu yao ya upendo

hazitasahauliwa kamwe na wanadamu wenzao wenye shukrani. Watakuwa katika kumbukumbu la milele. **Zaburi 112:6**.

Lakini ingawa utukufu unaoongezeka wa wanadamu hao wakamilifu **watakaounda** sehemu ya kidunia ya ufalme **utakuwa** mkuu, utukufu wa ile sehemu ya mbinguni **utakuwa** ndio utukufu ulio bora zaidi. Wakati wale wa kwanza **watang'aa** kama nyota milele, hawa wa pili **watang'aa** kama mwangaza wa anga—kama jua. (**Danieli 12:3**). Heshima za mbinguni na vilevile za duniani **zitawekwa** miguuni pa Kristo. Akili ya mwanadamu inaweza kukadiria, lakini haiwezi kufahamu waziwazi, ule utukufu **utakaofunuliwa** katika Kristo katika **zama** zisizohesabika za milele. **Warumi 8:18; Waefeso 2:7-12**.

Ni kupitia sehemu hizi mbili za ufalme ndipo ile ahadi kwa Ibrahimu **itathibitishwa**— "*Katika wewe na katika uzao wako jamaa zote za dunia zitabarikiwa.*" "*Uzao wako utakuwa kama mchanga wa bahari, na kama nyota za mbinguni*" —uzao wa kidunia na wa mbinguni, yote miwili ikiwa ni nyenzo za Mungu za kubariki ulimwengu. Sehemu zote mbili za ahadi hizi zilionekana wazi na kukusudiwa na Mungu tangu mwanzo, lakini ni ile ya kidunia tu **iliyoonekana** na Ibrahimu.

Na ingawa Mungu alichagua kutoka kwa uzao wa asili wakuu wa lile daraja la kiroho (mitume na wengine), na kutoa ofa ya baraka hiyo kuu, yaani ya kiroho, kwa taifa hilo lote lililoishi katika **wakati uliowekwa** kwa ajili ya mwito huo wa mbinguni, jambo hili lilikuwa ni zaidi sana ya kile Ibrahimu alichowahi kukiona katika agano hilo—neema juu ya neema.

Paulo (**Warumi 11:17**) anazungumzia agano la Ibrahimu kama mzizi ambao Israeli wa kimwili **walichipuka kutoka kwake kiasili**, lakini ambamo waamini wa Mataifa walipandikizwa wakati matawi ya asili yalipokatwa kwa sababu ya kutokuamini. Hili linathibitisha utimilifu wa pande mbili wa ile ahadi katika ukuzaji wa zao mbili, wa kidunia (wa kibinadamu) na wa

mbinguni (wa kiroho), ambazo zitauunda sehemu mbili za ufalme.

Agano hili la mzizi linabeba aina hizi mbili tofauti za matawi, ambayo kila moja katika ufufuo litazaa aina yake yenyewe ya matunda makamilifu yaliyo tofauti—madaraja ya kibinadamu na ya kiroho katika nguvu ya ufalme. Katika utaratibu wa maendeleo kwanza ulikuwa ni ule wa asili (wa kidunia), na baadaye watawala wa mbinguni; lakini katika utaratibu wa ukuu wa nafasi na wakati wa kusimikwa, utakuwa kwanza ule wa kiroho, baadaye ule wa asili; na hivyo wapo wa mwisho watakaokuwa wa kwanza, na wa kwanza watakaokuwa wa mwisho. **Mathayo 19:30; Luka 16:16**.

Ahadi aliyopewa Ibrahimu, ambayo Stefano anairejelea (**Matendo 7:5**), na ambayo Israeli waliitumainia, ilikuwa ya kidunia: ilihusiana na *nchi*. Mungu "*aliahidi kumpa iwe milki yake,*" alisema Stefano. Na Mungu alimwambia Ibrahimu,

> "*Inua sasa macho yako, tazama kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini, na wa mashariki na wa magharibi; maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. Nami nitaufanya uzao wako uwe kama mavumbi ya nchi; hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, uzao wako nao utahesabika. Ondoka, utembee katika nchi hii, katika mapana yake, na marefu yake; maana nitakupa wewe.*" *(**Mwanzo 13:14-17**).*

Stefano anaonyesha kwamba ahadi hii **bado haina budi** kutimizwa; maana anatangaza kwamba Mungu hakumpa Ibrahimu "*urithi wowote ndani yake [katika nchi hiyo], la, hata mahali pa kuweka mguu wake.*"

Mtume, akiandika juu ya kundi hili hili la **mababu wa imani**—Ibrahimu miongoni mwa wengine—anakubaliana na kauli ya Stefano kwamba ahadi kwa Ibrahimu bado haijatimizwa; na anaendelea zaidi na kuonyesha kwamba ahadi hizo za kidunia haziwezi na hazitatimizwa mpaka zile ahadi za juu zaidi za mbinguni zinazomhusu Kristo (Kichwa na mwili) zitimizwe.

Anasema juu yao: Hawa wote walikufa katika imani, **pasipo kupokea** [yaani, bila kuipata] [utimilifu wa] ile ahadi, kwa kuwa Mungu alikuwa ametuandalia kitu kilicho bora sisi [Kristo], ili wao pasipo sisi wasikamilishwe. (**Waebrania 11:13,39,40**).

Hivyo inaonyeshwa tena kwamba Mkombozi na Mrejeshi ni wa kiroho, akiwa ametoa ile asili ya kibinadamu kuwa dhabihu kwa ajili ya wote, na kwamba kutoka katika daraja hili la kiroho, likiwa limeinuliwa juu sana, baraka zote lazima zitoke, yeyote yule atakayeheshimiwa kuwa vyombo au mawakala wake. **Warumi 12:1; Wagalatia 3:29**.

Sehemu ya kidunia ya ufalme inaonekana kuwa ni ya Kiisraeli; na ukweli huu unakusanya pamoja unabii mwingi unaohusu nafasi ya mbele ya taifa hilo katika mpango wa Mungu wa baraka za baadaye kwa ulimwengu, wakati hema lao lililoanguka mavumbini litakaporejeshwa, na Yerusalemu itakapokuwa sifa katika dunia yote. Tunapata kauli za manabii na mitume zinazoonyesha wazi kwamba katika nyakati za urejesho, Israeli kama taifa litakuwa la kwanza miongoni mwa mataifa kupatana na utaratibu mpya wa mambo; kwamba Yerusalemu ya kidunia itajengwa upya juu ya magofu yake ya zamani; na kwamba mfumo wao wa utawala utarejeshwa kama hapo mwanzo chini ya wakuu au waamuzi. (**Isaya 1:26; Zaburi 45:16; Yeremia 30:18**).

Na ni nini kinachoweza kutazamiwa kwa usahihi zaidi kuliko kwamba Israeli kwanza kabisa wafurahie kuwatambua manabii na mababu? Na kwamba kufahamiana kwao na nidhamu ya muda mrefu chini ya sheria iwe imewatayarisha kwa ajili ya unyenyekevu na utii chini ya mamlaka ya ufalme? Na ingawa Israeli litakuwa taifa la kwanza kutambuliwa na kubarikiwa, imeandikwa pia juu ya Israeli kwamba, "*Bwana ataziokoa hema za Yuda kwanza.*"

Hatuzioni kuwa ni jambo la muhimu kuingia katika mjadala wa kutafuta ni wapi "kabila zilizopotea" za Israeli zinapaswa kutafutiwa. Inaweza kuwa kweli, au isiwe kweli—kama wengine

wanavyodai—kwamba kabila hizo zinaweza kufuatiliwa hadi kwenye mataifa fulani yaliyostaarabika ya siku hizi. Lakini, ingawa baadhi ya ushahidi unaotolewa una mantiki, kwa ujumla jambo hilo limejengwa zaidi juu ya mahitimisho na makisio.

Hata hivyo, ikiwa itakuja kuthibitishwa wazi kwamba baadhi ya mataifa yaliyostaarabika ni wazao wa kabila hizo zilizopotea, jambo hilo **halitawapa faida yoyote** chini ya ule "**mwito mkuu**" wa "**mbinguni**." Mwito huo, tangu taifa lao lilipokataliwa, hautambui tofauti kati ya Myahudi na Myunani, mtumwa na aliye huru. Ikiwa ushahidi huo utakuja kuwa wazi (jambo ambalo kwa sasa bado), ungekuwa unapatana kabisa na unabii na ahadi zinazohusu taifa hilo ambazo bado zinasubiri kutimizwa ndani ya na chini ya sehemu ya kidunia ya ufalme.

Mapenzi ya asili, pamoja na kiasi fulani cha tumaini kilichosalia katika ahadi ambazo hazijatimizwa kwa muda mrefu, na mielekeo yao yote ya asili, vitawasaidia Israeli kuwakubali watawala wapya kwa ujumla na kwa haraka; huku tabia zao za utii wa kiasi kwa sheria zikiwasaidia pia kuingia haraka katika upatanifu na kanuni za serikali mpya.

Kama vile Yerusalemu ilivyokuwa makao makuu ya himaya chini ya ule Ufalme wa Mungu wa mfano, itachukua tena nafasi hiyo hiyo, na kuwa "mji wa Mfalme Mkuu." (**Zaburi 48:2; Mathayo 5:35**). Mji ni ishara ya ufalme au utawala, na hivyo Ufalme wa Mungu unafananishwa na Yerusalemu Mpya, utawala mpya utakaoshuka kutoka mbinguni kuja duniani. Mwanzoni, utaundwa na daraja la kiroho pekee, yaani Bibi-arusi wa Kristo, ambaye, kama alivyoonekana na Yohana, atashuka duniani hatua kwa hatua; yaani, utaingia katika mamlaka hatua kwa hatua kadiri himaya za sasa zinavyovunjika vipande-vipande wakati wa Siku ya Bwana.

Hata hivyo, wakati utakapowadia, sehemu ya kidunia ya mji huu au serikali hii **itaanzishwa**, ambayo sehemu au washiriki wake watakuwa ni wale **mababu wa imani**. Hakutakuwa na miji

miwili (serikali mbili), bali mji mmoja, serikali moja ya mbinguni, ile ambayo Ibrahimu aliitazamia, "mji wenye misingi"—serikali iliyoanzishwa katika haki, ikiwa imejengwa juu ya msingi thabiti wa mwamba wa haki ya Kristo Mkombozi, thamani ya fidia ya mwanadamu aliyoitoa, na uimara wa haki ya kimungu, ambayo haiwezi tena kuwahukumu waliokombolewa kama vile ambavyo hapo awali isingeweza kuwaachilia wenye hatia. **Warumi 8:31-34; 1 Wakorintho 3:11**.

Mji Tukufu wa Amani! Ambao kuta zake huashiria wokovu, ulinzi, na baraka kwa wote wanaoingia humo; ambao misingi yake iliyowekwa katika haki haiwezi kamwe kutikiswa, na ambaye mjenzi na msanifu wake ni Mungu!

Ni katika mwangaza utakaong'aa kutoka katika mji (ufalme) huu tukufu wa Mungu ambapo mataifa (watu) **watatembea** katika Njia Kuu ya Utakatifu, hadi kufikia ukamilifu na upatanifu kamili na Mungu. (**Ufunuo 21:24**)*.

Wanadamu **watakapofikia** ukamilifu mwishoni mwa **Zama za Milenia**, kama ilivyokwisha kuonyeshwa, **watakaribishwa** kuwa washiriki wa Ufalme wa Mungu na kupewa mamlaka kamili juu ya dunia kama ilivyokusudiwa hapo mwanzo—kila mwanadamu akiwa mtawala huru, mfalme. Hili linaonyeshwa wazi katika unabii wa Yohana wa kimifano (**Ufunuo 21:24-26**); kwani katika maono hayo, hakuona tu watu wakitembea katika nuru yake, bali aliwaona wafalme wakiingia humo kwa utukufu; lakini hakuna aliyeweza kuingia ambaye angeunajisi mji huo.

Hakuna anayeweza kutambuliwa na mji huo (ufalme) ambaye hajajaribiwa kikamilifu kwanza; hakuna anayetenda, au anayependa kutenda, udanganyifu na udhalimu; ni wale tu ambao Mwana-Kondoo **atawaandika** kuwa wanastahili uzima wa

---

* *Maneno yafuatayo yameachwa katika mstari huu na miswada ya kale ya kuaminika zaidi, yaani, "ya wale waliookolewa," na pia "na heshima." Maneno haya ya mwisho pia hayapo katika mstari wa 26.*

milele, na ambao **atawaambia**, "*Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuwekwa misingi ya dunia.*"

Basi, inapaswa kukumbukwa kwamba ingawa bila shaka mji halisi wa Yerusalemu **utajengwa upya**, na ingawa pengine **utakuwa** mji mkuu wa ulimwengu, bado unabii mwingi unaotaja Yerusalemu na utukufu wake wa baadaye hurejelea—kwa kutumia mji huo kama ishara—Ufalme wa Mungu **utakaowekwa** kwa fahari kuu.

> *Kuhusu utukufu wa baadaye wa sehemu ya kidunia ya ufalme kama unavyowakilishwa katika Yerusalemu, manabii huzungumza kwa maneno yenye kusisimua, wakisema: "Pazeni sauti ya furaha, imbeni pamoja, enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa; kwa kuwa Bwana amewafariji watu wake, ameikomboa Yerusalemu." "Tazama, naumba Yerusalemu iwe shangwe, na watu wake wawe furaha." "Furahini pamoja na Yerusalemu, na mshangilie pamoja naye... mpate kufurahishwa kwa wingi wa utukufu wake; kwa maana Bwana asema hivi, Tazama, nitamwelekezea amani kama mto, na utukufu wa mataifa kama kijito kifurikacho." "Wakati huo watauita Yerusalemu kiti cha enzi cha Bwana, na mataifa yote watakusanyika kwayo." "Na watu wengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani [ufalme] wa Bwana, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo; naye atatufundisha njia zake, nasi tutatembea katika mapito yake; kwa maana katika Sayuni [sehemu ya kiroho] itatoka sheria, na neno la Bwana kutoka Yerusalemu" – yaani sehemu ya kidunia.* ***Isaya 52:9; 65:18; 66:10-12; Yeremia 3:17; Isaya 2:3****.*

Tunapozifikiria zile ahadi nyingi zenye thamani za baraka za baadaye zilizotolewa kwa Israeli, na tukitarajia utimilifu sahihi wa ahadi hizo kwa watu hao, ni vema tukumbuke kwamba kama taifa, wao ni **wa mfano**, na pia ni **halisi**. Katika upande mmoja, wao ni mfano wa ulimwengu wote wa wanadamu; na Agano lao la Sheria, la utii na uzima, lilikuwa mfano wa Agano Jipya **litakalowekwa** kwa ajili ya ulimwengu wakati wa **Zama za Milenia** na zama zijazo.

Ile damu ya upatanisho chini ya agano lao la mfano, na ukuhani uliotumia damu hiyo kwa taifa hilo, vilikuwa mfano wa damu ya Agano Jipya na ule Ukuhani wa Kifalme ambao, wakati wa

Milenia, **utaeneza** utakaso na baraka zake kwa ulimwengu wote. Hivyo, ukuhani wao ulifanywa kuwa mfano wa Kristo, na taifa lile likafanywa kuwa mfano wa wale wote ambao dhabihu ya kweli ilitolewa kwa ajili yao, na ambao baraka za kweli **zitawafikia**—"kila mwanadamu," "ulimwengu wote."

Basi, na tukumbuke kwamba ingawa baraka za baadaye, kama zilivyokuwa zile zilizopita, **zitakuwa** kwa Myahudi kwanza na pia kwa Mataifa, itakuwa ni katika suala la wakati tu ambapo Wayahudi **watakuwa** na kipaumbele cha kupata upendeleo wa kiungu; na hili tumeshaonyesha kuwa **litakuwa** tokeo la asili la mafunzo yao chini ya Sheria, ambayo katika wakati uliowekwa **itatimiza** kusudi lake la kuwaleta kwa Kristo.

Ingawa Sheria hiyo ilileta mabaki yao tu wakati wa **Kuja mara ya kwanza**, **itawaleta** kama taifa wakati wa **Kuja mara ya pili**, na kama taifa **watakuwa** malimbuko miongoni mwa mataifa. Hatimaye, kila baraka iliyoahidiwa kwa Israeli, isipokuwa zile zinazohusu madaraja yaliyochaguliwa, **itakuwa** na utimilifu wake halisi kwa watu hao, na pia utimilifu wake wa **kinyume cha mfano** katika jamaa zote za dunia.

Chini ya serikali hiyo, "*Mungu atamlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake—utukufu, heshima, na amani kwa kila mtu atendaye mema, kwa Myahudi kwanza, na pia kwa Mataifa; kwa maana kwa Mungu hakuna upendeleo.*" **Warumi 2:6, 10, 11**.

Mtume Paulo anaelekeza umakini wetu hasa kwenye uhakika wa ahadi za Mungu kwa Israeli katika siku zijazo, na anaonyesha ni upendeleo gani walioupoteza kwa sababu ya kutokuamini, na ni upendeleo gani ambao bado ni wa hakika kwao. Anasema kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya kiburi, ugumu wa moyo, na kutokuamini ndiyo maana Israeli kama taifa **hawakupata** kile walichokuwa wakikitafuta—ile nafasi kuu katika upendeleo na huduma ya kimungu.

Rejea ya Paulo hapa si kwa vizazi vyote vya Israeli kuanzia Ibrahimu na kuendelea, bali ni kwa vile vizazi vilivyoishi wakati wa

**Kuja mara ya kwanza**; na maneno yake yanahusu vizazi vyao vyote vilivyoishi wakati wa **Zama za Injili**, zama ambazo upendeleo mkuu umekuwa ukitolewa—ule **mwito mkuu** wa kuishiriki asili ya kimungu na kuwa warithi pamoja na Yesu. Upendeleo huu, Israeli kama taifa wameshindwa kuutambua na kuushika na ingawa Mungu aliwaangalia Mataifa na kuwaita wengi wao kupitia injili, wao pia, kama Israeli wa kimwili, **watashindwa** kupata ile tuzo ya mbinguni. Hata hivyo, daraja fulani, mabaki, **kundi dogo** miongoni mwa wote walioitwa, hutii mwito huo, na kwa utii na kujidhabihu, hufanya mwito na uteuzi wao kuwa thabiti. Hivyo, kile ambacho Israeli kama taifa walishindwa kukipata, na kile ambacho **Kanisa la Kikristo la jina tu** pia linashindwa kukipata, kinapewa lile daraja lililoteuliwa au lililochaguliwa, wale waaminifu—"mwili wa Kristo"—waliochaguliwa (kulingana na ujuzi wa Mungu wa tangu awali) kupitia kutakaswa na roho na kuamini kweli. **2 Wathesalonike 2:13; 1 Petro 1:2**.

Lakini ingawa, kupitia kumkataa Masihi, Israeli walipoteza upendeleo huu wote maalum, bado Paulo anaonyesha kwamba jambo hili halikuwathibitisha kuwa wamekatiliwa mbali kabisa na upendeleo; kwani bado walikuwa na fursa ile ile ya kupandikizwa ndani ya Kristo na kupata upendeleo wa kiroho ambao wanadamu wengine walifurahia, ikiwa, wakati mwito huo ulikuwa ukitolewa, wangeukubali kwa imani; kwani, Paulo anahoji, Mungu ana uwezo wa kuwapandikiza tena kama vile anavyoweza kupandikiza matawi ya mwitu, na yuko radhi kufanya hivyo, ikiwa hawatadumu katika kutokuamini. **Warumi 11:23, 24**.

Zaidi ya hayo, Paulo anahoji kwamba ingawa Israeli walipoteza ile baraka kuu, "ile anayoitafuta," yaani nafasi kuu katika ufalme wa Mungu, bado inabaki kuwa ahadi kuu bado zinapaswa kutimizwa kwa watu hao; kwani, anatoa sababu kwamba karama, miito, maagano, na ahadi za Mungu hazipaswi kuachwa bila kutimizwa. Mungu alijua mwisho tangu mwanzo; alijua

kwamba Israeli wangemkataa Masihi; na ahadi zake zisizo na shaka kwao akizingatia ujuzi huo zinatupa uhakika kwamba Israeli bado **atakuja kutumiwa** na Bwana katika huduma, kama chombo Chake cha kubariki ulimwengu, ingawa "Israeli hakupata kile alichokuwa akikitafuta"—ule upendeleo mkuu.

Kisha Paulo anaendelea kuonyesha kwamba ahadi za agano la Mungu kwa Israeli zilikuwa za asili ambayo iliacha wazi na bila kubainisha kama taifa wangekuwa uzao wa mbinguni au wa kidunia—kama wangeurithi na kuutimiza utumishi wa juu zaidi au wa chini uliotajwa katika ahadi hizo. Mungu aliufanya siri ule upendeleo wa juu zaidi wa kiroho hadi wakati uliowekwa, na ahadi walizopewa zilitaja upendeleo wa kidunia pekee, ingawa aliwapendelea kwa kuwapa ofa ya kwanza ya upendeleo huo wa kiroho pia, na hivyo akawatolea zaidi ya kile alichokuwa amewahi kuahidi.

Kwa neno moja, ahadi za mbinguni zilikuwa zimefichwa ndani ya zile za kidunia. Ahadi hizi, asema Paulo, haziwezi kushindwa, na kutoa ule upendeleo uliofichwa kwanza, na kukataa kwa Israeli kwa upofu, kwa namna yoyote hakuibatili au kuifuta sehemu nyingine ya ahadi. Hivyo anatangaza kwamba ingawa Israeli kama taifa wamekataliwa kutoka kwenye upendeleo wakati huu ambapo Bibi-arusi wa Kristo anachaguliwa kutoka kwa Wayahudi na Mataifa, bado **wakati utakuja** ambapo, Mkombozi (Kristo, Kichwa na mwili) atakapokuwa amekamilika, upendeleo wa kimungu **utarudi** kwa Israeli wa kimwili, na yule Mkombozi mtukufu ataondoa uovu katika Yakobo*, na hivyo Israeli wote wataokolewa [watarejeshwa kwenye upendeleo], kama ilivyoandikwa na nabii. Maneno ya Mtume ni haya:

> " *Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msiijue siri hii, ili msijione kuwa wenye akili; ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli, mpaka utimilifu wa Mataifa uwasili[mpaka idadi kamili iliyochaguliwa kutoka kwa Mataifa itakapokamilika]. Hivyo Israeli wote wataokoka; kama ilivyoandikwa, Mwokozi[Kristo, Kichwa na mwili]*

* *Israeli wa Kiroho hajawahi kuitwa Yakobo*

*atakuja kutoka Sayuni; Atamtenga Yakobo na maasia yake. Na hili ndilo agano langu nao, Nitakapowaondolea dhambi zao.Basi kwa habari ya Injili wamekuwa adui kwa ajili yenu; bali kwa habari ya kule kuchaguliwa wamekuwa wapenzi kwa ajili ya baba zetu. Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake. Kwa maana kama ninyi [mataifa] zamani mlivyomwasi Mungu, lakini sasa mmepata rehema kwa kuasi kwao;kadhalika na hao wameasi sasa, ili kwa kupata rehema kwenu wao nao wapate rehema[Kwenye mikono ya Kanisa lilotukuzwa]. Maana Mungu amewafunga wote pamoja katika kuasi ili awarehemu wote .[Linganisha **Warumi 5:17-19**.] Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! **Warumi 11:25-33**.*

## Warithi wa Ufalme

"N*i nani atakayeupanda mlima [kiuhalisia mlima, ishara ya ufalme] wa Yehova? Au ni nani atakayesimama katika mahali pake patakatifu [hekalu]? Ni yeye aliye na mikono safi na moyo mweupe."* ***Zaburi 24:3, 4***

Mji wa Yerusalemu ulijengwa juu ya kilele cha mlima—kilele pacha; kwani ulitenganishwa na bonde la Tyropoeon kuwa sehemu mbili. Hata hivyo, ulikuwa mji mmoja, uliozungukwa na ukuta mmoja, kukiwa na madaraja yanayounganisha sehemu hizo mbili. Juu ya kimoja cha vilele hivyo vya milima, Hekalu lilijengwa. Hili linaweza kueleweka kama ishara ya muungano wa sifa za kifalme na za kikuhani katika Kanisa lililotukuzwa; au, Ufalme mmoja wa Mungu wenye sehemu zake mbili—hekalu la kiroho, ambalo asili yake si ya kidunia, bali ni la asili mpya, ya mbinguni au ya kiroho (**Waebrania. 9:11**), likiwa limetengwa na, na bado limeunganishwa na, ile sehemu ya kidunia.

Daudi anaonekana kurejelea sehemu hizo mbili. Ilikuwa ni heshima kuwa mkaaji wa mji huo kwa vyovyote vile, na ilikuwa heshima kubwa zaidi kupanda katika hekalu takatifu, katika maeneo matakatifu ambayo makuhani pekee ndio walioruhusiwa kuingia. Na Daudi anaonyesha kuwa usafi wa maisha na unyoofu wa moyo ni muhimu kwa yeyote ambaye angefikia

heshima yoyote ile. Wale ambao wangekuwa wa Ukuhani wa Kifalme wanahimizwa kuwa na usafi, kama vile Kuhani Mkuu wa ungamo letu alivyo safi, ikiwa wanataka kuhesabiwa kuwa wanastahili kuwa warithi pamoja naye. Na kila mwenye tumaini hili ndani yake hujitakasa, kama yeye alivyo safi. Hii, kama ilivyokwisha kuonyeshwa, ni usafi wa **nia**, unaohesabiwa kwetu kama usafi kamili au halisi, huku usafi wa Kristo **uliohesabiwa kwetu** ukiziba mapungufu yetu yasiyoepukika, na kufidia udhaifu wetu usioepukika, tukiwa tunaenenda kwa *kufuata* roho na si *kufuata* mwili.

Lakini isisahaulike kwamba usafi, unyoofu, na kujiweka wakfu kikamilifu kwa Mungu ni mambo muhimu kwa wale wote ambao wangeingia katika Ufalme wa Mungu katika sehemu yoyote ile. Ilikuwa hivyo kwa wale **mababu wa imani** ambao watairithi sehemu ya kidunia ya ufalme chini ya Kristo. Walipenda haki na kuchukia uovu, na walihuzunika sana na kutubu walipokumbwa na kosa, au kukwazwa na udhaifu au jaribu. Vivyo hivyo, imekuwa hivyo kwa waaminifu wa **Zama za Injili**; na hivyo ndivyo **itakavyokuwa** kwa wote katika **Zama za Milenia**, wakati roho ya Mungu, roho ya kweli, **itakapomwagwa** juu ya wote wenye mwili. Washindi wa zama hiyo pia **watahitaji** kujitahidi kupata usafi wa moyo na maisha, ikiwa wanataka kuwa na haki chini ya mpango wa Mungu wa kuingia katika mji—ufalme uliowekwa tayari kwa ajili yao tangu kuwekwa misingi ya dunia—ule utawala wa awali uliorejeshwa.

### Utawala wa Chuma

Wengi wanadhani kimakosa kwamba wakati Ufalme wa Milenia wa Kristo **utakaposimikwa**, kila mmoja **atafurahishwa** na uongozi wake. Lakini sivyo. Kanuni zake **zitakuwa** kali zaidi kuliko zile za serikali yoyote ya awali, na uhuru wa watu **utawekewa mipaka** kwa kiwango ambacho **kitakuwa** cha kuumiza kwelikweli kwa wengi ambao sasa wanapiga kelele wakidai kuongezewa uhuru.

Uhuru wa kudanganya, kupotosha ukweli, kupata faida isiyo halali, na kudhulumu wengine, **utakatiliwa mbali kabisa**. Uhuru wa kujidhuru wenyewe au kudhuru wengine kwa chakula au kinywaji, au kwa njia yoyote ile kuharibu tabia njema, **utakataliwa kabisa** kwa wote. Uhuru au kibali cha kufanya uovu wa aina yoyote **hautatolewa** kwa yeyote. Uhuru pekee **utakaotolewa** kwa yeyote utakuwa ni ule uhuru wa kweli na mtukufu wa wana wa Mungu—uhuru wa kujitendea mema wao wenyewe na wengine katika kila njia; lakini hakuna kitu kitakachoruhusiwa kudhuru au kuharibu katika Ufalme huo wote Mtakatifu. (**Isaya 11:9; Warumi 8:21**).

Hivyo, utawala huo **utahisiwa** na wengi kuwa ni mkali, ukivunja-vunja mazoea na desturi zao zote za zamani, pamoja na kuvunja-vunja taasisi za sasa zilizojengwa juu ya mazoea hayo potofu na mawazo potofu ya uhuru. Kwa sababu ya uthabiti na nguvu zake, kwa njia ya mfano unaitwa utawala wa chuma—"*Atawatawala kwa fimbo ya chuma.*" (**Linganisha Ufunuo 2:26, 27; Zaburi 2:8-12 na 49:14**.) Hivyo ndivyo itakavyotimizwa kauli isemayo, "*Nitaifanya hukumu kuwa kamba ya kupimia, na haki kuwa timazi. Na mvua ya mawe [hukumu ya haki] itafagia kimbilio la uongo, na maji [ukweli] yatafurika mahali pa siri,*" *na kila jambo lililofichwa litafunuliwa.* **Isaya 28:17; Mathayo 10:26**.

Wengi **watajisikia** kuasi dhidi ya utawala huo mkamilifu na wa usawa kwa sababu huko nyuma, chini ya utawala wa mkuu wa sasa, walizoea kuwatawala wanadamu wenzao, na kuishi kwa kuwategemea wengine bila kutoa huduma inayolingana. Na mapigo **yatakuwa** mengi na makali ambayo maisha ya sasa ya kujifurahisha na kutosheleza tamaa **yatahitaji** kiasili na kuyapata chini ya utawala huo, kabla ya watu hao kujifunza masomo ya ufalme huo—usawa, haki, na uadilifu. (**Zaburi 89:32; Luka 12:47, 48**). Somo kuhusu jambo hili linakuja kwanza kwa kizazi kilicho hai sasa, nalo liko karibu sana. **Yakobo 5**.

Lakini, wazo la baraka! Mkuu wa Uzima **atakapokuwa** ameweka katika utendaji sheria za haki na usawa kwa utawala wa chuma,

umati wa wanadamu **utajifunza** kwamba "*Haki huinua taifa, bali dhambi ni aibu kwa watu wowote.*" **Watajifunza** kwamba mpango wa Mungu na sheria zake ndizo bora zaidi mwishowe kwa wote wanaohusika, na hatimaye **watajifunza** kupenda haki na kuchukia uovu. (**Zaburi 45:7; Waebrania 1:9**). Wote ambao chini ya utawala huo **hawatakuwa** wamejifunza kupenda yaliyo sawa **watahesabiwa** kuwa hawastahili uzima wa kudumu nao **watakatiliwa mbali** kutoka miongoni mwa watu. **Matendo 3:23; Ufunuo 20:9; Zaburi 11:5-7**.

### Ufalme wa Milele

"*Yehova **atakuwa** Mfalme juu ya nchi yote siku hiyo.*" (**Zekaria 14:9**). Ufalme ambao Yehova **atauanzisha** mikononi mwa Kristo wakati wa Milenia **utakuwa** ni ufalme wa Yehova, lakini **utakuwa** chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Kristo, kama mwakilishi wake mwenye mamlaka kamili (*vicegerent*). Hii ni sawa na namna ambavyo Majimbo ya Kusini yalishughulikiwa na serikali ya Marekani baada ya Uasi; kwa muda, majimbo hayo hayakuruhusiwa kujitawala yenyewe kwa kuchagua viongozi wao, ili yasije yakakiuka sheria za Kikatiba za Muungano; badala yake, magavana wenye mamlaka kamili waliteuliwa kusimamia kwa kusudi la kuyajenga upya majimbo hayo na kuyarudisha katika upatanifu kamili na serikali kuu.

Hivyo, utawala maalum wa Kristo juu ya mambo ya dunia ni kwa muda mfupi na kwa kusudi maalum, nao **utakoma** baada ya kusudi hilo kutimizwa. Mwanadamu, kupitia uasi, alipoteza haki alizopewa na Mungu—ikiwemo haki ya kujitawala kwa kupatana na sheria za Yehova. Mungu, kupitia Kristo, anazikomboa haki hizo zote, na kuhakikisha haki ya mwanadamu si tu kurudi binafsi katika hali yake ya awali, bali pia kurudi katika nafasi yake ya zamani kama mfalme wa dunia.

Lakini ili kumrudisha mwanadamu, kama Mungu alivyokusudia—kwa njia inayofaa zaidi kufundisha somo la uzoefu wa sasa (yaani kwa kumtaka yeye mwenyewe kuweka

juhudi katika urejesho wake)—**utahitajika** utawala wenye nguvu na mkamilifu. Na heshima hii ya kukamilisha urejesho wa mwanadamu, haki ambayo Kristo alikufa ili kuipata, imekabidhiwa kwake; na "sharti amiliki yeye, **hata** awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake"—mpaka kusiwepo na yeyote asiyemtambua, kumheshimu, na kumtii.

Kisha, akiwa amekamilisha utume wake kuhusu ujenzi upya au urejesho wa wanadamu, **ataukabidhi** ufalme kwa Mungu, yaani Baba, na wanadamu **watashughulika** moja kwa moja na Yehova kama hapo awali—ule upatanishi wa mwanadamu Kristo Yesu ukiwa umekamilisha kikamilifu kazi hiyo tukufu ya upatanisho. **1 Wakorintho 15:25-28**.

Ufalme huo, utakapokabidhiwa kwa Baba, bado **utakuwa** ni Ufalme wa Mungu, na sheria **zitakuwa** zile zile siku zote. Wanadamu wote, wakiwa wamerejeshwa kikamilifu wakati huo, **watakuwa** na uwezo wa kutoa utii mkamilifu, katika andiko (sheria) na pia katika roho; wakati ambapo sasa, roho ya utii au jitihada ya kuzishika sheria za Mungu ndivyo tu ambavyo wanadamu wanaweza kufanya. Maana andiko kamili la sheria hiyo kamilifu ingewahukumu kifo mara moja. (**2 Wakorintho 3:6**). Kukubalika kwetu sasa ni kupitia fidia ya Kristo pekee.

Mpaka mwanadamu atakapokuwa mkamilifu kikamilifu, "*Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai*." (**Waebrania 10:31**). Sasa, na mpaka ukamilifu halisi utakapofikiwa, hakuna anayeweza kusimama mbele ya sheria ya haki kamilifu: wote wanahitaji rehema inayotolewa bure chini ya sifa na dhabihu ya Kristo. Lakini Kristo **itakapofika** wakati wa kuukabidhi ufalme kwa Baba, **atawaasilisha** wakiwa **pasipo mawaa** mbele zake, wakiwa wanafaa na wanaweza kufurahia baraka za milele chini ya sheria kamilifu ya Yehova. Hofu yote wakati huo **itakuwa** imetoweka, na Yehova pamoja na viumbe wake waliorejeshwa **watakuwa** katika upatanifu mkamilifu, kama hapo mwanzo.

Wakati ambapo, mwishoni mwa **Zama za Milenia**, Kristo **atakapokabidhi** utawala wa dunia kwa Baba, anafanya hivyo kwa kuukabidhi kwa wanadamu kama wawakilishi wa Baba, ambao walikusudiwa tangu mwanzo kuwa na heshima hii. (**1 Wakorintho 15:24; Mathayo 25:34**). Hivyo Ufalme wa Mungu unadumu milele. Na ndivyo tunavyosoma katika maneno ya Bwana wetu: "*Kisha Mfalme **atawaambia** wale walioko mkono wake wa kuume [wale ambao, wakati wa utawala wa Milenia, **watakuwa** wamefikia nafasi ya upendeleo kwa upatanifu na utii], Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu [ninyi ambao Baba yangu amekusudia kuwabariki hivi], urithini ufalme mliowekewa tayari kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya dunia.*"

Ufalme huu na heshima hii iliyowekwa tayari kwa ajili ya mwanadamu haipaswi kuchanganywa na ule ufalme wa juu zaidi na heshima iliyowekwa tayari kwa ajili ya Kristo (Kichwa na mwili), ambao "*ulikusudiwa tangu zamani kabla ya ulimwengu kwa utukufu **wetu***" (**1 Wakorintho 2:7**), na ambao tulichaguliwa ndani ya Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Na ingawa uingiliaji kati maalum na utawala wa Kristo juu ya dunia **utakoma**, kama ilivyoonyeshwa, tusiishie kuhitimisha kwamba utukufu, utawala, na nguvu za Kristo zitakoma wakati huo. La hasha! Kristo ameunganishwa milele na utukufu na nguvu zote za kiungu katika mkono wa kuume wa upendeleo wa Yehova; na Bibi-arusi wake na mrithi mwenza **atashiriki** milele utukufu wake unaozidi kuongezeka. Ni kazi gani za ajabu katika ulimwengu mingine zinangojea nguvu ya chombo hiki kilichoinuliwa juu sana cha Yehova, hatutakisia hapa, zaidi ya kuashiria tu kutokuwa na mwisho na utendaji wa nguvu za kiungu, na upana usio na mipaka wa ulimwengu.

Kweli, basi, katika sehemu yoyote ya ufalme ambapo shauku yetu imejikita, huo ni "*shauku ya mataifa yote*"; kwani chini yake wote **watabarikiwa**. Kwa hivyo, wote wanaweza kutamani kwa dhati wakati huo; na wote wanaweza kusali kwa dhati, "*Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe duniani kama huko mbinguni.*" Ni

kwa ajili ya hili ambapo kwa kutokujua viumbe vyote vimekuwa vikilia na kungoja kwa muda mrefu—kungojea kufunuliwa kwa Wana wa Mungu, ufalme ambao **utaharibu** uovu na **utayabariki** na **uyaponye** mataifa yote. **Warumi 8:19; 16:20**.

## SOMO LA XV

# SIKU YA YEHOVA

"SIKU YA YEHOVA," "SIKU YA KISASI," "SIKU YA GHADHABU"—WAKATI WA TAABU KUU—CHANZO CHAKE—USHUHUDA WA BIBLIA KUIHUSU—MOTO NA DHORUBA YAKE, KUTETEMESHWA NA KUYEYUSHWA KWAKE, VINAONYESHWA KUWA NI VYA MFANO—USHUHUDA WA DAUDI—USHUHUDA WA MWANDISHI WA UFUNUO—HALI YA SASA NA MTAZAMO WA BAADAYE KAMA UNAVYOTAZAMWA NA PANDE ZINAZOPINGANA, WENYE MITAJI NA WAFANYAKAZI WA UJIRA—SULUHISHO AMBALO HALITAFANIKIWA—PAZIA LIMEINULIWA NA NURU KUINGIZWA SAWASAWA NA WAKATI ULIOWEKWA—UTHIBITISHO WA HILI—HALI YA WATAKATIFU WAKATI WA TAABU, NA MTAZAMO WAO SAHIHI KUELEKEA HIYO.

SIKU ya Yehova" ni jina la kipindi ambacho Ufalme wa Mungu, chini ya Kristo, utakuwa ukisimamishwa hatua kwa hatua hapa duniani, huku falme za ulimwengu huu zikipita na mamlaka ya Shetani pamoja na ushawishi wake juu ya wanadamu vikifungwa. Kila mahali inaelezewa kama siku ya giza yenye taabu kubwa, dhiki na fadhaa kwa wanadamu. Na haishangazi kwamba mapinduzi makubwa kiasi hiki, yanayohitaji mabadiliko makubwa, yatasababisha taabu. Mapinduzi madogo yamesababisha shida katika kila kizazi; na hili, ambalo ni kubwa zaidi kuliko mapinduzi yote yaliyotangulia, itakuwa … *kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa—naam, wala haitakuwako kamwe baada ya hayo*. (*Danel. 12:1; Mathayo. 24:21,22*)

Inaitwa "Siku ya Yehova" kwa sababu, ingawa Kristo atakuwepo katika siku hiyo ya taabu akisimamia mambo yote, akiwa na cheo na mamlaka ya kifalme kama mwakilishi wa Yehova, jukumu lake kuu halitakuwa la **Mfalme wa Amani** anayewabariki wote, Wakati huo, maoni na mifumo ya uongo na isiyo mikamilifu inapoanguka, mamlaka ya Mfalme mpya yatainuka, na hatimaye atatambuliwa na kukubaliwa na wote kama Mfalme wa wafalme. Hivyo ndivyo manabii wanavyoiwasilisha kazi ya kusimamisha utawala wa Kristo kama kazi ya Yehova:

*"Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako, na miisho ya dunia kuwa milki yako." (Zaburi. 2:8) "Na katika siku za wafalme hao, Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme." (Daniel. 2:44) Mzee wa Siku aliketi, na akaletwa mbele zake mmoja aliye mfano wa mwanadamu, naye akapewa mamlaka, ili falme zote zimtumikie na kumtii. (Daniel. 7:9,13,14,22,27) Zaidi ya hayo, kuna maelezo ya Paulo kwamba, Kristo atakapotimiza lengo la utawala wake, "ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye [Baba] ALI-YEWEKA VITU VYOTE CHINI YAKE." (1 Wakorinto. 15:28)*

Kipindi hiki kinaitwa "Siku ya Kisasi ya Mungu wetu," na "Siku ya Ghadhabu." (*Isaya. 61:2; 63:1-4; Zab. 110:5*) Lakini yeyote anayefikiria tu wazo la hasira, au kudhania kuwa ni uovu wa kimungu, anakosea sana. Mungu ameweka sheria fulani, ambazo anafanya kazi kulingana na hizo sheria, na wale ambao kwa sababu yoyote wanapingana na hizi, wanavuna adhabu au ghadhabu ya mwenendo wao wenyewe.

Ushauri wa Mungu kwa wanadamu umekataliwa kila mara, isipokuwa na wachache; na, kama tulivyoonyesha, aliwaruhusu waende njia zao wenyewe na kumwondoa yeye na mashauri yake mioyoni mwao. (*Rumi. 1:28*) Kisha akawaangazia kwa uangalifu maalum Ibrahimu na uzao wake, ambao walidai kutamani njia yake na utumishi wake. Ugumu wa mioyo yao kama taifa, na ukosefu wao wa unyoofu kwa Mungu, haukuwazuia tu kumpokea Masihi, bali pia uliwaandaa na kuwaingiza katika ile taabu iliyokomesha uwepo wao kama taifa.

Na hivyo nuru iliyoletwa ulimwenguni katika kipindi cha Injili na Kanisa la kweli la Kristo (kundi ambalo majina yao yameandikwa mbinguni) imetoa ushahidi kwa ulimwengu uliostaarabika kuhusu tofauti kati ya lililo sahihi na lisilo sahihi, jema na baya, na kuhusu wakati ujao ambapo moja litalipwa na lingine kuadhibiwa. (*Yohana. 16:8-11; Matendo. 24:25*) Hili lingekuwa na ushawishi mkubwa kwa watu kama wangeyazingatia maagizo ya Bwana, lakini, wakiwa wakaidi kama kawaida, hawakunufaika sana na ushauri wa Maandiko, na taabu ya Siku ya Bwana itakuja kama matokeo ya kupuuza. Tena, inaweza

kusemwa kuwa ni ghadhabu ya Mungu kwa kuwa inakuja kwa sababu ya kudharau mashauri yake, na kama thawabu ya uasi. Hata hivyo, likitazamwa kwa upande mwingine, taabu inayokuja ulimwenguni ni matokeo ya asili au halali ya dhambi, ambayo Mungu aliiona tangu mwanzo, na ambayo mashauri yake yangewalinda dhidi yake, kama wangeyafuata.

Wakati ujumbe wa Mungu kwa Kanisa umekuwa, "*itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai*" (*Rumi. 12:1*), ujumbe wake kwa ulimwengu umekuwa, " *Uuzuie ulimi wako na mabaya, Na midomo yako na kusema hila. Uache mabaya ukatende mema, Utafute amani ukaifuatie..*" (*Zaburi. 34:13,14*) Ni wachache waliosikiliza ujumbe wowote kati ya hiyo. Ni kundi dogo tu lililojitoa dhabihu; na kwa upande wa ulimwengu, ingawa uliweka kauli mbiu, "**Uaminifu ndiyo sera bora zaidi**," kwa ujumla umepuuza kuitenda. Badala yake, ulisikiliza sauti ya tamaa—pata utajiri, heshima na mamlaka yote uwezayo katika ulimwengu huu, haijalishi ni kwa njia gani unayapata, na haijalishi ni nani anayepoteza kwa faida yako. Kwa neno moja, taabu ya hii Siku ya Bwana isingekuja, isingeweza kuja, kama kanuni za sheria ya Mungu zingezingatiwa kwa kiwango chochote kile. Sheria hiyo kwa muhtasari ni—*Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na jirani yako kama nafsi yako*. (*Mathayo. 22:37-39*) Ni kwa sababu akili ya mwili iliyopotoka inapingana na sheria hii ya Mungu, na haitii, ndiyo maana, kama matokeo ya asili, taabu itakuja, kama kuvuna baada ya kupanda.

Akili ya kimwili au iliyopotoka, badala ya kumpenda jirani kama nafsi yake, daima imekuwa ya ubinafsi na tamaa—mara nyingi ikiongoza hata kwenye vurugu na mauaji ili kujipatia vitu vinavyomilikiwa na wengine. Hata iwe inatekelezwa vipi, kanuni ya ubinafsi daima ni ileile, isipokuwa tu inapoongozwa na mazingira ya kuzaliwa, elimu na mazingira. Imekuwa hivyo katika kila enzi ya ulimwengu, na itaendelea kuwa hivyo, hadi, kwa nguvu ya utawala wa chuma wa Masihi, si nguvu wala tamaa, bali upendo, utakapoamua lililo HAKI, na kulitekeleza, hadi wote

wapate fursa ya kujifunza faida kuu za utawala wa haki na upendo ukilinganishwa na ule wa ubinafsi na nguvu; hadi, chini ya ushawishi wa mwanga wa jua la ukweli na haki, moyo wa ubinafsi, moyo wa jiwe wa mwanadamu utakapokuwa tena kama Mungu alivyoutamka kuwa "mzuri sana"—moyo wa nyama. *Ezekieli. 36:26*

Tukitazama nyuma, tunaweza kuona bila ugumu jinsi badiliko kutoka katika upendo na wema kama wa Mungu kwenda kwenye ubinafsi mgumu lilivyotokea. Mazingira yenye kuelekea kuchochea ubinafsi yalianza mara tu mwanadamu, kupitia kutotii, alipopoteza kibali cha Mungu na kufukuzwa kutoka makao yake ya Edeni, ambapo kila hitaji lake lilikuwa limetimizwa kwa ukarimu. Wazazi wetu waliohukumiwa walipoondoka na kuanza vita ya maisha, wakijaribu kuongeza muda wa kuishi hadi kikomo chake, walikutana mara moja na miiba na mbigili na ardhi isiyo na rutuba; na kupambana na hivi kulileta uchovu na jasho la uso ambalo Bwana alikuwa ametangaza.

Hatua kwa hatua sifa za kiakili na kimaadili zilianza kudumaa kwa kukosa mazoezi, huku sifa za chini zikibaki na wigo mpana zaidi kutokana na mazoezi ya kila mara. Chakula kilikuwa lengo kuu na shauku ya maisha; na gharama yake katika kazi ikawa kipimo ambacho maslahi mengine yote yalipimwa, na Mali (Mammon) akawa bwana wa wanadamu. Je, tunaweza kushangaa kwamba chini ya hali kama hizi wanadamu wakawa wabinafsi, wenye tamaa na walafi, kila mmoja akijitahidi kupata zaidi—kwanza mahitaji ya lazima, na pili heshima na anasa zinazotolewa na Mali? Ni mwelekeo wa asili tu ambao Shetani ameutumia sana.

Katika enzi zilizopita, chini ya vishawishi mbalimbali (miongoni mwa vingine, ujinga, chuki za kikabila, na kiburi cha kitaifa), utajiri mwingi wa ulimwengu kwa ujumla umekuwa mikononi mwa wachache—watawala—ambao umati uliwatumikia kwa utii wa utumwa kama wawakilishi wao wa kitaifa, ambao katika utajiri wao walihisi fahari na maslahi kama ni yao wenyewe

kama wawakilishi. Lakini wakati ulipokaribia ambapo Yehova alipanga kuubariki ulimwengu kupitia Urejesho mikononi mwa Masihi, alianza kuinua pazia la ujinga na ushirikina, kupitia vifaa na uvumbuzi wa kisasa; na pamoja na haya kukaja kuinuliwa kwa jumla kwa watu na kupungua kwa mamlaka ya watawala wa kidunia. Utajiri wa ulimwengu haupo tena mikononi mwa wafalme wake, bali hasa miongoni mwa watu.

Ingawa utajiri huleta maovu mengi, pia huleta baraka kadhaa: matajiri hupata elimu bora—lakini hivyo wanainuliwa kiakili juu ya watu maskini na kwa kiasi fulani wanashirikiana na watu wa vyeo vya juu. Kwa hiyo, kunatokea tabaka la juu ambalo lina pesa na elimu ya kuliunga mkono, na kusaidia katika mapambano yake ya tamaa ya kupata kila liwezalo na kujiweka mstari wa mbele kwa gharama yoyote.

Lakini, kadiri akili inavyoenea, watu wanapotumia fursa za elimu, ambazo sasa ni nyingi, wanaanza kufikiri wenyewe; na kwa kujiheshimu na ubinafsi ulio ndani yao ukichochewa na elimu kidogo—ambayo wakati mwingine ni kitu cha hatari—wanawaza kuwa wanaona njia na mbinu ambazo maslahi na hali za watu wote, na hasa zao wenyewe, zinaweza kuendelezwa kwa gharama ya idadi ndogo ya watu ambao utajiri sasa uko mikononi mwao.

Wengi wa hawa, bila shaka, wanaamini kwa unyoofu kwamba maslahi yanayopingana ya waabudu Mali (wao wenyewe upande mmoja, na matajiri upande mwingine) yangeweza kurekebishwa kwa urahisi na kwa haki; na bila shaka wanahisi kwamba kama wangekuwa matajiri wangekuwa wakarimu sana, na tayari kabisa kuwapenda majirani zao kama nafsi zao. Lakini ni wazi wanajidanganya wenyewe; kwani katika hali yao ya sasa ni wachache sana wanaoonyesha roho kama hiyo, na yeye ambaye hangekuwa mwaminifu katika matumizi ya mali kidogo ya ulimwengu huu hangekuwa mwaminifu kama angekuwa na utajiri mkubwa zaidi. Kwa kweli, hali zinathibitisha hili; kwani baadhi ya watu wenye mioyo migumu na wabinafsi

zaidi miongoni mwa matajiri ni wale ambao wameinuka ghafla kutoka katika maisha ya hali ya chini.

Kinyume chake, ingawa hatutetei bali tunakemea tamaa na ubinafsi wa kuchukua kwa nguvu kwa upande wa matabaka yote, inafaa kutambua kwamba huduma zinazotolewa kwa wagonjwa, wasiojiweza na maskini, kwa njia ya hifadhi, hospitali, nyumba za maskini, maktaba za umma, shule na shughuli nyingine mbalimbali kwa ajili ya manufaa na faraja ya watu, badala ya matajiri, zinagharamiwa hasa na kodi na michango kutoka kwa matajiri. Taasisi hizi karibu kila mara zinatokana na watu wenye mioyo ya fadhili na wakarimu miongoni mwa matajiri, na ni mambo ambayo watu wa tabaka la chini hawana muda, wala kwa ujumla elimu au shauku inayohitajika, ili kuyaendesha kwa mafanikio.

Hata hivyo, leo tunaona upinzani unaokua kati ya tabaka la matajiri na la wafanyakazi—uchungu unaoongezeka kwa upande wa wafanyakazi, na hisia inayokua miongoni mwa matajiri kwamba hakuna kitu isipokuwa mkono wenye nguvu wa sheria utakaolinda kile wanachoamini kuwa ni haki zao. Kwa hiyo, matajiri wanavutiwa zaidi na serikali; na umati wa wafanyakazi, ukianza kufikiri kwamba sheria na serikali ziliundwa kuwasaidia matajiri na kuwakandamiza maskini, unavutiwa na Ukomunisti na Anarkia (uvurugaji), wakifikiri kwamba maslahi yao yangehudumiwa vizuri zaidi kwa njia hiyo, bila kutambua kwamba serikali mbaya zaidi, na yenye gharama kubwa zaidi, ni bora kuliko kutokuwa na serikali kabisa.

Maandiko mengi yanaonyesha wazi kwamba hii ndiyo itakuwa tabia ya ile taabu ambayo chini yake mifumo ya sasa ya kiraia, kijamii na kidini itapita; kwamba hii ndiyo njia ambayo ongezeko la maarifa na uhuru litaleta matokeo, kwa sababu ya kutokamilika kwa mwanadamu, kiakili, kimaadili na kimwili. Maandiko haya yatarejelewa wakati wake; lakini hapa tunaweza tu kutaja machache kati ya mengi, huku tukiwashauri wasomaji wetu kwamba katika unabii mwingi wa Agano la Kale ambapo

Misri, Babeli na Israeli vinatajwa sana, hakukukusudiwa tu utimilifu wa kiuhalisia, bali pia utimilifu wa pili ulio mkubwa zaidi.

Kwa mfano, utabiri kuhusu anguko la Babeli, n.k., lazima uonekane kama uliotiwa chumvi kupita kiasi, kama hatutatambua Babeli ya mfano na ya mfano mkuu pamoja na Babeli halisi. Kitabu cha Ufunuo kina utabiri ulioandikwa muda mrefu baada ya Babeli halisi kuwa magofu, na hivyo ni wazi unatumika tu kwa Babeli ya mfano; lakini kufanana kwa karibu kwa maneno ya manabii, ambayo yanaonekana kuelekezwa moja kwa moja kwa Babeli halisi, kunaonyesha kuwa yanahusu kwa maana maalumu  Babeli ya mfano. Katika utimilifu huu mkubwa zaidi, Misri inawakilisha ulimwengu; Babeli inawakilisha Kanisa la jina tu, liitwalo Jumuiya ya Wakristo; wakati, kama ilivyoonyeshwa tayari, Israeli mara nyingi inawakilisha ulimwengu wote katika hali yake ya kuhesabiwa haki, kama itakavyokuwa—Ukuhani wake wa Kifalme mtukufu, Walawi wake watakatifu na watu wake wanaoamini na kuabudu, waliohesabiwa haki kwa dhabihu ya Upatanisho, na kuletwa katika hali ya upatanisho na Mungu. Kwa Israeli baraka zimeahidiwa, kwa Misri mapigo, na kwa Babeli imara kupinduliwa kwa ajabu, kamili na kwa milele, "*kama jiwe la kusagia kubwa, akalitupa katika bahari*" (*Ufu. 18:21*), hautarejeshwa tena kamwe, bali utabaki katika dharau ya milele..

Mtume Yakobo anaelezea siku hii ya taabu, na anasema kuwa itakuwa ni matokeo ya tofauti kati ya wenye mitaji na wafanyakazi. Anasema:

> *"Haya basi, enyi matajiri! Lieni, mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia. Mali zenu zimeoza, na mavazi yenu yameliwa na nondo. Dhahabu yenu na fedha yenu zimeingia kutu, na kutu yake itawashuhudia, nayo itakula miili yenu kama moto. Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho. Angalieni, ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu, ninyi mliouzuia kwa hila, unapiga kelele, na vilio vyao waliovuna vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi." (Yak. 5:1-4)*

Anaongeza kuwa tabaka hilo linaloingia kwenye taabu limezoea anasa, iliyopatikana kwa kiasi kikubwa kwa gharama ya wengine, ambao miongoni mwao walikuwamo baadhi ya wenye haki, na kutoka kwa hao, kwa sababu hawakushindana nao, uhai wenyewe ulikuwa umekandamizwa.

Mtume anawahimiza "ndugu" kustahimili kwa subira sehemu yoyote watakayokuwa nayo, wakitazama mbele, na kutarajia ukombozi kupitia Bwana. Hali hii ya mambo sasa inaweza kuonekana ikikaribia; na ulimwenguni, miongoni mwa walio macho, "mioyo ya watu inawazimia kwa kutazamia mambo yatakayokuja duniani." Wote wanajua kwamba mwelekeo wa nyakati zetu ni kuelekea mishahara ya chini kwa wafanyakazi, isipokuwa pale ambapo bei zinashikiliwa au kupandishwa kwa njia isiyo ya asili na vyama vya wafanyakazi, migomo, n.k.; na kwa hisia za sasa za umati, wote wanaweza kuona kwamba ni suala la muda tu kabla ya kufikia kiwango cha chini kabisa cha uvumilivu, na uasi hakika utatokea.

Hili litatisha mitaji, ambayo itaondolewa kwenye biashara na njia za uzalishaji na kufichwa kwenye vyumba vya usalama na hazina, ili ijimalize yenyewe kwa gharama za ulinzi wake katika uvivu, kwa kero kubwa kwa wamiliki wake. Hili nalo hakika litazalisha kufilisika, mshtuko wa kifedha na kudorora kwa biashara, kwa sababu biashara zote kubwa sasa zinaendeshwa kwa kiasi kikubwa kwa mikopo. Matokeo ya asili ya yote haya yatakuwa ni kuwatupa nje ya ajira makumi ya maelfu wanaotegemea mishahara yao kwa mkate wa kila siku, na kuujaza ulimwengu na watu wasio na makazi na watu ambao mahitaji yao yatakiuka sheria zote.

Ndipo itakuwa kama ilivyoelezwa na nabii (*Ezekieli. 7:10-19*), wakati mnunuzi hatahitaji kufurahi, wala muuzaji kuomboleza; kwani taabu itakuwa juu ya umati wote na hakutakuwa na usalama wa mali. Ndipo mikono yote itakuwa dhaifu na isiyo na msaada ili kuepusha taabu. Watatupa fedha zao mitaani, na

dhahabu yao itaondolewa. Fedha yao na dhahabu yao havitaweza kuwaokoa katika siku ya ghadhabu ya Bwana.

Isisahaulike kwamba ingawa miaka arobaini ya mwisho ya Israeli kama taifa ilikuwa siku ya taabu, "siku ya kisasi" juu ya watu hao, iliyoishia katika kupinduliwa kabisa kwa taifa lao, bado siku yao ya ghadhabu ilikuwa kivuli tu au mfano wa taabu kubwa zaidi na pana zaidi juu ya Jumuiya ya Wakristo ya jina tu, kama vile historia yao ya zamani kama taifa wakati wa kipindi chao cha upendeleo ilivyokuwa mfano wa Enzi ya Injili, kama itakavyoonyeshwa kwa uthibitisho baadaye. Ndipo wote wataona kwa nini unabii huu kuhusu Siku ya Bwana ulipaswa, na unaelekezwa, kwa Israeli na Yerusalemu kwa kiasi fulani moja kwa moja, ingawa muktadha unaonyesha wazi kwamba wanadamu wote wamejumuishwa katika utimilifu kamili.

Chukua ushuhuda mwingine wa kinabii

> *(Sefania. 1:7-9,14-18). "kwa maana siku ya Bwana i karibu; Kwa kuwa Bwana ameweka tayari dhabihu, Amewatakasa wageni wake(Linganisha na Ufunuo 19:7). Na itakuwa, katika siku ile ya dhabihu ya Bwana, nitawaadhibu wakuu, na wana wa mfalme, na watu wote waliovaa mavazi ya kigeni. Na katika siku ile nitawaadhibu hao wote warukao juu ya kizingiti, waijazao nyumba ya bwana wao udhalimu na udanganyifu. ."*

[Hii inaonyesha kwamba sio tu kutakuwa na **anguko kuu** la mali na mamlaka katika kipindi hiki cha taabu, bali pia wale watakaotumika kama vyombo vya mbinguni katika kubomoa mifumo iliyopo sasa wataadhibiwa kwa mwenendo wao usio wa haki na usio sahihi; kwa maana, taabu inayokuja itahusisha matabaka yote, na kuleta dhiki kwa umati wote.]

> *" Hiyo siku ya Bwana iliyo kuu i karibu; I karibu, nayo inafanya haraka sana; Naam, sauti ya siku ya Bwana; Shujaa hulia kwa uchungu mwingi huko! Siku ile ni siku ya ghadhabu, Siku ya fadhaa na dhiki, Siku ya uharibifu na ukiwa, Siku ya giza na utusitusi, [kutokuwa na uhakika na wasiwasi, pamoja na dhiki ya sasa], siku ya mawingu [taabu] na giza la tufani, siku ya tarumbeta [tarumbeta ya saba ya mfano, ambayo inalia katika siku hii yote ya taabu – pia inaitwa*

*tarumbeta ya Mungu, kwa sababu inahusiana na matukio ya Siku hii ya Bwana] na kelele dhidi ya miji yenye maboma na ngome za juu [shutuma zenye kelele na zinazokinzana dhidi ya serikali imara na zilizojihami vizuri]. Nami nitawaletea wanadamu dhiki, nao watatembea kama vipofu [wakipapasa gizani bila kujua njia ya kufuata], kwa sababu wamemtenda Bwana dhambi. Damu yao itamwagwa kama mavumbi, na nyama yao kama mavi. Fedha yao wala dhahabu yao haitaweza kuwaokoa katika siku ya ghadhabu ya Bwana [ingawa hapo awali utajiri ungeweza kutoa raha na kila anasa], lakini nchi yote itateketezwa kwa MOTO wa wivu wake; kwa maana atawakomesha, naam, ghafula sana, wote [matajiri] wakaao katika nchi."*

Uharibifu huu utawaangamiza matajiri wengi kwa maana kwamba watakoma kuwa matajiri, ingawa bila shaka utahusisha pia kupotea kwa maisha ya wengi wa matabaka yote.

Hatutajaribu kuwafuata manabii katika maelezo yao ya kina, kutoka pande mbalimbali, kuhusu taabu ya siku hiyo, bali tutafuata kwa ufupi wazo lililotajwa mwisho na nabii hapo juu, yaani, kuteketezwa kwa dunia yote kwa MOTO wa wivu wa Mungu. Nabii huyu anataja moto huo tena (*Sefania. 3:8,9*), akisema: "*Ngojeni, asema Yehova, hata siku ile nitakaposimama kuteka; maana nia yangu ni kuyakusanya mataifa, na kuwakutanisha wafalme; ili kuwamwagia [wafalme] ghadhabu yangu, naam, ukali wote wa hasira yangu.*" [Kukusanyika kwa watu wa mataifa yote kwa maslahi ya pamoja kupinga serikali za sasa kunaongezeka; na matokeo yatakuwa ni kuungana kwa falme kwa ajili ya usalama wa pamoja, ili taabu iwe juu ya falme zote, na zote zitaanguka.] "*Kwa maana dunia yote itateketezwa kwa moto wa wivu wangu. Naam [basi, baada ya uharibifu huu wa falme, baada ya uharibifu huu wa utaratibu wa sasa wa kijamii katika moto wa taabu], ndipo nitakapowarudishia watu lugha iliyo safi [Neno safi – lisilochafuliwa na mapokeo ya wanadamu], wapate kuliitia jina la Bwana, wamtumikie kwa nia moja.*"

Moto huu wa wivu wa Mungu ni ishara, na ni ishara yenye nguvu, inayowakilisha ukubwa wa taabu na uharibifu utakaofunika dunia yote. Kwamba si moto halisi, kama wengine wanavyodhania, ni dhahiri kutokana na ukweli kwamba watu

wanabaki baada yake, na wanabarikiwa. Kwamba watu wanaobaki si watakatifu, kama wengine wanavyoweza kupendekeza, ni dhahiri kutokana na ukweli kwamba ndipo wanapogeuzwa kumtumikia Bwana, ambapo watakatifu tayari wamegeuzwa (wameongoka).*

Kote katika Maandiko, neno **dunia**, linapotumiwa kama lugha ya ishara, linawakilisha jamii; **milima** inawakilisha falme; **mbingu,** mamlaka za utawala wa kiroho; **bahari**, umati wa watu wasiotulia, wenye misukosuko, na wasioridhika duniani. **Moto** unawakilisha uharibifu wa chochote kinachoteketezwa—magugu, takataka, dunia (mfumo wa jamii), au chochote kile. Na **kiberiti** kinapoongezwa kwenye **moto** katika ishara hiyo, kinaongeza uzito wa wazo la uharibifu; kwani hakuna kitu chenye kuua zaidi kwa aina zote za uhai kuliko moshi wa salfa.

Tukiwa na wazo hili akilini, tukigeukia unabii wa ishara wa Petro kuhusu Siku ya Ghadhabu, tunaukuta unapatana kikamilifu na ushuhuda wa manabii hapo juu. Anasema: *Dunia ile ya wakati ule, ilipogharikishwa na maji, iliangamia.* [Si kwamba dunia halisi na mbingu halisi zilikoma hapo, bali ule utaratibu au mpangilio wa mambo, uliokuwapo kabla ya gharika, ulipita.] *Lakini mbingu na dunia ambazo zipo sasa [huu utaratibu wa sasa] kwa neno lilo hilo [la mamlaka ya kimungu] zimewekwa akiba, zikitunzwa kwa ajili ya moto.*

---

* *Tunalitaja hili ili kupinga hoja ya wengine wanaouona moto huo kuwa halisi, na wanaodai kwamba dunia halisi itayeyushwa, n.k. Hawa, ili kutosheleza nadharia yao, wanadai kwamba "watu," waliotajwa hapa, ni watakatifu, ambao, baada ya dunia kuyeyuka na kupoa, watarudi duniani na kujenga nyumba na kukaa ndani yake, kupanda mizabibu na kula matunda yake, na kufurahia kazi ya mikono yao kwa muda mrefu. Wanaiona miaka michache ya sasa kama mafunzo au maandalizi ya kurithi, na wanasahau kwamba mafunzo hayo yangeotea kabisa katika uzoefu wa angani wa miaka elfu moja au zaidi ya kusubiri dunia ipoe—kulingana na nadharia yao. Hili ni kosa kubwa, na linatokana na tafsiri ya moja kwa moja kupita kiasi ya mafumbo, mithali, alama na maneno ya fumbo ya Bwana wetu na mitume na manabii. Wakiendeleza kosa hilohilo, hawa wanadai kwamba hakutakuwa na milima wala bahari baada ya moto huu, wakishindwa kuona kwamba vyote hivi, pamoja na moto, ni alama.*

Ukweli kwamba maji yalikuwa halisi unawafanya wengine waamini kwamba moto nao lazima uwe halisi, lakini hii sivyo ilivyo. Hekalu la Mungu hapo zamani lilikuwa la mawe halisi, lakini hilo haliondoi ukweli kwamba Kanisa, ambalo ndilo hekalu la kweli, linajengwa kama jengo la kiroho, hekalu takatifu, si la vifaa vya kidunia. Safina ya Nuhu nayo ilikuwa halisi, lakini ilikuwa mfano wa Kristo na nguvu iliyo ndani yake itakayoijaza tena na kuipanga upya jamii.

> "*Siku ya Bwana itakuja kama mwivi usiku [bila kutazamiwa], ambayo katika hiyo mbingu [mamlaka ya sasa ya angani, ambayo Shetani ndiye mkuu au mfalme wake] zitatoweka kwa mshindo mkuu [wa kuvuma], na viumbe vya asili vitateketea [maandishi mengine yanasema vitafumuliwa] kwa moto mkuu; na dunia [mfumo wa jamii] pamoja na kazi zilizomo ndani yake [kiburi, vyeo, tabaka la juu, ufalme], zitateketea. Mbingu zikiwaka moto, zitayeyushwa, na viumbe vya asili vitateketea kwa moto mkuu. Lakini sisi, kwa kulingana na ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya [mamlaka mapya ya kiroho – ufalme wa Kristo] na nchi mpya" [jamii ya kidunia iliyopangwa kwa msingi mpya – kwa msingi wa upendo na haki, badala ya nguvu na ukandamizaji]. 2 Petro 3:6,7,10-13*

Ikumbukwe kwamba baadhi ya mitume walikuwa manabii pia—hasa Petro, Yohana na Paulo. Na ingawa kama mitume walikuwa vinywa vya Mungu vya kufafanua maneno ya manabii waliotangulia kwa manufaa ya Kanisa, walitumiwa pia na Mungu kama manabii kutabiri mambo yajayo, ambayo, yanapofikia wakati wa kutimizwa, yanakuwa chakula kwa wakati wake kwa ajili ya nyumba ya imani, ambacho, ili kukigawa, Mungu kwa wakati wake mwenyewe huinua watumishi au wafafanuzi wanaofaa. (Tazama maelezo ya Bwana wetu kuhusu ukweli huu—*Mathayo. 24:45,46*.)

Mitume kama manabii waliongozwa kuandika mambo ambayo, kwa kuwa hayakupaswa kutimia katika siku zao, waliweza tu kuyaelewa kwa sehemu, kama ilivyokuwa kwa manabii wa Agano la Kale (*1 Petro. 1:12,13*), ingawa, kama wao, maneno yao yaliongozwa kwa namna ya pekee ili yawe na maana ya kina

ambayo hawakuijua walipokuwa wakiyatumia. Hivyo kwa msisitizo, Kanisa daima linaongozwa na kulishwa na Mungu Mwenyewe, bila kujali ni nani vinywa vyake au njia zake za mawasiliano. Kutambua hili lazima kupelekee kuwa na imani na tumaini kubwa zaidi katika Neno la Mungu, licha ya kutokamilika kwa baadhi ya vinywa vyake.

Nabii *Malaki (4:1)* anaizungumzia Siku hii ya Bwana kwa kutumia ishara hiyohiyo. Anasema: "*Siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na wote wenye kiburi, naam, wote watendao uovu, watakuwa kama mabua; na siku ile inayokuja itawateketeza...hata haiwaachii shina wala tawi.*"

Kiburi, na kila sababu nyingine ambayo kutoka kwayo majivuno na ukandamizaji vinaweza kuchipuka tena, vitateketezwa kabisa na taabu kubwa ya Siku ya Bwana  na nidhamu za baadaye za zama ya Milenia—ambayo ya mwisho inaelezwa katika *Ufunuo. 20:9*.

Lakini, ingawa kiburi (katika aina zake zote ni dhambi na cha kuchukiza) kitang'olewa kabisa, na wote wenye kiburi na waovu wataangamizwa kabisa, haimaanishi kwamba hakuna tumaini la mabadiliko katika kundi hili. La, asante Mungu: wakati moto huu wa hasira ya haki ya Mungu utakapokuwa unawaka, Mwamuzi atatoa fursa ya *kuwanyakua wengine katika moto unaoteketeza* (*Yuda 23*); na ni wale tu wanaokataa msaada ndio watakaoangamia na kiburi chao; kwa sababu wamekifanya kuwa sehemu ya tabia zao, na wanakataa kubadilika.

Nabii huyohuyo anatoa maelezo mengine ya siku hii (*Malaki. 3:1-3*), ambapo tena, chini ya mfano wa moto, anaonyesha jinsi watoto wa Bwana watakavyotakaswa na kubarikiwa na kuletwa karibu naye kwa kuondolewa takataka za makosa.

> "*.. naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema Bwana wa majeshi.Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja kwake? Au ni nani atakayesimama[Jaribio] atakapoonekana yeye? Kwa maana yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha, ni mfano wa sabuni ya mtu afuaye nguo; naye ataketi kama asafishaye fedha na*

*kuitakasa, naye atawatakasa wana wa Lawi[mfano wa waumini, ambao waku wao ni Ukuhani wa Kifalme], atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea Bwana dhabihu katika haki."*

Paulo anautaja moto huuhuu, na mchakato huu wa kusafisha unaowaathiri waumini katika Siku ya Bwana (*1 Wakorinto. 3:12-15*), na kwa namna ambayo haiachi shaka yoyote kwamba moto wa mfano **utaharibu** kila kosa, na hivyo kuleta utakaso wa imani. Baada ya kutangaza kwamba anawazungumzia tu wale wanaojenga imani yao **juu** ya msingi pekee unaotambuliwa, kazi ya ukombozi iliyokamilishwa ya Kristo Yesu, anasema:

*"Lakini kama mtu akijenga[tabia] juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani[kweli za kimungu na tabia inayolingana nazo], au miti au majani au manyasi[makosa ya kimapokeo na tabia zisizo imara zinazolingana], kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani.[1 Wakorintho. 1:5-11]*

Hakika hata mtu mwenye chuki kali zaidi atakubali kwamba moto unaojaribu kazi ya kiroho si moto halisi; moto ni ishara inayofaa kuwakilisha uharibifu kamili wa hali zinazowakilishwa hapa na miti, majani na mabua. Moto huu hautakuwa na nguvu ya kuharibu muundo wa imani na tabia uliojengwa kwa dhahabu, fedha na mawe ya thamani ya kweli ya kimungu, na uliowekwa juu ya mwamba wa dhabihu ya fidia ya Kristo.

Mtume anaonyesha hili, akisema: "*Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake [juu ya Kristo] ikikaa, atapata thawabu.*" [Thawabu yake itakuwa kulingana na uaminifu wake katika kujenga, akitumia ukweli katika kukuza tabia ya kweli—akivaa silaha zote za Mungu.] "*Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara [hasara ya thawabu, kwa sababu ya kutokuwa mwaminifu], ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto*"—akiungua, kuunguzwa na kushtushwa. Wote wanaojenga juu ya msingi wa mwamba wa fidia ya Kristo wako salama: hakuna anayetegemea haki yake kama kifuniko chake atakayeaibishwa kabisa. Lakini wale wanaomkataa yeye na kazi yake kwa makusudi, baada ya kufikia ujuzi wa wazi na kamili

juu yake, watakuwa chini ya mauti ya pili. *Waebrania. 6:4-8; 10:26-31*

Kwa njia nyingine tena taabu hii ya Siku ya Bwana inaelezwa kwa ishara. Mtume anaonyesha (*Waebrania. 12:26-29*) kwamba uzinduzi wa Agano la Sheria huko Sinai ulikuwa mfano wa kuanzishwa kwa Agano Jipya ulimwenguni mwanzoni mwa zama ya Milenia, au utawala wa ufalme wa Kristo. Anasema kwamba katika mfano huo sauti ya Mungu iliitetemesha dunia halisi, lakini sasa ameahidi, akisema,

> *ambaye sauti yake iliitetemesha nchi wakati ule; lakini sasa ameahidi akisema, Mara moja[Mwisho] tena nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia. Kuhusu hili Mtume anafafanua, akisema, Lakini neno lile, Mara moja tena, ladhihirisha kuhamishwa vile viwezavyo kutetemeshwa[vya uongo, vimetungwa, si vya kweli], kama vitu vilivyoumbwa, vitu visivyoweza kutetemeshwa[vya kweli, vya haki, pekee] vikae. Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho; maana[kama ilivyoandikwa] Mungu wetu ni moto ulao.*

Hivyo tunaona mtume huyu anatumia dhoruba kuashiria taabu ya Siku hii ya Bwana, ambayo yeye na wengine mahali pengine wanaitaja chini ya ishara ya moto. Matukio yaleyale yametajwa hapa kama yale yaliyoelezwa chini ya ishara ya moto, yaani, kuondolewa kwa uongo wote, kutoka kwa waumini na kutoka kwa ulimwengu—makosa kuhusu mpango na tabia na Neno la Mungu, na pia makosa kuhusu mambo ya kijamii na kiraia ulimwenguni. Itakuwa vizuri kweli kwa wote kuondolewa vitu hivi vya kutungwa, vilivyomjia mwanadamu kwa kiasi kikubwa kupitia tamaa zake mwenyewe zilizopotoka, pamoja na ufundi wa hila wa Shetani, adui mjanja wa haki; lakini itakuwa kwa gharama kubwa kwa wote wanaohusika kwamba vitaondolewa. Utakuwa ni moto mkali sana, dhoruba ya kutisha, usiku wa giza wa taabu, ambao utatangulia mwangaza mtukufu wa Ufalme ule wa Haki ambao hauwezi kamwe kutikiswa, siku ile ya Milenia ambapo Jua la Haki litang'aa kwa utukufu na nguvu, likibariki

na kuponya ulimwengu mgonjwa na unaokufa lakini uliokombolewa. Linganisha *Malaki. 4:2* na *Mathayo. 13:43*.

Daudi, nabii ambaye kupitia Zaburi zake Mungu alipendezwa kutabiri mengi kumhusu Bwana wetu katika ujio wake wa kwanza, anatoa maelezo ya wazi ya Siku hii ya Taabu ambayo kwayo utawala wake mtukufu utaanzishwa; naye anatumia ishara hizi mbalimbali—moto, dhoruba na giza—kwa kubadilishana katika maelezo yake. Kwa mfano, anasema ;

> *(Zab. 50:3): " Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, Moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote.." Katika Zab. 97:2-6: " Mawingu na giza vyamzunguka, Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chake.Moto hutangulia mbele zake, Nao huwateketeza watesi wake pande zote.Umeme wake uliuangaza ulimwengu, Nchi ikaona ikatetemeka. Milima iliyeyuka kama nta mbele za Bwana, Mbele za Bwana wa dunia yote. Mbingu[mpya][basi] zimetangaza haki yake, Na watu wote wameuona utukufu wake." Zab. 46:6: " ataifa yalighadhibika, falme zikataharuki; Alitoa sauti yake, nchi ikayeyuka." Tena (Zab. 110:2-6), "Tawala wewe kati ya adui zako....Bwana aliyeko mkono wako wa kuume atawaponda wafalme siku ya ghadhabu yake. Atahukumu kati ya mataifa—kutakuwa na wingi wa maiti. Anawaponda wakuu [watawala] juu ya nchi nyingi." Tena (46:1-5), " Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi[jamii], Ijapotetemeka milima[falme] moyoni mwa bahari[ikimezwa na umati wenye misukosuko].Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake. Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu, Patakatifu pa maskani zake Aliye juu. Mungu yu katikati yake hautatetemeshwa; Mungu atausaidia[bibi Harusi, waaminifu, Kundi dogo] asubuhi na mapema." Na katika Zaburi hiyohiyo, mistari 6-10, hadithi hiyohiyo inarudiwa kwa ishara nyingine: "Mataifa yakaona, falme zikayeyushwa; alitoa sauti yake, dunia [jamii] ikayeyuka. Bwana wa majeshi yu pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni ngome yetu." Kisha, akitazama matokeo ya wakati huo wa taabu kutoka upande wa pili, anaongeza: "Njoni, yatazameni matendo ya Bwana, jinsi alivyofanya ukiwa katika nchi....Acheni [njia zenu za zamani, enyi watu] na mjue [fahamuni] ya kuwa mimi ni Mungu. Nitakuzwa katika mataifa, nitakuzwa*

*duniani." "Dunia mpya" au utaratibu mpya wa jamii utamtukuza Mungu na sheria yake, vikiwa juu na vikidhibiti yote.*

Ushahidi mwingine wa kuthibitisha ukweli kwamba Siku ya Bwana itakuwa siku kuu ya taabu na ya uharibifu kwa kila aina ya uovu (lakini si wakati wa kuteketezwa dunia yenyewe) unatolewa katika unabii wa mwisho wa mfano wa Biblia. Ikirejelea wakati huu ambapo Bwana atachukua uweza wake mkuu kutawala, dhoruba na moto vinaelezwa hivi—

*"Na mataifa walikasirika, hasira yako nayo ikaja." (Ufunuo. 11:17,18) Na tena, "Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi. Kisha nikamwona huyo mnyama[wa mfano], , na wafalme wa nchi, na majeshi yao, wamekutana kufanya vita na yeye aketiye juu ya farasi yule, tena na majeshi yake"Ufunuo 19:15,19*

atuwezi hapa kutoka nje ya mada ili kuchunguza mifano hii—"mnyama," "nabii wa uongo," "sanamu," "ziwa la moto," "farasi," n.k., n.k. Kwa hili msomaji anaelekezwa kwenye kitabu kitakachofuata. Sasa tungependa utambue kwamba VITA vikuu vya mfano, na mavuno ya mzabibu wa nchi yaliyoelezwa hapa kama yanamaliza zama ya sasa na kufungua zama ya Milenia (*Ufu. 20:1-3*), ni ishara nyingine tu zinazofunika matukio yaleyale makuu na ya taabu ambayo mahali pengine yameitwa kwa ishara moto, dhoruba, mtikisiko, n.k. Kuhusiana na mifano ya vita na shinikizo la mvinyo la Ufunuo, ona upatano wa ajabu wa *Yoeli 2:9-16* na *Isaya. 13:1-11*, katika kuelezea matukio yaleyale kwa mifano inayofanana. Aina mbalimbali za mifano ya ishara zinatusaidia kuthamini kikamilifu zaidi sifa zote za Siku ile kuu na mashuhuri ya Bwana.

**Hali ya Sasa**

Tunaacha hapa kauli za kinabii kuhusu siku hiyo, ili kuangazia zaidi hali ya sasa ya mambo duniani, kama tunavyoiona ikijipanga kwa ajili ya pambano linalokaribia kwa kasi—pambano ambalo, litakapofikia kilele chake cha kutisha, ni lazima liwe

fupi, vinginevyo jamii ya wanadamu ingeangamizwa. Pande mbili hasimu katika vita hivi tayari zinaonekana. Utajiri, majivuno na kiburi viko upande mmoja, na umaskini ulioenea, ujinga, ushupavu na hisia kali ya dhuluma viko upande mwingine.

Pande zote mbili, zikisukumwa na nia za ubinafsi, sasa zinapanga majeshi yao kote katika ulimwengu uliostaarabika. Macho yetu yakiwa yametiwa mafuta ya kweli, popote tunapotazama tunaweza kuona kwamba bahari na mawimbi tayari yananguruma na kupiga na kutoa povu dhidi ya milima, kama inavyowakilishwa katika vitisho na majaribio ya waasi na wasioridhika ambao idadi yao inaongezeka kila mara. Tunaweza kuona, pia, kwamba msuguano kati ya pande mbalimbali au vipengele vya jamii unafikia haraka kiwango kilichoelezwa na manabii, wakati dunia (jamii) itakapokuwa inawaka moto, na viumbe vya asili vitayeyuka na kusambaratika kwa joto linalotokana na pande zote.

Bila shaka ni vigumu kwa watu, upande wowote wa mzozo huu walipo, kuona kinyume na maslahi yao wenyewe, mazoea na elimu yao. Matajiri wanahisi kuwa wana haki ya kupata zaidi ya sehemu yao stahiki ya mali za ulimwengu huu; haki ya kununua kazi na kila bidhaa kwa bei ya chini kabisa wawezavyo; haki ya kupata matunda ya juhudi zao; na haki ya kutumia akili zao kuendesha biashara zao ili kujipatia faida na kuongeza utajiri wao waliorundika, haijalishi ni nani mwingine anayelazimishwa na hali kuvuta maisha akiwa na faraja chache, hata kama ana mahitaji yote ya lazima. Wanatoa hoja hivi:

Hili haliepukiki; sheria ya ziada na mahitaji lazima itawale; matajiri na maskini daima wamekuwepo duniani; na kama utajiri ungegawanywa sawasawa asubuhi, baadhi wangefanya hivyo, kwa njia ya anasa au ubadhirifu, wangekuwa maskini kabla ya usiku, huku wengine, walio waangalifu na wenye busara zaidi, wangekuwa matajiri. Kando na hilo, watatoa hoja yenye nguvu, Je, inaweza kutarajiwa kwamba watu wenye nguvu

kubwa za ubongo wataanzisha miradi mikubwa, wakiwaajiri maelfu ya watu, na hatari za hasara kubwa, isipokuwa kuwe na matumaini ya faida na manufaa fulani?

Fundi na mfanyakazi, kinyume chake, watasema: Tunaona kwamba ingawa wafanyakazi wanafaidika na fursa nyingi leo kuliko siku nyingine yoyote, ingawa wanalipwa vizuri zaidi, na hivyo wanaweza kupata faraja kubwa zaidi, bado katika kufurahia huku wanapata tu haki yao, ambayo wamenyimwa kwa kiasi fulani kwa muda mrefu; na hivyo wanapata ipasavyo sehemu ya manufaa ya uvumbuzi, ugunduzi, ongezeko la maarifa, n.k., vya wakati wetu. Tunatambua kazi kuwa ni ya heshima, na kwamba, inapoambatana na busara, elimu, uaminifu na kanuni, ni ya heshima sawa, na ina haki sawa, kama taaluma nyingine yoyote. Na, kinyume chake, tunauona uvivu kuwa ni aibu na fedheha kwa watu wote, haijalishi wana talanta gani au kazi gani maishani. Watu wote, ili wathaminiwe, wanapaswa kuwa na manufaa kwa wengine kwa namna fulani. Lakini ingawa tunatambua maendeleo yetu ya sasa kiakili, kijamii na kifedha, tunatambua kuwa haya ni matokeo ya mazingira zaidi kuliko mpango wa kibinadamu kwa upande wetu au waajiri wetu. Tunaona hali yetu iliyoboreshwa, na ya watu wote, kuwa ni matokeo ya ongezeko kubwa la akili, uvumbuzi, n.k., hasa katika miaka hamsini iliyopita. Haya yalikuja kwa kasi sana kiasi kwamba wafanyakazi pamoja na wenye mitaji walipata msukumo kutoka kwa wimbi kubwa, na wakabebwa hadi kiwango cha juu; na kama tungeweza kuona matarajio kwamba wimbi hilo la kujaa lingeendelea kupanda, na kuwanufaisha wote, tungeridhika; lakini sasa tuna wasiwasi na hatuna utulivu kwa sababu tunaona kwamba sivyo ilivyo. Tunaona kwamba wimbi la kujaa linaanza kupwa, na kwamba ingawa wengi wameinuliwa juu katika utajiri nalo, na wamewekwa imara na salama kwenye ufukwe wa raha, anasa na utele, bado umati haujawekwa na kulindwa hivyo, bali uko katika hatari ya kurudishwa chini kama zamani, au chini zaidi, na mkondo wa chini wa wimbi linalopwa sasa. Hii ndiyo sababu tuna mwelekeo wa

kushikilia kitu ili kuhakikisha hali yetu ya sasa na maendeleo yetu zaidi kabla haijachelewa.

Tukieleza jambo hili kwa maneno mengine, sisi (mafundi na wafanyakazi) tunaona kwamba ingawa wanadamu wote wamepata baraka za siku hizi kwa kiasi kikubwa, bado wale ambao kwa sababu ya talanta kubwa zaidi ya biashara, au kwa urithi, au kwa udanganyifu na ukosefu wa uaminifu, wamekuwa wamiliki wa makumi ya maelfu na mamilioni ya dola, hawana tu faida hii juu ya wengine wote, bali, wakisaidiwa na uvumbuzi wa mitambo, n.k., wako katika nafasi ya kuendeleza uwiano wa ongezeko lao la utajiri, sawia na upungufu wa mishahara ya wafanyakazi.

Tunaona kwamba tusipochukua hatua fulani kuelekea ulinzi wa idadi inayoongezeka ya mafundi dhidi ya nguvu inayoongezeka ya mamlaka ya wachache, pamoja na mitambo inayopunguza kazi, n.k., sheria ya kinyama ya ugavi na mahitaji itatumeza kabisa. Ni dhidi ya janga hili linalokuja, badala ya dhidi ya hali za sasa, ndiyo maana tunajipanga na kutafuta mipango ya kujilinda. Kila siku inaongeza idadi yetu kwa kiasi kikubwa kwa njia ya uzazi wa asili na uhamiaji; na kila siku inaongeza mitambo inayopunguza kazi. Kwa hiyo, kila siku, inaongeza idadi ya wanaotafuta ajira na inapunguza mahitaji ya huduma zao. Sheria ya asili ya upatikanaji na mahitaji, kwa hiyo, ikiachwa iendelee bila kuingiliwa, hivi karibuni itarudisha wafanyakazi pale walipokuwa karne moja iliyopita, na kuacha manufaa yote ya siku zetu mikononi mwa wenye mitaji.

Mwelekeo huu wa mwisho wa baraka nyingi za kweli kusababisha madhara, isipodhibitiwa na sheria za busara na za haki, ulionekana tangu zamani; lakini kasi ambayo uvumbuzi mmoja umefuata mwingine, na ongezeko la mahitaji ya wafanyakazi katika kutengeneza mitambo hii inayopunguza kazi, umekuwa mkubwa sana kiasi kwamba matokeo ya mwisho yamecheleweshwa, na badala yake, ulimwengu umekuwa na "mlipuko"—mfumuko wa bei za thamani, mishahara, utajiri,

